

# FASIRI YA BIBLIA ISIYOGHARIMIWA

**UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!**

***Ukuu wa Agano Jipya:  
Waebraania***

NA BOB UTLEY,  
PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFASIRI  
(UTAFASILI WA BIBLIA)

MWONGOZO WA USOMAJI WA FASIRI MFUATANO  
AGANO JIPYA, VOL.10

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS  
2013

## **ORODHA YA YALIYOMO**

Vifupisho Viliviyotumika katika Fasiri hii ..... i

Neno Toka kwa Mwandishi:Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia! ..... ii

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Ulithibitika ..... iii

Fasiri

Utangulizi wa Waebrania ..... 1

Waebrania 1 ..... 15

Waebrania 2 ..... 32

Waebrania 3 ..... 48

Waebrania 4 ..... 66

Waebrania 5 ..... 75

Waebrania 6 ..... 82

Waebrania 7 ..... 93

Waebrania 8 ..... 103

Waebrania 9 ..... 109

Waebrania 10 ..... 126

Waebrania 11 ..... 148

Waebrania 12 ..... 159

Waebrania 13 ..... 172

### **Viambatisho**

Maelezo mafupi ya Istilahi za Visarufi vya Kiyunani ..... 188

|  |     |
|--|-----|
| Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi ..... | 197 |
| Ufafanuzi/Faharasa.....                | 201 |
| Kauli ya Mafundisho .....              | 210 |

# MADA MAALUM: ORODHA YA YALIYOMO

|   |    |
|---|----|
| Enzi Hii na Enzi Ijayo, 1:2.....                                  | 17 |
| Nuru, 1:5 .....   | 22 |
| Mzaliwa wa Kwanza, 1:6.....                                       | 23 |
| Milele (Nahau za Kiyunani), 1:8 .....                             | 24 |
| Haki, 1:9 .....   | 26 |
| Upako katika Biblia(BDB 603), 1:9 .....                           | 29 |
| Wokovu (Njeo za Kitenzi cha Kiyunani), 1:14 .....                 | 30 |
| Dhamana, 2:2.....   | 34 |
| Majina ya Uungu, 2:7 .....  | 36 |
| Mpango wa Milele wa Ukombozi wa YHWH, 2:9 .....                   | 38 |
| Mwandishi/Kiongozi ( <i>Archēgos</i> ), 2:10.....                 | 40 |
| Utakatifu/Utakaso wa Agano Jipya, 2:11.....                       | 40 |
| Kanisa ( <i>Ekklesia</i> ), 2:12.....                             | 41 |
| Batili na Tupu ( <i>Katargeō</i> ), 2:15 .....                    | 43 |
| Shetani, 2:15 .....   | 43 |
| Yesu kama Kuhani Mkuu, 2:17.....                                  | 45 |
| Maneno ya Kiyunani kwa Majaribu na Visawe Vyake, 2:18 .....       | 46 |
| Kuitwa, 3:1 .....   | 49 |
| Ukiri, 3:1.....   | 50 |
| Tumaini, 3:6 .....  | 52 |
| Utatu, 3:7 .....  | 53 |
| Moyo, 3:8.....  | 54 |
| <i>YOM</i> , 3:9 .....  | 55 |
| Maneno kwa Ufunuo wa Mungu (kwa kutumia KUMB. na ZAB), 3:10.....  | 57 |
| Lugha ya Kibinadamu kuuelezea Uungu (Anthropomorphism), 3:10..... | 58 |
| Ukanaji wa Imani ( <i>Aphistēmi</i> ), 3:12 .....                 | 60 |
| Dhamana ya Mkristo, 3:14.....                                     | 63 |
| <i>Archē</i> , 3:14.....  | 64 |
| Mbingu na Mbingu ya Tatu, 4:14.....                               | 72 |
| Hitaji la Ustahimilivu, 4:14.....                                 | 72 |
| Umilele,6:2.....  | 85 |
| Kufanywa Upya ( <i>Anaikainōsis</i> ), 6:6.....                   | 87 |

|   |     |
|---|-----|
| Watakatifu, 6:10 .....  | 88  |
| Urithi wa Mwamini, 6:12 .....   | 89  |
| Mwisho au Kamili ( <i>telos</i> ), 7:11.....                              | 96  |
| Pasipo lawama, hatia, Kosa wala Mawaa, 7:26.....                          | 99  |
| Agano, 8:6 .....  | 106 |
| Sanduku la Agano, 9:4 .....   | 111 |
| Majina ya Uungu, 9:14.....  | 117 |
| Fidia/Komboa, 9:18.....   | 120 |
| Ujasiri ( <i>Parrēsia</i> ), 10:19 .....                                  | 132 |
| Moto, 10:27 .....   | 137 |
| Mwana wa Mungu, 10:29.....  | 138 |
| Ustahimilivu, 10:35 .....   | 141 |
| Amini, Tumaini, Imani na Uaminifu katika Agano la Kale (լՆՈ), 10:38 ..... | 143 |
| Miji Miwili katika Isaya, 11:10.....                                      | 152 |
| Toba katika Agano la Kale, 12:17 .....                                    | 166 |
| Ufalme wa Mungu, 12:28 .....  | 170 |
| <i>Koinōnia</i> ,13:16 .....  | 178 |
| Milele ('Olam), 13:20 .....   | 181 |
| Mapenzi ( <i>thelēma</i> ) ya Mungu, 13:21.....                           | 183 |
| Amina, 13:21.....   | 184 |

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

|         |  |
|---------|--|
| AB      | Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman                                    |
| ABD     | Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman   |
| AKOT    | Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens   |
| ANET    | Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard   |
| BDB A   | Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs                         |
| IDB     | The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick  |
| ISBE    | International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr   |
| JB      | Jerusalem Bible  |
| JPSOA   | The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America) |
| KB      | The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner                       |
| LAM     | The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa                                  |
| LXX     | Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970   |
| MOF     | A New Translation of the Bible by James Moffatt  |
| MT      | Masoretic Hebrew Text  |
| NAB     | New American Bible Text  |
| NASB    | New American Standard Bible  |
| NEB     | New English Bible  |
| NET     | NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition  |
| NRSV    | New Revised Standard Bible   |
| NIDOTTE | New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren            |
| NIV     | New International Version  |
| NJB     | New Jerusalem Bible  |
| OTPG    | Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith                                     |
| REB     | Revised English Bible  |
| RSV     | Revised Standard Version   |
| SEPT    | The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970   |
| TEV     | Today's English Version from United Bible Societies  |
| YLT     | Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young  |
| ZPBE    | Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenne   |

# **NENO TOKA KWA MWANDISHI**

## **NI KWA NAMNA GANI FASIRI HII ITAKUSAIDIA?**

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuvuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yejote mtafasiri mionganoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

### **KANUNI YA KWANZA**

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuvuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

### **KANUNI YA PILI**

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiwane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nydingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyopamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisheso la chapisho la Nne la (UBS<sup>4</sup>). Andiko hili iliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginez. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lilitoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today's English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenyewe nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS<sup>4</sup> na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenyewe mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoliki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving'ang'anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley  
 Juni 27, 1996  
 Haki Miliki © 2013 [Bible Lessons International](#)

# **MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:**

## **UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA**

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yejote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyyokuwa. Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yejote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliouunganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanawea kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko. Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru, lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:


## DHANIO

1. Ninaamini biblia ni uuvvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kuitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
  - Wapokeaji wa mwanzo
  - Ujumbe ulioandikwa
  - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kuitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo waliosoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyo simama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliye vuvviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
  - a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
  - b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
  - c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
  - d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
  - e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
  - f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-historia wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikajji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dharti uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:



vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya “mwitikio wa msomaji” (unamaanishwa nini kwangu). Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufaishi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipo ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

### III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kuititia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: “Biblia inaangazia zaidi katika fasihi”. Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekeea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

#### 1. Mzunguko wa kwanza wa usomaji

- a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti, kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
  - 1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
  - 2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
  - 3) Ufanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
- b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
- c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira

- d. Tambua fasihi tanzu yenyeye nguvu
  - 1) Agano la kale
    - a) Simulizi za waembrania
    - b) Mashairi ya waembrania (fasihi za hekima, zaburi)
    - c) Unabii wa ki-Ebrania (lughya ya mjazo, shairi)
    - d) Alama za siri za ki-sheria
  - 2) Agano jipya
    - a) Simulizi (Injili, matendo)
    - b) Hadithi za mafumbo (Injili)
    - c) Barua/nyaraka
    - d) Fasihi za mafunuo
- 2. **Mzunguko pili wa usomaji**
  - a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
  - b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
  - c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.
- 3. **Mzunguko wa tatu wa usomaji.**
  - a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
  - b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
    - 1) Mwandishi
    - 2) Tarehe
    - 3) Wapokeaji
    - 4) Kusudu mahsusini la uandishi
    - 5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
    - 6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
  - c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyangi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyangi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
  - d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji
- 4. **Mzunguko wa nne wa usomaji**
  - a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nynginezo nyangi
    - 1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
    - 2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
    - 3) Ufanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
  - b. Angalia fasihi au muundo wa kisarufi
    - 1) Misemo ya kujirudia Waefeso 1:6, 12, 14
    - 2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
    - 3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
  - c. Taja vipengele vifuatavyo:-
    - 1) Istilahi muhimu
    - 2) Istahili zisizo za kawaida
    - 3) Muundo muhimu wa kisarufi
    - 4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
  - d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
    - 1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
      - a) Vitabu vya thiolojia
      - b) Biblia za marejeo
      - c) Itifaki
    - 2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyangi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana

nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuvuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.

- 3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.
- e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
  - 1) Soma biblia
  - 2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
  - 3) Tangulizi za biblia
  - 4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

#### **iv. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.**

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama “uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi”. Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!

Maeleo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji #3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuvuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafasiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema “asema Bwana”lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwiningi kanuni zetu ni “zetu” na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

#### **v. Sura ya utafasiri wa kiroho.**

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekemu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18

"Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenyewe mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale amba Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."

2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm,*Protestant Biblical Interpretation(tafsiri ya biblia ya ki-protestanti)* Uk.75:

Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.

3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:

Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa fasihii umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:*

1. Maeleo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mzunguko wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihii imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihii kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maeleo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
  - a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
  - b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
  - c. The New King James Version (NKJV)
  - d. The New Revised Standard Version (NRSV)
  - e. Today's English Version (TEV)
  - f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyangi za kisasa kutoka tafsiri nyangi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu wa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyangi.
  - a. Mazingira ya fasihii
  - b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni

- c. Habari za kisarufi
  - d. Usomaji wa neno
  - e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
- a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa “Upokeaji wa Maandiko halisi”.
  - b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
  - c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
  - d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
- a. Tofauti za mswada
  - b. Maana ya maneno mbadala
  - c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
  - d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu                        ya                              utafsiri                              wa                              kifungu                              hicho

# UTANGULIZI WA WAEBRANIA

## KAULI MUHIMU YA UFUNGUZI

Kadiri nilivyokisoma kitabu hiki imekuwa dhahiri na dhahiri kwamba thiolojia yangu inatengenezwa na Paulo. Ni ngumu sana kwangu kuruhusu wingi wa waandishi wengine wa Agano Jipyä kuwasilisha mawazo yao yaliyovuviwa kwasababu natarajia kuyaweka katika vipengele vya Ki-Paulo. Hii hasa ni dhahiri katika msisistizo wa Waebrania juu ya kuendelea katika imani. Katika kitabu cha Waebrania, imani sio nafasi ya kisheria (uhalalalishaji kwa imani), bali maisha ya uaminifu mpaka mwisho (Ebr. 11-12).

Nina hofu kwamba mengi ya maswali ninayosumbuka nayo katika Waebrania yasingeulizwa na mwandishi wake (sio Petro wala Yakobo). Waebrania ni nyaraka ya kimazingira kama vitabu vyote vya Agano Jipyä. Inanibidi niruhusu mwandishi azungumze hata wakati hanifanyi kuwa na rahä; hata wakati hatumii vipengele vipendezavyo au hata kuondoa vipengele hivyo. Sithubutu kuweka mbadala wa thiolojia yangu ya darasani kwenye ujumbe uliovuviwa wa mwandishi wa Agano Jipyä.

Nachagua kugeuka mafundisho yangu ya kithiolojia na kuishi ndani ya mvutano wa Agano Jipyä ambao siuelewi kikamilifu au kuuchagua! Ninahofia kuwa natazama Agano Jipyä kupitia chujio la uinjilisti wa kisasa, vipimo vya mgeuko. Nataka nikiri ahadi za kibiblia; ahadi za upendo wa Mungu, utoshelevu na nguvu itunzayo; japo nashawishiwa kwa maonyo yenye nguvu na mamlaka ya waandishi wa Agano Jipyä. Kwa shauku sana ninahitaji kusikia Waebarnia, lakini ina maumivu sana! Nataka niondoe mvutano kwa maelezo. Nadhani, kiuhalisia, ninataka kukiri wokovu wa bure na maisha ya Mkristo yanayogharimu kila kitu. Lakini wapi ninapochora mstari wakati hatukutani na tulichokipata? Je ushirika wa milele pamoja na Mungu mwitikio wa kwanza wa imani au mrejesho wa imani inayoendelea? Waebrania kidhahiri inaelezea mamlaka ya mwitikio wa imani inayoendelea. Maisha ya Mkristo yanatazamwa kutokea mwisho, sio mwanzo!

Hii haijaku sudiwa kumaanisha wokobu wenye kujikita katika matendo bali uthibitisho wenye kujikita katika matendo. Imani ni ushahidi wala sio chombo (ambayo ni neema). Waaminio hawaokolewi kwa matendo balindani ya matendo. Matendo sio namna ya wokovu bali matokeo ya wokovu. Kufanana na Kristo ki-utauwa, na uaminifu wa kila siku sio kitu tunachofanya bali tulivyondani Yake. Ikiwa mabadiliko, na maisha ya imani yenye mabadiliko, hakuna ushahidi wa wokovu wetu, hakula usalama kwa mwamini. Ni Mungu tu anajua moyo na mazingira. Dhamana haikusudiwi kuwa mwenza katika maisha ya imani, sio tamko la kuanzia la kithiolojia linaloondo maisha ya ushahidi.

Maombi yangu ni kwamba tutaruhusu mwandishi huyu wa Agano Jipyä aliyevuviwa kuzungumza kwa udhahiri na sio kushusha Waebrania kwenyetanbihi ya kithiolojia katika vipimo vya kithiolojia vya darasani, iwe ni nadharia ya Calvin au wa-Armeni.

## TAMBUZI ZA UFUNGUZI

- A. Kitabu hiki kinatumia maandiko ya Agano la Kale yaliyofasiriwa na wataalamu wafasiri wa sharia za kiyahudi kuzungumzia ujumbe wake. Ili kuelewa makusudi ya asili ya mwandishi, kitabu hiki lazima kitafsiriwe katika ufahamu wa karne ya kwanza ya dini ya Kiyahudi ya sheria za Kiyahudi, sio katika wazo la kimagharibi la kisasa.
- B. Kitabu hiki kama mahubiri (bila kuwako na utangulizi au salamu zilizozoeleka) na kumalizia kama barua (namna ya ufungaji wa ki-Paulo wa sura ya 13). Inawezekana hekalu la nyumbani liliibadili kuwa barua. Mwandishi anaita kitabu chake "neno la kuonya" katika Ebr. 13:22. Tungo hiyo hiyo inatumika pia katika
- C. Fasiri hii ya maarifa ya Agano Jipyä juu ya agano la Musa:
  1. ni mtazamo wenye mamlaka ya Agano la Kale
  2. ulinganifu wa agano la kale na jipyä
  3. kitabu pekee cha Agano Jipyä ambacho kinamuita Yesu kuwa kuhani wetu mkuu

- D. Kitabu hiki kimejaa maonyo dhidi ya kuanguka ("kurudi nyuma" kama vile Ebr. 10:38), au kurudi katika Dini ya Kiyahudi (yaani sura za 2,4,5,6,10,12; kama vile *No Easy Salvation* cha R. C. Glaze, Jr., kilichochapishwa na Insight Press).
- E. Ingawa ni mjumuishowa jumla uliopitiliza, inasaidia kumuona Paulo akiwa na mkazo wake juu ya wokovu kama kazi iliyokwisha malizika ya Mungu Mkuu mwenye mamlaka (yaani kuhesabiwa haki kwa imani) kuelezea usalama kama kweli ya kuanzia (yaani Warumi 4). Petro, Yakobo na nyaraka za 1 na 2 Yohana zinaweka mkazo juu ya majuklumu yanayoendelea ya Agano Jipywa na kuelezea ulinzi wa kila siku, ikithibitishwa na maisha yaliyo badilika na yanayo badilika. Mwandishi wa Waebrania, akisisitiza maisha ya uaminifu (kama vile sura ya 11), anaelezea mtazamo wa kiulinzi wa maisha tokea mwisho wake. Fikra za kisomi za kimagharibi za kisasa zina tabia ya kugawa mitazamo hii, wakati waandishi wa Agano Jipywa (yaani Roho), anataka kuwashikilia katika mvutano na kukiri zote mitatu. Dhamana haijawahi kuwa lengo bali matokeo tu ya imani iliyo hai katika ahadi za Mungu.

## **UANDISHI**

- A. Ingawa uandishi wa Waebrania upo katika mgongano, kazi kadhaa za Wajuzi wa kale (kama vile *Gospel of Truth, Gospel of Philip* na *The Apocrypha of John*) zinazi nukuu mara kadhaa, jambo linaloonyesha kwamba ilikuwa inachukuliwa kuwa sehemu ya maandiko ya kikristo yenyenye mamalaka ya karne ya pili (kama vile Andrea Helmbold's *The Nag Hammadi Gnostic Texts and the Bible*, ukurasa wa 91)
- B. Kanisa la Mashariki (Iskandria, Misri) lilikubali uandishi wa Paulo kama ilivyoonekana katika orodha yake ya kuorodhesha Waebrania katika maandiko ya Paulo katika maandiko ya kale ya mafunjo P<sup>46</sup>. Maandiko haya yanaitwa Mafunjo ya Chester Beatty na yalinakiliwa mwishoni mwa karne ya Pili. Inaweka Waebrania baada ya Warumi. Baadhi ya viongozi wa Ki-Iskandria walitambua matatizo ya kifasihi yanayohusiana na uandishi wa Paulo.
  1. Clement wa Iskandria (150-215 b.k, aliyenukuliwa na Eusebius) anasema kwamba Paulo alikiandika katika Waebrania na Luka akakitafsiri katika Kiyunani.
  2. Origen (185-253 b.k) alielezea kwamba mawazo ni ya Paulo lakini kiliandikwa na mfuasi wa baadaye, kama vile Luka au Clement wa Rumi.
- C. Kitabu hiki kimeondolewa katika nyaraka za Paulo na kuchukuliwa na kanisa la Magharibi liitwalo Muratonian Fragment (orodha ya vitabu vya kikanoni vya Agano Jipywa kutoka Rumi mnamo mwaka 180-200 b.k).
- D. Kile tunachokijua juu ya mwandishi
  1. Alikuwa dhahiri kama Mkristo wa kiyahudi wa kizazi cha pili (Ebr. 2:3).
  2. Ananukuu kutoka fasiri ya Kiyunani ya Agano la Kale liitwalo Septuagint.
  3. Anatumia taratibu za hema ya kale na sio taratibu za hekalu la sasa.
  4. Anaandika akitumia misamiati ya Kiyunani ya kipindi kile na mfumo wa lugha yake (kitabu hiki hakifuati nadharia za ki-Plato. Mtiririko ni wa Agano la Kale, sio wa ki-Philo).
- E. Kitabu hiki hakijulikani bali mwandishi wake alikuwa akijulikana vizuri sana kwa wapokeaji (kama vile Ebr. 6:9-10; 10:34; 13:7,9).
- F. Kwanini kuna mashaka juu ya uandishi wa Paulo
  1. Aina ya uandishi ni tofauti sana (isipokuwa sura ya 13) kutoka maandiko mengine ya Paulo.
  2. Misamiati ni tofauti.
  3. Kuna tofauti kidogo katika neno na matumizi ya kifungu na msisitizo.

- Wakati Paulo anawaita rafiki zake watenda kazi pamoja naye "ndugu" jina la mtu siku zote hutangulia (kama vile Rum. 16:23; 1 Kor. 1:1; 16:12; 2 Kor. 1:1; 2:13; Flp. 2:25) lakini Ebr. 13:23 lina "ndugu yetu Timotheo."

#### G. Nadharia za Uandishi

- Clement wa Iskandria katika kitabu chake *Hypotyposes* (kilichonukuliwa na Eusebius) aliamini Luka kilitafsiriwa katika maandiko ya Waebrania ya asili ya Paulo (Luka alitumia Koine ya Kiyunani iliyo bora kuliko zote).
- Origen alisema aidha Luka au Clement wa Rumi alikiandika lakini akifuatisha mafundisho ya Paulo.
- Jerome na Augustine walikubali uandishi wa Paulo ili tu kuwezesha ukubalifu wa kitabu katika Kanoni kwa Kanisa la Magharibi.
- Tertullian (*De Pudic.* 20) alimwamini Barnaba (mlawi aliyekuwa na uhusiano na Paulo) kuwa ndiye aliyekiandika.
- Martin Luther anasema Apollo, msomi mwenye aliyefunzwa wa ki-Iskandria aliyekuwa na mahusiano na Paulo (kama vile Mdo.18:24), ndiye aliyekiandika.
- Calvin alisema kwamba Clement wa Rumi (alkuwa wa kwanza kokinukuu mnamo mwaka 96 b.k) au Luka alikuwa mwandishi.
- Adolph von Harnack alisema Aquila na Priscilla (walimfundisha Apollo injili kamili na walikuwa na mahusiano na Paulo na Timotheo, kama vile Mdo. 18:26) alikiandika.
- Sir William Ramsey anasema Philip (mwinjilisti) alikiandika kwa ajili ya Paulo wakati Paulo alipokuwa gerezani huko Kaisaria.
- Wengine wamewataja Philipo au Sila (Silvano).

## WAPOKEAJI

- Jina "kwa Waebrania" inawahu su watu Waebrania, hivyo kitabu kiliandikwa kwa Wayahudi wote (kama vile Clement wa Iskandria, kikinukuliwa na Eusebius, *Eccl. Hist.* VI, 14).
- Ushahidi wa kiundani kufuatia R. C. Glaze, Jr.'s *No Easy Salvation* kinalezeza kwamba kikundi fulani cha Wayahudi waaminio au hekalu ndilo linalohutubiwa (kama vile Ebr. 6:10; 10:32-34; 12:4; 13:7,19,23)
  - Wanaonekana kuwa waaminio wa Kiyahudi kwasababu ya nukuu kadhaa za Agano la Kale na maudhui (kama vile Ebr. 3:1; 4:14-16; 6:9; 10:34; 13:1-25).
  - Walikuwa wamepitia mateso kadhaa (kama vile Ebr. 10:32; 12:4). Dini ya Kiyahudi ilitambuliwa kama dini ya kisheria na mamlaka ya Kirumi wakati baadaye katika Ukristo wa karne ya kwanza ilionekana kuwa si halali kisheria wakati ilipotenganishwa kutoka ibada ya sinagogi.
  - Walikuwa waamini kwa muda mrefu japo bado walikuwa wachanga (kama vile Ebr. 5:11-14). Walikuwa na hofu kujitenga moja kwa moja kutoka katika dini ya Kiyahudi (kama vile 6:1-2).
- Andiko tata la Ebr. 13:24 lingemaanisha liliandikwa (1) kutoka Italia au (2) kwenda Itali, yavezekana Rumi.
- Eneo la mahali la wapokeaji linaunganishwa na nadharia mbali mbali juu ya uandishi.
  - Iskandria – Apollo
  - Antiokia – Barnaba
  - Kaisaria - Luka au Philipo
  - Rumi - Clement wa Rumi na kutajwa kwa Italia katika Ebr. 13:24.
  - Uhispasia - Hii ilikuwa ni nadharia ya Nikola wa Lyra (1270-1340 b.k)

## TAREHE

- Kabla ya uharibifu wa Yerusalem uliofanya na Kamanda wa Kirumi (baadaye kuwa mfalme) Titus, mnamo mwaka 70 b.k

1. mwandishi anamtaja mwenza wa Paulo Timotheo kwa jina (kama vile Ebr. 13:23)
  2. mwandishi anarejereea kuendelea kwa dhabihu (kama vile Ebr. 8:13; 10:1-2) katika Hekalu
  3. mwandishi anataja mateso ambayo yanaweza kushabihiana na nyakati za Nero (54-68 b.k)
  4. mwandishi anahamasisha wasomaji kutorudi katika dini ya Kiyahudi na ibada zao
- B. Baada ya mwaka 70 b.k
1. mwandishi anatumia taratibu za ibada za hema wala sio hekalu la Herode
  2. mwandishi anataja mateso
    - a. yawezekana chini ya Nero (kama vile Ebr. 10:32-34)
    - b. baadaye yawezekana chini ya Domitian (kama vile Ebr. 12:4-13)
  3. kitabu kinaweza kuhusiana na uamsho wa dini ya kiyahudi wa sheria zao (maandiko kutoka Jamnia) baadaye kutoka katika karne ya kwanza
- C. Kabla ya mwaka 95 b.k kwasababu kitabu kinanukuliwa na Clement wa Rumi.

## KUSUDI

- A. Wakristo wa Kiyahudi wanahamasishwa kuachana na Sinagogi na kujitangaza hadharani (kikamilifu) pamoja na kanisa (kama vile Ebr. 13:13).
- B. Wakristo wa Kiyahudi wanahamasishwa kuchukua mamlaka ya kimisionari ya injili (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo 1:8).
- C. Wayahudi wasioamini katika ushirika pamoja na wakristo hawa wa kiyahudi ni shabaha ya sura za 6 na 10.Tazama uwepo wa makundi matatu, "sisi," "ninyi," na "wao." Wanaonywa kurejerea kibin afsi kwenye ushahidi ulio wazi wa utoshelevu katika maisha ya marafiki zao wa Kikristo na wenze kuabudu pamoja nao.
- D. Matengenezo haya mapya ya kihistoria inachukuliwa kutoka *No Easy Salvation* cha R. C. Glaze, Jr.
 

"Tatizo halikuwa uvutano katika ya wengi walio wakristo na wachache wasio wakristo. Kinyume cha ukweli huu pia ni kweli. Wakristo Wayahudi wa kusanyiko hili walikuwa wameharibu imani yao na namna ya uwakala kwamba makundi mawili waweze kuabudu pamoja kama kundi moja. Hakukuwa na kundi mojawapo kati ya haya ambayo wangesumbua dhamiri ya ingine. Hakukuwepo tena na mahubiri ya kikundi cha Kikristo kupelekeea katika ushawishi na maamuzi upande wa washirika wasiookoka wa Sinagogi. Wakristo walikuwa katika hali ya mkwamo kwasababu ya kutokuwa kwao tayari kukubaliana na matakwa kamili yamaisha ya Wakristo ya Ujasiri. Wasioamini walikuwa wamefanywa sugu kwa mwendelezo wa kukataliwa mpaka dakika ya utofautiano makali. Makundi haya sasa yalikuwa yamekuwa na mrando na wenzao waliowakalibisha.

Ukosefu wa utayari wa kikundi cha Kikristo 'kuendelea katika ukamilifu' (6:1) kulihamasishwa na mazingira ya iana mbili: kujali sana desturi za dini ya kiyahudi na kukosekana kwa utayari wa kulipa gherama ya utambulisho kamili pamoja na Ukristo, jambo ambalo lilikuwa zaidi na zaidi hoja za upingaji za Mataifa" (ukurasa wa 23).

## UAINISHO WA MUHTASARI WA WAEBRANIA

- |      |   |
|------|---|
| Ebr. | 1:1-3 Ukuu wa Mwana juu ya manabii                                    |
| Ebr. | 1:4-2:18 Ukuu wa Mwana juu ya malaika                                 |
| Ebr. | 3:1-4:13 Ukuu wa Mwana juu ya Agano la Musa<br>4:14-5:10              |
| Ebr. | 6:13-7:28 Ukuu wa Mwana juu ya Ukuhani wa Haruni                      |
| Ebr. | 5:11-6:12 Ukuu wa Wayahudi waaminio juu ya Wayahudi wasioamini        |
| Ebr. | 8:1-10:18 Ukuu wa Mwana juu ya taratibu za Agano la Musa              |
| Ebr. | 10:19-13:25 Ukuu wa Mwana ikichagizwa na kufunuliwa ndani ya waaminio |

Huu ni mfano wa tafsiri ya maandiko ya sheria za kiyahudi iitwayo "Lesser to Greater (Ndogo kwenda Kubwa)."

## **MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (Kutoka "[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Dhamira ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi iliyotumika (uwasilishaji)

## **MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (Kutoka "[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Mada ya sehemu ya kwanza ya fasihi
2. Mada ya sehemu ya pili ya fasihi
3. Mada ya sehemu ya tatu ya fasihi
4. Mada ya sehemu ya nne ya fasihi
5. N.k.

# WAEBRANIA 1

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA* |                                   |                               |  |   |
|--|-----------------------------------|-------------------------------|--|---|
| UBS <sup>4</sup>                       | NKJV                              | NRSV                          | TEV                                    | NJB   |
| Mungu<br>Amezungunza na<br>Mwanae      | Ufunuo wa Ukuu<br>wa Mungu        | Dibaji                        | Neno la Mungu<br>Kupitia kwa<br>Mwanae | Ukuu wa<br>umbo-mwili...<br>Mwana wa<br>Mungu |
| 1:1-4                                  | 1:1-4                             | 1:1-4                         | 1:1-4                                  | 1:1-4   |
| Mwana ni Mkuu<br>Kwa Malaika           | Mwana Ametukuka<br>Juu ya Malaika | Ukuu wa Kristo<br>kwa Malaika | Ukuu wa Mwana<br>wa Mungu              | Mwana ni<br>Mungu Mkuu<br>Kuliko Maika        |
|  |                                   | (1:5-2:18)                    |  | (1:5-2:18)                                    |
|  |                                   |                               | 1:4-13                                 |   |
| 1:5-14                                 | 1:5-14                            | 1:5-14                        |  | 1:5-13  |
|  |                                   |                               | 1:14                                   | 1:14  |

\* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.

Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoewela kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunailewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: [Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani \(Brief Definitions of Greek Grammatical Structure\)](#), [Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi \(Textual Criticism\)](#), [Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko \(Glossary\)](#).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)

### KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

### TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Aya ya kwanza ni uwasilishaji wa kishairi /wa kiuimbaji wa mafanikio Yesu ya kiulimwengu na kiukombozi. Yeye ni Bwana wa uuumbaji wote na hasa Bwana wa sayari hii. Hili linalelezwa kinagaubaga katika vifungu bainishi saba. Hii ni moja ya mambo makuu sana yanayohusiana na Kristo katika Agano Jipy (kama vile Yohana 1:1-18; Flp. 2:6-11; na Kol. 1:15-17).
1. mrithi wa uumbaji wa Baba (Ebr. 1:2)
  2. wakala mkuu wa uumbaji wa Baba (Ebr.1:2)
  3. mng'ao wautukufu wa Baba (Ebr.1:3)
  4. chapa kamili ya nafsi ya Baba (Ebr.1:3)
  5. mchukuaji wa uumbaji wa Baba (Ebr.1:3)
  6. chimbuko la msamaha wa uunbaji wa Baba (Ebr.1:3)
  7. Masihi wa kifalme na kikuhanaliyetumwa na Baba (Ebr.1:3)
- B. Mistari ya 1-4 hasa inaongelea namna Mungu ailivyozungumza nasi katika njia mpya kupitia mwana, Yesuwa Nazarethi. Hatuupokei tena ufunuo wa papo kwa papo kupitiawatumishi (yaani., manabii wa Agano la Kale), bali sasa ni kupitia ufunuo kamili kndani ya mwana-familia ("mwana," kama vile Ebr. 1:2; 3:6; 5:8; 7:28).
- C. Waembrania 1:1-3 inamwonyesha Yesu, Aliyetiwa Mafuta, kama hatima ya utimilifu wa kazi zote tatu za upakwa mafuta za Agano la Kale (yaani., nabii, kuhani na mfalme).
- D. Aya ya pili (Ebr.1:5-14) inaendeleza wazo la ukuu wa Yesu. Katika Ebr.1:1-4 Yeye ni ufunuo mkuu kuliko manabii; katika Ebr.1:5-14 Yeye ni mpatanishi mkuu kuliko malaika; aliyethibitishwa kwa mfululizo wa maandiko saba ya Agano la Kale toka Agano la Kale la Kiebrania (hasa toka katika Zaburi: Zaburi 2:7; 2 Sam. 7:14; Zab. 97:7; Zab. 104:4; Zab. 45:6-7; Zab. 102:25-27 na Zab. 110:1).
- E. Elewa kwamba mwandishi anaumba andiko lake katika umakini wa njia saba. Saba ni namba ya utimilifu katika tarakimu za Kiyahudi (yaani., siku saba za Mwanzo 1).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 1:1-4

<sup>1</sup>Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,

<sup>2</sup>mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. <sup>3</sup>Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;

<sup>4</sup>amefanyika bora kupita malaika, kwa kadiri jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao.

**1:1 "Mungu, ambaye alisema"** Neno "Mungu" si la kwanza (elekezwa) katika utungo wa Kiyunani; hivyo, andiko hili halistiziki juu ya mafundisho ya ufunuo, bali tabia ya ufunuo ulio katika wakati uliopita (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usio timilifu).

▣"**katika manabii**" Wayahudi waliamini kwamba manabii ndiyo walioandika Maandiko. Ndiyo sababu Musa alifikiriwa kuwa nabii (kama vile Kumb. 18:15) na ndiyo sababu Wayahudi waliviandika vitabu vyta kihistoria vyta Yoshua kupitia Wafalme kama "manabii wa kale." Hivyo, kifungu hiki hakiwarejelei manabii wa Agano la Kale pekee, bali kwa waandishi wote wa Agano la Kale.

Hiki kifungu "katika (en) manabii" (mst.1) kinafanana na kifungu "katika (en) Mwana wake" (mst.2). Kuna tofauti dhahiri kati ya hizi maana mbili za ufunuo. Moja ilikuwa ya mtumishi na moja mwanafamilia. Ya kwanza ilikuwa ya ilikuwa na mipaka lakini ya pili ni imilifu na kamili (kama vile Kol. 1:15-17).

|      |  |
|------|--|
| NASB | "kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi"             |
| NKJV | "kwa wakati ofauti na katika namna tofauti"        |
| NRSV | "katika namna na njia tofauti"                     |
| TEV  | "mara nyingi na katika namna nyingi"               |
| NJB  | "kwa wakati mwingi wakati ule na kwa maana nyingi" |

Ufunuo wa Agano la Kale ulikuwa kidogo kodo katika muundo wake na muktadha. Kifungu hiki kinaondolewa kwanza (kueleka) katika andiko la Kiyunani la Ebr. 1:1 kuuonyesha msistizo wa mwandishi. Kila mwandishi wa Agano la Kale alikuwa na umuhimu, lakini usio timilifu, ujembe.

Mungu alijifunua mwenyewe:

1. kwa Musa katika kijiti kilichokuwa kikitoa mwali wa moto
2. kwa Kuhani Mkuu kupitia kwa Urimu naThummim
3. kwa Eliya katika utulivu, katika sauti ndogo
4. kwa Ezekieli katika maono
5. kwa Hosea kupitia ndoa ya kimakosa
6. kwa Yona kupita samaki

**1:2 "siku hizi za mwisho"** Hiki kipindi cha wakati kinapita kwa majina kadhaa.

1. siku za mwisho, Hes. 24:14; Kumb. 8:16; Dan. 2:28; 10:14
2. katika siku za mwisho, Yer. 23:20; 30:24; 49:39; Eze. 38:8,16; Hos. 3:5; Yoeli 2:28 (Matendo 2:17); Yohana 6:39,40,44,54; 11:24; 12:48; 2 Tim. 3:1; Yakobo 5:3
3. Katika wakati wa mwisho, 1 Pet. 1:5
4. mwisho wa zamani , 1 Pet. 1:20
5. katika siku za mwisho, 2 Pet. 3:3
6. wakati wa mwisho, 1 Yohana 2:18

Katika siku mwisho ni "siku ya Bwana" (yaani, "ukamilisho," Mt. 13:39,40; 24:3; 28:20; Ebr. 9:26).

Wayahudi wakipindi kile cha ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipy waliziona nyakati mbili: zama hizi za sasa za uovu wa uasi na dhambi (kwa kuanza na Mwanzo 3) na zama zijazo za haki zilizotambuliwa na ujio wa Masihi katika uweza wa Roho. Agano la Kale unasistiza juu ya ujio wa Masihi katika hukumu na uweza wa kuzihimarisha zama mpya. Hata hivyo, hili lilishindwa kuuona dhahiri ujio wa Yesu kama (1) "Mtumishi ateswaye" katika Isaya 53; (2) mnyenyeketu, amepanda pundakatika Zek. 9:9; na (3) yeye aliyechomwa wa Zek. 12:10. Kutokana na ufunuo endelevu wa Agano Jipy tunajua ya kwamba Mungu aliupanga ujio wa aina mbili wa Masihi. Kipindi kati ya kuutwaa mwili (ujio wa kwanza) na ujio wa pili kinahusisha kutamgulia kwa zama mbili za Kiyahudi. Hili linachaguliwa katika Agano Jipy kupitia kifungu "siku za mwisho." Tumekuwa katika kipindi hiki yapata miaka 2000.

### **MADA MAALUMU: ENZI HII NA ENZI IJAYO**

Manabii wa Agano la Kale waliutazama wakati ujao kama upanuzi wa wakati uliopo. Kwao wakati ujao utakuwa marejesho ya Israeli ya kijiografia. Hata hivyo, hata wao waliuona kama siku mpya (kama vile Isa. 65:17; 66:22). Kwa kwendelea kukataliwa YHWH kwa makusudi na uzao wa Abraham (hata baada ya uhamisho) ni kielelezo kiliicho dhihirika ndani ya hati ya Kiyahudi ya fasili ya mambo ya ufunuo wa matukio ya siku za mwisho (yaani, I Enoch, IV Ezra, II Baruch). Maandishi haya yanatengeneza utofauti kati ya zama hizi mbili: zama za uovu za sasa zinazomilikiwa na Shetani na zama zijazo za haki zinazomilikiwa na Roho na zilizozinduliwa na Masihi (apiganaye mwenyewe mara kwa mara).

Katika eneo hili la theolojia (hukumu, kifo na peponi) kuna maendeleo ya dhairi. Wanatheolojia wanalihita hili "ufunuo endelevu." Agano Jipy linakubaliana na ukweli huu mpya wa kiulimwengu wa zama hizi mbili (yaani, nyakati mbili

| Yesu                       | Paulo  | Webrania (Paulo)   |
|----------------------------|--|--------------------|
| Mt. 12:32; 13:22,39        | Warumi 12:2  | Ebr.1:2; 6:5; 11:3 |
| Marko 10:30                | 1 Kor. 1:20; 2:6,8; 3:18   |                    |
| Luka 16:8; 18:30; 20:34-35 | 2 Kor. 4:4<br>Wagalatia 1:4<br>Efe. 1:21; 2:2,7; 6:12<br>1 Timotheo 6:17<br>2 Timotheo 4:10<br>Tito 2:12 |                    |

Katika thiolojia ya Agano Jipyä zama hizi za Kiyahudi zimekuwa zikipishana kwa sababu ya tabiri zisizotarajiwa na ambazo hazikutiliwa maanani zilizohusu kuja kwa Masihi. Kuonekana kwa Yesu katika umbile la mwili kulitimiza unabii mwangi wa Agano la Kale uliohusu utambuzi wa zama mpya (Dan. 2:44-45). Hata hivyo, Agano la Kale pia liliutazama ujio Wake kama Hakimu na Mshindi, bado alikuja kwa mara ya kwanza kama Mtumishi Ateswaye (kama vile Isaya 53; Zek. 12:10), mnyenyeketu na mpole (kama vile Zekaria 9:9). Atarudi katika nguvu ile ile kama Agano la Kale liiliviyotabiri (kama vile Ufunuo 19). Utimilifu wa zama hizi mbili ulisababisha Ufalme kuwepo (uliotambuliwa), lakini zile zijazo (hazijatimilika ipasavyo). Huu ni mvutano wa Agano Jipyä wa uliopo tayari, lakini bado!

▣ "Mwana" Hiki kifungu anarthrous "mwana" hakipaswa kuandikwa kwa herufi kubwa kwa sababu hapa rejea ni kwa namna ya ufunuo, si jina la Yesu (kama vile Ebr. 3:5-6; 5:8; 7:28). Yesu si mtunishi kama Musa au manabii, bali mmoja wa familia (mwana).

▣ "aliywewka" Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usio timilifu, yenyé kudokeza tendo lililokamilishwa (wakati uliopita usiotimilifu) katika wakati uliopita (dhamira elekezi). Je! Mungu alimchagua Yesu wakati gani? Je! Alikuwepo katika ubatizo wake (kama vile Mt. 3:17) au ufufuo wake (kama vile Rum. 1:4)? Swali hili lilikuwa na mwelekeo wa uasi wa "uasilishaji" (tazama Kiambata), uliosemekana kwamba Yesu alikuwa Masihi kwa wakati. Hili, hata hivyo, linaitofautisha Yohana 1:1-18; 8:57-58; Flp. 2:6-7; na Kol. 1:17. Mara nyingi Yesu amekuwa Uungu (kama vile Yohana 1:1-2); hivyo, lazima urithi uutangulie utwaaji mwili katika maana ya asili ya uhai.

▣ "kuwa mrithi wa yote" Kama "Mwana wa Mungu,"mwana wa pekee wa Mungu (kama Yohana 3:16), Yeye ni mrithi (kama vile Mt. 21:33-46; Zab. 2:8). Kitu kinachoshangaza ni kwamba mwanadamu mwene dhambi, kuitia imani katika Yeye, anashiriki urithi wake (kama vile Ebr. 1:14; 6:12; Rum. 8:17; Gal. 4:1-7; 1 Pet. 1:4).

▣ "tena kwa yeye aliufanya ulimwengu" Mara nyingi ni vigumu kujua kiasi cha uhusiano wa naneno yanayopaswa kufasiriwa.Kuna mwingiliano wa kimantiki pekee kati ya visawe. Neno la kiufundi la Kiyunani la uumbaji pasipo kitu cho chote ni *ktizō*, bado ulimwengu ulio katika andiko hili ni *poieō*, ambali linamaanisha kitu kitokanacho na vitu vilivyokwisha kuwepo. Je! mwandishi anayatumia maneno haya kwa namna ya visawe au ni tofauti ya kipekee iliyokusudiwa? Inatia mashaka kwamba tofauti ya kiufundi inatajwa kwa sababu muktadha wa kithiolojia (yaani., Ebr. 1:3) inaurejelea uumbaji kwa neno lililonenwa (*ex nihilo*, kama vile Mwa. 1:6,9,16,20,24,26, lakini katika Ebr. 2:7 Mungu alimuumba mwanadamu). Tazama kitabu kipyä kilichoandikwa na John Walton, *The Lost world of Genesis One*.

Hili "neno" kiuhalsia "zama" (*aiōnos*).Hili liweza kuirejelea dunia (kama vile Mt. 28:20) au kwa zama (yaani., wakati). Hakika Yesuni muumbaji wa vyote (kama vile Yohana 1:3; Kol. 1:16; 1 kor. 8:6). Mwandishi wa kitabu cha Waembrania wanatumia maneno yote *aiōnos* (kama vile Ebr. 1:2; 6:5; 11:3) na *kosmos* (kama vile Ebr. 4:3; 9:26; 10:5; 11:7,38), kwa uwazi ni kama maneno ya kivisawe.

1:3

- NASB "mng'ao wa utukufu wake"  
NKJV "aliye ung'avu wa utukufu wake"  
NRSV, NJB "Yeye ni mfano wa utukufu wa Mungu"  
TEV "Yeye ni uang'avu wa mg'ao wa utukufu wa Mungu"

Hili neno "mg'ao" (*apaugasma*) linatumika hapa katika Agano Jipy. Katika Filo hili lilitumika katika uhusiano wa Masihi na YHWH katika maana kwamba neno *logos* liliuakisi Uungu. Makasisi wa kanisa la kale walilitumia neno hili katika maana ya Kristo kama mfano wa mwangaza wa Mungu. Katika maana pana kumwona Yesu ni kumwona Mungu (kama vile Yohana 14:8-9), kama kioo chenye kuakisi mwanga wa jua kamili. Hili neno la Kiebrania "utukufu" (*kabod*) lilitumika mara kwa mara katika maana ya uang'avu (kama vile Kut.16:10; 24:16-17; Law. 9:6).

Kuliweka neno hili katika kifungu kunaweza kuhusiana na Mit. 8:22-31, ambapo neno "hekima" (neno ni JINSI YA KIKE na yote ni ya Kiebrania na Kiyunani) linabainishwa kama Mungu uumbaji wa kwanza (kama vile Sirach 1:4) na wakili wa uumbaji (kama vile *Hekima ya Suleimani* 9:9). Dhana kama hii inaboreshwa katika kitabu cha matukio ya siku ya mwisho *Hekima ya Suleimani* 7:15-22a na 22b-30. Katika Mit. 8:22 hekima ndiyo yenyenye kuunda mambo yote; katika Ebr. 1:25 hekima ni ukombozi halisi wa utukufu wa Mungu Mkuu; katika Ebr. 1:26 hekima ni mwelekeo wa nuru ya milele, kioo kisicho na kutu cha Mungu atendaye; na katika Ebr. 1:29 alinganishwaye na nuru (yaani., jua na nyota) anagundulika kuwa mkuu sana."

Katika kitabu cha Agano la Kale neno la Kiebrania linalozungumzia "utukufu" (*kabod*) katika uhalisia wake lilikuwa neno la kibashara (ambalo lilirejelea joji za vipimo) ambalo lilimaanisha "kuwa na uzito." Uzito wa kitu ulisababisha kuwa cha thamani au cha gharama kubwa sana. Mara nyingi dhana ya mga'aro iliongezwa katika neno ili kuueleza ukuu wa Mungu wakati wa Kipindi cha Kutangatanga Jangwani (*Shekinah* Wingu la Utukufu). Yeye ndiye mkuu na wa kuheshimika. Yeye ndiye uangavu pekee kwa mwanadamu aliyeanguka. Mungu awezaye kujulikana vema kuititia Kristo (kama vile Mt. 17:2; Ebr. 1:3; Yakobo 2:1).

- NASB "chapa ya nafsi yake"  
NKJV "sura halisi ya nafsi yake"  
NRSV "ishara kamili ya kuwa Mungu"  
TEV "ufanano kamili wa kuwa Mungu mwenyewe"  
NJB "anauruhusu ufanano halisi wa kuwa Mungu mwenyewe"

Kifungu hiki kinapatikana hapa katika Agano Jipy pekee bali mara nyingi kinapatikana katika maandiko ya Philo, ambaye anakamilisha na kuongeza ubainishaji wa awali. Hili neno la Kiyunani kiuhalisia lilikuwa likitumika katika kutengeneza chombo, lakini baadaye lilikuja kuwakilisha alama iliyotengenezwa. Ni Yesu anayeukisi Uungu, anasimama kama chapa ya kipekee ya Uungu (kama vile Yohana 14:9).

Kuna maneno mawili ya Kiyunani yanayotumika kueleza uhusiano wa Kristo na Baba: (1) *eikon*, ambao unamaanisha sura yake (kama vile 2 Kor. 4:4; Kol. 1:15) na (2) *charaktér* (kama vile Ebr. 1:3). Hili la kwanza linajulikana sana katika Agano Jipy lakini neno linalofuata lina nguvu sana katika maana yake (kama vile KJV "chapa halisi"). Ni kitu gani kinachofana na Mungu? Yeye anafanana na Yesu wa Nazareti, ambaye ni ufunuo kamili wa Mungu asiyeonekana!

▣ "akivichukua vyote" Hili ni neno jumuishi la kifungu "kuchukua au kubeba" (*pherō*), bali katika muktadha huu lina maana nyingine ya "kushikilia," "kuhimili," "kubaliana na." Hili linaikamilisha dhana ya kithiolojia ya "Kushikana (kama vile Kol. 1:17 na dokezo lingine kama hilo la kitabbu cha *Hekima ya Suleimani* 8:1). Si Yesu pekee aliyeumba ulimwengu (maana nyingineyo ya neno *pherō*) kwa neno lililonenwa (kama vile Mwa. 1), bali anahimili kwa neno lililonenwa!

▣ "kwa amri ya uweza wake" Katika lugha ya Kiyahudi ilifikiriwa kuwa uweza wa Mungu uliwakilishwa kwa neno lililonenwa. Elohimu anaumba kwa neno lenye kunenwa (kama vile Mwa. 1:3,6,9,14,20,24). Neno la YHWH

lilikuwa na nguvu yenye kujitegemea katika kuyatimiza mapenzi yake (kama vile Isa. 55:11). Si kwa kushutukiza kwamba Kristo anaitwa "Neno" katika Yohana 1:1.

■ "**akiisha kufanya utakaso wa dhambi**" Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopita usio timilifu yenye kuweka mkazo wa jambo (kauli ya kati) na kueleza juu ya tendo kamili (kauli ya wakati uliopita usio timilifu, kama vile Ebr. 7:27; 9:12,28; 10:10). Yesu ametenda badala ya mwanadamu mwenye dhambi (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21).

Neno hili "utakaso" linatumika katika maana kadhaa za Agano Jipya.

1. utakaso wa jadi (kama vile Luka 2:22; 5:14; Yohana 2:6)
2. uponyaji wa kimwili (kama vile Marko 1:44)
3. stiari ya kulipia kosa (kama vile Ebr. 1:3; 2 Pet. 1:9, ndivyo anavyosema William D. Mounce katika kitabu cha *Analytical Lexicon to the Greek New Testament*, uk. 257)

Tunalipata neno la Kiingereza "kupoza" kutokana na neno hili la Kiyunani.

Kielewe kifungu bainishi "wa dhambi." Kuna njia mbili za kukielewa kifungu hiki: (1) ni shamirisho milikishi ya kifungu "wa dhambi," si kikanushi "toka dhambini." Kifo cha Yesu kilishughulika na tatizo la dhambi; (2) huu ni wingi usiodokeza asili ya Adamu kwa mwanadamu, "tatizo la dhambi," bali tendo la dhambi ya mtu binafsi. Yesu alishughulika na hatia ya uasi wa mwanadamu (wakati uliopita na uliopo).

Uchaguzi huu wa kiuandishi unakubaliwa na wasomi wa toleo la UBS<sup>4</sup>, lakini kuna uwezekano mwininge. Katika familia ya maandiko ya ki- Iskanda yaliyowasilishwa na P<sup>46</sup> kifungu "kupitia mwenyewe (*dia heautou*) kinajitokeza badala ya "yake" (*autou*), chenyeye kufanya kirejeree kifungu cha awali. Aina hii ya tofauti ya machapisho yenye kufanana inapatikana katika 1Yohana 5:18b. Inafurahisha kwamba hiki kifungu "kupitia ye" kinaukosa uwasilishaji mwininge wa familia ya maandishi ya ki-Iskanda (¶ na B). Hakika inawezekana kwamba waandishi walihofia kwamba kifungu "kupitia ye" na kufanya utakaso wa dhambi" kinaweza kuwa na uelekeo wa madhanio ya mafunuo ya uongo na kulibadili neno"*di'heautou*" kuwa "*autou*." Kwa mjadala zaidi wa uelekeo wa waandishi angalia Bart D. Ehrman's, *The Orthodox Corruption of Scripture*, Oxford Press, 1993.

■ "**aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu**" Hii ni njia ya kitaswira ya kueleza kazi ya Yesu iliyokwisha kumalizika na kutukuka kwake (kama vile Zab. 110:1; Luka 22:69). Mungu hana mkono. Hii ni stiari ya kibiblia (lugha ya kibinadamu) ya uweza, mamlaka, na ukoo. Hakua kuhani wa Agano la Kale aliywai kukaa chini! Kazi ya Yesu iliyomalizika mapema. Katika maana hii huu ni usemi wa kifalme, stiari ya kimamlaka (kama vileZab. 2; 45; na 110:1-3) wenye kuhusianishwa na na kazi ya ukuhani (kama vile Zab. 110:4 na Zekaria 4). Jumuiya ya Magombo ya Kale iliwaterajia Masihi, mmoja ni wa kikuhanu (yaani., uzao wa Aruni, kabila la Lawi), mwininge ni wa kifalme (yaani., uzao wa Yesu, kabila la Yuda). Yesualizikamilisha kazi tatu za Agano la Kale zilizofanya upatanisho: nabii (kama vileKumb. 18:18), kuhani (kama vile Zab. 110:4), na mfalme (kama vile 2 Sam. 7:13,16; Zab. 2; 110:1-3).

**NASB, NKJV,**

**NRSV**            "**mkono wa kuume wa Ukuu huko juu**"

**TEV**            "**wa Mungu, Uweza Mkuu**"

**NJB**            "**Ukuu wa Kiungu wa ukuu**"

Huu ni mzunguko. Wayahudi walikuwa na hofu ya kulitumia jina la Mungu walidhani kuwa ni kukufuru (kama vileKutoka.20:7) hivyo waliongeza maneno mengine na vifungu vingine (yaani., "Ufalme wa mbinguni" "kiti cha enzi," n.k.) au walitumia kauli tendewa kumrejelea Yeye.

**1:4** Mstari huu unaonekana kuwa mabadiliko kati ya Ebr. 1:1-3 na Ebr. 1:5-14. Toleo la Today's English Version (TEV) linauanza mjadala uhusuo ukoo wa Yesu kwa malaika na Ebr. 1:3. Jina ambalo alilopewa Yesu ni kuu kuliko malaika (kama vile Rum. 8:38-39; Efe. 1:21; Kol. 2:15) ni "mwana" (kama vile Ebr. 1:5 [mara mbili] na 8) au "Bwana" (kama vile Ebr. 1:10 na Flp. 2:9-11).

Kwa ajili ya "bora zaidi" tazama dokezo kamili katika Ebr. 7:7.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 1:5-14**

<sup>5</sup>Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wo wote,

Ndiwe mwanangu,

Mimi leo nimekuzaa?

Na tena,

Mimi nitakuwa kwake baba,

Na yeze atakuwa kwangu mwana?

<sup>6</sup>Hata tena, amletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni,

asema, Na wamsujudu malaika wote wa Mungu.

<sup>7</sup>Na kwa habari za malaika asema,

Afanyaye malaika zake kuwa pepo,

Na watumishi wake kuwa miali ya moto.

<sup>8</sup>Lakini kwa habari za Mwana asema,

Kiti chako cha enzi,

Mungu,ni cha milele na milele;

Na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili.

<sup>9</sup>Umependa haki, umechukia maasi;

Kwa hiyo Mungu, Mungu wako,

amekutia mafuta,

Mafuta ya shangwe kupita wenzio.

<sup>10</sup>Na tena, Wewe,Bwana,hapo mwanzo uliitia misingi ya nchi,

Na mbingu ni kazi za mikono yako;

<sup>11</sup>Hizo zitaharibika, bali wewe unadumu;

Nazo zote zitachakaa kama nguo,

<sup>12</sup>Na kama mavazi utazizinga, nazo zitabadilika;

Lakini wewe u yeze yule, Na miaka yako haitakoma.

<sup>13</sup>Je! Yuko malaika aliywambia wakati wo wote,

Uketi mkono wangu wa kuume

Hata nitakapoweka adui zako chini ya nyayo zako?

<sup>14</sup>Je! Hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?

**1:5 "Ndiwe mwanangu"** Mhuu ni mtiririko wa kwanza wa vifungu saba vya Agano la Kale vilivyonukuliwa toka Agano la Kale la Kiebrania ili kuuthibitisha ukuu wa Masihikwa malaika. Kifungu cha kwanza kinatoka katika Zab. 2:7, ambapo cha pili kinatoka katika 2 Sam. 7:14. Hiki kifungu cha kwanza kinatumika mara kadhaa katika Injili kumrejelea Kristo:

1. katika ubatizo wake (kama vile Mt. 3:17; Luka 3:22)
2. katika tendo la Kubadilika kwake (kama vile Mt. 17:5; Marko 9:7)
3. katika Ufufuko wake (kama vile Matendo ya Mitume 13:33; Rum. 1:4)

Hili neno "mwana," linalotumika katika nukuu zote za Ebr. 1:5, linatoka katika kitabu cha Agano la Kale ambapo linaweza kuwarejelea watu/makundi mbalimbali (tazam maelezo katika Ebr. 2:7).

1. malaika (kama vile Mwa. 6:2,4; Ayubu 1:6; 2:1; 38:7; Zab. 29:1, mara nyingi ni wengi)
2. taifa la Israeli (kama vile Hos. 11:1)
3. mfalme wa Israeli (kama vile 2 Sam. 7:14; Zab. 89:27)
4. Masihi (kama vile Zab. 2:7)

**□"Mimi leo nimekuzaa"** Mara nyingi Yesu amekuwa Uungu (kama vile Yohana 1:1-18). Hivyo, kifungu hiki hakiwezi kuirejelea asili ya chimbuko lake, bali uthihirisho wake kwa wakati (kuutwaa mwili). Baadhi ya watoa maoni wanakihuianisha kifungu hiki na ufufuo (kama vile Rum. 1:3-4). Baadhi ya Walimu wa sheria za Kiyahudi waliiiona Zab. 2:7 kama Masihi aliyefufuwa baada ya kupata mateso ya Kiungu (kama vile Isaya 53). Hiki ni kitenzi tendaji elekezi cha wakati timilifu chenye kumaanisha "uliyeumbwa." Hili linaweza kuwa dokezo la walimu wa sheria za Kiyahudi la Mit. 8:22-31, ambapo neno "hekima" (ambacho ni jinsia ya kike katika Kiebrania) lilikuwa

hekima ya uumbaji wa kwanza Mungu na kuwa wakala wa Mungu katika uumbaji uliofuatia (pia tazama *Hekima ya Sulemani* 7:1-8:1). Hili linadokezwa, si kukiweka hali ya jinsi ya kike katika Uungu, si kumkiri Yesu kama kiumbe kilichoumbwa, bali kumkiri Yesu wa Nazarethi kama wakili uumbaji wa Mungu Baba (kama vile Ebr. 1:10; Yohana 1:3; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16 ambao unatajwa katika Ebr. 1:2).

▣ "Mimi nitakuwa kwake baba" Nukuu hii inatoka katika Agano la Kale la Kiyunani ya 2 Sam. 7:14, ambayo kihalisia inamrejelea Suleimani. Mwandishi wa kitabu cha Waembrania anaitumia kwa Yesu. Hii rejea ya uwili ni sawa na kifungu "bikira atachukua mimba", cha Isa. 7:14. Mifano yote ya unabii wa ukamilifu mara dufu. Waandishi wa Agano Jipyä chini ya uvuvio alikitumia kitabu cha Agano la Kale katika mbinu za walimu wa sheria za Kiyahudi, mbinu za ufanano, na mchezo wa maneno ambao si sahihi kwa wafasiri wa baadaye. Tazama mjadala kamili.

## MADA MAALUM: NURU

Mungu ametenda hapo mwanzo ilikujidhihirisha wazi kwa wanadamu. Kithiolojia, huu unaitwa ufunuo. Alichagua watu kadhaa kuweka kumbukumbu na kueleza ufunuo wake huu. Katika thiolojia, huu unaitwa uvuvio. Ametuma Roho kusaidia wasomaji kuelewa neno lake. Katika thiolojia, huu unaitwa mwangaza. Tatizo linatokea pale tunapobisha kuwa Roho anahuksika katika kuelewa neno la Mungu-Sasa, kwa nini panakuwa na tafsiri nyingine kiasi hicho? Sehemu ya tatizo ipo kwa uelewa wa nyuma wa wasomaji au uzoefu binafsi. Daima hoja binafsi inaelezwa kwa kutumia Biblia katika uthibitisho wa kimaandishi au mtindo wa kuhakiki. Daima thiolojia inachagua maneno ya kusoma Biblical ikiruhusu kusoma maneno kadha na kwa njia zilizopendekezwa. Mwangaza hauwezi kulinganishwa na uvuvio ingawa sehemu zote mbili Roho mtakatifu anahuksika. Njia rahisi ya kusoma ni kujaribu kufafanua wazo kuu katika aya, na siyo kutafsiri kila neno kwa kina katika maandiko. Ni wazo la juu tu ambalo linapeleka ukweli hasili wa mwandishi wa kwanza. Kudokezea kitabu au sehemu ya kifasihii inasaidia kufuatilia kusudio la mwandishi wa awali aliyevuviwa. Hakuna mfasili aliyevuviwa. Hatuwezi kuzalisha njia ya tafsiri ya mwandishi wa Kibiblia. Tunaweza na lazima tujaribu kuelewa walichokuwa wakisema enzi za nyakati zao na kuwakilisha ukweli huo nyakati zetu. Kuna sehemu za Biblia ambazo ni tata au zimefichika (hadi wakati/kipindi kingine). Daima patakuwapo kutokukubaliana katika baadhi ya maandiko na masomo lakini lazima tuseme wazi kweli halisi na kuruhusu uhuru wa tafsiri binafsi ndani ya mipaka ya kusudio la mwandishi wa mwanzo. Wafasiri lazima watembee ndani ya mwanga walio nao, na siku zote wakiwa tayari kwa mwanga zaidi kutoka katika Biblia na Roho. Mungu atatuhukumu kutokana na kiwango cha uelewa wetu na jinsi tulivyoishi katika uelewa huu.

1:6

NASB "Hata tena, amletapo"

NKJV "Bali amletapo tena"

NRSV "Na tena, amletapo"

TEV "Bali hata Mungu alipokatibia kumtuma"

NJB "Tena, amletapo"

Hiki haurejelei ujio wa pili wa mwana. Hii ni mbinu ya kiuandishi ya kuitambulisha nukuu mpya (kama vile Ebr. 1:5d; 2:13; 4:5; 10:30).

Tambua kwamba matoleo ya NASB, NKJV, NRSV, na NJB yana neno "amletapo" ambapo toleo la TEV lina neno "kumtuma." Neno la kwanza linakazia tendo la kupaa la Kristo aliyetukuzwa; la pili lingelirejelea tendo la kutwaa umbo mwili huko Bethlehemu. Kwa sababu ya Baba na Mwana ufanano unaanza na tendo la Yesu kutwaa umbo mwili, toleo la TEV linaendana sana na muktadha.

▣ "mzaliwa wa kwanza" Kifungu hiki kinatumika

1. katika Agano la Kale ambapo mzaliwa wa kwanza alipokea urithi mara mbili ili kuwatunza wazazi wake
2. katika Zab. 89:27 kumrejerea mfalme wa Israeli

- katika sheria za Dini ya Kiyahudi hii ilikuwa kuwa kifungu kwa wale walitanguli (kama vile Rum. 8:29; Kol. 1:15,18; Ufu. 1:5).

Kifungu hiki kilikuwa kitovu cha mkanganyiko wa Arius/Athanasius. Arius anadai kwamba Yesu alikuwa uumbaji mkuu sana wa Mungu, kwa kukinukuu kifungu hiki na Zab. 89:27. Athanasius anadai kwamba Yesu alikuwa Uungu kamili na anainukuu mistari ya 2 na 3; (4) katika maana ya vielelezo, Kristo ni "mzaliwa wa kwanza wa wanadamu mpya ambao ni lazima utukuzwe, kama alivyotukuzwa Bwana anavyotukuzwa. . .mtu atokaye kwa Mungu halisi ili kuitafuta jumuiya mpya ya watakatifu" (kutoka *A Greek-English Lexicon* na Bauer, Arndt, Gingrich, na Danken, uk. 726); na (5) katika ulimwengu wa Uyunani wa Kirumi mzaliwa wa kwanza alitenda kama kuhani kwa ajili ya nyumba yake (kama vile *The Vocabulary of the Greek Testament* na Moulton na Milligan, uk. 557).

## MADA MAALUM: MZALIWA WA KWANZA

Neno hili "mzaliwa wa kwanza" (*prōtotokos*) limetumika katika Biblia kwa maana tofauti mbali mbali.

- Mazingira yake ya nyuma yanarejelea kwa
  - Mzaliwa wa kwanza anamhusu YHWH (BDB 114, KB 131, kama vile Kut. 13:2,12; 22:29; 34:19; Hes. 3:13)
  - Ukaribu uliokuwepo kabla wa mzaliwa wa kwanza wa kiume katika familia (kama vile Kumb. 21:17; Zab. 89:27; Lk. 2:7; Rum. 8:29; Ebr. 11:28)
- Matumizi yake katika Kol. 1:15 yanazungumza juu ya Yesu kama mzaliwa wa kwanza wa uumbaji ambacho kinawezekana katika kidokezo cha Agano la Kale Mit. 8:22-31, au wakala wa Mungu wa uumbaji (kama vile Yn 1:3; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:15-16; Ebr. 1:2)
- Matumizi yake katika Kol. 1:15,18; 1 Kor. 15:20,23; Ufu. 1:5 inarejelea kwa Yesu kama mzaliwa wa kwanza toka katika wafu
- Ni wasifu wa Agano la Kale uliotumika kwa Masihi (kama vile Zab. 89:27; Ebr. 1:6; 12:23); ni wasifu unaojumuisha dhana mbali mbali za Yesu kama kitovu na mmiliki wa mambo yote.

■ "ulimwenguni" Kipengele hiki kinadokeza uwepo wa awali wa Yesu, ambaye mara zote amekuwa Uungu, lakini hatua mpya ya huduma ya ukombozi wake ilianza huko Bethlehemu wakati alipoutwaa mwili wa kibinadamu (kama vile Flp. 2:6-8a). Hii si zaidi neno la kawaida *kosmos*, bali *oikoumenē*, ambalo linatumika kumaanisha uso wa nchi ambao ulikaliwa na wanadamu. Neno hili pia linatumika katika Ebr. 2:5 kistiani kama rejea ya enzi mpya.

■ "asema, Na wamsujudu malaika wote wa Mungu" Hii ni nukuu toka Maandiko ya Agano la Kale la Kiebrania la aidha Kumb. 32:43 au Zab. 97:7. Neno la Kiebrania la neno "malaika" linalotumika katika Zab. 97:7 ni *Elohim*. Kutoka Pango #4 la Magombo ya Bahari ya Chumvi tunao uthibitisho wa tafsiri hii ya Agano la Kale la Kiebrania. Hili neno *Elohim* linamrejelea Mungu, viumbe vyta kimalaika, waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; 22:8-9), au roho ya mwanadamu aliyekufa (kama vile 1 Sam. 28:13).

Nukuu hii haimaanishi kwamba malaika hawakumwabudu Kristo hadi alipotwaa umbo mwili. Katika muktadha huu inaonyesha ukuu wa Mwana kwa maana kwamba malaika wanamwabudu yeye.

**1:7 "Afanyaye malaika zake kuwa pepo,"** Kifungu hiki kinaanza na ulinganifu kati ya malaika kubadilika (kama vile LXX ya Zab. 104:4) katika mkanganyiko na Yesu aliye wa kudumu na asiyebadilika (kama vile Ebr. 1:8,11,12; 13:8). Walimu wa sheria za Kiyahudi, wakiinukuu Omb. 3:23 au Dan. 7:10, wanasema kwamba Mungu waliwaumba malaika wapya kila asubuhi.

**1:8 "Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele"** Hii ni nukuu toka katika Agano la Kale la Kiyunani la Zab. 45:6, lenye kutoa ufanuzi wa Mfalme wa ki-Masihi. Katika Agano la Kale muktadha wa kiwakilishi ni cha utata sana na kinawenza kumrejelea Mungu Baba au Mungu Mwana. Hata hivyo, katika andiko hili inaonekana kwamba hii ni moja ya ukiri wenye nguvu juu ya Uungu wa Kristo anaepatikana kila mahali katika Maandiko (kama vile Yohana 1:18; 20:28).

Kuna umuhimu wa tatizo la machapisho ya Kiyunani katika kiwango hiki. Baadhi ya machapisho ya kale (P<sup>46</sup>, ፲, na B) yana kiwakilishi (*autou*, yaani, "kiti chake cha enzi") ambacho kinaongeza utata. Toleo la United Bible Society' toleo la nne linakiunga mkono kifungu "chako" pamoja na daraja "B" (kwa kiasi fulani andiko halijulikani). Muundo huu unapatikana katika machapisho ya herufu kubwa A na D na ni nukuu halisi toka Agano la Kale la Kiebrania la Zab. 45:6. Mara nyingi waandishi wa kale walielekea kuyafanya maandiko yawe wazi zaidi, hasa ikiwa yanahusiana na mijadala ya imani ya Kristo ya siku zao (kama vile Bart D. Ehrman *The Orthodox Corruption of Scripture*, Oxford Press, 1993, uk. 265).

Mjadala huu haumaanishi njia yo yote ya kuukana Uungu wa Kristo, bali kuonyesha uelekeo wa waandishi wa kale kwa maandiko kwa makusudi ya kisarufi. Hii ndiyo sababu wataalam wa mafundisho ya sasa ya Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi wanazihukumu tofauti za kimachapisho zilizojikita katika mambo yafuatayo.

1. usomaji zaidi usio wa kawaida huenda ni halisi
2. usomaji wenyewe kueleza juu ya tofauti nyingine huenda ni halisi
3. usomaji pamoja na mgawanyiko wa kijiografia ulio mpana (usio wa familia moja ya machapisho) huenda ni halisi

Pia kitabu cha Bart Ehrman kinatengeneza hoja kwamba waandishi walifanya mabadliko ya andiko la Kiyunani kwa makusudi ya kithiolojia, hasa wakati wa vipindi vya migogoro juu ya mambo yamhusuyo Kiristo na Utatu (yaani.., karne ya tatu na ya nne).

▣"milele na milele" kwa namna iliyodhahiri kabisa kifungu hiki hakiurejelei utawala wa kimilenia, buali utawala wa milele (kama vile Isa. 9:8; Dan. 7:14,18; Luka 1:33; 2 Pet. 1:11; Ufu. 11:15).

## **MADA MAALUMU: MILELE (NAHAU ZA KIYUNANI)**

Maelezo ya asili ya neno la Kiebrania 'olam, עולם (BDB 761, KB 798) hayajulikani (NIDOTTE, juzu. 3, uk. 345). Yametumika katika maana mbali mbali (mara nyingi yanapimwa na maudhui). Ifuatayo ni mifano iliyochaguliwa tu.

1. vitu vya kale
  - a. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
  - b. mahari, Isa. 58:12; 61:4
  - c. Mungu, Zab. 93:2; Mith. 8:23; Isa. 63:16
  - d. Vitu, Mwa. 49:26; Ayubu 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
  - e. mda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
2. muda/ wakati ujao
  - a. maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
  - b. heshima ya hali ya juu kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
  - c. uwepo endelevu
    - 1) dunia, Zab. 78:69; 104:5; Mhu. 1:4
    - 2) mbinguni, Zab. 148:5
  - d. uwepo wa Mungu
    - 1) Mwa. 21:33
    - 2) Kut. 15:18
    - 3) Kumb. 32:40
    - 4) Zab. 93:2
    - 5) Isa. 40:28
    - 6) Yer. 10:10
    - 7) Dan. 12:7
  - e. Agano
    - 1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19
    - 2) Kut. 31:16
    - 3) Ufu. 24:8

- 4) Hes. 18:19
- 5) 2 Sam. 23:5
- 6) Zab. 105:10
- 7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8
- 8) Yer. 32:40; 50:5
- f. Agano maalumu na Daudi
  - 1) 2 Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
  - 2) 1 Fal. 2:33,45; 9:5
  - 3) 2 Nya. 13:5
  - 4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
  - 5) Isa. 9:7; 55:3
- g. Masihi wa Mungu
  - 1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4
  - 2) Isa. 9:6
- h. Sheria za Mungu
  - 1) Kut. 29:28; 30:21
  - 2) Ufu. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
  - 3) Hes. 18:8,11,19
  - 4) Zab. 119:89,160
- i. Ahadi za Mungu
  - 1) 2 Sam. 7:13,16,25; 22:51
  - 2) 1 Fal. 9:5
  - 3) Zab. 18:50
  - 4) Isa. 40:8
- j. Uzao wa Abrahamu na nchi ya ahadi
  - 1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
  - 2) Kut. 32:13
  - 3) 1 Nya. 16:17
- k. Sikukuu za ahadi
  - 1) Kut. 12:14,17,24
  - 2) Ufu. 23:14,21,41
  - 3) Hes. 10:8
- l. umilele, kudumu milele
  - 1) 1 Fal. 8:13
  - 2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
  - 3) Isa. 26:4; 45:17
  - 4) Dan. 9:24
- m. Zaburi inasema yapi yanayowapasa kufanya milele
  - 1) kushukuru, Zab. 30:12; 79:13
  - 2) kudumu katika uwepo Wake, Zab. 41:12; 61:4,7
  - 3) amini katika huruma zake, Zab. 52:8
  - 4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
  - 5) imba nyimbo za sifa, Zab. 61:8; 89:1
  - 6) tangaza haki zake, Zab. 75:7-9
  - 7) tukuza jina lake,Zab. 86:12; 145:2
  - 8) baliki jina lake, Zab. 145:1
- n. linatumiwa na Isaya kueleza enzi mpya
  - 1) agano la milele, Isa. 24:5; 55:3; 61:8
  - 2) YHWH kama mwamba wa milele, Isa. 26:4
  - 3) furaha ya milele,Isa. 35:10; 51:11; 61:7

- 4) Mungu wa Milele, Isa. 40:28
- 5) Wokovu wa milele, Isa. 45:17
- 6) Wema wa milele, Isa. 54:8
- 7) Ishara ya milele, Isa. 55:13
- 8) Jina la milele, Isa. 56:5; 63:12,16
- 9) Nuru ya milele, Isa. 60:19,20

Matumizi yenye hali ya ukarusha kuhusiana na adhabu ya milele kwa waharifu inapatikana katika Isa. 33:14, "moto wa milele." Isaya kila wakati anatumia "moto" kuelezea hasira ya Mungu (kama vile. Isa. 9:18,19; 10:16; 47:14), lakini katika Isa. 33:14 "ndipo anasema wa milele"

3. Wakati wa kurudi nyuma na kwenda mbele ("toka milele hadi milele")
  - a. Zab. 41:13 (sifa kwa Mungu)
  - b. Zab. 90:2 (Mungu pekee)
  - c. Zab. 103:17 (huruma zake)

Kumbuka,muktadha huamua maudhui ya maana ya neno. Maagano ya ahadi za milele ni ya masharti (yaani , Yeremia 7, tazama Mada Maalum: Agano). Kuwa mwangalifu unaposoma maoni ya kisasa kuhusu muda au Agano Jipya la theolojia iliyopangwa katika matumizi ya kila siku ya neno hili dhaifu katika Agano la Kale.

Kumbuka pia, Agano Jipya linajumuisha ahadi zote za Agano la kale (tazama Mada Maalum: utabiri wa mambo yajayo ya Agano la Kale dhidi ya utabiri wa mambo yajayo ya Agano Jipya.).

Kifungu kimoja cha nahau ya Kiyunani ni "utakuwa hauna mwisho" (kama vile Luka 1:33; Rum. 1:25; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 1 Tim. 1:17), ambacho kingeliakisi neno la Kiyunani '*olam*. Angalia Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kr. 321-319. Vifungu vingine vyenye kuhusiana ni "utakuwa hauna mwisho" (kama vile Mt. 21:19 [Marko 11:14]; The. 1:55; Yohana 6:58; 8:35; 12:34; 13:8; 14:16; 2 Kor. 9:9) na "vya milele na milele" (kama vile Efe. 3:21). Inaonekana kutokuwepo na tofauti kati ya nahau hizi ya neno "milele." Hili neno "milele" linaweza kuwa wingi katika maana ya ishara ya utungaji wa sarufi za walimu wa sheria za Kiyahudi iitwayo "wingi wa ukuu" au inaweza kuirejelea dhana ya "zama" kadhaa katika maana ya Kiyahudi ya kifungu cha "zama zisizo za hatia," "zama za udharimu," "zama zijazo," au "zama za haki."

**1:9"Umependa haki, umechukia maasi"** Hii ni nukuu itokayo katika Agano la Kale la Kiebrania la Zab. 45:7 yenye kuhusiana na maisha ya kidunia ya Yesu Kristo.

## MADA MAALUMU: HAKI

"Haki" ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya ni upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana yenewe.

Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinazelewa kama "halali" au "haki" (kitenzi, BDB 842, KB 1003; nomino jinsi ya kiume, BDB 841, KB 1004; nomino jinsi ya kike, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii inatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.

Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wanadoa wa mwanzo walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21).

Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu:

Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae. Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko, hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya agano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

- A. kutangaza haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya mahakama)
- B. kwa kutoa haki huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kuzuliwa)
- C. kumtoa Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
- D. kurejesha ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

- A. Toba
- B. Imani
- C. Utii kwenye stadi ya maisha
- D. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, ulijojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinagsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo. Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa mwalimu wa sheria aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiosunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiebrania, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethhibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyangi limendwa katika maneno ya kimaagan (tazama Mada Maalum: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipyta ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipyta (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana). Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utotauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihuiana na jamii)na "mwenye haki" (ikihuiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungud [utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoleka]).

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu pale Edeni. Biblia inaanza kati ya Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

Ili kuthhibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

- A. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
  - 1. Warumi 3:26
  - 2. 2 Wathesalonike 1:5-6

- 3. 2 Timotheo 4:8
- 4. Ufunuo 16:5
- B. Yesu ni haki
  - 1. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
  - 2. Mathayo 27:19
  - 3. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
- C. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki. Mambo ya Walawi 19:2
  - a. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
- D. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
  - 1. Warumi 3:21-31
  - 2. Warumi 4
  - 3. Warumi 5:6-11
  - 4. Wagalatia 3:6-14
- E. Iliyotolewa na Mungu
  - a. Warumi 3:24; 6:23
  - b. 1 Wakorintho 1:30
  - c. Waefeso 2:8-9
- F. Iliyopokelewa kwa imani
  - a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
  - b. 2 Wakorintho 5:7,21
- G. kupitia matendo ya Mwana
  - a. Warumi 5:21
  - b. 2 Wakorintho 5:21
  - c. Wafilipi 2:6-11
- H. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
  - 1. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
  - 2. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
  - 3. Waefeso 1:4; 2:10
  - 4. 1 Timotheo 6:11
  - 5. 2 Timotheo 2:22; 3:16
  - 6. 1 Yohana 3:7
  - 7. 1 Petro 2:24
- I. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
  - 1. Matendo 17:31
  - 2. 2 Timotheo 4:8

Haki ni atabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

- A. agizo la Mungu
- B. zawadi ya Mungu
- C. tendo la Kristo

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudini, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoa nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na barua zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa dhana ya kuwa huru. Calvin anasistiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

- A. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
- B. injili ni ukweli (msistizo wa Augustine na Luther)

C. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

■ "amekutia mafuta" Hili neno la Kiebrania "amekutia mafuta" (*mashiach*, BDB 603) ni neno la Agano la Kale lenye kumzungumzia Masihi (*masiah*). Katika Agano la Kale manabii, makuhani, na wafalme walikuwa wakiminiwa mafuta kama ishara ya uchaguzi wa Mungu na utoaji kwa ajili ya kazi iliyokusudiwa. Katika muktadha huu pia neno hili linayarejelea matumizi ya mafuta ya mzeituni wakati wa furaha na kusheherekeea sikukuu (kama vile Isa. 53:11).

## MADA MAALUMU: "KUTIWA MAFUTA KATIKA BIBLIA" (BDB 603)

(kitenzi cha Kiebrania, BDB 602, KB 643 I; nomino, BDB 603)

- A. Yaliyumika kwa ajili ya urembeshaji (BDB 691 I kama vile Kumb. 28:40; Ruthu 3:3; 2 Sam. 12:20; 14:2; 2 Nya. 28:15; Dan. 10:3; Mik. 6:15)
- B. Yalitumika kwa ajili ya wageni (BDB 206, kama vile Zab. 23:5; Luka 7:38,46; Yohana 11:2)
- C. Yalitumika kwa ajili ya uponyaji (BDB 602, kama vile Isa. 61:1; Marko 6:13; Luka 10:34; Yakobo 5:14) [yalitumika kwa maana ya tiba na kinga katika Eze. 16:9]
- D. Yalitumika katika maandalizi ya mazishi (kama vile Marko 16:1; Yohana 12:3,7; 19:39-40; 2 Nya. 16:14, lakini likiwa bila kitenzi "kutiwa mafuta")
- E. Yalitumika katika maana ya kidini (ya jambo, BDB 602, kama vile Mwa. 28:18; 31:13 [nguzo]; Kut. 29:36 [madhabahu]; Kut. 30:26; 40:9-16; Law. 8:10-13; Hes. 7:1 [hema])
- F. Yalitumika kuwasimika viongozi
  1. Makuhani
    - a. Haruni (Kut. 28:41; 29:7; 30:30)
    - b. Wana wa Haruni (Kut. 40:15; Law. 7:36)
    - c. waliowekwa wakfu (Hes. 3:3; Law. 16:32)
  2. Wafalme
    - a. Na Mungu (kama vile 1 Sam. 2:10; 2 Sam. 12:7; 2 Fal. 9:3,6,12; Zab. 45:7; 89:20)
    - b. Na manabii (kama vile 1 Sam. 9:16; 10:1; 15:1,17; 16:3,12-13; 1 Fal. 1:45; 19:15-16)
    - c. Na makuhani (kama vile 1 Fal. 1:34,39; 2 Fal. 11:12)
    - d. na wazee (kama vile Amu. 9:8,15; 2 Sam. 2:7; 5:3; 2 Fal. 23:30)
    - e. juu ya Yesu kama mfalme wa Kimasihi  
(kama vile Zab. 2:2; Luka 4:18 [Isa. 61:1]; Matendo 4:27; 10:38; Heb. 1:9 [Zab. 45:7])
    - f. wafuasi wa Yesu (kama vile 2 Kor. 1:21; 1 Yohana 2:20,27 [mafuta])
  3. Juu ya manabii kadri iliyowezekana (kama vile 1 Fal. 19:16; Isa. 61:1)
  4. Kuvikombo vyombo visivyoaminika vya ki-Uungu
    - a. Koreshi (kama vile Isa. 45:1)
    - b. Mfalme wa Tiro (kama vile Eze. 28:14, ambapo alitumia stirahi za Bustani ya Edeni)
  5. Neno au cheo "Masihi" maana yake ni "Mtiwa mafuta" (BDB 603), kama vile Zab. 2:2; 89:38; 132:10

Matendo 10:38 ni msitari ambapo nafsi tatu za Uungu zinazwekwa pamoja katika kutiwa mafuta. Yesu alipakwa mafuta (kama vile Luka 4:18; Matendo 4:27; 10:38). Dhana inapanuliwa ili kuwajumuisha waamini wote (kama vile 1 Yohana 2:27). Mpakwa mafuta anakuwa wapakwa mafuta! Hii inaweza kuwa sambamba na Mpinga Kristo na wapinga kristo (kama vile 1 Yohana 2:18). Tendo la ishara ya Agano la Kale la kumiminiwa mafuta mwilini (kama vile Kut. 29:7; 30:25; 37:29) linahusiana na wale walioitwa na kuandaliwa na Mungu

kwa kazi maalumu (yaani, manabii, makuhani, na wafalme). Neno "Kristo" ni tafsiri ya neno la Kiebrania "mpakwa mafuta" au Masihi.

■"**kupita wenzio**" Huu ni mwendelezo wa nukuu kutoka Agano la Kale la Kiebrania la Zab. 45:6-7. Kila maelezo ya kitabu cha Zaburi hayapaswi kulazimishwa kuwa katika ukubalifu wa kithiolojia wenyewe kumhusu Yesu. Kifungu hiki kingeweza kuurejelea ukuu wa Yesu juu ya (1) malaika; (2) Wafalme wa Israeli; (3) watawala wa kidunia; au (4) mwanadamu aliyekombolewa.

**1:10 "Wewe, Bwana"** Ni tafsiri ya Agano la Kale la Kiebrania ya Zab. 102:25 yenyewe kuhusisha neno "Bwana" lenye kumrejelea YHWH, bali katia muktadha huu neno hili linamrejelea Yesu. Hii ni sababu nyiningine ya kimuktadha kwamba kwa nini Ebr. 1:9 pia inamrejelea Yesu kama "Mungu."

■"**uliitia misingi ya nchi, Na mbingu ni kazi za mikono yako**" Hili ni dokezo la 1:2 la Yesu kuwa wakala wa Baba katika uumbaji. Tazama Maalum: *Archē* katika Ebr. 3:14.

Kitabu cha Mwanzo 1 kinaueleza uumbaji wa *Elohim* kwa neno lililonenwa (kama vile Mwa. 1:3,6,9,14,20,24,26), ambapo Mwanzo 2 inakiri uhusika binafsi wa YHWH wa moja kwa moja, wenyewe kudokeza kifungu "kumfinyanga" kumuumba Adamu na Hawa kutokana na udongo (kama vile Mwa. 2:7,8,19,22). Hii nukuu (Zab. 102:25) kinaipanua stiari binafsi kwa uumbaji wa kimwili.

**1:11 "Hizo zitaharibika, bali wewe unadumu; Nazo zote zitachakaa kama nguo"** Tena usemi huu unaonyesha umilele wa Mwana. Katika Agano la Kale mara nyigi manabii walitumia mandhari ya kimahakama katika kuituliza ghadhabu ya YHWH wakati wa uasi wa mke, Israeli. Alimchukua "yeye" (Israeli) kumtarakisha mahakamani na kuwaita mashahidi waliohitajika (kama vile Kumb. 19:15)—meshahidi wawili zaidi wa kudumu, "wa mbinguni a duniani"—kuuthibitisha ushuhuda wake. Hata hawa mashahidi wawili wa kudumu watapita. Nukuu hii wanapendekeza mandhari za aina mbili: (1) kitenzi cha kwanza (*apollumi*) kina maana nyiningine ya machafuko ya uharibifu (kama vile 2 Pet. 3:10) na (2) kifungu cha pili kinadokeza kupita kwa vitu vya kale kama kipande cha nguo.

Huu ni ulinganifu mwingine wa kuvurugika kwa mtitiko wa uumbwaji (malaika, uumbaji) dhidi ya kudumu na uimara wa Kiti cha enzi cha Mungu na Mwana!

**1:12 "Lakini wewe u ye ye yule"** Hii ni nukuu kutoka Agano la Kale la Zab. 102:27. Hii dhana ile ile (kutobadilika) inatumika katika Ebr. 13:8 kutoa ufanuzi wa kutobadilika kwa Yesu. Malaika hubadilika, mbingu na dunia hubadilika, Yesu habadiliki, hapa kuna tumaini la mwanadamu (kama vile Mal. 3:6; Yakobo:17).

■"**Na miaka yako haitakoma**" Kama vifungu vilivytangulia vilivyoeleza sifa ya uhimara Yesu, hiki kinaeleza kudumu kwa utu wake.

**1:13 "mkono wangu wa kuume"** Hii ni nukuu toka Agano la Kale la Kiebrania la Zab. 110:1. Hii ni Zaburi ya ki-Masihi yenyewe kushangaza iliyonukuliwa na kudokezwa mara nyigi katika kitabu cha Waebrania (kama vile Ebr. 1:3,13; 5:6,10; 6:20; 7:3,11,17,21; 8:1; 10:12-13; 12:2). Hii inajumuisha kipengele cha ufalme (Ebr. 1:1-3) na ukuhani (Ebr. 1:4-7) cha Masihi (kama ifanyavyo miti miwili ya mizeituni ya Zek. 4). Itambue miundo miwili ya neno "bwana"; wa kwanza ni YHWH, wa pili ni *Adon* (Bwana). Bwana wa Daudi (Masihi) amekaa juu ya kti cha enzi cha YHWH (bwana), katika sehemu yenyewe mamlaka na uweza. Hii haiwezi kutokea kamwe, kamwe, kamwe kwa malaika!

**1:14 "Hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu"** Malaika wapo kwa ajili ya kumtumikia Mungu na mwanadamu. Mwanadamu aliyekombolewa yu juu ya mpangilio uumbaji wa kiroho kuliko malaika. Waamini watawahukumu malaika (kama vile 1 Kor. 6:3). Yesu hakufa kwa ajili ya kuwakomboa malaika (kama vile Ebr. 2:14-16).

## **MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA VITENZI VYA KIYUNANI)**

Wokovu siyo kitu, bali ni uhusiano. Haiishii hapo mtu anapomwamini Kristo; ndiyo safari imeanza! Siyo Sera ya bima ya moto, wala tiketi ya kwenda mbinguni, bali ni kukua kumfanana Kristo. Tunao usemi katika Amerikaunaosema, kadiri wawili katika ndoa wanavyoendelea kuishi, ndiyo wanaendelea kufanana. Hili ndilo lengo la wokovu!

### **WOKOVU KAMA KITENDO KILICHO KAMILISHWA (WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU)**

- Matendo 15:11
- Warumi 8:24
- 2 Timotheo 1:9
- Tito 3:5
- Warumi 13:11(inajumuisha WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ukiwa na mazingira ya WAKATI UJAO )

### **WOKOVU KAMA HALI YA KUWA (TIMILIFU)**

- Waefeso 2:5,8

### **WOKOVU KAMA MCHAKATO UNAOENDELEA (WAKATI ULIOPPO)**

- 1 Wakorintho 1:18; 15:2
- 2 Wakorintho 2:15
- 1 Petro 3:21

### **WOKOVU KAMA UKAMILISHO WA WAKATI UJAO (WAKATI UJAO KATIKA NJEO YA KITENZI au MAZINGIRA)**

- Warumi 5:9, 10; 10:9,13
- 1 Wakoritho 3:15; 5:5
- Wafilipi 1:28;
- 1 Wathesalonike 5:8-9
- Waebania 1:14; 9:28
- 1 Petro 1:5,9

Kwa hivyo, wokovu unaanza na uamuzi wa imani ya awali (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum 10:9-13), lakini hili lazima liendane na mchakato wa imani katika mtindo ya maisha (kama vile Rum. 8:29; Gal. 3:19; Efe.1:4; 2:10), ambao siku moja utakuja kukamilishwa kwa kuonekana (kama vile 1Yoh. 3:2). Hatua hii ya mwisho inaitwa utukufu. Hili linaweza kuelezwa kama.

1. Utukufu wa awali – udhihirisho (kukombolewa kutoka katika adhabu ya dhambi)
2. Wokovu endelevu–utakaso (kuokolewa toka katika nguvu ya dhambi)
3. Wokovu wa mwisho – utukufu (kuokolewa kutoka katika uwepo wa dhambi)

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini msisitizo gani wa Ebr. 1:1?
2. Nini tofauti kati ya ufunuo asilia na ufunuo wa kipekee?
3. Orodhesha vipengele saba vya utu wa Yesu na kazi iliyo katika mistari ya 2-3.
4. Kwa nini unyambulishaji huu kumhusu Yesu ni muhimu sana kwa wapokeaji?
5. Ni kwa namna gani malaika wanahusiana na huduma ya Yesu?

## WAEBRANIA 2

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b> |   |                                       |  |  |
|--|---|---------------------------------------|--|--|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                       | <b>NKJV</b>   | <b>NRSV</b>                           | <b>TEV</b>                                       | <b>NJB</b>   |
| Wokovu mkuu<br>2:1-4                         | Usiupuze wokovu<br>2:1-4                                  | Onyo dhidi ya anguko<br>2:1-4         | Wokovu mkuu<br>2:1-4                             | Ushawishi<br>2:1-4                                       |
| Mtangulizi wa<br>Wokovu<br>2:5-9             | Mwana amefanywa<br>mdogo punde kuliko<br>Malaika<br>2:5-9 | Fedheha na Furaha ya<br>Yesu<br>2:5-9 | Mmoja atuongozae<br>sisi katika wokovu<br>2:5-10 | Wokovu umeretwa<br>na Kristo sio na<br>malaika<br>2:5-8a |
|  | Kuwaleta wana<br>Wengi katika utukufu                     |                                       |  | 2:8b-9   |
| 2:10-18                                      | 2:10-18   | 2:10-13<br>2:14-18                    | 2:10-13<br>2:11-13<br>2:14-18                    | 2:10-13<br>2:14-18                                       |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Sura ya kwanza na ya pili ni kipengele cha fasihi. Kinaendeleza ukuu wa Yesu juu ya ufunuo wa Agano la kale (kama vile. Ebr. 1:1-3) na ukuu wa Yesu juu ya malaika (kama vile. Ebr. 1:4-2:18).
- B. Mkazo mpya wa sura ya pili ni uhusiano wa Yesu na watu wake (kama vile. Ebr. 2:10-18). Yesu ni utambulisho halisi kwao, kama matokeo ya kushiriki katika utukufu wake. Makusudi ya ukuu wa maagano ni kwamba kurejesha anguko la mwanadamu (kama vile. Ebr. 2:9-11,14-18) katika ukuu wake kwenye uumbaji (kama vile. Zab. 8). Yesu ni mwanadamu kamili, mfano wetu kamili.
- C. Sura ya pili kwanza ni mfuatano wa maonyo (Ebr. 2:1-4; 3:7-4:11; 5:11-6:12; 10:19-39; 12:14-29). Onyo la kwanza linalekezwa kwa wale ambao wameukataa ufunuo wa maagano mapya (injili). Hii inawezekana kurejelea watu wenye utaratibu wa kiyahudi ambao wanaheshimu sana maagano ya Musa, hivyo wanahitaji rehema.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 2:1-4

<sup>1</sup>Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa. <sup>2</sup> Kwa maana, ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, <sup>3</sup>sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia; <sup>4</sup> Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nydingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenywewe.

2:1 "Kwa hiyo" Hii inarejelea ukweli wa sura ya 1.

◻ "imetupasa" hili ni neno "dei," ambalo linamaanisha kuhitaji maadili mema. Hii ni ya kwanza (yaani, Ebr. 2:1-4) kati ya maonyo mengi kwenye kitabu cha Waebrania yanayoelezea kundi la Wayahudi waaminio amba bado wanaabudu kwenye sinagogi na Wayuhudi wasioamini. Baadhi ya maonyo ya kitabu yanawalenga waaminio kuchukua hatua kali, kuijunga na kanisa kwa wazi na kutembea kwa ujasiri na ukomavu ulimwenguni kote kwa kazi ya injili (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo 1:8). Maonyo mengine yameelezewa kuwalenga Wayahudi wasioamini waliosikia injili na kuziona nguvu zake kwenye maisha ya Wayahudi marafiki zao waaminio na waabudio, lakini kwa ubinafsi walikataa kumpokea Yesu kama masihi aliyehadiwa na kuziendea tamaduni zao za waalimu wa sheria (kama vile Waebrania 6; 10).

NASB    "kuyaangalia zaidi"

NKJV    "tuyape moyo wa uangalifu zaidi"

NRSV    "imetupasa kuyaangalia zaidi"

TEV    "tuyashikilie yote kwa umakini"

NJB    "tugeuze fikra zetu kwa umakini zaidi"

Hiki ni Kiyunani linganishi na kitenzi jina ambacho humaanisha jambo maalumu, umakini kamili na kujali kitu au mtu fulani (kama vile Mdo. 8:6,10; 16:14). Maagano mapya ya mwana (injili) yote ni ya thamani na hatari! Ukweli wa Mungu ni lazima uongozwe kwa kufaa.

◻ "tusije tukayakosa" Neno hili limetumika hapa pekee kwenye Agano Jipy. Ni dhahili linamaanisha "kububujika kwa" au "kuponyokea mbali." Imetumia sitiari ya sasa ya upepo au maji unaomsababisha mtu fulani sasa kuchukua nanga imara.

Onyo hili linaelezewa kama kauli tendwa tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu kwanza kwa wingi wa mtu. Kuna kipengele cha matukio yasiyonekana yanayosababishwa na mpatanishi wa nje asiyelezea (sauti isiyooonesha hisia) na hali tegemezi. Kuyakosa au mbali na ukweli unakua ni uwezekano wa wazi. Pia inawezekana kwamba sitiari imelengwa kwa wapokeaji waliosimama ambapo ukweli unajongea. Hii yumkini inaweza kuwa ni kidokezo katika Mit. 3:21 kwenye tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania ambapo kitenzi kile kile kimetumika.

Kuna njia tatu za kuangalia onyo hili.

1. kama rejelea kwa wale wote walioskataa kuipokea injili (kama vile Ebr. 2:3)
2. kama rejelea kwa wale walioamini (kama vile "kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa,"mst. 1), lakini sio wakomavu
3. kama rejelea kwa wale walioamini na wako katika hatari ya kutoshikilia kazi zao za asili/ukiri wa imani katika Kristo.

Ya kwanza inngeweza kuwarejelea Wayahudi wasioamini, ambapo ya pili na ya tatu inaweza kurejelea Wayahudi waaminio. Kutumia wingi wa mtu wa kwanza kunaonekana kumaanisha kwamba makundi ya mwandishi mwenywewe na wale wanaoelezewa na inaweza kudokeza kwamba walikua ni waaminio au hata katika sinagogi ambapo walishirikiana injili (kama vile Ebr. 2:3). Hata hivyo, wingi wa kisarufi umejitokeza kwenye fasihi, sio dhahiri, matumizi ya kwenye Ebr. 10:26.

**2:2 "ikiwa"** Hii ni sentensi hali daraja la kwanza ambayo inathibitisha kuwa ukweli kutoka katika taswira ya mwandishi au kwa ajili ya makusudi yake ya fasihi. Mara nyingi limetafsiriwa katika kiingereza kama "kama" au "kwa sababu."

■**"neno lililonenwa na malaika"** Hii inarejelea kwa sheria ya Musa. Wayahudi wanaamini kwamba walitenda kama wapatanishi kati ya YHWH na Musa katika mlima Sinai (kama vile Kut.3:2; 14:19; 23:20-23; 32:34; 33:2; Zab. 68:17; Mdo 7:38,53; Gal. 3:19).

|             |                          |
|-------------|--------------------------|
| <b>NASB</b> | "lilikuwa imara"         |
| <b>NKJV</b> | "lilikuwa thabiti"       |
| <b>NRSV</b> | "lilikuwa halali"        |
| <b>TEV</b>  | "lilionyesha kuwa kweli" |
| <b>NJB</b>  | "lilikuwa la kuaminiwa"  |

Mungu ni mwaminifu katika neno lake, Baraka zote na/au laana (kama vile Kumb. 27-28).

## MADA MAALUM: DHAMANA

Hili ni neno la Kiyunani *bebrios*, lenye vidokezo vitatu

1. Kile ambacho ni hakika (kama vile Rum 4:16; 2 Kor 1:7; Ebr 2:20; 3:6,14; 6:19; 2 Pet 1:10,19
2. Mchakato ambao kitu chenye hali ya kuaminika kinaonyeshwa au kuwekwa wazi (kama vile Louw na Nida, *Greek-English Lexicon of the New Testament*, Uk 1, Kur. 340,377,670).
3. Maandiko katika magombo yakawa ndiyo kifungu cha dhamana ya kisheria (kama vile Moulton na Milligan, *Vocabulary of the Greek New Testament*, kurasa.107-80).

Hii inawezekana kuwa kinyume na mstari wa 14. Ahadi za Mungu ni za kweli.

■**"kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki "** maagano ya Musa yalisisitiza utiifu! Dhamira ya kutokutii ilikua wazi na mara moja matokeo yake ni adhabu (kama vile Ebr. 10:28).

Maneno haya mawili yanaundwa na kihusishi kile kile; *parabasis* na *parakoē*, ambayo yumkini ikawa ni mchezo wa neno la kimataifa (sauti).

**2:3 "Tutapataje kupona"** Kitabu cha Waebrania kina maonyo kadhaa mengi juu kutokujali ukweli wa Mungu (kama vile Ebr. 2:1-4; 3:7-4:11; 5:11-6:12; 10:19-39; 12:14-29).

□ **"tusipojali wokovu mkuu namna hii"** Neno "tusipojali" (*ameleō*) linamaanisha "kuwa mwangalifu" au "kutojali juu ya" kitu au mtu fulani. Limetumika kwenye Agano Jipywa ajili ya (1) onyo dogo kwa ajili ya Timotheo sio kwa kutojali kipawa chake cha kiroho (kama vile 1 Tim. 4:14) na (2) uthibitisho wa kuhitajika umakini kwa Israeli kwa sababu hawakuyaheshimu maagano yake (kama vile. Ebr. 8:9).

Hili ni lengo kuu la mabishano kwamba ikiwa maagano ya Musa yalikua na matokeo ya kutisha kwa ajili ya kutojaliwa ni kwa namna gani matokeo makali zaidi kwa ajili ya kutojali Agano jipywa na bora zaidi liliiloletwa Yesu (mwana). Kutokuelewa matokeo ya kutokujali ujumbe unasimuliwa kwa ukuu wa yeze aliyereta ujumbe (yaani, mfano wa harusi ya kifalme, kama vile. Mt. 22:2-14).

Swali la kifasiri linakuja, "Je! hii inarejelea kwa (1) kutojali maagano mapya (injili) au (2) kutojali maagano mapya?" matumizi ya kisasa ya neno yanadokeza #2. Baadhi ya wafasiri wanaweza kuongeza matumizi ya "sisi" kama ushahidi wa utambulisho wa mwandishi na kundi la waaminio, lakini kwenye Ebr. 10:26 mwandishi ametumia kiwakilishi nomino hiki hiki (wingi wa mtu wa kwanza) katika kuelezea kundi la wasioamini. Wapokeaji hawa hawakuikataa injili, lakini ilipunguza kabisa ushawishi wake kwenye maisha yao.

□ "Ambao kwanza ulinenwa na Bwana" Yesu anaitwa na YHWH mmiliki wa maagano ya Agano ya Kale "Mimi niko ambaye Niko" (kama vile. Kut.3:14, ambalo baadaye lilisomwa kama "Bwana" [adon]). Tazama Mada Maalumu katika Ebr. 2:7. Hii ni moja ya njia kwamba waandishi wa Agano Jipy a wanaonyesha Uungu wa Yesu wa Nazareti. YHWH mwenyewe umechukua ushahidi wa uaminifu wa ujumbe wa Yesu (kama vile Ebr. 2:4). Tazama mada Maalumu: *Archē* katika Ebr. 3:14.

□ "na wale waliosikia" Wote Yohana Calvin na Martin Luther wanasesma kwamba tungo hii inarejelea kwa kizazi cha pili cha Wakristo. Ni wazi hii haimaanishi kwa Paulo (kama vile Gal. 1:11). Paulo hakuwa mwandishi kwa Waembrania. Tazama muhtasari katika Ebr. 13:23.

**2:4 "Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nydingi"** ishara na maajabu ilifanyika yote ili kuwatia moyo waaminio na kuwasaidia wasioamini kuipokea kweli (kama vile. Mdo 2:22). Mungu anaendelea (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo) kuchukua ushahidi wa kweli wa injili. Kulikuwa na ishara za nguvu zote za uovu na kiroho zilizozunguka ujio wa kwanza Yesu, kama zitakavyo zunguka ujio wake wa pili.

□ "na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu" kila mwaamini angalau ana kipawa cha kiroho alichopewa na Roho wakati wa mabadiliko (kama vile. 1 Kor. 12:7,11,18; Efe. 4:11,12). Vipawa hivi vya kiroho kwa waaminio ni moja ya ushahidi wa nyakati za leo wa nguvu za injili, ambazo baadhi ya wapokeaji wa nyaraka wamezikana au kuzikataa!

□ "kama alivyopenda mwenyewe" Roho huchagua na kugawa vipawa (kama vile. 1 Kor. 12:7,11,18). Vipawa vya waaminio havisisitizi katika thamani ya mtu au uchaguzi binafsi wa mtu! Ikiwa kipawa cha kiroho kinasimuliwa katika uwezo wa asili, kinatiwa nguvu na hivyo kuelekezwa kama kuleta utukufu kwa Kristo, sio kwa mkristo mmoja mmoja. Vipawa vyote vinatumikia mwili. Kila mwaamini kwa ajili ya afya na kukua katika mwili!

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 2:5-9

<sup>5</sup> Maana hakuuweka chini ya malaika ulimwengu ule ujao tunaounena, <sup>6</sup>ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema,

"Mwanadamu ni nini hata umkumbuke,

Ama mwana wa binadamu, hata umwangalie?

<sup>7</sup> Umemfanya mdogo punde kuliko malaika,

Umemvika taji ya utukufu na heshima,

Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako;

<sup>8</sup> Umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake."

Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake.

Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake. <sup>9</sup>ila twamwona ye ye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu.

**2:5 "Maana hakuuweka chini ya malaika ulimwengu ule ujao"** ni kweli kwamba malaika wako kwenye sehemu ya ukuu kiroho sasa (kama vile Kumb. 32:8 katika tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania na kitabu cha Danieli, sura ya 10). Hata hivyo, katika ulimwengu ujao, itakuwa ni wanadamu, kwa maana ya wao kucaa mwili, utukufu kwa Mwokozi, ambae atakua kwenye sehemu ya mamlaka. Huu ni mfano mwingine unaosimulia ukuu wa Yesu na wafuasi wake juu ya malaika ambao wanatazamwa kama wahusika kwenye maagano ya Musa (kama vile Ebr. 1:4-14).

**2:6 "ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema"** Hii ni Nahau ya Kiebrania kwa ajili ya ufunuo wa Agano la kale lote, sio kupoteza kumbukumbu kama wapi haya madondoo yanapatikana (kama vile Ebr. 4:4). Kuna mfuatano wa madondoo ya Agano la kale, ambayo yamezoleka kwa kiebrania.

■ "Mwanadamu ni nini hata umkumbuke" Hii ni dondo kutoka kwenye tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania ya Zab. 8:4-6 yanasisitiza teolojia katika Mwa. 1:26,28. Mistari ya 6, 7, na 8 haimrejelei Masihi ("mwana wa mtu"), lakini kwa ubinadamu. Katika Zaburi neno "mwana wa mtu" ni mfanano unaohusiana na neno "mtu"na haina herufi kubwa. Ni Nahau ya kiebrania kwa ajili ya ubinadamu, *ben adam*, hivyo ni la kawaida kwenye Ezekieli (kama vile. Ezek. 2:1; 3:1,3,4,10,17, nk.).

**2:7 "Umemfanya mdogo punde kuliko malaika"** huu ni mwendelezo wa dondo ya Zab. 8:5-6 kutoka kwenye tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania. Swali kwa ajili ya tafsiri na watafsiri wote ni, ni kwa namna gani linafahamika neno la kiebrania "*Elohim*"?

1. Tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania linaitafsiri Zab. 8:5 kama "malaika," kama vile tafsiri za Kiaramu Targums na Peshitta, Vulgate, na KJV.
2. Toleo la jamii ya kiyahudi ya marekani inalitafsiri kama "mdogo punde kuliko Mungu." Tafsiri kadhaa za kiingereza zina "Mungu" (kama vile Toleo la ASV, NASB, RSV, NEB, NRSV, REB, JB, NJB, TEV). Neno, linapotumika kwenye Agano la kale na kitenzi kimoja, kama Mwa. 1:1, kinamrejelea Mungu. Yesu ametumika kwenye maana hii katika Yohana 10:31-39. Pia imetumika kwa "miungu" ya mataifa ya kipagani. Inaweza kurejelea kwa malaika kwa maana ya baraza la mbinguni la Mungu linaloundwa na yeze na malaika watumishi (kama vile 1 Fal. 22:19; Dan. 7:10).
3. kuna uwezekano kwamba hata inarejelea hakimu wa Israeli (kama vile Kut.21:6; 22:8-9,28; Zab. 82:1,6).

Katika muktadha huu lengo la kiteolojia ni kwamba Yesu na wafuasi wake (kama vile Ebr. 1:14) ni wakuu kwa malaika.

Kuna machapisho mbalimbali ya kiyunani katika mwisho wa Ebr. 2:7. Baadhi ya machapisho ya kale ya kiyunani (x, A, C, D\*, P) yanaendeleza dondo kutoka Zab. 8:7, lakini mengine yamesitisha katika " Umemvika taji ya utukufu na heshima " (P<sup>46</sup>, B. D<sup>C</sup>, K, L) kama vile mengi ya matoleo haya mbalimbali, hayafanyi tofauti kwenye tafsiri ya andiko.

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

Huu ulikuwa ni usemi wa kawaida wa Agano Jipyka kwa uwepo binafsi na nguvu itendayo kazi ya utatu wa Mungu katika kanisa.Haikuwa kanuni ya miujiza, bali rufaa kwa tabia ya Mungu. Daima, usemi huu unamhusu Yesu kama Bwana (kama vile Flp.2:11)

1. Weredi wa imani ya mtu katika Yesu wakati wa ubatizo (kama vile Rum. 10:9-13; Mdo. 2:38; 8:12,16; 10:48; 19:5; 22:16; 1 Kor. 1:13; 15; Yak. 2:7)
2. katika upungaji pepo, (kama vile Mt. 7:22; Mk. 9:38; Luka 9:49; 10:17; Mdo. 19:13)
3. katika uponyaji (kama vile Mdo. 3:6,16; 4:10; 9:34; Yak. 5:14)
4. katika tendo la huduma (kama vile Mt. 10:42; 18:5; Luka 9:48)
5. katika muda wa kutekeleza nidhamu kanisani (kama vile Mt. 18:15-20)
6. wakati wa kuhubiria watu wa Mataifa (kama vile Luka 24:47; Mdo. 9:15; 15:17; Rum.1:5)
7. katika maombi (kama vile Yn.14:13-14; 15:2,16; 16:23; 1 Kor 1:2)
8. kama njia ya kurejea Ukristo (kama vile Mdo 26:9; 1Kor 1:10; 2 Tim 2:19; Yak. 2:7; 1 Pet. 4:14)

Chohote tukifanyacho kama wahudumu, wasaidizi, waponyaji, watoa mapepo, n.k, tunafanya hivyo kwa tabia yake, nguvu Zake, upaji Wake - katika jina Lake.

■ "Umemvika taji ya utukufu" Tazama muhtasari katika Ebr. 1:3.

**2:8** Hii inatoka katika Zab. 2:6, lakini ni dokezo la Mwa. 1:26,28-30. Mwanadamu ameumbwa kwa sura ya Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27) ili kufanya kazi kama mtawala ulimwenguni (kama mwakilishi wa Mungu). Lakini anguko la mwanadamu katika kitabu cha Mwanzo 3 kulizuia kusudi hili (kama vile Ebr. 2:9c).

**2:9 "ila twamwona"** toleo la NASB lina viwakilishi nomino vyote kwa herufi ndogo kwenye Ebr. 2:7 na 8 (yaani, mwandishi anadondoo katika Zaburi), lakini katika Ebr. 2:9 yapo katika herufi kubwa (mwandishi anatumia

Zaburi), hivyo kulinganisha anguko la mwanadamu na mtu kamili. Mungu alimweka mwanadamu kwenye sehemu ya heshima ya mamlaka, lakini mwanadamu alitenda dhambi na kuipoteza sehemu hiyo. Mungu akiwa ameuvaa mwili wa Yesu ili kukamilisha hatima ya mwanadamu na kwa kifo chake kuwarejesha wanadamu waaminio katika sehemu ya heshima. Yesu kwa ukweli alikuwa mwanadamu! Hii ni aina nyingine ya uanishi Adam-Kristo (kama vile Rum. 5:12-21; 1 Kor. 15:21-22,45-49; Fil. 2:6-11).

■ "yeye aliyefanya mdogo punde kuliko malaika" huu ni mfanano wa wazi na mstari wa 6 na 7. Unaongelea Yesu kuutwaa mwili na maisha ya duniani.

■ "Yesu" mwandishi Kwa Waebrania anatumia tabia ya "Yesu" bila kuongeza maelezo yoyote yale (kama vile Ebr. 2:9; 3:1; 6:20; 7:22; 10:19; 12:2,24; 13:12). Inawezekana kwamba huu ni mchezo wa uanishaji kwa Yesu kama Yoshua mpya. Majina kwa hakika ni yale yale. Mwandishi kwa Waebrania ametumia nyezo za kitabu cha Kutoka kwa mapana zaidi. Kama vile Yoshua alivyowareta watu wa Mungu kwenye pumziko la nchi ya ahadi, hivyo pia, Yesu atawaleta mbinguni (yaani, kupumzika siku ya saba).

■ "kwa sababu ya maumivu ya mauti" Hii inaaksi Mwa. 3:15; Zaburi 22; Isaya 53. Alikuwa ni mpatanishi wa Mungu kwenye ukombozi!

■ "amevikwa taji ya utukufu na heshima" hii ni kauli timilifu tendwa endelevu ya hali ya kuendelea. Alikuwa na anaendelea kuvikwa taji yeze! Tazama Muhtasari katika Ebr. 1:3.

■ "ili kwa neema ya Mungu" tafsiri hii (*chariti Theos*) inapatikana kote kwenye Biblia za kiingereza na kuungwa mkono na machapisho ya kale ya kiyunani (P<sup>46</sup>, Χ, A, B, C, D). Hata hivyo, usomaji wa kudadisi "mbali na Mungu" (*chōris Theos*), imejitokeza kwenye maandiko ya kale mengi baadae. Katika *A Textual Commentary On The Greek New Testament*, Bruce M. Metzger wanasema kwamba huu ulikuwa ni mng'ao wa asili wa pembeni unaosimuliwa katika 1 Kor. 15:27, ambao ulikuwa haufahamiki kama sahihisho kwa "*chariti Theos*" (uk. 664).

Toleo la United Bible Society's *A Handbook on the Letter to the Hebrews* na Paul Ellingworth na Eugene A. Nida wanatoa uchaguzi mwingine, kwamba "kuwa mbali na Mungu" yumkini likadokeza katika Zaburi 22, ambalo Yesu alitumia kuelezea maana yake ya kuwa peke yake kwenye msalaba (kama vile. Marko 15:34) uk. 37. Uchaguzi huu huu umetolewa na Myles M. Bourke kwenye *Jerome Biblical Commentary* (uk. 385).

Kuna uchaguzi wa tatu pia (umechukuliwa kutoka kwa Bart D. Ehrman's, *The Orthodox Corruption of Scripture*, Oxford Press, 1993, uk. 146-150) kwamba waandishi kwa makusudi walibadilisha "kuwa mbali na Mungu" kwa ajili ya sababu za theolojia, kwa uhalisi theolojia ya kitisho cha mafunuo.

Hii tofauti ilikuwa inafahamika kwa Origen na Jerome. Pia neno "mbali" (*chōris*) limetumika mara kumi na tatu katika kiebrania, ambayo inaonyesha mwelekeo wa mwandishi kutumia neno hili. Pia kulingana na Ehrman (uk. 148), mara zote inafuatwa na anarthrous (hakuna makala) nomino.

■ "aionje mauti" ni muhimu kutambua kwamba mateso yalikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa ajili ya Yesu Kristo (kama vile Mwa. 3:15; Isa. 53:4,10; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21). Dhana hii ya mateso iliendelea kwenye Agano la kale dondoo zinapatikana kwenye sura ya 2 iliyobakia.

■ "kwa ajili ya kila mtu" Muktadha huu unarejelea kuwakilishwa, mbadala wa upatanisho wa Yesu Kristo (kama vile. Isa. 53:6; Rum. 5:6,8,10,17-19; 1 Kor. 15:22; 1 Tim. 2:4,6; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9). Yesu alikuwa ili kuhusika sana na tatizo la dhambi za mwanadamu. Jambo pekee ambalo huwafanya wanadamu wote kuokolewa ni kutokubali kupokea kipawa cha bure cha Mungu katika kazi iliyokamilishwa na Yesu kristo kwa imani (kama vile. Yn 3:17-21).

## MADA MAALUM: MPANGO WA UKOMBOZI WA MILELE WA YHWH

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Yer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31), wale wote walio umbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maangano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipy, sio Israeli, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.

Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu katи ya watu wawili.

1. St. Augustine anaunganisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani., iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israel, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12
2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abraham ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israel. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbukumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihilisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Abraham, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, "kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu"). Israel ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakfisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
  - a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
  - b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19
  - c. Mika 4:1-3
  - d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa "agano jipy" (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna "moyo mpya," "mawazo mapya," na "roho mpya." Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipy linaimalisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani., ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yn 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipy – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni "fumbo la Mungu," lililofichika lakini sasa limedhihilisha (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipy linaangazia juu ya Yesu, na sio Israeli. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israel ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumai utapata wasaa wa kusoma [Mada Maalum: kwa nini ahadi za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti toka ahadi za Agano Jipyा](#). Waweza kupata katika mtandao [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 2:10-13

<sup>10</sup> Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso. <sup>11</sup> Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake; <sup>12</sup> akisema,

"Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu;

Katikati ya kanisa nitakuimbia sifa.

<sup>13</sup> Na tena,

Nitakuwa nimemtumaini yeye.

Na tena, Tazama,mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu."

**2:10 "Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo"** Tena viwakilishi vina utata. Hii inaweza kumrejelea Mungu baba (kama vile Rum. 11:36) au Mwana (kama vile Ebr. 1:2,3; Kol. 1:15-17). Kwa sababu Yesu amerejelewa kama "muumbaji" kwenye sehemu ya mwisho ya mstari huu, kiwakilishi cha awali ni lazima kitarejelea kwa Baba. Hata hivyo, Yesu alikuwa ni mpatanishi wa Baba kwenye uumbaji (kama vile. Ebr. 1:2; Yn. 1:3; 1 Kor. 8:6; 15:25-27) kama alivyokuwa kwenye ukombozi na atakavyokuwa kwenye hukumu.

▣ "akileta wana wengi waufikilie utukufu" Familia ni sehemu ya maagano mapya yaliyofunuliwa kamili kwenye mistari inayobakia sura ya 2. Tambua idadi ya maneno familia yalivyotumika. Lengo la maagano mapya ni kurejesha sura ya Mungu ya mwanadamu aliyeanguka. Neno "wengi" halimaanishi "baadhi" kama kinyume cha "wote" (kama vile. Ebr. 2:9, "kila mmoja"). Maneno "wote" na "wengi" yametumia sitiari kwenye Biblia (linganisha Isa. 53:6 na 11, 12 na Rum. 9:18 na 19). Hivyo basi, Marko 10:45 na 14:24 lazima itarejelea kwa "wote," sio "baadhi"! Hii haiwezi kufanya kazi kama andiko la kuhakiki kwa ajili ya msingi wa mafundisho ya Calvin (yaani., supra-lapsarian).

**NASB**      "kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao"

**NKJV**      "kumfanya kamili kiongozi mkuu wa wokovu waoto "

**NRSV**      "wataimarisha njia ya wazi ya wokovu wao kamili"

**TEV**      "kumkamilisha Yesu"

**NJB**      "kukamilisha ...kiongozi wa wokovu wao"

Neno "kamili" (kauli tendaji ya kitenzi jina ya wakati uliopita usiotimilifu) linamaanisha "kukamilika, ukomavu, tayali kwa ajili kuteuliwa kwa kazi" (kama vile. Efe. 4:12). Mwandishi kwa Waeranania ametumia "kumkamilisha" mara tatu kwa kumwelezea Yesu (kama vile Ebr. 2:10; 5:9; 7:28) na mara tatu kuwaelezea wafuasi wake (kama vile Ebr. 10:14; 11:40; 12:23). Tazama Mada Maalumu katika Ebr. 7:11.

Yesu alikuwa mwanadamu kweli (kama vile. Luka 2:40,52). Alikuwa katika imani na utiifu (kama vile. Luka 2:40,52). Alijaribiwa na dhiki (kama vile Ebr. 5:8-9). Alivikabili na kuvishinda vizuizi vya kila aina vya kiroho (kama vile. Ebr. 4:15). Alikuwa mfano mkuu kwa mwanadamu (kama vile 1 Pet. 2:21).

#### MADA MAALUM: MWANDISHI/KIONGOZI (ARCHĒGOS)

Neno "mwandishi" au "kiongozi" nineno la Kiyunani *archēgos*. Hili linatokana na mzizi wa Kiyunani "mwanzo" (*archē*) na "kwenda" au "kuongoza" (*agō*). Huu uambatani ulikuja kutumika kwa kiongozi, mkuu, au kiongozi (mwanadamu au kimalaika). Neno hili halitumiki mara nne pekee katika Agano Jipyा kurejea juu ya Yesu:

1. Mkuu wa uzima katika, Matendo ya Mitume 3:15
2. Mkuu na Mwokozi, Matendo ya Mitume 5:31
3. Kiongozi Mkuu wa wokovu wao katika Ebr. 2:10
4. Aliyeanzisha (au mtangulizi) na mkamilishaji wa imani katika Ebr. 12:2

Yesu nimwanzilishi, mtoaji, na mmaliziaji wa wokovu.

■ "kwa njia ya mateso" Yesu alikuwa mkamilifu, akiongea kibinadamu, kwa mateso (kama vile Ebr. 5:8-9). Yesu mara nyingi aliongelea majoribu na mateso ambayo wafiasi wake watakutana nayo (kama vile. Mt. 5:10-12; Yn 15:18-19; 17:14).

Kanisa la awali lilikutana na upinzani kutoka kwa Wayahudi, wapagani, utawala wa Kirumi, na yule mwovu, lakini Mungu aliuchukua upinzani huu na kuugeuza kuwa chombo cha kuonyesha uaminifu na kumfanana kristo (kama vile Rum. 8:17; Fil. 1:29; 2 Tim. 3:12; Yakobo 1:2-4; na 1 Pet. 4:12-19). Uaminifu unaweza kuelezeewa kwa picha kutoka (1) Agano la kale (kama vile Ebr. 11) na (2) huduma ya Paulo (kama vile 1 Kor. 4:9-12; 6:4-10; 11:24-27).

**2:11**

|            |  |
|------------|--|
| NASB, NRSV | " Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa"                          |
| NKJV       | "kwa ajili ya wote atakasaye na wao waliotakaswa"                    |
| TEV        | "aliwatakasa watu na dhambi zao, na wale wote aliowafanya kuwa safi" |
| NJB        | "kwa ajili ufanyaji wakfu na kuwekwa wakfu"                          |

Huu ni mchezo katika neno "takatifu" au "kutakaswa" (kama vile Ebr. 10:10, 14). Matumizi ya kwanza ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo (Yesu) na ya pili ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo (watu wake, kama vile. Yn 17:19). Yesu anafanana na watu wake (kama vile Ebr. 1:14 na 2:6-8, 9-18).

Waaminio wanatakaswa na Baba (kama vile. Yn 17:17; 1 Thes. 5:23); kuitia kwa upatanishi wa mwana (kama vile. 1 Kor. 1:2; Efe. 5:26; Ebr. 10:10,14,29; 13:12); madai haya yanaungana kwenye Ebr. 2:11.

1. Baba mtakatifu
2. Mwana mtakatifu
3. Watakatifu waaminio (kama vile 1 Pet. 1:13-25)

Hii ni kweli mahali na uzoefu pote. Sisi ni watakatifu katika Kristo na tumeitwa kuwa watakatifu kama Kristo.

## MADA MAALUMU: UTAKATIFU/UTAKASO WA AGANO JIPYA

Kitabu cha Agano jipyä kinadai kwamba wenyе dhambi wanapomgeukia Yesu kwa toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21), huthibitishwa na kutakaswa papo kwa papo. Hii ni nafasi mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wametangaziwa haki na utakatifu (tendo la ki-Mungu la kumto mtu hatiani).

Lakini Agano Jipyä pia linawasistiza waamini kuwa katika utakatifu au utakaso. Hii ni nafasi ya kitheolojia katika kazi ya Yesu Kristo iliyomalizika na wito wa kufanana na Kristo katika mtazamo na matendo katika maisha ya kila siku. Kwa kuwa wokovu ni neema ya bure na gharama ya kila kitu cha mtindo wa maisha, hivyo hata hii, niutakaso.

### Mwitikio wa Awali

- Matendo 26:18
- Warumi 15:16
- 1 Wakorintho 1:2-3; 6:11
- 2 Wathesalonike 2:13
- Waembrania 2:11; 10:10,14; 13:12
- 2 Petro 1:2

### Ufanano na Kristo Endelevu

- Warumi 6:19
- 2 Kor. 7:1
- Waefeso 1:4; 2:10
- 1 Wathesalonike. 3:13; 4:3-4,7; 5:2
- 1 Timotheo 2:15
- 2 Timotheo 2:21

▣ "wote pia watoka kwa mmoja Baba" Neno "Baba" haliko kwenye andiko la kiyunani (kama vile toleo la NASB, NRSV, TEV). Kiwakilishi "yeye" kwenye kifungu kinachofuata kinarejelea kwa Yesu (kama vile toleo la NRSV, TEV, NIV). Hivyo basi, labda tafsiri ya toleo la NJB, "wote katika akiba ile ile" au toleo la NIV "kwa familia ile ile" unafaa muktadha huu zaidi. Ikiwa ni hivyo, inatilia mkazo ubinadamu wa Yesu (kama vile Ebr. 2:14).

▣ "Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake" Yesu anajitambulisha yeye mwenyewe kikamilifu na wanadamu waaminio. Kupitia mateso yake sura Mungu inarejeshwa kwao. Dondoo tatu zifuatazo za Agano la kale (kama vile Ebr. 2:12-13) zinaonekana ziko nje ya muktadha, lakini zinatoka kwenye kifungu cha Kimasihi kinachotumia mchezo wa neno la walimu wa kiyahudi. Muktadha wa Ebr. 2:10-18 unafananisha ukamilifu wa Yesu na wafiasi wake:

1. wote walimtangaza Baba
2. wote walimsifu Baba
3. wote waliweka imani zao kwa Baba
4. Yesu (kama vile "mimi" ya Ebr. 2:13b) na wafiasi wake ("watoto" ya Ebr. 2:13b) inaunganisha kipawa cha Mungu Baba kwa mwana
5. wote Yesu na wafiasi wake wanashiriki asili ya mwanadamu
6. wote Yesu na wafiasi wake walijaribiwa

**2:12-13** mfuatano huu wa dondo za Agano la kale unaelezea ni kwa namna gani Yesu anafanana na waaminio kwa kutumia maandiko haya ya Agano la kale.

**2:12** "Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu" Hii ni kutoka Zab. 22:22 ambayo inasimulia unabii wa kusulubiwa.

▣ "kanisa"

## MADA MAALUM: KANISA (EKKLESIA)

Neno hili la Kiyunana, *ekklesia*, linatokana na maneno mawili, "nje ya"na "kuitwa." Neno hili linatumika kidunia (yaani., jamii iliyoitwa kwenye kikao, k.v Mdo. 19:32,39,41) na kwa sababu ya utumiaji wa maandiko ya kale ya Kiyunani ya neno hili kwa ajili ya "kusanyiko" la Israel (*Qahal*, BDB 874, KB 1078, k.v. Hes. 16:3; 20:4; Kumb. 31:30), na matumizi ya kidini Kanisa la mwanzo walijiona wao kama mwendelezo wa Agano la Kale la watu wa Mungu. Walikuwa Waisrael wapya (k.v. Rum. 2:28-29; Gal. 3:29; 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6), utimilizo wa kusudi la Mungu kidunia (k.v. Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH

Neno lililotumika kwa maana nyangi katika injili na matendo.

1. Mikusanyiko ya kidunia, Mdo. 19:32,39,41
2. Watu wa Mungu ulimwenguni katika Kristo, Mt. 16:18 na Waefeso
3. Kusanyiko la waumini wa mahali katika Kristo, Mt. 18:17; Mdo. 5:11 (katika aya hii, ni kanisa huko Yerusalem); Mdo. 13:1; Rum. 16:5; 1 Kor. 16:19; Kol. 4:15; Filemoni uk. 2
4. Watu wa Israel kwa ujumla, Mdo. 7:38, katika hotuba ya Stephano
5. Watu wa Mungu kwenye Miji, Mdo. 8:3; Gal. 1:2 (Yuda au Palestina)

Kanisa ni watu waliokusanyika, na sio jengo. Hapakuwepo na majengo ya kanisa kwa muda wa miaka mingi. Katika Yakobo (moja ya kitabu cha mwanzoni kabisa cha Wakristo) kanisa lilitajwa kwa neno "*synagōgē*" (kusanyiko). Neno kanisa limetokea tu kwa Yakobo (k.v. Yakobo 2:2; 5:14).

**2:13 "Nitakuwa nimemtumaini yeye"** tungo hii ni dondo kutoka Isa. 8:17. Katika lengo hili ngoja mimi niongeze neno juu ya mwandishi kuendelea kutumia tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania ambayo ni tofauti, mara nyingi ni tofauti kabisa, kutoka katika andiko la kiebrania (Kimasoret). Kuna mabishano yanayoonekana zaidi kwenye nyakati zetu yanayosimulia utofauti wa tafsiri za kiingereza. Baadhi hurejea mmoja juu ya mwingine, wakati mwingine hata kuuliza hamasa na wafasiri wa kikristo. Ikiwa Roho wa Mungu anaweza kutumia tafsiri ya kiyunani kuwasilisha injili kwa mashariki ya karibu ya kale, kwa uhakika anaweza kutumia tafsiri tofauti kufanya hivyo hivyo katika nyakati zetu. Sio swalii la nadharia ya tafsiri lakini ni mapenzi ya Mungu kwamba wanadamu wasikie na kuiamini habari njema za Kristo.

▣ "Tazama, mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu" hii ni dondo kutoka tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania ya Isa. 8:18. Lengo zima ni kutilia mkazo umoja wa Yesu na waaminio (kama vile Ebr. 2:17).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 2:14-18**

<sup>14</sup> Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi,<sup>15</sup> awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa.<sup>16</sup> Maana ni hakika, hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahim.<sup>17</sup> Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake.<sup>18</sup> Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipajaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.

**2:14 "Basi"** hii ni sentensi hali daraja la kwanza ambayo inathibitisha kuwa kweli kutoka katika taswira ya mwandishi au kwa ajili ya kusudi la fasihi yake.

▣ "kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo" Kitenzi "wameshiriki," (*koinōnia*) kauli timilifu tendaji elekezi ya hali ya kuendelea] inaongelea asili na kuendeleza ubinadamu kamili wa Yesu kristo. Mistari ya 14 na 17 inatilia mkazo ukweli wa ubinadamu wa Yesu ambao ni tatizo la kitheolojia la mafunuo ya awali (kama vile 1 Yn. 4:1-6).

Ni dhahili kuwa tungo iko kwenye Kiyunani "damu na mwili." Hiki ni kinyume kabisa kutoka katika matumizi ya kawaida ya tungo. Walimu wa Kiyahudi wametumia tungo hii kwa ajili ya udhaifu wa mwanadamu. Inawezekana mwandishi kwa Waebrania alirudisha tungo nyuma kuonyesha kwamba ingawa Yesu alikuwa ni mwanadamu, hakuathiriwa na anguko la dhambi za wanadamu (kama vile Rum. 8:3; Flp. 2:7-8).

Waebraania inatilia mkazo pote katika uungu (kama vile Ebr. 1:1-3; 4:14) na ubinadamu wa Yesu.

1. Ebr. 2:14 alichukua asili ya mwanadamu
2. Ebr. 4:15 alijaribiwa kwa njia zote kama mwandamu
3. Ebr. 5:7 alimwomba Baba kwa kulia sana na machozi
4. Ebr. 5:8-9 alikamilishwa kwa mateso

▣ "ili kwa njia ya mauti" kwa kifo cha Yesu, kifo kilikufa! Hii ni teolojia ya Kiyahudi inayoshirikisha sadaka (kama vile Law. 1-7). Mwenye haki mmoja anapokufa kwa niaba ya wote (kama vile Rum. 5:12-21; 2 Kor. 5:14-15,21).

**2:15 "amharibu yeye"** Hili ni neno lile lile (*katargeo*) kwamba toleo la tafsiri ya KJV linatafsiri "kuharibu" yote hapa na kwenye Rum. 6:6. Bila shaka kuna hiki kidokezo katika 2 The. 2:8. Mara nyingi ni vigumu, hata kwenye muktadha, kujua kwamba ikiwa kitenzi hiki kinaweza kutafsiriwa "kuharibu/ondoa kabisa" au "kulitangua na batilika" (kama vile 1 Kor. 15:24, 26; Efe. 2:15). Hata hivyo, neno pia lina kidokezo cha "kuleta katika dharau, kuliharibu na kubatilisha, kuacha isiwe na kazi" (kama vile Rum. 3:3, 31; 4:14; 6:6; 1 Kor. 2:6; 13:8; 2 Kor. 1:7).

#### **MADA MAALUM: BATILI NA UTUPU (KATARGEŌ)**

Hili neno (*katargeō*) liliwa ni moja ya maneno pendwa ya Paulo. Aliyatumia takribani mara ishirini na tano lakini liliwa na utofauti mpana.

- A. Mzizi wa kiasili wa neno unatoka kwenye neno *argos* linalo maanisha
  - 1. Isio tendaji
  - 2. Isio na kazi
  - 3. Isiotumika
  - 4. Isiofaa
  - 5. Isiofanya kazi
- B. Neno ambani likiwa na *kata* lilitumika kuelezea
  - 1. Isiofanya kazi
  - 2. Isiofaa kabisa
  - 3. Iliyo imebatilishwa
  - 4. Lililofanyikia mbali
  - 5. Ambalo liliwa halifanyi kazi kabisa
- C. Limetumika mara moja tu katika Luka kuelezea lisilozaa matunda, kwa hiyo ni mti usiofaa (kama vile Lk 13:7)
- D. Paulo analitumia kwa maana ya kitamathari kwa njia mbili za msingi
  - 1. Mungu anafanya vitu visivyotumuka ambavyo havina faida kwa mwanadamu
    - a. Asili ya dhambi ya mwanadamu-Rum. 6:6
    - b. Sheria za Musa ukilinganisha na ahadi ya Mungu ya "mbegu"-Rum. 4:14; 3:17; 5:4,11; Efe. 2:15
    - c. Nguvu za kiroho-1 Kor. 15:24
    - d. "Mtu asiye wa sheria"-2 The. 2:8
    - e. Mauti ya mwili-1 Kor. 15:26; 2 Tim. 1:10 (Ebr. 2:14)
  - 2. Mungu anaweka ktu kingine cha zamani (Agano, zama) kwa kipyta
    - a. Vitu vinavyohusiana na sheria za Musa – Rum. 3:3,31; 4:14; 2 Kor. 3:7,11,13,14
    - b. Mshabihiano wa ndoa uliotumia sheria – Rum. 7:2,6
    - c. Mambo ya zama hizi – 1 Kor. 13:8,10,11
    - d. Mwili huu – 1 Kor. 6:13
    - e. Viongozi wa zama hizi – 1 Kor. 1:28; 2:6

Neno hili linatafasiliwa kwa njia mbali mbali, lakini maana yake kuu ni kukifanya kitu kisichofaa, batili na utupu, kisichofanya kazi, kisicho na nguvu, lakini sio muhimu kuwa hakiishi, kilichoharibiwa au angamizwa

▣ "aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi" Huyu shetani hana nguvu kamili juu ya kifo (kama vile Ayu 2:4-6; 1 Kor. 5:5), lakini ameshikilia nguvu ya hofu juu ya kifo (kama vile Ebr. 2:15) ambayo ameishikilia juu ya wanadamu wote (kama vile 1 Kor. 15:54-57). Kuna nguvu binafsi ya uovu inayotoka ili kuzuia mapenzi yote ya Mungu kwenye hii dunia (kama vile Yn. 12:31; 14:30; 16:11; 2 Kor. 4:4; Efe. 2:2; 1 Yn. 4:4; 5:19). Yesu alikiondoa kifo kabisa (kama vile 2 Tim. 1:10) na ana funguo za kuzimu na kifo (kama vile Ufu. 1:18).

## MADA MAALUM: SHETANI

Hili suala gumu sana kutokana na sababu kadhaa.

- 1. Kitabu cha Agano la Kale hakimfunui adui mkuu apingaye mema, bali mtumishi wa YHWH (angalia. B. Davidson, OT Theology, kr. 300-306), ambaye anampa mwanadamu uchaguzi wa bure na pia kumlaumu mwanadamu juu ya kutokuwa kwake mwenye haki. Kuna Mungu mmoja pekee (angalia Mada Maalum: Mungu aliye mmoja, uweza wa aina moja, sababu moja iliyo ndani ya Agano la Kale—YHWH (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6).
- 2. Hii dhana ya huyu adui mkuu wa Mungu wa kipekee ilikuwa katika kipindi cha ukimya wa fasihi ya Agano la Kale na Agano Jipya (pasipo sheria za kikanisa) chini ya ushawishi wa pande mbili za dini za Kiajemi (Dhana ya Zoroaster). Hii, katika kurudia, kwa kiwango kikubwa hizi ziliwashawishi viongozi wa

dini za Kiyahudi na jamii ya Essene (yaani, Magombo ya Kale ya Bahari ya Chumvi).

3. Kitabu cha Agano Jipy kiliikuza dhana ya Agano la Kale katika namna yaugumu wa kushangaza, lakini wa kipekee, wa aina nyingi.

Ikiwa moja ya mitazamo ya somo la uovu kutokana na kipengele cha theolojia ya kibiblia (kila kitabu au mwandishi au aina ya somo lililofundishwa na maelezo ya kimuhtasari yaliotengwa), tena ni mawazo tofauti sana ya uovu unaofunuliwa. Ikiwa, kwa vyo vyote, moja ya mitazamo ya somo la uovu kutoka mtazamo usio wa kibiblia au mtazamo wa ziada wa kibiblia wa dini za ulimwengu au dini za mashariki, tena maendeleo mengi ya kitabu cha Aagano Jipy yanatabiriwa katika ule uwili wa Kiajemi na ukiroho wa utawala wa Wagiriki-Waroma.

Ikiwa wazo la awali lilijikita juu ya Andiko la mamlaka ya Kiungu (kama Mimi Niko!), kasha ukuaji wa kitabu cha Agano Jipy lazima uonekane kama ufunuo endelevu. Yawapasa Wakristo kujilinda dhidi ya kuyaruhusu mafunzo ya mila na desturi za Kiyahudi au fasihi ya mashariki (Dante, Milton) kwa ajili ya ushawishi wa dhana ya baadaye. Kuna siri fulani na utata katika eneo hili la ufunuo. Mungu amechagua kutovifunua vipengele vyote vya uovu, chimbuko lake (angalia Mada Maalum: Lusfa), uendelevu wake, sababu yake, lakini Yeye amelifunua ondoleo lake!

Katika neno la Agano la Kale "shetani" au "mshtaki" (BDB 966, KB 1317) anaweza kuhusiana na makundi matatu taliyojitenga.

1. washtaki wa mwanadamu (kama vile 1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 11:14,23,25; Zab. 109:6)
2. washtaki wa kimalaika (kama vile Hes. 22:22-23; Ayubu 1-2; Zek. 3:1)
3. washtaki wa kimapepo (kama vile 1 Nya. 21:1; 1 Fal. 22:21; Zek. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha ukimya wa Agano la Kale na Agano Jipy tu ndipo yule nyoka wa Mwanzo 3 alipotambujishwa kama Shetani (kama vile Book of Wisdom 2.23-24; II Enoch 31:3), na baadaye hili liliuja kuwa uchaguzi wa sheria za Kiyahudi. Sot 9b na Sanh. 29a). Wale "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 walikuja kuwa malaika katika I Enoch 54:6. Nalitaja hili, si usahihi wa kitheolojia, bali hili linaonyesha maendeleo yake. Katika Kitabu cha Agano Jipy kazi hizi linapewa kundi la kimalaika, uovu wa kibinadamu (kama vile 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9). Chimbuko la uovu wa kibinadamu ni gumu au haliwezekani (linategemeana na hoja ya mtazamo wako) kuibainisha kutokana na kitabu cha Agano la Kale. Moja ya sababu ya hili ni kuwepo kwa Mungu wa Israeli Aliye mmoja (angalia Mada Maalum: Mungu Aliye Mmoja;pia nukuu 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amosi 3:6). Usababishi wote (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6) alikpewa YHWH ili kuonyesha upekee na ubora Wake (kama vile Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Chimbuko la uhakika wa habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo Shetani ni mmoja wa "wana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14 na Ezekiel 28, ambapo wafalme wenyewe majivuno waliokuwa karibu na mashariki (Babeli na Tiro) kwa hakika wanatumika kueleza juu ya majivuno ya Shetani (kama vile 1 Tim. 3:6). Nimechanganywa kihisia kuhusu mtazamo huu. Ezekieli anatumia stiari za Bustani ya Edeni, si kwa mfalme wa Tiro pekee kama Shetani (kama vile Eze. 28:12-16), bali pia kwa mfalme wa Misri kama Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya (Ezekiel 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa mist. ya. 12-14, anaonekana kuufanua uasi wa kimalaika kupitia majivuno. Ikiwa Mungu alitaka kuifunua kwetuj ile asili ya kipekee na chimbuko la Shetani, hii ni njia isiyo wazi na ni sehemu ya kulifanya hili. Yatupasa kujilinda dhidi ya uelekeo wa theolojia ya mfululizo wa kuchukulia mambo madogo madogo, sehemu za utata wa semi mbalimbali, waandishi, vitabu, aina na kuziunganisha kama vipande vya mafumbo ya Uungu.

Nakubaliana na Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzu. 2, viambaisho XIII [kr. 748-763] na XVI [kr.770-776]) kwamba Sheria za Dini ya Kiyahudi kwa kiasi kikubwa zimepewa ushawishi na zile pande mbili za Kiajemi na kisiko la kimapepo. Hawa Walimu wa sheria za Kiyahudi si chimbuko zuri la ukweli ndani ya eneo hili. Kimsingi Yesu anaachana na mafundisho ya Masinagogi ndani ya eneo hili. Nafikiri kwamba ile dhana ya adui wa YHWH aliyejikuwa katika umbo la kimalaika iliendelezwa kutokana na miungu mikuu miwili ya pande mbili za ki-Irani, Ahkiman na Ormaza, ambapo iliendelezwa tena na Walimu wa Sheria katika pande

mbili za YHWH na Shetani.

Kuna uhakika wa ufunuo endelevu katika kitabu cha Agano Jipya kama sifa ya, lakini si kama wanavyoeleza Walimu wa Sheria za Kiyahudi. Mfano mzuri wa utofauti huu ni "vita ya mbinguni." Anguko la Shetani kimantiki lina umuhimu, lakini ubatana haokutolewa (angalia Mada Maalum: Anguko la Shetani na Malaika Zake). Hata kile kilichotolewa kinafunika katika aina ya ukiyama (kama vile Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa Shetani anaondolea kwa Yesu na kutupwa duniani, bado anafanya kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20). Katika eneo hili yatupasa kuzuia uchunguzi. Kuna nguvu binafsi ya ushawishi na uovo, lakini bado kuna Mungu mmoja pekee na bado tunawayibika kwa ajili ya chaguzi zetu. Kuna mapambano ya kiroho, wakati wote kabla na baada ya wokovu. Ushindi unaweza kuja tu na kubaki pale pale kupitia Mungu wa Utatu. Uovo Umeshindwa na utaondoshwa kama vile Ufu. 20:10)!

## 2:16

|           |                   |
|-----------|-------------------|
| NASB      | "maana ni hakika" |
| NKJV      | "maana kwa kweli" |
| NRSV, TEV | "maana kwa uwazi" |
| NJB       | --kwa kushindwa-- |

Toleo la NRSV na TEV yanaeleza wazo bora zaidi.

▣ "hatwai asili . . . atwaa asili" Hizi zote ni kauli za kati (shahidi wa maandishi) elekezi. Neno "hatwai" imewekwa awali kwenye sentensi ya Kiyunani kwa ajili ya mkazo. Kitenzi ni *epilambanō*, ambacho kinatoka kwenye asili *lambanō*, "kuchukua" au "kushika" na labda kwa makusudi chanya au hasi. Kwenye muktadha huu inarejelea matendo bayana ya Yesu (kama vile Ebr. 8:9) badala ya wanadamu waaminio, ambao kamwe hawakuelekezwa kwa malaika. Tena Yesu na wafuasi wake wanatofautiana na ulimwengu wa kimalaika.

▣ "mzao wa Ibrahimu" Hii ni dhahili kuwa kifungu "uzao wa Ibrahimu." YHWH alimwahidi Ibrahimu asiye na mwana kwamba atakuwa Baba wa taifa kubwa na uzao mwingi (kama vile Mwa. 12:2; 15:2-6; 17: 4-7; 18:10, 18). Neno "uzao" linaweza kuwa wingi au umoja. Hivyo basi, inarejelea pote kwa taifa la Israeli na Masihi aje. Kutoka katika baadhi ya maandiko ya Agano la kale tunatambua kwamba yanasmulia juu ya imani, sio tukio au utendaji (kama vile Yn 8:31-59; Gal. 3:7,9,29; Rum. 2:28.29). Ahadi za Ibrahimu hazina masharti (kama vile Hasa Mwa. 15:12-21; Rum. 4), ambapo maagano ya Musa yana masharti katika utiifu.

2:17 "Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote" Maombi ya Yesu yafanyayo kazi badala ya mwanadamu yanasmulia ukamilifu wa ufahamu wa asili yetu (kama vile. Ebr. 2:11,18; 4:15) hivyo anaweza kuwa kuhani wetu mkuu.

▣ "apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu"

## MADA MAALUMU: YESU KAMA KUHANI MKUU

Kitabu cha Waebrania ni cha pekee katika Agano Jipya kwa kumwita Yesu kuhani mkuu. Kuna sehemu mbili katika Agano la Kale ambalo Masihi anaelezewa katika suala la kuhani (tazama Zab. 110: 4; Zek. 3-4). Mandhari hii itaendelezwu kikamilifu katika Ebr. 4: 14-5: 10 na 6: 13-7: 28.

Waebrania inaeleza kazi ya Kuhani Mkuu wa Yesu kwa njia kadhaa.

1. hufanya upatanisho wa dhambi (kama vile Ebr. 2:17, 7:27; 9:14)
2. huwapa nguvu wale wanaojaribiwa na dhambi (kama vile Ebr. 2:18)
3. hutoa neema wakati wa uhitaji (kama vile Ebr. 4: 15-16)
4. huleta uzima wa milele (kama vile Ebr. 5: 9-10)

5. anaomba kwa niaba ya waamini kama vile Ebr. 7:25; 9:24)
6. hutoa ujasiri kumkaribia Mungu Mtakatifu (kama vile Ebr. 10: 19-21)

■"ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake" Hili neno neno "suluhu" limetumika kwenye tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania kwa ajili kitu cha rehema (kifuniko) juu ya sanduku la Agano kwenye Patakatifu pa Patakatifu. Hata hivyo, kilikua ni kidokezo cha Kiyunani cha kuituliza miungu iliyokasilika, hivyo kuondoa vizuizi kati ya "miungu"na mwanadamu. Kwa sababu ya matumizi ya tafsiri ya kisasa ya neno linalochanganya juu ya kidokezo kinachomrejelea YHWH (kama vile.toleo la RSV na NJB) na kulitafsiri kama "fidia kosa." Yesu anaileta kwa pamoja haki na rehema ya YHWH (kama vile 1 Yn. 2:2; 4:10). Hata hivyo, ni muhimu kuona hili kuwa si hasira ya uungu wa Agano la kale na upendo wa Yesu. Baba alimtuma mwana (kama vile Yn. 3:16). Mwana anawakilisha na kumuiga Baba.

**2:18"Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa"** Neno "aliteswa" ni kauli timilifu tendaji elekezi ya hali ya kuendelea ambayo kwamba inaongelea majaribu yanayoendelea kumkabili Yesu. Neno "alipojaribiwa" (*peirazō*) lina kidokezo cha kujaribiwa na mtazamo wa karibu na kuangamizwa (kama vile Ebr. 4:15; Mt. 4:1). Mwovu alijaribu kumwangamiza katika Kalvari, lakini Mungu alibadiri hii kuwa ushindi mkuu wa ukombozi.

## MADA MAALUMU: MANENO YA KIYUNANI YAHUSUYO JARIBU NA VIDOKEZO VYAKE

Kuna maneno mawili ya Kiyunani ambayo yana kidokezo kwa ajili ya kumjaribu mtu kwa kusudi fulani.

### 1. *Dokimazō, Dokimion, Dokimasia*

Neno hilini neno la mtu yule afuaye vyuma kwa ajili ya kujaribu uhalisia wa kitu fulani (yaani, kistiari mtu fulani) kwa moto (tazana Mada Maalumu: Moto). Moto hudhihilisha chuma halisi na huteketeza (yaani, husafisha) dongo la chuma. Kitendo hiki cha kifizikia kinakuwa nahau yenye nguvu kwa Mungu na/au Ibilisi na/au binadamu kuwajaribu wengine. Neno hili linatumika tu katika maana chanya ya kujaribu kwa kuangalia hadi kuufikia ukubalifu (tazama Mada Maalumu: Mungu Huwajaribu Watu Wake [Agano la Kale]).

Linatumika katika Agano la Kale kwa ajili ya

- a. Madume ya ng'ombe – Luka 14:19
- b. sisi wenyewe – 1 Kor. 11:28
- c. imani yetu – Yakobo 1:3
- d. hata Mungu –Ebr. 3:9

Matokeo ya majaribu hayajafikiriwa kuwa chanya (kama vile. Rum. 2:18; 14:22; 16:10; 2 Kor. 10:18; 13:3,7;

Flp. 2:27; 1 Pet. 1:7), hivyo, neno husilisha wazo la mtu aliyepimwa na kuhakikishwa

- a. kuwa wa thamani
- b. kuwa wazuri
- c. kuwa halisi
- d. kuwa wa maana
- e. kuwa wa kuheshimiwa

### 2. Peirazō, Peirasmus

Neno hili mara nyingi lina maana nyingine ya kupimwa kwa kusudi la utafutaji au ukataaji. Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu ya Yesu nyikani.

- a. Linabeba jaribio la kumtega Yesu (kama vile Mt. 4:1; 16:1; 19:3; 22:18, 35; Marko 1:13; Luka 4:2; Ebr. 2:18).
- b. Neno hili (*peirazōn*) linatumika kama wadhifa kwa Ibilisi katika Mt. 4:3; 1 The. 3:5 (yaani, "mjaribu").
- c. Matumizi
  - 1) Lilitumiwa na Yesu alipokuwa akiwaonya wanadamu kutomjaribu Mungu (kama vile Mat. 4:7; Luka 4:12, [au Kristo kama vile 1 Kor 10:9]).
  - 2) Pia linamaanisha jaribio la kufanya kitu fulani ambacho kimeshindikana (kama vile Ebr.11:29).

- 3) Linatumika katika maana nyingine kwa majoribu na masumbufu ya waamini (kama vile 1 Kor. 7:5; 10:9, 13; Gal. 6:1; 1 The. 3:5; Ebr. 2:18; Yakobo. 1:2, 13, 14; 1 Pet. 4:12; 2 Pet 2:9).

■ "aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa" ukweli huu huu unajirudia katika Ebr. 4:15. Yesu anajifungamanisha kikamilifu na watu wake wenye mahitaji (kama vile Ebr. 2:17)!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha njia ambazo maagano mapya ni makuu kwa maagano ya Musa.
2. Kwa nini mwandishi ametoa dondo mara kwa mara kutoka katika maagano ya Musa?
3. Ni kwa akina nani maonyo ya sura ya 2 yanawalenga?
4. Je 2:6-8 inarejelea kwa mwanadamu au Yesu?
5. Kwa nini Yesu aliteseka na kwa namna gani Wakristo wanaathiriwa kwa mateso?
6. Kulingana na mstari wa 14 je shetani ana nguvu za kifo juu ya Wakristo?
7. Orodhesha sababu za kwa nini Yesu alikuja.

## WAEBRANIA 3

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>                |  |   |   |   |
|---|--|---|---|---|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                                      | <b>NKJV</b>  | <b>NRSV</b>                                 | <b>TEV</b>  | <b>NJB</b>  |
| Yesu Mkuu juu ya Musa<br>3:1-6                              | Mwana wa Uaminifu<br>3:1-6   | Kristo ni mkubwa kwa Musa<br>3:1-6          | Kristo ni Mkuu kuliko Musa<br>3:1-6                                     | Kristo ni Mkuu kuliko Musa<br>3:1-6   |
| Pumziko la Watu Wa Mungu<br>(3:7-4:13)<br>3:7-11<br>3:12-19 | Kuwa Mwaminifu<br>3:7-15<br>Kushindwa kwa safari<br>Ya Jangwani<br>3:16-19 | Maonyo na Maelekezo<br>(3:7-4:13)<br>3:7-19 | Pumziko kwa Watu Wa Mungu<br>(3:7-4:13)<br>3:7-11<br>3:12-15<br>3:16-19 | Namna ya Kufikia Ardhi ya Mungu ya Pumziko<br>(3:7-4:13)<br>3:7-11<br>3:12-19 |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA WAEBRANIA 3:1-4:13**

- A. Sehemu hii inashughulika na ukuu wa Yesu juu ya viongozi pacha wa Agano la Musa, Musa na Haruni. Hii inatupelekea sisi katika mjadala wa wazi wa ukuhani wa Melkizedeki wa Ebr.4: 14-7: 28.
- B. Sehemu hii ni tamthiliya ya dhana mbili: (1) "nyumba ya Mungu," katika Ebr. 3: 1-6 (kama vile Hes. 12: 7-8; 2 Samweli 7) na (2) ile "inayobakia" katika Ebr. 3: 7-4: 13 (kama vile Zab. 95: 7-11).
- C. Hoja inakua kama ifuatavyo.
  1. Musa alikuwa sehemu ya nyumba ya Mungu, lakini Yesu alikuwa mjenzi wa nyumba
  2. Musa ni mtumishi katika nyumba wakati Yesu ni mwana katika nyumba
  3. Musa alishindwa kuleta pumziko wakati Yesu hakushindwa
- D. Msukumo wa kithiolojia wa kipengele cha kifasihi ni onyo kuwa mtii na mwaminifu, lakini Waisraeli hawakuwa. Agano la Musa lilikuwa na madhara kwa kutotii ambalo halikuwa na athari. Je ni zaidi kiasi gani madhara ya kukataa au kukaidi agano jipya (kama vile 2: 1-4)?
- E. Sehemu hii ni sehemu ya uanishaji. Nalitazama Agano Jipya kama jipya na safari ya kiroho!

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 3:1-6

<sup>1</sup>Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenyewe kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu, <sup>2</sup>aliyekuwa mwaminifu kwake ye ye aliyweweka, kama Musa naye alivyokuwa, katika nyumba yote ya Mungu. <sup>3</sup>Kwa maana huyo amehesabiwa kuwa amestahili utukufu zaidi kuliko Musa, kama vile ye ye aitengenezaye nyumba alivyo na heshima zaidi ya hiyo nyumba. <sup>4</sup>Maana kila nyumba imetengenezwa na mtu; ila ye ye aliyevitengeneza vitu vyote ni Mungu. <sup>5</sup>Na Musa kweli alikuwa mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu kama mtumishi, awe ushuhuda wa mambo yatakayonenwa baadaye; <sup>6</sup>bali Kristo, kama mwana, juu ya nyumba ya Mungu; ambaye nyumba yake ni sisi, kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho.

3:1

NASB, NKJV "ndugu watakatifu"

NRSV "ndugu wa kike na wakiume"

TEV "Rafiki zangu Wakristo"

NJB "ndugu watakatibu"

Je kwa nani kitabu hiki kinaandikwa? Neno "ndugu" linatumika kwa kurudia rudia (kama vile Ebr. 2: 11; 3:1,12; 10:19; 13:22) ambalo (pamoja na mada) linamaanisha waaminio wa Kiyahudi.

□"kuushiriki mwito wa mbinguni" Dhana hii inatumika katika Biblia kwa namna kadhaa.

1. Israeli iliitwa na Mungu kuwa ufalme wa kikuhanu kuurejesha ulimwengu tena kwa Mungu (kama vile Mwanzo 12:3; Kut.19: 5). Katika Agano la Kale hii iliitwa huduma, sio wokovu wa mtu mmoja mmoja na wito wa pamoja wa kijamii (wa taifa la Israeli ) kwa jukumu walilojipangia (uinjilishaji wa ulimwengu).
2. Waaminio mmoja mmoja wanapewa wito (kama vile Yohana 6:44, 65) kuelekea wokovu wa milele.
3. Kila mkristo mmoja mmoja anaitwa kutumikia mwili wa Kristo kuitia kipawa cha kiroho (kama vile 1 Kor. 12: 7, 11).

### MADA MAALUMU: KUITWA

Siku zote Mungu anachukua uwezo wa kuanzisha jambo katika mwito, uchaguzi, na akiwatafuta waumini waje kwake (kama vile. Yohana 6:44, 65; 15:16; 1 Kor. 1:1-2; Efe. 1:4-5, 11). Neno "kuitwa" limetumika kwa maana nyingi za kithiolojia.

- A. Katika Agano la Kale "uitaji wa jina" mara nyingi ulikuwa katika mazingira ya kuabudu (kama vile. Mwa. 4:26; 12:8; 21:33; 26:25; Kut. 34:5).
- B. Wenyewe dhambi wanaitwa kwenye wokovu kwa neema ya Mungu (yaani, Kut. 34:6-7) kuitia katika kazi aliyoimaliza Kristo na kwa kusadikishwa na Roho (yaani, *klētos*, kama vile. Rum. 1:6-7; 9:24, ambayo kithiolojia inafanana na 1 Kor. 1:1-2 na 2 Tim. 1:9; 2 Petr. 1:10).
- C. Wenyewe dhambi wanaliitia jina la Bwana ili waokolewe (yaani, *epikaleō*, kama vile. Mdo. 2:21; 22:16; Rum. 10:9-13). Maelezo haya ni nahahu ya Kiyahudi katika taratibu za kuabudu.
- D. Waumini huliita jina lake nyakati za migogora na msongo wa mawazo (yaani, Mdo.7:59).
- E. Waumini wameitwa kuishi maisha yanayomfanana Yesu i.e., *klēsis*, kama vile. 1 Kor. 1:26; 7:20; Efe. 4:1; Fil. 3:14; 2 The. 1:11; 2 Tim. 1:9).

Waumini wameitwa kwenye kazi ya huduma (kama vile. Mdo. 13:2; 1 Kor. 12:4-7; Efe. 4:1).

□"mtafakarini Yesu" Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Inamaanisha kufikiria kiundani (kama vile Ebr. 10: 24).

Katika muktadha huu inamaanisha kulinganisha nafsi Yake na kufanya kazi na viongozi wa agano la Musa.

■ "Mtume na Kuhani Mkuu" Majina haya mawili yanashughulikia ukoo wa Yesu juu ya Musa kama mjumbe rasmi na Haruni kama kuhani mkuu wa kilawi. Sura ya 3 na 4 zinashughulikia ukoo wa Yesu juu ya Haruni. Kwakuwa neno la Kiyunani kwa ajili ya "mjumbe" na "malaika" yanafanana, "mtume," ambalo lilikuwa ni neno la Kiyunani "kutuma," linaweza kuhusiana na vyote malaika waliotumwa na Mungu kuwatumikia wale wanaookolewa (kama vile Ebr. 1: 14) na kwa Yesu alitumwa na Mungu kukomboa wale wanaookolewa (kama vile Yohana 3:17). Hii ni sehemu pekee katika Agano Jipyä kwamba Yesu anaitwa "mtume," ingawa Yohana anatumia kitenzi juu na juu ya kurejerea kwake yeche kuwa "kutumwa" kutoka kwa baba (kama vile Yohana 3:17, 34; 5: 36, 38; 6:29, 57; 7:29; 8:42; 10: 36; 11: 42; 17:3,18, 21, 23, 25; 20: 21).

■ "Mtume" Hii inakuja kutoka kitenzi "kutuma" (angalia [Mada Maalum: Kutuma \(apostellō\)](#)) na ilitumika na walimu mwa kiyahudi kwa namna ya mtu kutumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine. Musa alitumika katika nyumba ya Mungu kama mtumwa wakati Yesu alikuwa "mwana," mwana familia. Mungu alimuita Musa kutumikia lakini alimtuma Yesu kutoka mbinguni.

■ "Kuhani Mkuu" Waebrania ni kitabu pekee cha Biblia kumuita Yesu kuhani mkuu (kama vile Waebrania 2:17; 3: 1; 4: 14, 15; 5: 5, 10; 6: 20; 7:26, 28; 8: 1,3; 9:11; 10: 21). Inagharimu hoja pana ya kisheria kushawishi wayahudi wa karne ya kwanza kwamba Yesu, kutoka kabila la Yuda kweli alikuwa kuhani. Jamii ya magombo ya bahari ya chumvi walitarajia Masihi wawili, mmoja wa kifalme (kabila la Yuda) na mmoja wa kikuhani (kabila la Lawi, kama vile Zab.110; Zekaria 3-4).

■ "maungamo yetu" Hili ni neno la Kiyunani homologia, ambalo ni ambatani ya "kusema" na "kile kile." Wasomaji walikuwa wameshafanya ukiri wao katika Yesu Kristo. Sasa sharti washikilie sana ukiri/maungamo (kama vile Ebr.4:14; 10:23). Hii ni moja ya jambo kubwa katika Kitabu.

## MADA MAALUMU: KUTUBU (AGANO JIPYA)

Toba (sambamba na imani) ni hitaji la pande zote mbili yaani Agano la Kale (Nacham, BDB 636, KB 688, mf., Kut. 13:17; 32:12,14; Shuv, BDB 996, KB 1427, m.f. 1 Flm. 8:47; Eze. 14:6; 18:30; tazama [Mada Maalumu: Toba \[Agano la Kale\]](#)) na Agano Jipyä.

1. Yohana Mbatizaji (Mt. 3:2; Marko 1:4; Luka 3:3,8)
2. Yesu (Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3)
3. Petro (Matendo 2:38; 3:19; 8:22; 11:18; 2 Petro. 3:9)
4. Paulo (Matendo 13:24; 17:30; 20:21; 26:20; Rum. 2:4; 2 Kor. 2:9-10)

Lakini Toba ni nini? Ni huzuni ya kiroho? Ni kumaanisha kuacha dhambi? Eneo zuri katika Agano la Jipyä katika kuelewa maana tofauti ya dhana hii ni 2 Wakorintho 7:8-11, ambapo hizo tatu zinanahusiana, lakini ni tofauti, maneno ya Kiyunani yanatumiika.

1. "huzuni" (*lupeō*, kama vile. mst. 8 [mara mbili], 9 [mara tatu], 10 [mara mbili], 11). Inamaanisha kupata maumivu au kutambua na ina maana ya kitheolojia isiyofungamana na upande wo wote.
2. "toba" (*metanoeō*, kama vile mst. 9,10). Ni muunganiko wa neno "baada ya" na "kumbukumbu," ambayo inadokeza akili mpya, njia mpya ya kufikiri, mtazamo mpya kuhusu maisha na Mungu. Hii ni toba ya kweli.
3. "majuto" (*metamelomai*, kama vile mst. 8 [mara mbili], 10). Ni muungano wa "baada ya" na "uangalifu." Linatumika juu ya Yuda katika Mt. 27:3 and Esau katika Ebr. 12:16-17. Linadokeza sikitiko juu ya matokeo, si juu ya matendo. Toba na imani ni matendo ya kimaagano yanayohitajika (kama vile Marko 1:15; Matendo 2:38,41; 3:16,19; 20:21). Kuna baadhi ya maandiko ambayo yanadokeza kwamba Mungu hutoa toba (kama vile Matendo 5:31; 11:18; 2 Tim. 2:25). Lakini maandiko mengi yanatalizama hili kama mwitikio muhimu wa agano la mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu ya wokovu huru.

Maelezo ya maneno yote ya Kiebrania na Kiyunani yanahitajika ili kuelewa maana kamili ya toba. Neno la Kiebrania linadai "mabadiliko ya tendo," ambapo neno la Kiyunani linadai "mabadiliko ya akili." Mtu aliyeokolewa anapokea akili na moyo mpya (kama vile Eze. 36:26-27). Anafikiri tofauti na kuishi tofauti. Badala

ya "Kilicho ndani ni kwa ajili yangu?" sasa swalni "Mapenzi ya Mungu ni nini?" Toba si hisia ambazo hufifia au dhambi ya moja kwa moja, bali uhusiano mpya na Aliye Mtakatifu ambaye humbadilisha mwamini kwa uendelelevu na kuwa ni ya utakatifu. Si rahisi mtu akasitisha kufanya kitu au kuachana nacho, bali ni kwa mtazamo na uelekeo mpya katika maisha. Anguko linatusabisha sisi kujitazama wenyewe lakini injili inaturuhusu sisi kumtazama Mungu. Toba ni tendo la kugeuka na imani ni tendo la kugeukia kitu/kifikra!

**3:2"aliyekuwa mwaminifu kwake ye ye aliyemweka"** Katika muktadha msisitizo upo juu ya (1) Baba kuchagua na kumuwezesha Yesu kwa ajili ya jukumu la kiukombozi (kama vile Marko 3:14) na (2) Yesu kufanya kazi imani (wakati uliopo endelevu) ikatika Baba kama waaminio wanatakiwa kufanya kazi imani. Yeye hakika ndiye. Hatahivyo, moja inayowezekana kwa ajili ya "kuteuliwa" ni "kuumba." Arius alitumia kitenzi kitenzi "kuteuliwa" katika utata wake pamoja na Athanasius kuelezea kwamba Yesu alikuwa uumbaji wa Juu kupita wote (kama vile Mithali 8: 22) ya Mungu, lakini sio Mungu ye ye mwenyewe (kama vile Mdo.2:36; Rum. 1:4; Kol.1:15). Huu mkanganyiko wa karne ya nne ilizalisha mafundisho halisia ya umuhimu wa kiungu, lakini udhihirisho m-tatu wa kinafsi wa milele, Baba,. Mwana na Roho (Utatu). Hizi nafsi zote tatu za kiungu kimilele zinaunda mjadala wa Arianism (kama vile Yohana 1:1-18). Kwa mjadala mzuri mfupi wa Arianism, *angalia Christian Theology* (Toleo la Pili) cha Millard J. Erickson, ukurasa wa 711-715.

■"**nyumba Yake yote**" Hii ni rejea ya Hes. 12:7, 8. Watu wa Mungu kuwa katika nyumba ya Mungu ni sitiari inayojirudia rudia ya Kiblia (kama vile Ebr. 3: 6, "nyumba," Gal. 6:10; 1 Tim. 3:15; "nyumba ya kiroho," 1 Pet. 2: 5; "nyumba ya Mungu," 4: 17). "Nyumba" inatumika mara sita katika aya hii, wakati mwingine pamoja na visawe vya ujenzi na wakati mwingine familia. Hoja inaonekana kuwa kama ifuatavyo

1. Musa alikuwa sehemuya nyumba ya Mungu lakini Yesu alikuwa mjenzi wa nyumba hiyo
2. Musa ni mtumishi wakati Yesu ni mwana wa familia
3. Musa alishindwa kuleta pumziko la Mungu wakati Yesu hatashindwa

**3:3"alihesabiwa heshima zidi ya utukufu kuliko Musa"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu. Hii ingekuwa kauli ya kushangaza kwa Wayahudi (kama vile 2 Kor.3:7-11).

**3:4"Maana kila nyumba imetengenezwa na mtu"** Hii imetumika kwa ajili Kifalsafa/kithiolojia "sababu ya kilele" katika jaribio la kuthibitisha uwepo wa Mungu (kama vile Thomas Aquinas). Hatahivyo mstari huu wa kimantiki ("dhamira ya kwanza") haiwezi kamwe kufika katika ufunuo wa Mungu Baba wa Bwana Yesu Kristo, wala Mungu kama rafiki wa wenyewe dhambi.

■"**ila ye ye aliyevitengeneza vitu vyote ni Mungu**" Baba ni muumbaji wa wote (kama vile Rum. 11:36; 1 Kor.15: 25-27). Yesu alikuwa msaidizi wa Baba katika uumbaji (kama Yohana 1: 3; 1 Kor. 8: 6; Kol. 1: 16; Ebr.1: 2). 3:5-6 "lakini Kristo alikuwa mwaminifu kama Mwana juu ya nyumba Yake" Yesu Mwana (hakuna kiambata, Kama vile Ebr. 1: 2; 3: 6; 5: 8; 7: 28) inalinganishwa na Musa, mtumishi (kama vile Ebr. 1: 2; 3: 5; 5: 8; 7: 28; Kut. 14: 31; Hes.12:7). Musa alikuwa mtumishi mwaminifu (kama vile Hes. 12: 7), lakini Yesu alikuwa Mwana wa familia!

**3:5** Musa alimzungumzia Kristo katika Kumb.18: 18-19 (kama vile 1 Pet. 1: 11). Hii inarudia juu ya ukweli wa Ebr.1:1.

**3:6 "ambaye nyumba yake ni sisi"** Hii ni familia ya imani inayoelezewa kama nyumba (kama vile Gal. 6:10; 1 Ti m. 3:15; 1 Pet. 2:5; 4:17). Aina hii hii ya ujenzi wa pamoja wa kisitiari unatumiwa wakati kanisa linapoitwa hekalu (kama vile 1 Kor. 3:16). Shabaha iko kwenye (1) umiliki wa Yesu na (2) watu wa Mungu kama chombo cha pamoja.

Sio kawaida kuzungumzia kanisa kama nyumba ya Yesu. Kwasababu ya hii baadhi ya maandiko ya kale ilibadilisha kiwakilishi ili kwambailirejeree kwa Baba (kama vile MSS P<sup>46</sup> na D\*).

■"**kama**" Hii ni sentensi daraja la tatu yenyeye masharti ambayo inamaanisha kitendo kinachoweza kutokea (pamoja na tegemezi). Hii inaipa kauli kiashiria cha utegemezi (kama vile Ebr.3:14; 4:14; Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2).

■ "tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu" "kushikilia sana" ni msisitizo endelevu wa ustahimilivu (kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu, kama vile Ebr. 3:14; 4:14, angalia Mada Maalum katika Ebr. 4: 14). Yanayobakia ya sura hii na Sura ya 4 ni moja ya mwendelezo wa maonyo (1) kwa waaminio wa Kiyahudi kuelekea katika ukomavu na (2) kwa wale waliokwisha sikia injili na kuiona kuwa ni yenye nguvu katika maisha ya marafiki zao wa Kiyahudi waaminio kuikubali kikamilifu wao wenyewe.

■ "kujivunia tumaini letu" Msisitizo huu jii ya tumaini ni tabia ya Waebrania (kama vile Waebrania 3:6; 6:11; 7:19; 10:23; 11:1). Tumaini linarejerea kwa utimilishwaji wa imani yetu!

## MADA MAALUM: TUMAINI (*elpis*, kwa Paulo)

Paulo alilitumia neno hili mara nyingi kwa namna tofauti lakini katika maana zinazoshabihiana. Mara nyingi lilihusiana na utimilifu wa imani ya waamini (mfano., 1 Tim. 1:1). Hili laweza kuellezewa kama utukufu, maisha ya milele, hatma ya wokovu, ujio wa mara ya pili, n.k. Utimilifu huu unajulikana, bali sula la muda ni mbeleni na halijulikani. Tumaini mara nyingi lilihusiana na "imani" na "upendo" (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16). Orodha ya muda ya baadhi ya matumizi ya Paulo ni:

1. Ujio wa mara ya pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tit. 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1 (Mungu ni tumaini letu, 1 Tim. 5:5; 1 Pet. 3:5)
3. Waamini kuwasilishwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 The. 2:19
4. Tumaini likewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Imani katika injili, Kol. 1:23; 1 The. 2:19
6. Hatma ya wokovu, Kol. 1:5; 1 The. 4:13; 5:8
7. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2, 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
8. Wokovu wa watu wa mataifakupitia Kristo, Kol. 1:27
9. Uhakika wa wokovu, 1 The. 5:8
10. Maisha ya milele, Tit. 1:2; 3:7
11. matokeo ya ukomavu wa Mkristo, Rum. 5:2-5
12. ukombozi wa uumbaji wote, Rum. 8:20-22
13. kukubali utimilifu, Rum. 8:23-25
14. wadhifa wa Mungu, Rum. 15:13
15. shauku ya Paulo kwa waamini, 2 Kor. 1:7
16. agano la Kale kama mwongozo wa waamini wa Agano Jipy, Rum. 15:4

■ "mpaka mwisho" Tungo hii haitoeki katika maandiko ya kale ya Kiyunani P<sup>46</sup> au B na, hivyo inawezekana sio asili. Hatahivyo, inajumuishwa katika maandiko ya kale ya Kiyunani (K, A, C, D, K, na P). Inajumuishwa katika Ebr.3:14 na inawezekana ikahamishiwa hapa na mwandishi kwa ajili ya kusudi la uwiano. Hakika inashabihiana na thiolojia ya muktadha. Angalia Mada Maalum katika Ebr.7: 11.

## ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 3:7-19 (aya kamili inajumuisha 3:7-4:13)

<sup>7</sup>Kwa hiyo, kama anenavyo Roho Mtakatifu,

"Leo, kama mtaisikia sauti yake,

<sup>8</sup>Msifanye migumu mioyo yenu,

Kama wakati wa kukasirisha,

Siku ya kujaribiwa katika jangwa,

<sup>9</sup>Hapo baba zenu waliponijaribu,

wakanipima, Wakaona matendo yangu miaka arobaini.

<sup>10</sup>Kwa hiyo nalichukizwa na kizazi hiki, Nikasema,

Sikuzote ni watu waliopotoka mioyo hawa; Hawakuzijua njia zangu;

<sup>11</sup>Kama nilivyoapa kwa hasira yangu, Hawataingia rahani mwangu."

<sup>12</sup>Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. <sup>13</sup>Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. <sup>14</sup>Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho;

<sup>15</sup> hapo inenwapo,

“Leo, kama mtaisikia sauti yake,

Msifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha.”

<sup>16</sup>Maana ni akina nani waliokasirisha, waliposikia?

Si wale wote waliotoka Misri wakiongozwa na Musa? <sup>17</sup>Tena ni akina nani aliochukizwa nao miaka arobaini?

Si wale waliokosa, ambao mizoga yao ilianguka katika jangwa? <sup>18</sup>Tena ni akina nani aliowaapia ya kwamba hawataingia katika raha yake, ila wale walioasi? <sup>19</sup>Basi twaona ya kuwa hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao.

**3:7"kama anenavyo Roho Mtakatifu"** Hii inaelezea uvuvio wa Agano la Kale kwa Roho Mtakatifu. Katika muktadha hii ni muhimu sana kwasababu maandiko yanamuelezea Baba katika Ebr. 1:5,13; 2:6, 11;4:3, 4;10: 9; 13:5. Hivyo hiki ni kifungu chenye nguvu juu ya Uuungu na nafsi ya Roho (Angalia [Mada Maalum: Utu wa Roho](#), kama vile Ebr.9: 8; 10:15).

## MADA MAALUMU: UTATU

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno “utatu,” kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

- A. Injili
  - 1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
  - 2. Yohana 14:26
- B. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39
- C. Paulo
  - 1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
  - 2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
  - 3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
  - 4. Gal. 4:4-6
  - 5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
  - 6. 1 The. 1:2-5
  - 7. 2 The. 2:13
  - 8. Tit. 3:4-6
- D. Petro – 1 Pet. 1:2
- E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

- A. Matumizi ya uwingi kumuhusu Mungu
  - 1. Jina Elohim liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
  - 2. “Sisi” katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7
- A. “Malaika wa Bwana” (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
  - 1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
  - 2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
  - 3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  - 4. Zakaria 3:1-2
- B. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14
- C. Mungu (YHWH) na Masihi (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12

D. Masihi na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10

E. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
2. Origin-aliihusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
4. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhihilisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelizewa na maneno ya Kibiblia.

1. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)
2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Constantino
3. Mafundisho ya Uungu yameelezewa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipyä linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja) ikiwa na udhihirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho)

■ "Leo, kama mtaisikia sauti yake," Mistari ya 7-11 ni nukuu kutoka Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani ya Zab.95: 7-11, ambalo ni onyo kwa Israeli wakati wa safari ya jangwani dhidi ya kutokuamini. Waebrania 3:17 mpaka 4: 13 imejikita katika maelezo ya kifungu hiki. Hii ni sentensi daraja la tatu yenye masharti. Walikuwa na fursa ya kuona na kusikia (kama vile Ebr.3: 9) lakini kwa kupenda walikataa na kufanywa mioyo migumu.

3:8 "Msifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha" Maelezo ya kihistoria ni kwa kipindi cha safari ya Jangwani ya Israeli. Maandiko ya Kiebrania ya Kimasoteri yanaorodhesha maeneo ya kijiografia ya uasi wa Israeli kama *Meribah* (kama vile Kut.17:7; Hes.20:13) na *Massah* (kama vile Kut. 17: 7; kama vile Kumb. 6: 16). Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani inayatafsiri yenye kwa asilia yao (*Meribah*—sehemu ya ugomvi na *Massah*—majaribu, kama vile Ebr. 3:9).

Neno "moyo" linarejea mtu mzima kamili (kama vile Kumb. 6:4-5). Wana wa Israeli hawa mwanzoni walikuwa na imani lakini baadaye hawakufanya kazi imani (yaani taarifa ya wapelelezi 12, kama vile Hes.12). Matokeo yake walikuwa hawaruhusiwi kuingia Nchi ya Ahadi.

## MADA MAALUMU: MOYO (AGANO JIPYA)

Neno la Kiyunani *kardia* limetumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani na Agano Jipyä kuashiria neno la Kiebrania lëb (BDB 523, KB 513). Limetumika kwa njia tofauti kadhaa (kama vile. Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, *A Greek-English Lexicon*, 2nd ed. kur. 403-404).

1. Kitovu/Kituo cha maisha ya kimwili, neno mbadala kwa mtu (kama vile. Matendo 14:17; 2 Kor. 3:2-3; Yakobo 5:5)
2. Kitovu cha maisha ya kiroho (yaani, adilifu)
  - a. Mungu anatujua mioyo (kama vile. Luka 16:15; Rum. 8:27; 1 Kor. 14:25; 1 The. 2:4; Ufu. 2:23)
  - b. Imetumika kwa maisha ya kiroho ya mwanadamu (kama vile. Mt. 15:18-19; 18:35; Rum. 6:17; 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 2:22; 1 Pet. 1:22)
3. Kitovu cha maisha ya kifikra (yaani, uwezo wa kufikiri, kama vile. Mt. 13:15; 24:48; Matendo 7:23; 16:14; 28:27; Rum. 1:21; 10:6; 16:18; 2 Kor. 4:6; Efe. 1:18; 4:18; Yakobo 1:26; 2 Pet. 1:19; Ufu. 18:7; moyo ni sawa na mawazo katika 2 Kor. 3:14-15 na Flp. 4:7)
4. kitovu cha maamuzi binafsi (yaani, matakwa, kama vile Mdo. 5:4; 11:23; 1 Kor. 4:5; 7:37; 2 Kor. 9:7)
5. Kitovu cha hisia za ndani (kama vile. Mt. 5:28; Mdo. 2:26,37; 7:54; 21:13; Rum. 1:24; 2 Kor. 2:4; 7:3; Efe. 6:22; Flp. 1:7)
6. Mahali pa pekee kwa shughuli za kiroho (kama vile. Rum. 5:5; 2 Kor. 1:22; Gal. 4:6 [yaani, Kristo katika

- mioyo yetu, Efe. 3:17])
7. Moyo ni njia mbadala ya ki-sitiari ya kumrejere ya mtu (kama vile. Mt. 22:37, kwa kunukuu Kumb. 6:5). Mawazo, sababu, na matendo vikichangia kikamilifu kwenye moyo kubainisha kikamilifu mtu alivyo. Agano la Kale lina baadhi ya matumizi ya maneno ya kushangaza.
    - a. Mwa. 6:6; 8:21, "Mungu alihuzunishwa katika moyo," pia tazama Hosea 11:8-9
    - b. Kumb. 4:29; 6:5; 10:12, "kwa moyo wako wote na nafsi yako yote"
    - c. Kumb. 10:16; Yer. 9:26, "Roho zisizo na tohara" na Rum. 2:29
    - d. Ezek. 18:31-32, "moyo mpya"
    - e. Ezek. 36:26, "moyo mpya" dhidi ya "moyo wa jiwe" (kama vile Ezek. 11:19; Zak. 7:12)

■"Kama wakati" Huu hapa ni mfano wa neno la Kiebrania "yom" inayotumika kwa namna ya mafumbo (kama vile Yohana 8: 56; Ebr. 8:9), sio katika namna ya ubayana wa kipindi cha masaa 24.

## MADA MAALUM: SIKU (YOM BDB 398, KB 399)

Nadharia za maana ya *yom* (siku) ikichukuliwa na kufanyiwa kazi na Dr. John Harris' (Mnadhimu wa School of Christian Studies na Profesa wa Agano la Kale katika chuo cha East Texas Baptist ) OT Survey I Notebook:

1. Nadharia ya kipindi cha masaa 24 ya uhalisia

Hii ni nadharia inayoleta mkabiliano wa moja kwa moja (kama vile Kutoka 20:9-11). Maswali yanayotokana na mbinu hii:

- a. ilikuwaje kukawa na nuru siku ya kwanza ambapo jua lilikuwa bado halijaumbwa mpaka siku ya nne?
- b. Ni kwa namna gani wanyama wote (hasa wale watokao sehemu zingine za ulimwengu) waliweza kupewa majina wote ndani ya siku moja? (kama vile Mwanzo. 2:19-20)?

2. Nadharia ya Umri-wa siku

Nadharia hii ianajaribu kupatanisha sayansi na maandiko (hasa jiolojia) pamoja na maandiko. Nadharia hii inasema kwamba "siku" zilikuwa "nyakati/umri wa kijiolojia" kwa urefu. Urefu wake si sawasawa na unakisia tabaka mbalimbali zinazoelezewa katika mfumo unaofanana kijiolojia. Wanasyansi wanafanya kukubaliana na ukuaji wa jumla wa Mwanzo 1: mvuke na aga la maji lilitangulia kutenganishwa kwa ardhi na maji kabla ya kutokea kwa uhai/maisha. Maisha ya mimea ya kondeni yalikuja kabla ya maisha ya wanyama na binadamu aliwakilisha mfumo wa kisasa na ulio mgumu zaidi. Maswali yanayoibuka kutoka katika mbinu hii:

- a. Ni kwa namna gani mimea iliweza kuishi kwa "miaka" bila kuwepo kwa jua?
- b. Mchavusho uliwezaje kufanyika katika mimea ikiwa wadudu na ndege walikuwa bado hawajaumbwa mpaka "miaka mingi" laterbaadaye?

3. Nadharia ya mbadilishano wa Nyakati-Siku

Siku kusema ukweli ni kipindi cha saa 24, lakini kila siku ikitenganishwa na miaka/zama ambazo kila kilichoumbwa kilikua. Maswali yanayoibuka kutoka katika mbinu hii.

- a. Matatizo hayohayo yanaibuka katika nadharia ya Siku-Nyakati.

- b. Je andiko linaonesha "siku" kutumika kote kote kama saa 24 na kama nyakati?

4. Nadharia ya uumbaji endelevu-machafuko

Nadharia hii inaenda namna hii: Kati ya Mwanzo. 1:1 na 1:2, kulikuwa na kipindi ambapo nyakati za kijiolojia zilitokea; wakati wa kipindi hiki, viumbe vyta kabla ya historia katika utaratibu vilipendekezwa na mabaki ya viumbe hai yakaumbwa; karibia miaka 200,000 iliyopita, baa kubwa la kimiujiza lilitukia na kuaribu maisha katika sayari hii na kufanya wanyama wengi baadaye siku za Mwanzo 1 ikatukia. Nyakati hizi zinamaanisha kuumbwa upya, kuliko uumbaji wa asili.

5. Nadhari ya Edeni pekee

Simulizi za uumbaji inamaanisha uumbaji tu na vipengele vya kimwili vya Bustani ya Edeni.

6. Nadharia ya Ombwe

Kulingana na Mwanzo 1:1, Mungu aliumba ulimwengu mkamilifu. Kulingana na Mwanzo 1:2, Lusifa (Shetani) alikuwa amewekwa zamu ya kusimamia ulimwengu wote na akaasi. Hivyo Mungu alihukumu Lusifa na

ulimwengu kwa uharibifu wa kushangaza. Kwa miaka mingi mamilioni, ulimwengu uliachwa peke yake na nyakati za Biblia zilipita. Kulingana na Mwanzo 1:3-2:3, katika 4004 k.k., siku sita za kawaida za masaa 24 za uumbaji upya zilitokea. Askofu Ussher (1654 b.k) alitumia vizazi vya Mwanzo 5 na 11 kupiga hesabu na tarehe ya uumbaji wa mwanadamu ca. 4004 k.k Hata hivyo, vizazi haviwakilishi utaratibu kamili wa mfuatano.

#### 7. Nadharia ya Wiki takatifu

Mwandishi wa kitabu cha Mwanzo alitumia dhana ya siku na wiki kama mbinu ya kifasihi ili kuweka sawa ujumbe wake wa kiungu wa shughuli za ki-Mungu katika uumbaji. Muundo wa namna hiyo unaelezea uzuri na mlingano wa kazi ya uumbaji na ubunifu wa Mungu.

#### 8. Uanzishwaji rasmi wa Hekalu la Ki-ulimwengu

Katika maoni ya hivi karibuni ya John H. Walton, *The Lost World of Genesis One*, IVP. 2009, ambayo yanaona siku sita kama "elimu ya viumbe hai inayofanya kazi, na sio ya kawaida ya kushikika. Wanamuelezea na kumfunua Mungu kwa mfululizo au kuweka rasmi ulimwengu ufanyao kazi kwa ajili ya wema wa mwanadamu. Hii inashabihiana na elimu juu ya ulimwengu ya kale. Kwa mfano siku za kwanza tatu zingemwalikisha Mungu anayetoa "majira (yaani muda)," "hali ya hewa (yaani kwa mazao)" na chakula. Tingo inayojirudia "ni vyema" ingeweza kumaanisha hali ya ufanyaji kazi.

Siku ya saba ingermuelezea Mungu akiingia katika "hekalu la kiulimwengu" linalofanya kazi asilimia mia moja na lisiloishiwa na mtu kama mmiliki halali mwenyewe, mwendeshaji na mwongozaji. Mwanzo 1 haina kitu kinachohusiana na uumbaji wa vitu vinavyoonekana vya uumbaji wa maada lakini kwa kuweka utaratibu wa maada hiyo kwa ajili ya nafasi ifanyayo kazi kwa ajili ya Mungu na mwanadamu kuwa na ushirika.

Hizi "Siku/nyakati" zinafanya chombo cha kifasihi cha kuzungumzia makubaliano ya jumla ya ANE(Ancient Near Easten - Mashariki ya Karibu ya Kale) ya kwamba:

- a. Hakuna utofautisho kati ya "asili" na "kilicho zaidi ya asili"
- b. Uungu unahusishwa katika kila kipengele cha maisha. Upekee wa Israeli haukuwa katika mtazamo wake wa kidunia wa kiujumla lakini katika vifuatavyo
  - 1) hali yake ya kuamini Mungu mmoja
  - 2) Uumbaji ulikuwa umelengwa kwa ajili ya wanadamu na sio kwa ajili ya miungu
  - 3) hakuna mgogoro kati ya miungu au miungu na ubinadamu katika taarifa ya Israeli.

Hakuazima uumbaji wake kutoka kwa wengine lakini walishirikisha mtazamo wao wa kiulimwengu. Neno "siku" mara nyangi hurejlea mduara wa masaa 24 ya mzunguko wa dunia (yaani., Kut. 20:9-10), lakini yaweza kurejlea kipindi cha muda usiojulikana (kama vile Mwa. 2:4; 5:2; Ruth 1:1; Zab. 50:15; 90:4; Wimb. 7:14; Isa. 4:2; 11:2; Zak. 4:10).

**3:9"waliponijaribu, wakanipima,"**Neno "kujaribu" katika Ebr. 3:8 na neno "jaribu" katika Ebr. 3: 9 ni Andiko la Masoteri ambayo ni "meribah" na "massah," Maeneo mawili ya kijiografia yanayotajwa katika Kut. 17: 1-7 ambapo Israeli aliasi dhidi ya Mungu.

Katika tafsiri za Kiyunani maneno tofauti kwa "jaribu" "kujaribisha" yanatumika. Ya kwanza (*peirazō*) siku zote lilikuwa na kisawe cha "kujaribu kwenye mtazamo wa kuelekea upotevuni" na ya pili (*dokimazō*) "kujaribu kwenye mtazamo wa kuelekea uthhibitisho," lakini katika muktadha huu yote yanafanana. Angalia Mada Maalum katika Ebr.2:18.

▣"**"Wakaona matendo yangu"** Namna ya Mungu kushughulikia wana wa Israeli kimiujiza wakati wa kipindi cha miaka arobaini cha safari ya jangwani haikuwaletea tumaini kamilifu. Mfano katika Luka 16 wa Lazaro na mtu tajiri unaunganishwa pamoja na Mt. 24: 24 unaonesha kwamba miujiza kimsingi sio iwe ni ishara ya Mungu wala chombo bora kwa kuweza kuwapata watu kuingia katika imani (kama vile jaribu la shetani kwa Yesu katika Mt. 4:3, 6).

▣"**"miaka arobaini"** Hesabu hii inatumika mara kwa mara katika Biblia. Lazima ni nahau ya Kiebrania kwa kipindi kirefu kisichojulikana. Ukweli ni kwamba, katika muktadha huu, inarejerea miaka 38 (kama vile Hes.14: 34).

Mwandishi wa Waebrania amerekebisha yote maandiko ya Kiebrania na maandiko ya Kiyunani ya Zaburi hii (mfano, nukuu ya Paulo ya Zab. 68:18 katika Efe. 4: 8) kwa kuunganisha "miaka arobaini" pamoja na Wana wa

Israeli kuona miujiza ya YHWH wakati wa kipindi cha safari ya Jangwani. Hatahivyo Maandiko ya kimasoteri na Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani linalinganisha tungo ya hasira ya YHWH kwa watu wakati wa kipindi hiki (kama vile Zab. 95: 10). Waandishi wa Agano Jipyä chini ya uvuvio mara kwa mara wanatafsiri Agano la Kale kwa matumizi ya maneno ya sheria ya Kiayahudi. Hii inaonekana kuvunja kujizatiti kwetu kwa kisasa kwa kusudio la kimamlaka kama njia sahihi ya kutafsiri Biblia. Lazima turuhusu waandishi wa Agano Jipyä matumizi sahaihi ya Agano la Kale katika njia ambayo ingekuwa sahihi kwa wafasiri wa kisasa. Hatuwezi kuzalisha upya mijongeo ya utafsiri wa maandiko ya waandishi waliovuviwa.

**3:10 "nalichukizwa na kizazi hiki"** Mfano mzuri wa hasira ya YHWHna hukumu inapatikana katika Hesabu 14: 11, 22-23, 27-30, 35.

▣"**kujuua**" Neno la Kiebrania lina kiashiria cha uhusiano wa kibinafsi (kama vile Mwa. 4: 1; Yer.1: 5), sio kweli tu kuhusu mtu au kitu. Imani ya Kibiblia ina vyote kiashiria cha ufahamu (kweli) na kipengele binafsi (tumaini).

▣"**njia zangu**" Kuna maneno yanayofanana katika Waembrania yanayorejere Sheria ya Mungu (kama vile Zab.19: 6-9; 119). Mapenzi ya Mungu yalikuwa wazi kwao (yaani waisraeli wa Agano la Kale), lakini kwa mapenzi yao wenyewe walikataa. Hili ilikuwa ni tatizo la wapokeaji wasioamini wa Kiyahudi. Ujumbe wa Yesu ulikuwa umebadilisha "njia za Mungu" (yaani Mt.5: 21-48; Marko 7: 19; 10: 5-6). Ilikuwa ngumu kwa waamini hawa wa Kiyahudi kumuacha Musa na kuamini kwa asilimia zote ujumbe wa Kitume wa "agano Jipyä" (yaani Yer.31: 31-34; Ezek. 36: 22-38) kutenganisha kabisa na utendaji wa kibinadamu!

## **MADA MAALUM: ISTILAHI KWA AJILI YA UFUNUO WA MUNGU (akitumia Kumbukumbu la Torati na Zaburi**

- I.     "Amri ya Serikali," BDB 349, "fanya kuwa sheria, tamko, au agizo"
  - A. JINSI YA KIKE, *רִנֵּסֶת* (KB, 346) – Kumb. 4:1,5,6,8,14,40,45; 5:1; 6:1,24; 7:11; 11:32; 16:12; 17:19; 26:17; 27:10; Zaburi 2:7; 50:16; 81:4; 99:7; 105:10,45; 148:6
  - B. JINSI YA KIUME, *רִנֵּסֶת* (KB, 347) – Kumb. 6:2; 8:11; 10:13; 11:1; 28:15,45; 30:10,16; Zab. 89:31; 119:5,8,12,16,23,26,33,48, 54,64,68,71,80, 83,112,124,135, 145,155,171
- II.    "Sheria," BDB 435, KB 1710, "maelekezo"
  - Kumb.1:5;4:44;17:11,18,19;27:3,8,26;28:58,61;29:21,29;30:10;31:9; Zaburi 1:2;19:7;78:10;94:12; 105:45;119:1,18,29,34,44,51,53,55,61,70,72,77,85,92,97,109,113,126,136,142,150,153,163,165,174
- III.   "Shuhuda" BDB 730, KB 790, "Sheria za ki-Ungu"
  - A. WINGI, *שׁוֹהֵד* – kumb. 4:45; 6:17,20; Zaburi 25:10; 78:56; 93:5; 99:7; 119:22,24,46,59,79,95,119,125,138, 146,152,167,16
  - B. שׁוֹהֵד – Zaburi 19:7; 78:5; 81:5; 119:2,14,31,36,88,99,111,129,144,157
- IV.    "Maagizo" BDB 824, KB 959, "Shitaka"
  - Zaburi 19:8;103:18;111:7;119:4,15,27,40,45,56,63,69,78,87,93,94,100,104,110,128,134,141,159,168,173
- V.     "Amri" BDB 846, KB 622
  - Kumb. 4:2,40; 5:29; 6:1,2,17,25; 8:1,2,11; 10:13; 11:13; 15:5; 26:13,17; 30:11,16; Zab. 19:8;119:6,10, 19,21,32,35,47,48, 60,66,73,86,96,98,115,127,131,143,151, 166,176
- VI.    "Hukumu/Maagizo," BDB 1048, KB 651, "maamuzi" au "haki"
  - Kumb. 1:17; 4:1,5,8,14,45; 7:12; 16:18; 30:16; 33:10,21; Zab. 10:5; 18:22; 19:9; 48:11; 89:30; 97:8; 105:5,7; 119:7,13,20,30,39,43,52,62, 75,84,102,106,120,137, 149,156,160,164; 147:19; 149:9
- VII.   "Ngia zake" BDB 202, KB 231, Mwongozo wa YHWH kwa maisha ya watu wake
  - Kumb. 8:6; 10:12; 11:22,28; 19:9; 26:17; 28:9; 30:16; 32:4; Zab. 119:3, 5,37,59
- VIII.   "Maneno yake"
  - A. BDB 182, KB 211 – Kumb. 4:10,12,36; 9:10; 10:4; 17:19; 18:19; Zab. 119:9,16,17,25,28,42,43,49, 57,65,74, 81,89,101,105,107,114,130,139,147, 160,161,169
  - B. BDB 57, KB 67

1. "Neno" – Kumb. 33:9; Zaburi 119:11,67,103,162,170,172
2. "Ahadi" – Zaburi 119:38,41,50,58,76,82,116,133,140,148,154
3. "Amri" – Zaburi 119:158

Haya yote yanarejerea ufunuo maalum Wake Mungu kwa Israeli. Kimsingi yanafanana. Angalia Mada Maalum: Uvuvio.

**3:11 "Kama nilivoopa kwa hasira yangu"** Ghadhabu ya Mungu ni kweli kibiblia kama ulivyo upendo wa Mungu. Lazima usemwe; hatahivyo kwamba yote ni sitiari za lugha ya kibinadamu kuuelezea uungu kwa kutumia hisia za kibinadamu na misamiati. Hakika zenyewe ni kweli kuhusu Mungu lakini si kilele. Mungu kwa utoshelevu amejifuna mwenyewe kwetu sisi lakini kuna mengi kuhusu Mungu ambayo ni kwamba hatuwezi kuyapokea wakati bado tupo nje ya uhalisia huu wa muda, wa mwili wa dhambi.

## MADA MAALUMU: LUGHA YA WANADAMU KUELEZEA UUNGU

- I. Aina hii ya lugha (yaani., Uungu kuelezewa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
  - A. Viungo vya mwili
    1. Macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zak. 4:10
    2. Mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
    3. Viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15
    4. Masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; 2 Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
    5. Uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
    6. Vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
    7. Sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
    8. Miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
    9. Umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
    10. Malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  - B. Matendo ya mwili (angalia mifano)
    1. Kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
    2. Kutembea (yaani., sauti ya)- Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
    3. Kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
    4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
    5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
    6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6
  - C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
    1. Majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
    2. Hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
    3. Wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
    4. Karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19
  - D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
    1. Baba
      - a. Wa Israel- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
      - b. Wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
      - c. Sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17
    2. Mzazi – Hosea 11:1-4
    3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)

#### 4. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

##### II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

- A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu. Hakuna misamiati mingine kuliko ile ya maneno ya kiulimwengu, ulioanguka. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni Roho!
- B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihilisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (Baba, Mama, Wazazi, Wapendwa)
- C. Ingawa ni muhimu kwa wakati mwingine (yaani., Mwa. 3:8), Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yejote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kut. 20; Kumbu. 5)
- D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-18).

III. kwa umakinika wa maelezo, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, ukurasa 10, "Tabia ya mwanadamu kwa Mungu," katika The International Standard Bible Encyclopaedia, kurasa za. 152-154

**3:12**

**NASB, NRSV,**

**NJB** "angalieni wapendwa"

**NKJV** "kuweni waangalifu"

**NJB** "kuweni waangalifu"

Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo; kuendelea kuwa makini! Sio tu mwanzo wa maisha ya imani ambayo ni muhimu bali pia mwisho (kama vile sura ya 11)!!!

**NASB, NKJV** "wapendwa"

**NRSV** "ndugu wa kike na wa kiume"

**NJB** "ndugu zangu"

Angalia dokezo katika Ebr.3:1. Maelezo haya yanaonekana kurejerea kwa Wayahudi waaminio, ingawa inaweza kuashiria ufananao wa uzao wa kibaba.

▣**"moyo mbovu wa kutokuamini"** Hii inaelezea mwamini anayemuacha Mungu aliye hai. Moyo unaoamini ni ume ambaa unaendelea thabiti mpaka mwisho (kama vile Ebr 3: 14 na sura ya 11). Tungo "moyo usioamini" inaaksi nahau ya Kiebrania "moyo wa kukosa imani" (kama vile Ebr. 4: 6), kama inavyokuwa "kuanguka," ambayo inaaksi Kiebrania shuv ("kurudi" au "geuka").

▣**"kwa kujitenga na Mungu aliye hai"** Hii ni kauli tendaji ya wakati uliopita usio timilifu yenye kitenzi jina. Kitendi hiki ni chanzo cha neno la Kingereza "ukanaji wa imani." Hii inazungumzia hali ya kukosa imani inayokua (ni kinyume cha Ebr.3:14). Kifungu hiki cha habari kinahusiana na nani: (1) Wayahudi waaminio au (2) Wayahudi wasioamini? Matumizi ya "ndugu" katika Ebr. 3: 1 na tungo iliyoongezwa "washiriki wa wito wa kimbingu" na "ndugu" katika Ebr. 3: 12 inarejerea kwa waaminio.

Ni nini basi ambacho onyo hili linahuasianisha: (1) wokovu au (2) uaminifu? Katika muktadha inaonekana inarejerea kwa uaminifu; Yesu alikuwa mwaminifu. Lazima wawe waaminifu. Waebrania inatazama maisha ya mkristo kutokea mwisho (kama vile Waebrania 3: 14), sio mwanzo (kama Paulo). Kule "kuanguka" kwa Ebr.3:13 lazima kuhusiane na imani endelevu na uaminifu. Wana wa Israeli walikuwa na imani lakini sio imani yenye kufannya kazi kwa bidii. Walikataa ahadi ya Mungu ya nchi itirikayo maziwa na asali kwa kukubaliana na taarifa ya wapelelezi (kama vile Hes. 13-14), sio imani yao kwa Mungu. Kwa muktadha huu "kuanguka" haimaanishi "kuanguka kutoka katika imani," bali "anguko la kutoka katika uaminifu"! Hatahivyo vyote vinahitajika kwa ajili ya imani yenye afya. Angalia dokezo katika Ebr.3:16-18.

Mungu siku zote hutujia katika uhusiano wa kiagano. Sharti tuitikie kwa imani na uaminifu. Mungu mwenye mamlaka ameturuhusu sisi kushiriki katika maamuzi yetu ya mwanzo na uanafunzi unaoendelea. Mwandishi wa Waembrania ni mgumu kumfuata kwasababu

1. anatumia mantiki za kisheria za kiyahudi na tafsiri ya maandiko
2. anazungumza na makundi mawili
  - a. Wayahudi waaminio
  - b. Wayahudi wasioamini
3. anatazama dhamana ya Mkristo na ushindi kutoka katika kigezo cha uaminifu na pia imani
4. anaweka shabaha yake kwenye uaminifu mpaka mwisho (kama vile Ebr. 4: 14; sura ya 11). Anayatazama maisha ya Mkristo kutoka katika mwisho wake na wala sio mwanzo.

Tungo "Mungu aliye hai" ni mbinu ya kiuandishi juu ya jina la Mungu wa Agano YHWH, ambayo inatoka katika kitenzi cha Kiebrania "kuwa" (kama vile Kut. 3:14). Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika Ebr. 2:7. Wasomaji hawa hawakuwa wanamkataa YHWH, bali kinyume chake ni kwamba walikataa injili ya Yesu Kristo ambayo kisema ukweli ni kukataliwa kwa YHWH (kama vile 1 Yohana 5: 9-12).

## **MADA MAALUMU: UKANAJI WA IMANI (APHISTĒMI)**

Neno la Kiyunani *aphistēmi* lina uwanja mpana wa elimu-maana. Hata hivyo, Neno la Kiingereza "uasi" limetokana na neno hili na athari za matumizi yake kwa wasomaji wa sasa. Muktadha, kama iliyo kawaida, ndio ufunguo, sio maelezo ya wakati uliopo.

Hili ni neno lililounganishwa kutokana na KIHUSISHI *apo*, ambacho kinamaanisha "kutokana na" au "mbali na" and *histēmi*, "kukaa," "kusimama," au "kupachika." Angalia matumizi yafuatayo (yasiyo ya kitheolojia):

1. kuondoa kimwili
  1. kutoka Hekaluni, Luka 2:37
  2. kutoka katika nyumba, Marko 13:34
  3. kutoka kwa mtu, Marko 12:12; 14:50; Matendo 5:38
  4. kutoka katika vitu vyote, Mat. 19:27,29
2. kuondoa kisiasa, Matendo 5:37
3. kuondoa kimahusiano, Matendo 5:38; 15:38; 19:9; 22:29
4. kuondoa kisheria (tarakisha), Kumb. 24:1,3 (LXX) na Agano Jipy, Mat. 5:31; 19:7; Marko 10:4; 1 Kor. 7:11
5. kuondao deni, Mat. 18:7
6. kuonyesha kutokuhusika kwa kuondoka, Mat. 4:20; Yohana 4:28; 16:32
7. kuonyesha kutokuhusika kwa kutoondoka, Yohana 8:29; 14:18
8. kuruhsu au kutoa kibali, Mat. 13:30; 19:14; Marko 14:6; Luka 13:8

Katika maana ya kitheolojia KITENZI pia kina matumizi mapana:

1. kufuta, kusamehe, kuifuta hatia ya dhambi, Kut.32:32 (70) (LXX); Hes. 14:19; Yak. 42:10 na Agano Jipy, Mat. 6:12,14-15; Marko 11:25-26
2. kujiiondoa toka dhambini, 2 Tim. 2:1
3. kukataa kwa kujiiondoa toka kwenye
  - a. Sheria, Mat. 23:23; Matendo 21:21
  - b. imani, Ezek. 20:8 (LXX); Luka 8:13; 2 The. 2:3; 1 Tim. 4:1; Ebr. 3:12

Waamini wa sasa wanauliza maswali mengi ya kitheolojia ambayo waandishi wengi wa Agano Jipy wasingalifikiri kuyahuusu. Moja ya haya yangeliweza kuhusiana na uelekeo wa sasa wa kuitenga imani (uthibitisho) kutoka kwenye imani (utakaso).

Kuna watu katika Biblia walihusisha mionganoni mwa watu wa Mungu na jambo lililotokea na kusababisha wao kuondoka.

- I. Agano la Kale
- A. Wale walioisikia taarifa ya wale wapelelezi kumi na wawili (kumi), Namba 14 (kama vile Heb. 3:16-19)
- B. Kora, Namba 16

- C. Wana wa Eli, 1 Samueli 2, 4
  - D. Sauli, 1 Samueli 11-31
  - E. Manabii wa uongo (mifano)
    - 1. Kumb. 13:1-5 18:19-22 (njia za kumtambua nabii wa uongo)
    - 2. Jeremia 28
    - 3. Ezekieli 13:1-7
  - F. Manabii wa uongo
    - 1. Ezekieli 13:17
    - 2. Nehemia 6:14
  - G. Uovu wa viongozi wa Israeli (mifano)
    - 1. Yeremia 5:30-31; 8:1-2; 23:1-4
    - 2. Ezekieli 22:23-31
    - 3. Mika 3:5-12
- II. Agano Jipyा
- A. Hili neno la Kiyunani kifasihi linamaanisha "kuasi." Vitabu vyote vya Agano la Kale na Agano Jipyा vinathibitisha uchochezi wa uovu na mafundisho ya uongo kabla ya Ujio wa Pili (kama vile Mat. 24:24; Marko 13:22; Matendo 20:29,30; 2 The. 2:9-12; 2 Tim. 4:4). Neno hili la Kiyunani linaweza kuyaakisi maneno ya Yesu katika Mfano wa Udongo unaopatikana katika Mathayo 13; Marko 4; na Luka 8. Kwa kudhaniwa walimu hawa wa uongo si Wakristo, bali waamini wachanga (kama vile Ebr. 3:12). Swali la kitheolojia ni hili walimu wa uongo wanawapeleka wapi waamini? Hili ni vigumu kulijibu kwa kuwa kulikuwa na walimu wa uongo katika makanisa anzilishi (kama vile 1 Yohana 2:18-19). Mara nyingi tamaduni au madhehebu yetu yanajibu swali hili pasipokuwa na marejeo ya maandiko ya Biblia mahususi (isipokuwa njia ya kuhakiki kwa nukuu mstari ulio nje ya muktadha ili kwa uangalifu kuhakiki madhara yaliyomo).
  - B. Imani Thabit
    - 1. Yuda, Yohana 17:1
    - 2. Simoni mchawi, Matendo 8
    - 3. Wale waliozungumziwa katika Mat. 7:13-2
    - 4. Wale waliozungumziwa katika Mathayo 13; Marko 4; Luka
    - 5. Wayahudi wa Yohana 8:31-59
    - 6. Alexandra na Himenayo, 1 Tim. 1:19-20
    - 7. Wale wa 1 Tim. 6:21
    - 8. Himanayo na Fileto, 2 Tim. 2:16-18
    - 9. Dema, 2 Tim. 4:10
    - 10. Walimu wa uongo, 2 Peter 2:19-22; Yuda 1:12-19
    - 11. wapinga Kristo, 1 Yohana 2:18-19
  - C. mani isiyo kuwa na matunda
    - 1. 1 Wakorintho 3:10-15
    - 2. 2 Petro 1:8-11

Mara chache tunafikiri juu ya haya maandiko kwa kuwa mfumo wa injili yetu (Ufuatao mtazamo wa Calvn, Arminian, n.k.) unaamuru mwitikio wa kimamlaka. Tafadhari usinihukumu kabla kwa kuwa nafundisha somo langu. Shauku yangu ni hatua ya kiufasiri. Tunapaswa kuipa nafasi Biblia ili izungumze nasi na si kuiumba katika mpangilio wa thiolojia iliyopita. Mara nyingi hii inaumiza na kushtua kwa kuwa thiolojia zetu zilizo nyingi ni za kimadhehebu, kitamaduni, kimahusiano (mzazi, rafiki, mchungaji), si za kibiblia (tazama [Mada Maalumu: Nini maana ya neno "Kupokea," "Kuamini," "Kiri/Ungama," na "kuita"?](#)). Wengine walio mionganoni mwa watu wa Mungu wanarudi nyuma na kutokuwa mionganoni mwa watu wa Mungu (m.f. Rum. 9:6).

**3:13 "Lakini mwonyane"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Waaminio wanatakiwa kuiga Roho na Mwana katika kutia moyo imani na uaminifu (kama vile Ebr. 10: 24). Hii ni sawa na mzizi ule ule wa neno

paraclete ambalo linamaanisha "mtu aliyeitwa kwenda pamoja ili kusaidia" na anatumwiwa na Roho (kama vile Yohana 14: 16,26; 15:26;16:7) na ya Yesu (kama vile 1 Yohana 2: 1).

■"**maadamu iitwapo leo**" ikitumiwa katika Zab. 95, inaonesha kwamba muda wa kutumaini katika Mungu na kutafuta pumziko ulikuwa bado wazi kama ilivyokuwa katika siku za Daudi. Mwandishi anasisitiza kwamba sasa ni muda wa maamuzi kwasababu kunamuda unakuja ambapo kukataliwa kunakoendelea kutapelekea matokeo ya macho yenye upofu (yaani dhambi isiyosameheka ya Injili na dhambi mpaka mauti ya 1 Yohana).

Hakuna mtu anachagua wakati wa kuja kwa Mungu (kama vile Yohana 6: 44, 65). Uchaguzi wetu pekee ni kurejerea na kurejerea mapema. Kukataa kunakoendelea na kuchagua kutoamini kunasababisha ugumu wa roho wa moyo wa mwanadamu (kama vile kauli tendwa tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu, "kufanya kugumu kwa udanganyifu wa dhambi"). Haya sio mapenzi ya Mungu bali madhara yasiyopingika ya kukataliwa. Watu wa Mungu waliondoka Misri katika imani walisita sita katika ahadi za Mungu ikihsiana na kumiliki Nchi ya Ahadi. Waaminio mara kwa mara wanafanya kazi hali ya kutoamini iliyowazi. Kuwa mwangalifu juu ya kugawanyisha imani ya kwanza na imani inayoendelea (kama vile Ebr. 3: 6, 14).

■"**ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi**" Hii ni kauli tendwa tegemezi ya wakati uliopita usio tegemezi. Dhambi inapewa uhusika kama adui ambaye anafanya moyo kuwa mgumu. Tazama namna ambavyo ukweli huu unawasilishwa:

1. angalieni wapendwa (Ebr. 3:12)
2. asije mtu (Ebr. 3:12)
  - a.moyo wa kutoamini
  - b.akajitenga na Mungu
3. kutiana moyo sisi kwa sisi (Ebr. 3:13)
4. msije mkafanywa wagumu na dhambi (Ebr. 3:13)
5. tu washiriki, ikiwa tutag'ag'ana (Ebr. 3:14)

Utiaji moyo wa namna gani huu mkuu na mistari hii inawasilisha.

**3:14 "tumekuwa washirika wa Kristo,"** Hii ni kauli endaji elekezi ya wakati timilifu. Hii inamaanisha maendeleo kwamba matokeo ya kuendelea kukaa.

■"**kama**" Hii ni sentensi ya daraja la tatu lenye masharti ambayo inamaanisha kitendo kinachowezekana kutokea. Hili ni onyo lingine linaloonya Wakristo kushikilia maungamo yao (kama vile Ebr. 3:6; 4:14; 10:23).

**NASB** "kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho"

**NKJV** "kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho"

**NRSV** "kama tutashikilia tu ujasiri wetu thabiti mpaka mwisho"

**TEV** "kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho"

**NJB** "kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho"

Huu ni msisitizo wa ustahimilivu. Ni msisitizo wa kibiblia unaoaminika kama ilivyo usalama. Sharti viwekwe pamoja kwa ajili ya mtazamo wa uwiano wa kibiblia (kama vile 3: 6; 4:14; Marko 13:13; Rum. 11:22;1 Kor.15:2;Gal. 6:7-9; 1 Yohana 2:19; Ufu. 2:7, 11, 17, 26; 3:5,12,21;21:7). Angalia [MADA MAALUM: DHAMANA](#) katika Ebr.2:2. Kwa ajili ya "mpaka mwisho" angalia Mada Maalum katika Ebr.7: 11.

Mafundisho mengi zaidi huja kilahaja au katika jozи za ukinzani. Biblia ni kitabu cha kimashariki ambacho kinatumia lugha ya kimafumbo kuuelezea ukweli kwa kauli zenye nguvu sana lakini pia inaweka uwiano na kauli zingine zenye kauli kinzani. Hivyo ukweli unapatikana kati ya kupitiliza huku kulikotajwa. Watu wa magharibi wanajaribu kuthibitisha maandiko upande mmoja wa mkanganyiko na kug'ag'ania msimamo wa ukweli kwa ubayana na kimafundisho kwa kutafsiri maelezo ya ukweli bila kutafuta na kuwa wazi kwa kweli ya upande mwengine. Kwa njia nyingi hiki ni chanzo kikubwa cha mvutano kati ya madhehebu ya magharibi ya kisasa! Angalia Mada maalum hapa chini.

## MADA MAALUMU: DHAMANA YA MKRISTO

- A. Je! Wakristo wanaweza kutambua kwamba wameokolewa (kama vile 1 Yohana 5:13)?Yohana ana majaribio matatu au ushahidi.
  - 1. Kimafundisho (imani, 1 Yohana 1:1,5,10; 2:18-25; 4:1-6,14-16; 5:11-12)
  - 2. Mtindo wa maisha (utii, 1 Yohana 2:2-3; 2:3-6; 3:1-10; 5:18)
  - 3. Kijamii (upendo, 1 Yohana 1:2-3; 2:7-11; 3:11-18; 4:7-12, 16-21)
- B. Dhamana imekuwa ni suala la kimadhehebu
  - 1. John Calvin alijikita katika uchaguzi wa Mungu. Amesema kuwa katika maisha haya kamwe hatuwezi kuwa na uhakika.
  - 2. John Wesley aliegemea juu ya dhamana ya uzoefu wa kidini. Aliamini kuwa tunao uwezo wa kuishi juu ya dhambi inayofahamika.
  - 3. Waamini wa Kanisa Katoriki na Kanisa la Kristo wanaegemea juu ya Kanisa la kimamlaka. Kundi alilomo mtu huyu ni jawabu la neno dhamana.
  - 4. Walokole wengi wameweka dhamana zao juu ya ahadi za Biblia, zilizoungamanishwa na tunda la Roho (kama vile Gal. 5:22-23) katika maisha ya mwamini (yaani, ufanano na Kristo wa kila siku).
- C. Dhamana ya awali ya waaminio imeungamanishwa na sifa za Mungu wa Utatu
  - 1. Upendo wa Mungu Baba
    - a. Yohana 3:16; 10:28-29
    - b. Warumi 8:31-39
    - c. Waefeso 2:5,8-9
    - d. Wafilipi 1:6
    - e. 1 Petro 1:3-5
    - f. 1 Yohana 4:7-21
  - 2. Matendo ya Mungu mwana
    - a. kifo badala yetu
      - 1) Matendo 2:23
      - 2) Warumi 5:6-11
      - 3) Wakorintho 5:21
      - 4) 1 Yohana 2:2; 4:9-10
    - b. maombi ya kuhani mkuu (Yohana 17:12)
    - c. maombi endelevu ya kusihis
      - 1) Warumi 8:34
      - 2) Waembrania 7:25
      - 3) 1 Yohana 2:1
  - 3. Huduma ya Roho wa Mungu
    - a. wito (Yohana 6:44,65)
    - b. kutia mhuri
      - 1) 2 Wakorintho 1:22; 5:5
      - 2) Waefeso 1:13-14; 4:3
    - c. hakikisha
      - 1) Warumi 8:16-17
      - 2) 1 Yohana 5:7-13
- D. Lakini wanadamu yawapasa kukubali kujitolea kwa Mungu kupiitia agano lake (katika nafasi zote, ya awali na ile endelevu)
  - 1. waamini yawapasa kugeuka kutoka dhambini (toba) na kumwelekea Mungu kupitia Yesu (imani)
    - a. Marko 1:15
    - b. Matendo 3:16,19; 20:21
  - 2. waamini yawapasa kukupokea kujitolea kwa Mungu katika Kristo (tazama [Mada Maalumu: Je! Kunamaanisha nini "kupokea," "Kuamini," "Kukiri/Kuungama," "Kusihii"](#))

- a. Yohana 1:12; 3:16
  - b. Warumi 5:1 (na kwa mfanano 10:9-13)
  - c. Waefeso 2:5,8-9
  - 3. waamini yawapasa kuendelea katika imani (tazama [Mada Maalumu: Ustahimilivu](#))
    - a. Marko 13:13
    - b. 1 Wakorintho 15:2
    - c. Wagalatia 6:9
    - d. Waebrania 3:14
    - e. 2 Petro 1:10
    - f. Yuda 20-21
    - g. Ufunuo 2:2-3,7,10,17,19,25-26; 3:5,10,11,21
  - E. Dhamana ni ngumu kwa sababu
    - 1. mara kwa mara waamini hutafuta uzoefu fulani ambao haukuhaidiwa katika Biblia
    - 2. mara kwa mara waamini hawailewi injili kwa ukamilifu
    - 3. mara kwa mara waamini wanaendelea na dhambi kwa makusudi (kama vile Kor. 3:10-15; 9:27; 1 Tim. 1:19-20; 2 Tim. 4:10; 2 Pet. 1:8-11)
    - 4. aina ya mtu fulani (yaani, mtu aaminiye katika kushinda) asiyeweza kamwe kukubali upendo na ukubalifu usio na masharti wa Mungu
    - 5. katika Biblia kuna mifano ya maungamo ya uongo (kama vile Mat. 13:3-23; 7:21-23; Marko 4:14-20; 2 Pet. 2:19-20; 1 Yohana 2:18-19, tazama [Mada Maalumu: Ukanaji wa Imani](#))
- Tazama [Mada Maalumu: Dhamana ya Mkristo](#) kwa maelezo ya mihtasari tofauti tofauti ya mafundisho haya.

## MADA MAALUMU: *ARCHÉ*

Neno la Kiyunani *archē* linamaanisha "mwanzo" au "asili" ya kitu.

1. mwanzo wa mpangilio ulioumbwa (kama vile. Yohana 1:1; Ebr. 1:10)
2. mwanzoni mwa injili (kama vile. Mk. 1:1; Flp. 4:15; 2 The. 2:13; Ebr. 2:3; 1 Yohana 1:1)
3. mwanzo wa jicho la kwanza la ushahidi (kama vile. Luka 1:2)
4. mwanzo wa dhambi (miujiza, kama vile. Yohana 2:11)
5. mwanzo wa mafundisho (kama vile. Ebr. 5:12)
6. mwanzo wa udhihirisho uliojikita katika kweli ya injili (kama vile. Ebr. 3:14)
7. mwanzo, Kol. 1:18; Ufu. 3:14

Ilikuwa kutumika juu ya "utawala" au "mamlaka"

1. juu ya wanadamu rasmi watawalao
  - a. Luka 12:11
  - b. Luka 20:20
  - c. Warumi 13:3; Tito 3:1
2. juu ya mpangilio wa mamlaka
  - a. Warumi 8:38
  - b. 1 Kor. 15:24
  - c. Efe. 1:21; 3:10; 6:12
  - d. Kol. 1:16; 2:10,15
  - e. Yuda 1:6

**3:15 "kama"** Hii ni sentensi nyingine ya daraja la tatu yenye masharti, kama Ebr. 3:14, ambayo inamaanisha kitendo chenyeye uwezekano wa kutokea. Hii ni nukuu kutoka Zab. 95:7-8, ambayo imekuwa ni shabaha ya sura ya 3.

**3:16-18** Kuna maswali matatu yasiyokuwa na majibu (kama vile Ebr. 3:16, 17, 18). Ikiwa ufanano huu utachukuliwa kibayana, inaonekana kwamba wote waliofariki katika jangwa (kama vile Hes.14), akiwemo Musa,

Haruni na makuhani waaminifu wakati wa uasi wa Kora, walikuwa wamepotea milele kiroho. Hii haiwezekani. Haya ni matumizi ya kisarufi ya maneno "pumziko" na "kutotii." Kuna maneno mawili ya msingi ya muktadha huu. Mungu ana "pumziko" kwa wale wanaomtumainia Yeye (na kuendelea kumtumainia Yeye), bado kuna madhara kwa "kutotii," wote wasioamini na waaminio!

**3:19** Hali ya kutotumaini ya Ebr.3: 19 inashughulikia hali ya kukosa imani kwa Israeli wakati wa kipindi cha safari ya jangwani!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Yesu anaitwa "mtume" katika Ebr. 3:1?
2. Orodhesha matumizi mbali mbali ya "pumziko."
3. Toa maana ya "ustahimilivu wa watakatifu."

## WAEBRANIA 4

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>             |  |   |  |  |
|--|--|---|--|--|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                                   | <b>NKJV</b>  | <b>NRSV</b>   | <b>TEV</b>   | <b>NJB</b>   |
| Pumziko kwa watu<br>Wa Mungu<br><br>(3:7-4:13)<br>4:1-11 | Ahadi ya Pumziko<br>4:1-10<br>Neno linafunua hali<br>Zetu<br>4:11-13<br><br>4:12-13<br>Yesu kama Kuhani<br>Mkuu Sana<br><br>(4:14-5:10)<br>4:14-16 | Maonyo na uangalifu<br>(3:7-4:13)<br>4:1-11<br><br>4:12-13<br><br>Kuhani Wetu Mkuu<br>Mwenye Huruma<br><br>(4:14-5:14)<br>4:14-16 | Pumziko kwa Watu wa<br>Mungu<br><br>(3:7-4:13)<br>4:1-7<br>4:8-11<br><br>4:12-13<br><br>Yesu Kuhani Mkuu<br>Sana<br><br>(4:14-5:10)<br>4:14-16 | Namna ya kufikia<br>Ardhi ya Mungu ya<br>Pumziko<br><br>(3:7-4:13)<br>4:1-11<br><br>4:12-13<br><br>Yesu Kuhani Mkuu<br>Sana mwenye<br>Huruma<br><br>(4:14-5:10)<br>4:14-16 |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Mwandishi anarudi nyuma na kwenda mbele kati ya ukuu wa Yesu na onyo la kuendelea kushikilia.
- B. Ukuu wa Yesu (agano jipya) juu ya agano kuu kuu
  1. Yeye ni ufunuo mkuu (manabii, Ebr. 1: 1-3)
  2. Yeye ni mpatanishi mkuu au (malaika, Ebr.1:4-2:18)
  3. Yeye ni mtumishi mkuu (Musa, Ebr.3:1-6)
  4. Yeye ni kuhani mkuu (Haruni, Ebr. 4: 14-5: 10; 6: 13-7: 28)
  5. Yeye ni agano kuu (Agano la Kale, Ebr. 8: 1-13; 9: 15-22)
  6. Yeye ni madhababu kuu (hekalu, Ebr. 9: 1-11, 23-28)
  7. Yeye ni madhababu kuu (wanyama, Ebr. 9: 12-14; 10: 1-18)
  8. Yeye ni mlima mkuu (agano la kale kama Mlima Sinai na agano jipya kama Mlima Sayuni, Ebr. 11: 18-29)

C. Katika ufahamu wa ukoo wa Yesu kuna mfululizo wa maonyo dhidi ya kukataa injili Yake (yaani Agano Jipya, kama vile Yer. 31: 31-34; Ezek. 36: 22-38) au kurudi katika dini ya Kiyahudi (yaani Agano la Kale).

1. Ebr. 2: 1-4
2. Ebr. 3: 7-4: 13
3. Ebr. 5: 11-6: 12
4. Ebr. 10: 19-39
5. Ebr. 12: 14-29

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 4:1-13

<sup>1</sup>Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.

<sup>2</sup> Maana ni kweli, sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia. <sup>3</sup>Maana sisi tulioamini tunaingia katika raha ile; kama vile alivyosema,

“Kama nilivyoapa kwa hasira yangu,

Hawataingia rahani mwangu:

<sup>4</sup>Kwa maana ameinena siku ya saba mahali fulani hivi, Mungu alistarehe siku ya saba, akaziacha kazi zake zote; <sup>5</sup>na hapa napo,

“Hawataingia rahani mwangu.

<sup>6</sup>Basi, kwa kuwa neno hili limebaki kwamba wako watu watakaoingia humo, na wale waliohubiriwa habari ile zamani walikosa kuingia kwa sababu ya kuasi kwao,<sup>7</sup>aweka tena siku fulani, akisema katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii, Leo; kama ilivyonenwa tangu zamani,

“Leo,kama mtaisikia sauti yake,

Msifanye migumu mioyo yenu.

<sup>8</sup>Maana kama Yoshua angaliwapa raha, asingaliinena siku nyingine baadaye. <sup>9</sup>Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. <sup>10</sup>Kwa maana ye ye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake. <sup>11</sup>Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi. <sup>12</sup>Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. <sup>13</sup>Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu.

4:1

NASB, NKJV    “ogopeni”

NRSV, TEV    “kuweni makini”

NJB            “kuweni makini”

Kitenzi ni kauli tendwa tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu (wenye ushahidi) ("na tuogope"). Maonyo ya Waebrania (kama vile Ebr. 2: 1-4; 3: 7-13; 4: 1-13; 5: 11-6: 12; 10: 26-39; na 12: 14-17) yanaleta hali ya hofu (kama vile Ebr. 4: 11). Maonyo haya yanagusa mambo ya kilele ya wokovu na dhamana.

▣ "Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake" Huu ni mwendelezo wa mbinu ya kisarufi (yaanmi "pumziko Lake," kama vile Ebr.. 4: 1, 3, 5, 8, 9, 10, 11) ambamo ndani yake waandishi wanatumia mbinu ya utafsiri wa maandiko wa Kiyahudi kuzungumzia sehemu nne za watu wa historia ya Mungu.

1. Mwanzo 2: 2, pumziko la Mungu siku ya saba ya uumbaji
2. Hes. 13-14, pumziko la Yoshua ambalo lilikuwa Nchi ya Ahadi
3. Zab. 95: 7-11 pumziko la Mungu lilikuwepo katika siku za Daudi

4. Ebr. 4: 1, 10-11 siku ya pumziko kama rejea ya amani pamoja na Mungu na maisha pamoja na Mungu (mbinguni)

**NASB, NKJV** “**asije akaonekana ameikosa**”

**NRSV** “**kushindwa kuifikia**”

**TEV** “**kushindwa kuipokea ile ahadi**”

**NJB** “**kwamba amekuja amechelewa kwa ajili ya ahadi ya kuingia mahali pa pumziko**”

Hii inaaksi neno la kiebrania *chatha* ("kukosea alama") ikitafsiriwa kama *hamartia* na Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani, lililo na maana ya "kupungukiwa" au "kuwa na mapungufu" (kama vile Ebr. 12: 15; Rum. 3:23). Maana inayofanana na hiyo ni "kuja kwa kuchelewa" (kama vile NJB).

**4:2 "nasi tumehubiriwa habari njema"** Hii inarejerea kwa injili kuhusu Yesu Kristo ambayo wote wanawenza kukubali kwa imani. Kabla ya Kristo inarejerea kwa Neno la Mungu ambalo lilitolewa katika Agano la Kale kwa namna tofauti (yaani "msile mtunda ya mti"; "jenga safina"; "nifuate mimi mpaka nchi"; "ishike sheria"; "ingia katika nchi ya Ahadi," n.k.). Kila mtu au kundi lilitakiwa kumwamini Mungu na kuitikia kwa imani (yaani, kutendea kazi) Neno Lake kwao. Katika Kutoka wale walioamini walikuwa ni Yoshua na Kalebu. Waliamini ahadi ya Mungu juu ya Nchi ya Ahadi; Waisraeli wengi hawakuamini.

■**"vile vile kama hao"** Hii inarejerea kwa wana wa Israeli waliosikiliza taarifa mbaya ya wapelelezi kumi. Yoshua na Kalebu hatahivyo hawakuona mashaka ahadi ya Mungu juu ya kutawala Nchi ya Ahadi (kama vile Hes.13-14), hivyo wangeingia Kanaani, bali wale wasioamini wasingeingia.

**NASB** “**kwasababu halikuchanganywa na imani kwa wale waliosikia**”

**NKJV** “**halikuchanganywa na imani kwa wale walioamini**”

**NRSV** “**kwasababu hawakuunganisha na imani kwa wale waliosikia**”

**TEV** “**hawakulipokea kwa imani**”

**NJB** “**kwasababu hawakushirikisha imani ya wale waliosikia**”

Kuna utofautiano wa maandiko ya Kiyunani hapa. Maandiko yaliyothibitishwa yana kauli tendwa yenye shitaka ya wakati timilifu ya jinsi ya kike ya wingi endelevu (kama vile NASB, NKJV, NRSV, REB). Chaguzi nyingine ni kauli tendwa yenye nomino ya wakati timilifu ya jinsi ya kike yenye wingi ya wakati endelevu (kama vile TEV, NJB, NIV).

Jambo la kithiolojia linajumuisha imani (wokovu) au kukosekana kwa imani kwa wana wa Israeli wenye umri wa watu wazima (kuanzia miaka 20 na kuendelea) walioshiriki katika safari ya Kutoka. Je kukoswa kwao imani katika taarifa ya wapelezi kulimaanisha (1) walikuwa hawaruhusiwi kuingia Kanaani au (2) walikuwa hawaruhusiwi kuingia mbinguni? Swali hili si rahisi kulijibu kwasababu ya mbinu ya kisarufi ya mwandishi ya neno "pumziko." Inaonekana bora kukiri imani yao kwa YHWH (yaani wokovu), lakini wakubali kwamba walikosa imani ya kuamini kila ahadi Yake (yaani ya kuwapeleka Kanaani). Hili ni swali lenyewe linalohusiana na wasomaji wa karne ya kwanza. Je kukosa kwao ustahimilivu ni ishara kwamba hawakuwa wameokolewa au walionesha imani yao dhaifu? Katika Fasiri yake juu ya Waembrania katika *The New International Commentary Series*, F. F. Bruce anasema, "Maana halisia iko wazi: si kusikia injili kunakoleta wokovu wenyewe, bali uwekeaji imani inayotakiwa; na ikiwa imani ni halisia, itakuwa ni imani g'ag'anizi" (ukurasa wa 73).

**4:3 "kama vile alivyosema"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu ambayo kwa kurudiwa rudiwa inatumiwa kurejerea maandiko yaliyovuviwa (kama vile Ebr. 1:13; 4:3,4; 10: 5, 9; 13:5), ambayo yanaweza kurejerea kwa Mungu Baba au Mungu Mwana .

■ Hii ni nukuu ya Zab. 95: 11 (kama hapa ni Ebr. 4: 5 na 3: 11), lakini pia maelezo yaliyoongezwa ya Agano la Kale yakirejerea Mwa. 2: 2, Sabato ya Mungu (pumziko la siku ya saba ya uumbaji).

**4:4 "Kwa maana ameinena siku ya saba mahali fulani hivi"** Hii inaaksi nahau ya kisheria ya kiyunani ya imani katika uvuvio wa Agano la Kale lote (Kama vile Ebr. 2: 6). Ile "wapi" (yaani eneo halisia la andiko) na "nani" (yaani mwandishi mwanadamu wa maandiko), hakuwa muhimu kama Mungu aliye mwandishi wa maandiko yote. Hii haimaanishi mwandishi alisahau wapi rejea ya Agano la Kale lingepatikana.

▣**"siku ya saba"** Walimu wa Kiyahudi walielezea kwamba Sabato ya Mungu (yaani "Siku ya Pumziko") haijawahi kuisha kwasababu kanuni iliyozoleka ya Mwanzo 1, "kukawa jioni na kukawa asubuhi, siku.....," Haitajwi kwa muunganiko na siku hii ya saba ya uumbaji katika Mwa. 2: 2,3 (kama vile Kut. 20: 11).

**4:5** Hii ni nukuu ya Zab. 95:11.

**4:6 "kwa sababu ya kuasi kwao"** Kukosa imani kunakuja na ushahidi wa kutotii (kama vile Ebr. 3: 18; 4: 6, 11). Muktadha mkubwa wa sura ya 4 inaaksi matukio yaliyoandikwa katika Hes.13-14, Lakini rejea ya kimaandiko hasa ni Zab. 95: 7-11, ambayo inahusiana na tajiriba ya Israeli iitwayo *Meribah*.

Neno "kutokutii" liko katika maandiko ya kale ya Kiyunani A, B, D, wakati "kukosa kuamini" kupo katika maandiko ya mafunjo ya P<sup>46</sup>, na maandiko ya kale ya  $\chi$ .

**4:7 "aweka tena siku fulani, akisema katika Daudi"** Neno la Kiyunani "fixes" ni neno la Kingereza "horizon (mpaka)," lililo namaana ya kuweka mipaka. "Kupitia Daudi" halipo katika andiko la Kiebrania la Zab. 95:7-8, bali Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani kwa ufasaha inalitafsiri na kuingiza mwandishi wa kijadi wa Zaburi. Hoja ya mwandishi imejikita katika pumziko la Mungu bado liko wazi hata wakati wa utawala wa Daudi.

Zaburi 95: 7-11 imenukuliwa mara kadhaa katika muktadha wa sura ya 3 na 4. Kila wakati tofauti wa sehemu ya kifungu cha Agano la Kale kinasisitizwa (kama mahubiri).

1. Ebr. 3: 7-11 inasisitiza "msiifanye migumu mioyo yenu" ya Zab. 95: 8
2. Ebr. 3: 15 inasisitiza "waliponichokoza mimi" ya Zab. 95: 9
3. Ebr. 4: 3, 5 inasisitiza "hawataingia katika pumziko langu" ya Zab. 95: 11
4. Ebr. 4: 7 inasisitiza "leo" ya Zab. 95: 7

**4:8 "kama"** Hii ni sentensi daraja la pili yenye masharti ambayo mara kwa mara inaitwa "inakinzana na kweli." Yoshua hakuwapeleka wana wa Israeli katika pumziko. Haya ni matumizi ya neno "pumziko" sio kwa namna ya Kanaani, bali pumziko la kiroho (kama vile Ebr. 4: 9-10). Kutoke Ebr. 4: 8-10 ni wazi kwamba mwandishi wa Waembrania anatumia "pumziko" kwa namna tatu za kihistoria na kithiolojia:

1. nchi ya Ahadi ya Kanaani (Ebr. 4: 8, siku za Yoshua, Hes. 13-14)
2. nafasi ya kumtumaini Mungu (kama vile Ebr 4: 9 yaani siku za Daudi, Zab. 95)
3. Mwanzo 2 (Ebr. 4: 4) pumziko la Mungu wakati wa uumbaji (Ebr. 4: 10)
4. mbingu (Ebr. 4: 1 na 11)

▣**"mioyo"** Angalia Mada Maalum katika Ebr. 3:8.

▣**"Yoshua"** Toleo la King James lina "Yesu," ambayo inafuatia fasiri ya Geneva na Maaskofu lakini muktadha unadai Agano la Kale "Yosh u a." Majina yote yanatajwa sawasawa yaani Yoshua-Waembrania; Yesu-Kiaramu)! Kanisa la kwanza mara kwa mara lilimtumia Yoshua kama aina ya Yesu (kama vile Mdo. 7: 45, ambapo kosa lile lile katika tafsiri linafanyika).

▣**"Yeye"** Hii lazima inarejerea juu ya mwandishi wa kiungu wa Zaburi 95.

**4:9** Huu ni muhtasari wa maelezo ya Zaburi 95. Kulikuwa na ahadi ya kuanzia ya pumziko (kama vile Mwanzo 2:2); kulikuwa na kutimilizwa kwa mara ya pili kwa kihistoria (Yoshua); kulikuwa na fursa ya baadae ya tatu (siku za Daudi); na bado kuna fursa ya nne kwa mtu yejote ambaye anachagua kutumia imani kwenye ahadi za Mungu. Tazama mwandishi anatumia kichwa cha habari "watu wa Mungu" kwa wale wanaoamini katika Kristo (sio wayahudi tu).

**4:10, 11** Vitenzi vyote vya Ebr. 4: 10-11 ni vya wakati uliopita usiotimilifu, ambayo aidha ni (1) alama ya kitendo kilichomalizika (2) kuyatazama maisha yote kama kitu kimoja. Mistari ya 10 na 11 inalifanya wazi kwamba "pumziko" la Ebr. 4: 10 linarejereza mbingu. Waaminio siku moja wataacha bidii yao (kama vile Ufu. 14: 13), lakini Ebr. 4: 11 kiufasaha inaelezea kwamba wakati maisha ya mwilini yanabakia, waaminio lazima waendelee katika imani, toba, utii na ustahimilivu. Mstari wa 11 ni onyo kali. Wokovu kwa asilimia zote ni bure katika kazi iliyokwisha malizika ya Kristo. Ni kipawa cha neema kutoka kwa Baba na kazi ya ushawishi ya Roho. Hata hivyo, utawala wa Mungu wa Utatu umechagua kushughulikia binadamu katika mahusiano ya kiagano. Mwanadamu lazima arejeree na kuendelea kurejerea. Wokovu sio tiketi ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto bali imani ya kila siku kwa siku pamoja na mahusiano na mungu ambayo inazalisha kufanana na Kristo kunakoendelea! Agano lina faida na masharti ya uwajibikaji.

#### **4:11**

|                   |  |
|-------------------|--|
| <b>NASB, NKJV</b> | "na tufanye bidii katika kuingia katika pumziko"       |
| <b>NRSV</b>       | "na tufanye kila bidii kuingia katika ile pumziko"     |
| <b>TEV</b>        | "na tufanye bidii kulipokea lile pumziko"              |
| <b>NJB</b>        | "na tufanye bidii kuingia katika eneo hili la pumziko" |

Katika Kingereza hii inaonekana kuchagiza matendo ya kibinadamu katika kufikia pumziko la Mungu lakini neno la Kiyunani linamaanisha "kuwa na shauku," "kuharakisha" (kama vile 2 Thes. 2:17; 2 Tim. 4: 9).

▣ "mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi" Angalia 3: 18 na 4: 6.

**4:12 "neno la Mungu"** Mistari ya 12 na 13 inatengeneza sentensi moja kwenye Kiyunani. Neno (logos) hairejerei kibin afsi kwa Yesu kama inavyotokea katika Yohana 1: 1, bali kwa iliyozungumzwa na Mungu (kama vile Ebr. 13: 7) au ujumbe ulioandikwa aidha kupitia maandiko ya Agano la Kale. Ufunuo wa Mungu mwenyewe unaelezewa katika namna tatu:

1. inapewa sifa za ubinadamu yakuwa na uhai wake mwenyewe
2. ni kama nguvu inayopenya ya upanga
3. ni kama hakimu anayejua kila kitu (kama vile Ebr. 4: 13)

Katika kitabu chake *Jewish Christianity*, H. E. Dana anapendekeza akijikita katika mafunjo ya Misri ya matumizi ya "word (neno)" (*logos*) ikimaanisha "kupiga hesabu" au "kuzingatia hesabu." Anaelezea hii inashabihiana na hoja ya jumla ya mwandishi ya asili, kwamba kutakuwa na kutoa hesabu kiungu kupitia mtihani kwa kutumia sitiari ya daktari wa upasuaji (ukurasa wa 227). Hivyo andiko hili sio maelezo ya neno la Mungu lililofunuliwa bali utambuzi wa hukumu ya Mungu. Hii inafurahisha sana lakini mwandishi wa Waebrania alitumia *logos* mara kwa mara kwa ajili ya neno la Mungu (kama vile Ebr. 2:2; 4:2; 5:13; 7:28; 13:7) na pia neno la Kiyunani kwa neno lililozungumzwa, *rhēma* (kama vile Ebr. 6:5; 11:3).

▣ "li hai, tena lina nguvu" Hii inaksi dhana ya Kiebrania ya nguvu ya neno linalozungumzwa (kama vile Mwa. 1: 1, 3, 6, 9, 14, 20, 24, 26; Zab. 33: 6, 9; 148: 5; Isa. 40: 8; 45:23; 55:11; 5: 17-19; Mt.5:17-19; 24: 35; 1 Pet . 1: 23).

▣ "tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili" Hii inazungumzia nguvu ipenyayo ya Neno la Mungu (kama vile Yohana 12: 48 na Ufu. 1: 6; 2:12,16, ambapo linatumika na Yesu).

▣ "nafsi na roho" Huu si mtazamo wa kugawanyika sehemu mbili kwa kwa wanadamu, bali uhusiano unaokuwa pamoja kwa vyote sayari hii na Mungu. Neno la Kiebrania *nephesh* linatumika kwa wote wanadamu na wanyama katika Mwanzo, wakati "roho" (*ruah*) linatumika kipekee juu ya mwanadamu. Neno la Mungu linapenya utu wa ndani sana wa mwanadamu. Huu sio uthibitisho wa kimaandiko juu ya asili ya mwanadamu kwamba anaundwa na sehemu kuu mbili (dichotomous) au kuwa ni kiumbe chenye sehemu tatu (trichotomous) (kama vile 1Thes. 5:23). Mwanadamu kimsingi anawakilishwa katika Biblia kama umoja (kama vile Mwa. 2:7). Kwa muhtasari mzuri wa nadharia za mwanadamu kama mwenye sehemu tatu, mbili au vyote vimeungana, angalia Millard J. Erickson 's

Christian Theology (toleo la pili) kur. 538-557 na kitabu cha Frank Stagg kitiwacho *Polarities of Man's Existence in Biblical Perspective*.

■ "kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo" Katika Kiebrania walifikiri "moyo" unawakilisha mtu mzima na msukumo wa ndani. Angalia Mada Maalum katika Ebr. 3: 8. Mungu anajua imani ya kweli na isiyo ya kweli.

**4:13 "lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa"** Mungu anatujua kwa ukamilifu (kama vile 1 Sam. 16:7; Zab.7: 9; 33:13-15; 139:1-4; Mith. 16: 2; 21: 2; 24: 12; Yer. 11: 20; 17: 10; 20: 12; Luka 16:15; Mdo. 1: 24; 15: 8; Rum. 8:27).

|      |  |
|------|--|
| NASB | "kwa macho Yake"   |
| NKJV | "wazi wazi kwa macho"                                    |
| NRSV | "wazi wazi na kuachwa wazi"                              |
| TEV  | "iliyo wazi na hajafichwa"                               |
| NJB  | "isiyofunikwa na iliyotandazwa na kufunuliwa kikamilifu" |

Sitiari hii kibayana inamaanisha "kufanya shingo ioneckane kwa kuinua sehemu ya chini ya kidevu." Sitiari hii ya Agano la Kale ilikuwa ni onyo kwa hakimu; hapa inarejereea kwa kukutana na Mungu uso kwa uso siku ya hukumu ambaye anajua misukumo yetu.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 4:14-16 (kipengele kamili cha kifasihi kwa 5:10)**

<sup>14</sup>Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. <sup>15</sup>Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali ye ye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. <sup>16</sup>Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

**4:14 "kuhani mkuu"** Mwandishi anataja kwa mara ya kwanza Yesu kama kuhani Mkuu katika Ebr. 3:1-6. Baada ya maonyo na miongozo ya Ebr. 3:7-4:13, ye ye sasa anarudi kwenye mada. Utaratibu huu huu unafuatiwa katika maonyo katika Ebr. 5: 11-6:12 na katika mijadala ya kazi za kikuhanai za Yesu katika Ebr. 6:13-10:39. Angalia Mada Maalum katika Ebr. 2:17.

Waebrenia ni kitabu pekee katika Agano Jipya ambacho kinamuita Yesu "kuhani mkuu." Ulinganifu wa mwandishi wa agano la Musa na agano jipya unaendelea. Hii ingekuwa ngumu kwa watu wa kiyahudi kukubali na kuelewa. Yesu hakuwa kuhani kutoka kabilia la kikuhanai la Lawi. Hatahivyo Yesu anaitwa "kuhani mkuu" katika Ebr. 1: 3; 2: 17, 18; 3: 1. Katika Agano la Kale Masihi anarejerewa kama kuhani katika muktadha wa ina mbili tu: Zab. 110 na Zek. 4, zote mbili zina viashiria vya kifalme na ukuhani.

■ "aliyeingia katika mbingu" Hii iko katika njeo ya wakati timilifu. Yesu amepita katika mbingu (ikiwa ziko 3 au 7), Alirudi kwenye uwepo wa Baba yake na matokeo ya Kuja kwake (kuvaa mwili ) na kwenda (kupaa ) kunabakia. Hivyo waaminio sasa wanaweza kwa kuititia usaidizi pia wakapita katika mbingu. Kwa mawazo ya walimu wa Juzi, mbingu ni vikwazo vya kimalaika (*aeons*), lakini katika Agano la Kale ni

1. anga ambao ndege wanalitumia kupaa
2. madirisha ya mbinguni ampo mvua inatoka
3. mbingu zenye nyota, juu na mwezi
4. uwepo wa Mungu kabisa

Kumekuwepo na mijadala inayofanywa na walimu wa Kiyahudi ikiwa kuna mbingu tatu au saba (kama vile Efe. 4: 10; 2 Kor. 12: 2). Tungo hii pia ilitumika na walimu wa Kiyahudi kuelezea hema ya kimbingu ambayo inashabihiana na muktadha vizuri zaidi (kama vile Ebr. 9:23-28).

## MADA MAALUMU: MBINGU NA MBINGU YA TATU

Katika Agano la Kale neno "mbingu" mara nyingi iko kwenye hali ya wingi (yaani , shamayim, BDB 1029, KB 1559). Neno la Kiebrania hii inamaanisha "urefu." Mungu anaishi mahali pa juu. Dhana hii inaakisi utakatifu na uwezo mkuu wa Mungu.

Katika Mwa.1:1, wingi, "mbingu na dunia," vimetazamwa kama vitu vilivyoumbwa na Mungu (1) angani juu ya hii sayari au (2) njia ya kuitaja kweli yote (yaani, ya kiroho na ya kimwili). Kutokana na uelewa huu wa kimsingi maandiko mengine yalitajwa kama marejeo kwa viwango vya Kimbingu:"mbingu ya mbingu" (kama vile Zab. 68:33) au "mbingu na mbingu ya mbingu" (kama vile Kumb.10:14; 1 Fal. 8:27; Neh. 9:6; Zab. 148:4).

Wanasheria walidhani kwamba kungekuwa na

1. mbingu mbili (yaani, R. Yuda, Hagigah 12b)
2. mbingu ya tatu (Test. Law. 2-3; Uzao wa Isa. 6-7; Midrash Tehillim juu ya Zab. 114:1)
3. mbingu ya tano (III Baruch)
4. Mbingu ya saba (R. Simon b. Lakish; ukoo wa Isa. 9:7)
5. mbingu ya kumi (II Enoch 20:3b; 22:1)

Hizi zote zilikuwa na maana ya kuonyesha utenganisho wa Mungu kutoka katika uumbaji uonekanao na /au mipaka Yake. Zaidi ya namba za kawaida za mbingu katika sheria za Kiyahudi zilikuwa saba. A. Cohen, *Everyman's Talmud* (uk. 30), anasema hii ilihuushwa na elimu sayari, lakini nafikiri inataja juu ya saba kama namba timilifu (yaani, siku za uumbaji na kuwakilisha pumziko la Mungu siku ya saba katika Mwanzo 2:2). Paulo, katika 2 Kor. 12:2, anataja mbingu "ya tatu" (Kiyunani ouranos)kama njia ya kuutambulisha upekee wa Mungu, uwepo wa ukuu. Paulo alikutana na Mungu binafsi.

■"**Yesu**" Inawezekana kwaba uainishi huu wa kimbinu juu ya Yesu kama Yoshua mpya. Majina yao yanafanana ni yale yale (yaani Yoshua-Waebrania; Yesu- Kiaramu). Mwandishi wa Waerania anaelezea kwa safari ya Kutoka kwa upana. Kama Yoshua alivyo waleta watu wa Mungu katika nchi ya Ahadi, ndivyo itakavyokuwa pia Yesu kuwaleta katika mbingu.

■"**Mwana wa Mungu**" Hivi ni vyote cheo cha Agano la Kale kikitumika kwa Yesu wa Nazareti na pia msisitizo unaoendelea wa mwandishi juu ya Yesu kama "mwana" (kama vile Ebr. 1: 2; 3: 6; 5: 8; 7: 28). Sio kwa ajali kwamba uanadamu na uungu wa Yesu unasisitizwa kwa pamoja (kama vile Ezek. 2: 1 – mwanadamu; Dan. 7:13 – Mungu). Hii ni nguzo kuu ya ukweli wa Agano Jipya kuhusu nafsi ya Yesu (kama vile Yohana 1: 1, 14; 1 Yohana 4:1-6).

■"**tuyashike sana maungamo yetu**"Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo. Huku ni kuendelea kwa msisitizo juu ya jitaji la ustahimilivu (kama vile Ebr. 2: 1; 3: 6, 14). Lazima tuwianishe maamuzi yetu ya mwanzo (kama vile Yohana 1: 12; 3: 16; Rum. 10: 9-13) na uanafunzi wetu unaoendelea (kama vile Mt. 7: 13-27; 28: 19-20; Efe. 1: 4; 2: 10). Vyote vya muhimu! Imani lazima ifanye kazi katika uaminifu! Kwa ajili ya Mjadala wa neno "maungamo," angalia dokezo katika Ebr. 3:1.

## MADA MAALUM: USTAHIMILIVU

Mafundisho ya Kibiblia yenyeye kuhusiana na maisha ya Kikristo ni magumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika joji halisi ya upembusi wa kimashariki (angalia Mada Maalum: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya Kibiblia]). Joji hizi zinakinzana, ingawa bado zote ni za Kibiblia. Wakristo wa Kimagharihi yamejaribu kuchagua ukweli mmoja na kuachana na ukweli wa pili. Ngoja nielezee kwa mifano.

- A. je wokovu ni maamuzi ya mwanzo kumwamini Kristo au ni kuyatoa maisha yako yote kwenye uanafunzi?
- B. je wokovu ni uchaguzi kwa neema itokayo kwa Mungu Mkuu au kuamini kwa mwanadamu na mwitikio wa toba kwenye ahadi ya Kiungu?

C. je wokovu, mara unapoupatu, ni vigumu kuupoteza, au kunahitajika kwa ajili ya kuongeza jithada? Suala la ustahimilivu limekuwa lenye mkanganyo kwa muda wote wa historia ya kanisa. Tatizo lilianza inavyoonekana na mgongano wa sura za agano Jipy:

- A. maandiko juu ya ahadi
  - 1. maelezo ya Yesu (Yohana 6:37; 10:28-29)
  - 2. maelezo ya Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Fil. 1:6; 2:13; 2 The. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
  - 3. maelezo ya Petro (1 Pet. 1:4-5)
- B. maandiko juu ya hitaji la ustahimilivu
  - 1. maelezo ya Yesu (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13; Yohana 8:31; 15:4-10; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21)
  - 2. maelezo ya Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Fil. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
  - 3. maelezo ya mwandishi wa Waembrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
  - 4. maelezo ya Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9)
  - 5. maelezo ya Baba (Ufu. 21:7)

Masuala ya wokovu wa Kibiblia toka kwa pendo, rehema, na neema ya Mungu Mkuu wa Utatu. Hakuna mwanadamu atakaye okolewa pasipo kuanzishwa na Roho (kama vile Yohana 6:44, 65). Uungu huja kwanza na kuweka ajenda, lakini huhitaji kwamba lazima wachukue hatua katika imani na toba, kwa hali zote mwanzoni na kuendelea. Mungu hutenda na wanadamu katika ushirika wa agano. Kuna faida na uwajibikaji! Wokovu hutolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kinashughulika na tatizo la dhambi ya uumbaji la mwanadamu aliyeanguka. Mungu amekwisha kutoa njia na kuwataka wale wote walioumbwa kwa sura yake kuitikia kwenye pendo lake katika Yesu.

Kama ukihitaji kusoma zaidi juu ya somo hili toka kwenye mtizamo wa wale wasio wafuasi wa Calvin, angalia

- 1. Dale Moody, *The Word of Truth*, Eerdmans, 1981 (kur. 348-365)
- 2. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
- 3. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inayaainisha matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuzichukulia ahadi kama kibali cha kuishi pasipo mafanikio, maisha ya ubinafsi na (2) kuwatia moyo wale wote wanaojitahidi na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kuwa makundi potofu yanachukua jumbe zisizo sahihi na kujenga miundo ya kithiolojia juu ya sura za Kibiblia. Baadhi ya Wakristo huhitaji ujumbe wa ahadi, wakati wengine huhitaji onyo kali! Ni kundi lipi ulilopo wewe?

**4:15 "kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu"** A. T. Robert son anatoa fasiri ingine inayowenza kutumika, "kuchukuliana na udhaifu wetu" (kama vile Ebr. 2: 17-18). Yesu hakuwahi kuwa na asili ya dhambi na hakuwahi kutenda dhambi japo alikuwa anakutana na majoribu mazito kweli kwasababu ya dhambi za wanadamu.

▣ "alijaribiwa" Neno (*peirazō*) lina visawe vya "kujaribu kwenye lengo la kusababisha ucharibifu" (kama vile Ebr. 2: 18; 3: 9; 11: 37). Ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu ambayo inahamasisha hali ya kumalizika kwa namna ya msaidizi wan je kama vile mjaribu. Neno hili ni kwa ajili ya Shetani ("yeye ajaribuye") katika Mt . 4:3 (pia tazama katika Marko 1:13). Angalia Mada Maalum katika Ebr. 2: 18.

▣ "katika mambo yote, bila kufanya dhambi" Yesu ni vyote Mungu kamili na mwanadamu kamili na bado anatuelewa! Hatahivyo hataki tushiriki katika uasi wa mwanadamu aliyeanguka na uhuru kutoka kwa Baba (yaani wasio na kosa, wasio na dhambi, kama vile Ebr. 2: 17-18; 7:26; Luka 23:41; Yohana 8: 46; 14: 30; 2 Kor. 5: 21; 2:78; 1 Pet. 1:19; 2:22; 3:18; 1 Yohana 3:5).

**4:16 "hivyo tujongee karibu"** Hii ni kauli ya kati ya wakati uliopo (yenye ushahidi) tegemezi, ambayo inasisitiza kuhusishwa kunakoendelea kwa mada lakini pamoja na kiashiria cha uwezekano wakutokea. Hili ni neno la

kiufundi katika Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani (LXX) kwa ajili ya kuhani anayemkaribia Mungu. Katika Waebrania neno hili linatumika juu ya uwezo wa mwanadamu aliyeanguka kumkaribia Mungu kwasababu ya dhabihu ya Yesu (kama vile Ebr.4:16;7:25;10:1,22;11:6). Yesu amewafanya wafuasi wake "ufalme wa kikuhanu" (kama vile Kut. 19: 5, 6; 1 Pet. 2: 5, 9; Ufu. 1:6).

■"**kwa ujasiri, ili tupewe rehema**" Neno "ujasiri" humaanisha "uhuru wa kuzungumza kwa ujasiri." Tuna ujasiri na hivyo, ujasiri wa kukaribia uwepo wa Mungu kuitia Yesu Kristo (kama vile Ebr. 10: 19, 35). Hii ni sawasawa na ishara ya pazia lililochanika katika hekalu la Herode huko Yerusalemu katika siku Yesu aliyofariki (kama vile Mt. 27: 51; Marko 15: 38; Luka 23:45). Kuitia Yesu watu wenye dhambi wanaweza kuja mbele ya Mungu mtakatifu amabapo wanapokea rehema na neema, sio hukumu.

■"**kiti cha neema**" Huu unaweza kuwa mzunguko kwa Mungu kama matumizi ya sauti irabu. Mwandishi (kama vile Ebr. 9:11, 24), lakini pia kiti cha enzi cha mbinguni (kama vile Ebr. 1: 8; 4: 16; 8: 1;12:2).

■"**kutusaidia wakati wa mahitaji**" Muktadha unazungumzia maonyo zaidi ya kushikilia maungamo yetu. Mungu hakika atatusaidia nyakati za majoribu na magumu (1) kuitia Yesu na (2) kwa tabia Yake mwenyewe.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki.

Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini sura hii ni ngumu sana kwetu kuilewa?
2. Kwanini msisitizo umewekwa kwenye "ngoja" inajirudia rudia katika Waebrania?
3. Je kuna umuhimu wa kithiolojia kwa Yesu kuitwa vyote "Yesu" na "Mwana wa Mungu" katika Ebr. 4: 4?
4. Nini kinamaanishwa kwamba Yesu "alipita katika mbingu"?
5. Ni kwa namna gani ustahimilivu unahusiana na usalama wa mwamini?

## WAEBRANIA 5

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>               |  |  |  |  |
|--|--|--|--|--|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                                     | <b>NKJV</b>  | <b>NRSV</b>                            | <b>TEV</b>   | <b>NJB</b>   |
| Yesu Kuhani<br>Mkuu wa Juu<br><br>(4:14-5:10)<br><br>5:1-4 | Dhamira ya Yesu<br>Kuhani wetu Mkuu<br><br>Sifa za Ukuhani<br>Mkuu<br>5:1-4<br><br>Kuhani Milele<br><br>5:5-10 | (4:14-5:14)<br><br>1:1-6<br><br>5:7-10 | Yesu Kuhani Mkuu<br><br>(4:14-5:10)<br><br>5:1-6<br><br>5:7-10 | Yesu Kuhani Mkuu<br>Mwenye Huruma<br><br>(4:14-5:10)<br><br>5:1-10 |
| Onyo Dhidi ya<br>Kujitenga na<br>Mungu<br><br>(5:11-6:12)  |  |  | Onyo Dhidi ya<br>Kuiacha Imani<br><br>(5:11-6;17)              | Maisha ya Kikristo<br>na Thiolojia                                 |
| 5:11-6:8   | Ukomavu wa<br>Kiroho   | 5:11-14                                | 5:11-14  | 5:11-14  |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Katika Waebrania Ebr. 3:1 maneno yanawekwa katika utangulizi ili kumwelezea Yesu: "mtume" na "kuhani mkuu." Ya pili inaboreshwu kwa upekee katika Waebrania (kama vile Ebr. 2:17; 3:1; 4:14-15; 5:5,10; 6:20; 7:26,28; 8:1,3; 9:11; 10:21).
- B. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania alijua kwamba dhana ya Yesu kama kuhani mkuu katika mlolongo wa Melkizedeki ingekuwa ya muhimu kwa Wakristo wa Kiyahudi walio wapokeaji wa dhana hii.

- C. Mkusanyiko wa kiuandishi, 5:11-6:20, uko katika mabano ndani ya mjadala wa mwandishi kuhusu Melkizedeki ili kuwaasa Wayahudi waaminio na Wayahudi wasioamini.
- D. Katika Ebr. 5:11-6:20 tuna viwakilishi vitatu vya msingi: "sisi" (5:11); "nanyi" (5:11-12—mara tatu); na "hao"/"hao" (6:4-8). Viwakilishi hivi vinayaakisi akundi matatu.
  1. "sisi" na "yetu," 5:11; 6:1-3, mwandishi na kundi lake la kimisheni
  2. "nanyi," 5:11-12; 6:9-12, Wayahudi wamwaminio yule anayeandikiwa na mwandishi
  3. "hao" na "wale," 6:4-8, Wayahudi wasio amini walio na pande mbili za marafiki wa wapokeaji wa barua

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 5:1-4

<sup>1</sup>Maana kila kuhani mkuu aliyetwaliwa katika wanadamu amewekwa kwa ajili ya wanadamu katika mambo yamhusuyo Mungu, ili atoe matoleo na dhabihu kwa ajili ya dhambi; <sup>2</sup>awezaye kuwachukulia kwa upole wao wasiojua na wenye kupotea, kwa kuwa yeye mwenyewe yu katika hali ya udhaifu; <sup>3</sup> na kwa sababu hiyo imempasa, kama kwa ajili ya watu, vivyo hivyo kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe, kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi. <sup>4</sup>Na hapana mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima hii, ila yeye aitwaye na Mungu, kama vile Haruni.

**5:1-4** Mistari ya1-4 inaeleza juu ya makuhani wakuu wa Kilawi wa Agano la Kale.

1. atokaye katika moja ya makabila (Lawi)
2. asimamaye mbele za Mungu badala ya wanadamu
3. atoaye sadaka na dhabihu kwa ajili ya dhambi (kama vile Ebr. 8:3; 9:9)
4. anayeshughulika na wenye dhambi kwa upole kwa kuwa naye ni mwenye dhambi (kama vile 16:3,6)
5. hachukui heshina binafsi, bali aneheshimishwa kwa uchaguzi na matumizi ya Mungu

### 5:2

NASB, NRSV " kwa upole "

NKJV "kwa huruma"

TEV "awezaye kuwa mpole"

NJB "atambuaye"

Hili neno la Kiyunani linatumika hapa tu katika Agano Jipyä na halijitokezi katika Maandiko yote ya Kiebrania. Hili linatumika katika Aristea 256 kuirejelea falsafa ya wastani (kama vile Moulton na Milligan, *The Vocabulary of the Greek New Testament*, uk. 406).

▣"wasiojua na wenye kupotea" Katika Agano la Kale dhambi za kutojuanashauku zinasamehewa kuitia dhabihu (kama vile Law. 4:2,22,27; 5:15-18; 22:14; Hes. 15:22-31), lakini dhambi za kukusudia hazikusamehewa kwa namna hiyo (kama vile Kumb. 1:43; 17:12,13; 18:20; Zaburi 51).

Katika *Word Pictures in the New Testament*, Juzu. 5, A. T. Robertson anatengeneza uhusiano wa kthiolojia kati ya dhambi za kukusudia za Agano la Kale ambapo hapakuwa na msamaha kuitia dhabihu na maonyo ya Ebr. 310:26. Usemi wake ni "kwa kujitenga" (3:12; 10:26) hakuna radhi inayotolewa" (uk. 368).

Paulo aliamini juu huruma aliyokuwanayo Mungu juu yake kwa sababu ya kutokuelewa kwake juu ya kweli na si dhamira yake ya kuikataa injili.

**5:3 "na kwa sababu hiyo imempasa, kama kwa ajili ya watu, vivyo hivyo kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe, kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi"** Maelezo haya yanarejelea hatua za kuhani mkuu ajipatanishaye yeye mwenyewe yanapatikana katika Law. 9:7-17 (uwekwaji wakfu wa awali; 16:6-19 Siku ya Upatanisho; na Ebr. 9:7. Tunajifunza kutokana na Ebr. 7:26,27 kwamba kamwe Yesu hakujifanya sadaka kwa ajili ya dhambi yake, bali yeye analilewa hitaji letu (kama vile Ebr. 4:15).

**5:4 "hapana mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima"** Mungu analichagua kabilia Fulani (Lawi) na nyumba fulani (nyumba ya Haruni, kama vile Kut.28:1; 1 Nya. 23:13) kutenda kama kuhani (kama vile Hes. 16:40; 18:7; 1 Sam. 12:9-14; 2 Nya. 16:18).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 5:5-10**

<sup>5</sup> Vivyo hivyo Kristo naye hakujitokuza nafsi yake kufanywa kuhani mkuu, lakini yeye aliywambia,

"Ndiwe mwanangu,

Mimi leo nimekuzaa."

<sup>6</sup> kama asemavyo mahali pengine,

"Ndiwe kuhani wa milele

Kwa mfano wa Melkizedeki."

<sup>7</sup> Yeye, siku hizo za mwili wake, alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu; <sup>8</sup>na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata; <sup>9</sup>naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii; <sup>10</sup>kisha ametajwa na Mungu kuwa kuhani mkuu kwa mfano wa Melkizedeki.

**5:5 "Kristo naye hakujitokuza nafsi yake"** Tazama Yohana 8:50,54.

◻ "kufanywa kuhani mkuu" Ingekuwa vigumu sana kulishawishi kundi la Wayahudi kwamba Yesu alikuwa kuhani mkuu wakati alipokuja kutoka uzao wa Lawi. Hii ndiyo shabaha ya majadiliano haya mapana (kama vile Ebr. 4:14-5:10; 6:13-7:28) yaliyojikita katika nukuu za Agano la Kale.

◻ "lakini yeye aliywambia" Mwandishi anaeleza kwamba Baba anaikiri nafasi ya Yesu iliyotukuzwa kuitia msingi wa Zaburi ya kikuhanu, 2:7. Baba anainukuu Zaburi hii hii iliyounganishwa na Isa. 42:1 wakati wa ubatizo wa Yesu (kama vile Ebr. 3:17) na kubadilika kwake (kama vile Mt. 17:5).

Arius yaani., katika karne ya nne b.k.) katika mgogoro wake wa kithiolojia pamoja na Athanasius kuhusiana na Uungu kamili wa Yesu) anaitumia sehemu ya pili ya nukuu kueleza kwamba Yesu alikuwa uumbaji wa kwanza na wa Mungu mkuu sana (kama vile Mit. 8:22-31), lakini msukumo wa nukuu ni uana wa Yesu (kama vile Ebr. 1:2; 3:6; 5:8; 7:28). Zaburi asilia ilikuwa sherehe za mwaka za urejesho wa Mfalme wa Israeli na Yuda.

#### **5:6 "Ndiwe kuhani wa milele**

**Kwa mfano wa Melkizedeki**" Hii ni nukuu itokayo katika Zab. 110:4. Zaburi hii ni ya kipekee katika ukweli kwamba kwa upekee inampa Masihi vyote kazi ya ukuhani na ya kifalme (yaani., miti miwili ya mizeituni, kama vile Zek. 4:3,11-14; na yaani., Yoshua kama tawi, kama vile Ebr. 6:13). Tunajifunza kutoka katika Magombo ya Bahari Chumvi kwamba Wa-essene walikuwa wakiwatarajia Masihi wawili, mmoja wa kifalme na mwingine wa kikuhanu. Yesu alizikamilisha kazi zote mbili. Kama ilivyo kweli, Yeye alizikamilisha kazi tatu za Agano la Kale za kupakwa mafuta: nabii, kuhani na mfalme (kama vile Ebr. 1:1-3).

◻ "Melkizedeki" Maboresho kamili ya wazo hili yako katika sura ya 7. Mfano unachukuliwa katika Mwa. 14:17-20,

ambapo ye ye ni kuhani wa Kikanaani/mfalme wa Salemu (Yebusi, Yerusalem).

**5:7 "siku hizo za mwili wake"** Maelezo haya yanamrejelea Yesu, si Melkizedeki. Haya hayanaamishi kudokeza kwamba Yesu hayuko katika hali ya ubinadamu. Yesu Alitwaa umbo mwili na kubaki umbo mwili milele.

▣ "maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi" Kifungu hiki kinaweza kuhusiana na tendo la Yesu ndani ya Gethsemane lilliozungumziwa katika Mt. 26:37 na Luka 22:44. Hakika hili lilihusiana na viwango vitatu vya maombi ya walimu wa sheria za Kiyahudi, yenye kuonyesha undani wa hisia za Yesu ndani ya Bustani ya Gethsemane au maombi yake ya kikuhani yaliyo katika Yohana 17 usiku wa kalamu ya Pasaka ya wanafunzi kabla ya kwenda Gethsemane.

▣ "awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti" Je! Yesu alikuwa na hofu ya mauti? Mauti ni asili ya woga wa mwanadamu na Yesu alikuwa mwanadamu kamili. Kwa hali ya juu nafikiri alikuwa akiogopa kuupoteza ushirika pamoja na Baba (kama vile Marko 15:34, kwa kunukuu Zaburi 22). Alijua ye ye ni nani na kwa nini alikuja (kama vile Marko 10:45; Mt. 16:21).

Nafsi zote za Uungu zilihusishwa katika ufufuo wa Yesu, si baba pekee kama vile Roho, Rum. 8:11; na Yesu, Yohana 2:19-22; 10:17-18). Mara nyingi Agano Jipya linaleza kwamba ni Baba aliyemfufua Yesu (kama vile Matendo 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 6:4,9; 10:9; 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14; Gal. 1:1; Efe. 1:20; Kol. 2:12; 1 The. 1:10.

Kifungu hiki kinaweza kuakisi maandiko kadhaa ya Agano la Kale yanayoeleza kwamba YHWH atamwokoa Masihi dhidi ya kifo cha kimwili (kama vile Zab. 33:19; 56:13 au Hos. 13:14) au kumfufua kutoka mauti (kama vile Zab. 16:10; 49:15; 86:13). Ikiwa muktadha huu unayaakisi maombi ya Yesu aliyoyafanya ndani ya Gethsemane, kisha uchaguzi #1 ni bora zaidi.

**NASB** "pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu"

**NKJV** "na akasikilizwa kwa sababua ya woga wake wa utukufu"

**NRSV** "akasikilizwa kwa sababua ya staha ya unyenyekevu wake"

**TEV** "Kwa sababu ya utii na moyo wa kujitoa, Mungu akamsikia"

**NJB** "akafanikiwa kusikilizwa kwa hofu"

Kifungu hiki, kama Rum. 1:4, kilitumika ili kuiunga mkono dhana ya kithiolojia ya kujitenga ijulikanayo kama "ukubalifu," ambayo inaleza kwamba Mungu alimkirimia Yesu kwa sabu ya Uungu wake, maisha ya utii. Kitabu cha Agano Jipya kama chenye maneno yote yanayowasilisha fumbo kwamba Yesu alikuwa Uungu wenye umbo mwili na alikirimiwa kwa huduma yake nzuri! Kwa kiasi fulani, yote yako sahihi.

Tofauti zilizo katika tafsri za lugha ya Kiingereza zinatokana na utata wa neno la Kiebrania "ogopa," hasa kama linavyotumika kwa mwanadanu aliye na uhusiano na Mungu. Inaonekana kwamba hili linamaanisha kwamba "kustahii kwa hofu" au uchaji, si "woga." Maana yake ya msingi ni "kushikiria pasipo hofu" katika maana ya kuyafanya mapenzi ya Mungu yanayojulikana.

**5:8 "ingawa ni Mwana"** Hili neno "mwana" Halipaswi kuwekwa katika herufi kubwa. Huu ni mlolongo mwininge wa ulinganifu kati ya mwanafamilia dhidi ya mtumishi wa familia (kama vile Ebr. 1:2; 3:6; 5:8; 7:28).

▣ "alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata" Hiki kipengele chote kimesisitiza vyote Yesu kama "mwana" wa Mungu (kama vile Ebr. 4:14) na bado ni mwanadamu (kama vile "katika siku za mwili wake" Ebr. 5:7, 5:7). Yeye alijaribiwa; Aliomba; Alilia; Aliiteswa; Alijifunza kutii! Kithiolojia ni vigumu kuuelewa Uungu halisi wa Yesu na

ubinadamu wake halisi kama moja ya uhalisia (asili moja). Historia nzima ya Kanisa, kwa vyo vyote vile tendo la kujitenga limeshamiri wakati upande fulani ulipokashifiwa (kama vile 1 Yohana 4:1-3).

Ni vigumu kwa waanimi kubaini kwamba yawapasa kuufuatisha mfano wa Yesu. Hili ndilo tatizo walilokumbana nalo wale waliokupokea kuamini. Je! Wangkuwa, kama Yesu, kumfuatisha hadi mwisho, hata yakijitokeza mteso? Mteso ni sehemu ya mkusanyiko (kama vile Ebr. 2:10; Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-21; 16:1-2; 17:14; Rum. 8:17; 2 Kor. 4:16-18; 1 Pet. 4:12-19).

Ni kwa namna gani angeathiriwa ikiwa alikuwa mmoja wa Uungu? Lazima hili liyarejelee maendeleo ya mwanadamu (kama vile Luka 2:40,52). Mteso yalilikombua kusudi la kuliendeleza kusudi kama ambavyo isingefanya. Ikiwa ni kweli kwamba shabaha ya Mungu kwa kila mwamini ni kumfanana Kristo (yaani., Rum. 8:29; Efe. 4:13), na kwa nini Wakristo wa sasa wa kimagharibi wanalikwepa kila jambo ambalo huwa na matunda ya ukomavu?

**5:9 "naye alipokwisha kukamilishwa"** Hii ni kauli tendwa endelevu (yenye ushahidi) ya wakati uliopita usio timilifu. Hili neno "alipokwisha kukamilishwa" linaamanisha "asili" au "kutengwa moja kwa moja kwa ajili ya kazi iliyoelekezwa." Huu ukamilifu au ukomavu wa wote Yesu na wafuasi wake ndicho kitovu cha dhana katika Waebrania (kama vile Ebr. 2:10; 5:9,14; 6:1; 7:11,19,28; 9:9,11; 10:1,14; 11:40; 12:2,23). Tazama Mada Maalum katika Ebr. 7:11.

▣**"kwa watu wote wanaomtii"** Utii ni ushahidi wa uanafunzi wa kweli (kama vile Luka 6:46). Yesu ni mfano ulio katika maeneo yote. Utii hutoa ushahidi wa wokovu wa kweli!

**5:10 "ametajwa na Mungu kuwa kuhani mkuu"** Kwa kadri fulani katika Waebrania kumekuwana majina matatu ya Yesu yaliyotajwa: (1) mwana, (2) mtume, na (3) kuhani mkuu. Tazama [MADA MAALUM: YESU KAMA KUHANI MKUU](#) katika Ebr. 2:17.

▣**"kwa mfano wa Melkizedeki"** Melkizedeki anadokezwa kwa sababu ni mtu pekee katika Agano la Kale anayetwa khani na mfalme, na ambaye kwa utosherevu aliyakamilisha ahitaji ya kithiolojia ya majadiliano haya sheria za Kiyahudi. Melkizedeki ni mfano wa kivuli fulani cha Mwa. 14:17-20 na Zab. 110:4 anayetumika kueleza ukuu wa ukuhani wa Yesu juu ya Ukuhani wa Aruni. Tazama mjadala kamili katika sura 7.

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 5:11-14

<sup>11</sup>Ambaye tuna maneno mengi ya kunena katika habari zake; na ni shida kuyaeleza kwa kuwa mmekuwa wavivu wa kusikia. <sup>12</sup>Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. <sup>13</sup>Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. <sup>14</sup>Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwu kupambanua mema na mabaya.

**5:11-6:12** Huu ni muungano mmoja wa kiuandishi. Migawanyo ya Sura na mstari haikuvuviwa na iliongezwa baadaye. Tazama Tambuzi za Kimuktadha za sura ya 6.

**5:11 "zake"** Hiki kiwakilishi kwa vyo vyote kinaweza kuwa jinsi ya kiune au isiyo na upande. Nafikiri hii isiyo na upande inaendana zaidi (kama vile NRSV, TEV, NJB, NIV). Hivyo, hii ingeurejelea u-Melkizedeki wa ukuhani wa Yesu. Waebrania 5:11-6:20ni mabano ya kitheolojia. Mwandishi atarudi kwa Melkizedeki katika Ebr. 7.

▣ "tuna" Kifasihi huu ni wingi, na wingi huu unamrejelea mwandishi mwingine.

▣ "mmekuwa wavivu wa kusikia" Muktadha huu ni wa kipekee katika Waebrania katika viwakilishi hivi vilivyotumika: "mmekuwa" (Ebr. 5:11,12; 6:9-12), "tuna" na "kwetu" (Ebr. 5:11; 6:1-3,9), na "wale" (Ebr. 6:4-8). Tazama Tambuzi za Kimuktadha, D. Huu unaonekana kuyaunga mkono matengenezo mapya ya kihistoria ambayo kitabu cha Waebrania kiliyaandika kwa ajili ya kundi la Wayahudi waaminio ambao bado walikuwa akiendelea kufanya ibada ndani mazingira ya sinagogi pamoja na Wayahudi wasio amini, ambao kamwe hawakuwai kuyakumbatia matokeo ya injili.

Hii ni sentensi tendaji elekezi ya wakati timilifu, yenye kusisitiza hali ya kuwa katika utulivu. Hili neno "wivu" linatumika mara mbili tu katika Agano Jipy, hapa na katika Ebr. 6:12. Mwandishi alikuwa na maelezo magumu, si kwa sababu ya jambo linalozungumziwa, bali ni kwa sababu ya kutokomaa kwa wasomaji. Hawa wamekuwa wagumu kusikia na kuwa wavivu katika masuala ya kiroho.

**5:12 "Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu"** Ingawa hawa waamini wamekuwa Wakristo kwa muda mrefu hado hawajakomaa. Urefu wa wakati hausiani moja kwa moja na kutokomaa. Inaonekana hawa walikuwa wakiendelea kuwa na ushirika na Wayahudi wasio amini katika msingi wa mkanganyiko masuala yasiyo ya Kiyahudi (kama vile Ebr. 6:1-2). Huenda hili ni tendo la (1) kuyakwepa mateso ya kiserikali na /au (2) kulikwepa "agizo kuu" ahadi ya Wakristo iliyohitajika.

**NASB "mafundisho ya kwanza"**

**NKJV "mafundisho ya awali"**

**NRSV "mambo ya msingi"**

**TEV "masomo ya kwanza"**

**NJB "mambo ya mafundisho"**

Neno hili linawenza kuwa na maana zenyе kudhaaniwa (yaani., uwanja mpana wa kimantiki).

1. mafundisho yamsingi kuhusiana na jambo fulani
2. chimbuko la jambo
3. nguvu ya kimalaika (kama vile Gal. 4:3,9; Kol. 2:8)

Katika muktadha huu #1 inaonekana kuwa bora zaidi. Mwandishi anaeleza kwamba hawa waamini ambao hawajakomaa wanahitji misingi ya fundisho la Kiktisto (tumia # 1), lakini katika Ebr. 6:1, maelezo #2 yaendana vema kwa sababu 6:1-2 ina muoanisho wa mafundisho Kiyunani, si upekee wa mafundisho ya Kikristo, ambayo yanatakiwa kurejea nyuma. Hapa neno la Kiyunani ni *stoichea*, ambapo katika Ebr. 6:1 ni *archē* (Tazama Mada Maalum: *Archē* katika Ebr. 3:14)

▣ "maneno ya Mungu" Neno hili linazitumia kweli za Agano la Kale katika Matemdo ya Mitume 7:38 na Rum. 3:2.

▣ "maziwa . . . chakula kigumu" Hayayote yametolewa na Mungu na yoteyanahusiana na nyakati fulani. Hata hivyo, maziwa hayahusiani na ukonavu (kama vile 1 Kor. 3:2; 1 Pet. 2:2).

**5:13 "neno la haki"** Swali lenye kufasirika ni ni kwa namna gani kifungu hiki kinaoana na kifungu "mema na mabaya" cha Ebr. 5:14? Toleo la NJB linatafsiri swali la kwanza kama lenye mafundisho yenye kuhusiana, "mafundisho ya kuikomboa haki." Toleo la TEV linavitafriri hivi kama ufanano "haki na kosa" (Ebr. 5:13) na "mema na mabaya" (Ebr. 5:14). Kifungu cha kwanza kinashughulikia tatizo la kutokomaa, ambapo cha pili kinashughulikia

tatizo la uhaba wa tendo /uzoefu.

Inawezekana kwamba kifungu hiki kiko katika tofauti "mafundisho ya awali" ya Ebr. 5:12; 6:1. Kwa namna fulani kinaweza kuirejelea kama chenye kuyarejelea mafundisho ya Kiyahudi ya Ebr. 6:1-2.

Kwa neno la kujifunza linalohusiana na haki tazama mada maalum katika Ebr. 1:9.

**5:14 "akili"** Neno hili linatokana na asili unaotafsiriwa kama "ukamilifu" katika Ebr. 5:9. *Telos* lenye kumaanisha ukomavu, kutengwa kwa ukamilifu kwa ajili yazi fulani iliyokusudiwa. Tazama Mada Maalum katika Ebr. 7:11. Familia ya Yesu ni mfano wa uaminifu na ukuaji unaoelekea ukomavu (kama vile Ebr. 5:8-9), kama yanavyotakiwa kuwa maisha ya waamini. Wayahudi hawa waaminio walikuwa wamezoea baadhi ya mateso (kama vile Ebr. 12:4), lakini walikuwa na tabia ya kurudi nyuma (kama vile "rudi nyuma," 10:38) katika uhusiano na Dini ya Kiyahudi.

**▣"ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu, yenye kuzungumzia tendo lenye kurudiwa rudiwa ambalo liliunganishwa katika kuwa katika hali tulivu—mazoea huleta utimilifu!

Kitenzi hiki hiki kinatumika kuwazungumzia wanafunzi wa Mungu katika Ebr. 12:11.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini ni vigumu sana kwa watu wa Kiyahudi kuikubali kweli kwamba Yesu alikuwa kuhani mkuu?
2. Ni kwa namna gani mateso yanawiana na ukonavu, kwa wote Yesu na waamini?
3. Ni sababu gani zilizowasababisha viongozi hawa kutokomaa?

## WAEBRANIA 6

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>      |   |  |   |   |
|---|---|--|---|---|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                            | <b>NKJV</b>                             | <b>NRSV</b>                                | <b>TEV</b>                                    | <b>NJB</b>                                      |
| Onyo dhidi ya ukana<br>ji wa Imani<br>(5:11-6:12) |   |  | Onyo dhidi ya<br>kuikana imani<br>(5:11-6:12) | Mwandishi<br>anaelezea dhamira<br>yake          |
| 5:11-6:8  | Hatari kuu iliyo mbele<br>6:1-8         | Ushawishi na kusudi<br>la tangazo<br>6:1-8 | 6:1-3   | 6:1-8   |
|   | Kadirio bora                            |  | 6:4-8   | Maneno ya<br>Tumaini na kutia<br>moyo<br>6:9-12 |
| 6:9-12  | 6:9-12                                  | 6:9-12                                     | 6:9-12  |   |
| Ahadi za Mungu<br>za uhakika                      | Kusudi la Mung la<br>uhakika kwa Kristo |  | Ahadi za Mungu<br>za uhakika                  |   |
| 6:13-20   | 6:13-20                                 | 6:13-20                                    | 6:13-20                                       | 6:13-20   |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

#### **KUFUATATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. Nk.

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA WAEBRANIA 5:11-6:12**

- A. Kwa sababu ya kutumia viwakilishi vya "sisi" katika Ebr. 6:1-3, "wale/wao" katika Ebr. 6:4-8, na "wewe" kwenye Ebr. 6:9-12 na 5:11-12, ninaamini kwamba makundi mawili tofauti yameelezewa kwenye sura ya 6: Wayahudi waaminio na Wayahudi wasioamini. Pia, Wayahudi (sio Mkristo) asili ya msingi wa mafundisho ya Ebr. 6:1-2 lazima yalenge katika ukweli unaoshirikiana na Uyahudi. Yanaonekana makundi matatu yametajwa.
  1. Mwandishi na /kikosi chake cha kazi ("sisi" na "tu," Ebr. 6:1-3,9; 5:11)
  2. Wayahudi wasioamini ("wale" na "wao," Ebr. 6:4-8)
  3. Wayahudi waaminio ("wewe," Ebr. 6:9-12 na 5:11-12)
- B. Kuna nadharia kadhaa juu ya nani anaelezewa.

1. Ni nadharia tete (ambayo kwa kawaida inatoa mahitaji "ikiwa" kwenye Ebr. 6:6)
  2. Inarejelea kwa Wayahudi wasioamini
  3. Inarejelea kwa uasi wa kweli (Wayahudi wanaamini juu ya kuja kwa matumaini ya Agano la kale na utaratibu badala ya kuendelea kuwa na imani katika Kristo kama Mashihi)
  4. Inarejelea kwa hali ya karne ya kwanza pekee (ambayo intambua mpangilio wa kihistoria kama utaratibu wa sinagogi la waaminio na Wayahudi wasioamini)
  5. Inarejelea mifano ya wasiokuwa na imani wa Agano la kale, sio waaminio wa sasa
- C. Maonyo ya Ebr. 6:1-12 lazima yasimuliwe kwenye maonyo yaliyopita kwa
1. Kuwa na tahadhali ya kuchukuliwa sasa na nanga imara, Ebr. 2:1
  2. Kuwa na tahadhali ya ukaidi wa wasio na imani (kama Waisraeli wa Agano la kale), Ebr. 3:12-19
  3. Kuwa na tahadhali ya waaminio wachanga walioachwa, Ebr. 5:11-14
- D. Majadiliano ya sasa kwenye kanisa juu ya "wataokolewa sasa wataokolewa daima"; "wataokolewa, waliopotea, na kisha wataokolewa tena"na "walio nje watakuwa nje daima" inazungusha:
1. Kutumia maandiko yaliyoachwa (maandiko ya kuhakiki)
  2. Kutumia mambo yaliyofasiriwa yenye mantiki (kipaumbele cha sababu juu ya machapisho)
  3. Kutumia teolojia ya mpangilio wa ramani (mafundisho ya Kalvin, mafundisho ya Armenia, ya Nadharia ya Mgao, n.k.)
- E. Kuna mifano mingi ya kibiblia ya watu wenye matatizo yanayosimuliwa katika imani yao (tazama mada maalumu katika Ebr. 6:5); lakini hakuna jibu rahisi ambalo litawafunika wote.
1. Waaminio wanakuwa hawafai kwa ajili ya huduma
    - a. Wakristo wa mwilini au viongozi wakristo wazembe (1 Kor. 3:10-15)
    - b. Wakristo watoto (Ebr. 5:11-14)
    - c. Wakristo wasio na haki (1 Kor. 9:27)
    - d. Wakristo wasio na desturi (1 Tim. 1:19-20)
    - e. Wakristo wasio zaa matunda (2 Pet. 1:8-11)
  2. Washuhudiaji waongo wa imani
    - a. Mfano wa udongo (Mt. 13; Marko 4)
    - b. Matunda bila uhusiano binafsi (Mt. 7:21-23)
    - c. Waalimu wa uongo (1 Yn. 2:18-19; 2 Pet. 2:1-19)
  3. Yawezekana uasi wa kidini
    - a. Sauli (Agano la kale)
    - b. Yuda (Agano jipya)
    - c. Waalimu wa uongo (2 Pet. 2:20-22)
    - d. Wafasiri wa mwisho (Ufunuo 22:19 )

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 6:1-8

<sup>1</sup>Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu, <sup>2</sup> na wa mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele. <sup>3</sup>Na hayo tutafanya Mungu akitujalia. <sup>4</sup> Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, <sup>5</sup> na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo, <sup>6</sup> wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsilibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri. <sup>7</sup>Maana nchi inayoinyuwa mvua inayoinyeshea mara kwa mara, na kuzaa mboga zenye manufaa kwa hao ambaa kwa ajili yao yalimwa, hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu; <sup>8</sup> bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.

**6:1-2** orodha hii ya mafundisho inasimulia jambo lililosirikishwa kati ya Uyahudi na Ukristo. Hata hivyo, walikuwa ni wayahudi wa awali (yaani, kuosha na kuweka mikono). Haya yatakuwa ni mafundisho kwamba waaminio na Wayahudi wasio amini watayakubali kirahisi. Hawakuwa na jambo la muhimu la kiteolojia linalomsimulia Yesu wa Nazareti kama Masihi aliyetabiriwa.

Kuna nadharia ya kuaminika kwamba tungo ya awali inaweza kutafsiri *archē* (mafundisho ya kwanza) kama "asili ya Masihi" (kama vile. A. B. Bruce, *The Epistle to the Hebrews*, uk. 197). Inaweza kuwa kwamba kundi la Wayahudi liliishiwa imani na kukua katika mataifa kwa mtindo wa Ukristo na wakauliza ni kwa namna gani Yesu atatimiza unabii wa Agano la kale na unaotarajiwa? Inawezekana orodha ya mafundisho ya Kiyahudi yakalenga mjadala juu ya uwezekano wa kurudi maagano ya Musa kwa ajili ya wokovu, badala ya Yesu?

## 6:1

|           |   |
|-----------|---|
| NASB, NJB | "mafundisho ya kwanza ya kristo"            |
| NKJV      | "mjadala wa kwanza wa kanuni za Kristo"     |
| NRSV      | "mafundisho ya msingi juu ya Kristo"        |
| TEV       | "mafundisho ya awali ya ujumbe wa Wakristo" |

Neno la kiyunani *archē* lina kama uwanda mkubwa sana (tazama mada maalumu katika Ebr. 3:14). Msingi unaosukuma ni mwanzo wa kitu (cha awali kinacho sababisha mamlaka/utawala). Ni kinyume cha muktadha wa *teleios* ("ukomavu" Ebr. 6:1b).

Tatizo la kuifahamu tungo hii ni kwamba kanuni zimetajwa moja moja kwenye Ebr. 6:1-2 haisimuliwi kwa Masihi kama mapokeo zaidi ya mafundisho ya Uyahudi. Hii ni moja ya sababu ya andiko kwa ajili ya kukisia kwamba kitabu kiliandikwa kwa ajili ya wasikilizaji wa Kiyahudi ndani ya sinagogi (kama vile Ebr. 10:25) kwa wote waaminio na Wayahudi wasioamini (kama vile. R. C. Graze, *No Easy Salvation*).

■"**tukaze mwendo**" hii ni kauli tendwa tegemezi ya wakati uliopo, "tuvumilie sisi." Lengo ni kuendelea kuweka akiba kwa mpatanishi wa kiroho! Watazidi kukua katika ukomavu ikiwa wataruhusu uhuru wa Roho kuwatia hamasa wao. Hili ni neno la Kiyunani lilitotumiwa na wanafalsafa kwa ajili ya kutia kiwango cha juu cha ufahamu (kama vile A. T. Robertson's *Word Pictures in the New Testament*, uk. 373).

|            |              |
|------------|--------------|
| NASB, TEV  | "utimilifu"  |
| NKJV, NRSV | "ukamilifu"  |
| NJB        | "ukamilisho" |

Huu ni muundo wa neno la Kiyunani *teleios*, ambalo limetuka hapa pekee kwenye Agano jipya. Tazama Mada Maalumu katika Ebr. 7:11. Ni kinyume cha muktadha wa *archē* katika Ebr. 6:1a (kanuni za msingi). Waaminio hawa ni lazima warudi nyuma ya mada za kiteolojia ambazo zimezoleka kwa marafiki wao wa kiyahudi na waabudio.

■"**kuzitubia . . . imani**" Haya ni masharti ya maagano ya kale na mapya, moja hasi na moja chanya. Kutubu ni mada ngumu kwa sababu ya utata juu ya maana yake. Neno la Kiebrania linaloaksi badiliko la tendo ambapo neno la Kiyunani linaaksi kubadili mtizamo. Kutubu ni kugeuka kutoka kujifikilia binafsi, maisha kujiongoza mwenyewe kwenda kumfikilia Mungu, maisha ya kuongozwa na Mungu.

1. Yesu anaunganisha upungufu wa kutubu na kuangamia (kama vile. Luka 13:3,5 na 2 Pet. 3:9)
2. Kutubu ni muunganiko kama wajibu wa kirafiki katika imani (kama vile. Marko 1:15; Mdo 2:38, 41; 3:16; 19; 20:21)
3. Hata Mungu amethibitisha kama kuwa chanzo cha kutubu (kama vile. Mdo 5:31; 11:18; 2 Tim. 2:25)

**6:2 "mabatizo"** WIngi hakutumika kamwe kwa ajili ubatizo wa Kikristo, lakini kwa ajili ya kutawadha katika Agano la kale (kama vile Mark 7:4; Ebr. 9:10). Mafundisho haya matatu ya njozi sio ya kipekee kwa Mkristo. Yalionekana kuzoleka na mafundisho ya Uyahudi, hasa wale Mafarisayo ambaa walishirikiana na Ukristo.

◻ "kuwekea mikono" Hii imetumika katika maana kadhaa katika Agano la kale na Agano jipya. Inaonyesha uhusiano na

1. Kumtenga mtu kwa kazi iliyochaguliwa na Mungu (kama vile Hes. 27:18,23; Kumb. 34:9; Mdo. 6:6; 13:3; 1 Tim. 4:14; 5:22; 2 Tim. 1:6)
2. Kufanana na sadaka ya kuteketezwa
  - a. Kuhani (kama vile Kut.29:10,15,19; Law. 16:21; Hes. 8:12)
  - b. Kuweka mikono kichwani (kama vile Law. 1:4; 3:2,8; 4:4,15,24; 2 Nya. 29:23)
3. Kufanana na mtu apigwae mawe (kama vile Law. 24:14)
4. Kuomba kwa ajili ya baraka (kama vile Mt. 19:13,15)
5. Kuomba kawa ajili ya uponyaji (kama vile Mt. 9:18; Marko 5:23; 6:5; 7:32; 8:23; 16:18; Luka 4:40; 13:13; Mdo 9:17; 28:8)
6. Kuomba kwa ajili ya kumpokea Roho (kama vile Mdo. 8:17-19; 19:6)

◻ "kufufuliwa wafu... hukumu ya milele" Mafarisayo na Wa-Essene (yaani, jamii ya hati za kukunjwa za bahari mfu) wanashikilia mafundisho haya matukio ya siku za mwisho kuwa yamezoleka na Ukristo.

## MADA MAALUM: UMILELE (*aiōnios*)

Robert B. Girdlestone, katika kitabu chake *Synonyms of the Old Testament*, ana maoni ya kushangaza juu ya neno "umilele":

"Kivumishi *aiōnios* kimetumika zaidi ya mara arobaini katika Agano Jipya. Kwa kuzungumzia uzima wa milele, ambao unachukuliwa kwa sehemu kama zawadi tuliyonayo sasa, kwa sehemu kma ahadi kwa ajili ya ubaadaye. Pia inafanya kazi kwa uwepo wa Mungu usio na ukomo katika Rum. 16.26; kwa thamani ya ondoleo la dhambi lisilokuwa na ukomo la Kristo katika Ebr. 9.12; 13.20; na nyakati zilizopita katika Rum. 16.25; 2 Tim. 1.9; Tito 1.2.

Neno hili linatumika kurejerea moto wa milele, Mt. 18.8; 25.41; Yuda 1:7; adhabu ya milele, Mt. 25.46; hukumu ya milele au shutuma, Marko 3.29; Ebr. 6.2; uharibifu wa milele, 2 The. 1:9. Neno katika vifungu hivi inamaanisha hitimisho na kwa dhahiri ikiashiria kwamba wakati hukumu hizi zikitolewa, muda zaidi zwa uanganizi, mabadiliko au nafasi ya kurudisha nafasi ya mtu ya kwanza, vitakuwa vimekwisha ondoka kikamilifu na milele. Tunaelewa kidogo juu ya wakati wa baadaye, kuhusu mahusiano ya maisha ya mwanadamu na maisha mengine. Ikiwa upande mmoja, sio sawa kuongeza neno la Mungu, upande mwingine lazima tusiondoe; na ikiwa tutayumba yumba katika fundisho la adhabu ya milele kama inavyowekwa katika maandiko, lazima tukubaliane kusubiri tukishikiria injili ya upendo wa Mungu katika Kristo wakati tuktambua kwamba kuna historia isijojulikana ambayo hatuna uwezo wa kuielewa" (kur. 318-319).

**6:3 "kitujalia"** Hii ni sentensi hali daraja la tatuambayohumaanisha tendo linalowezekana. Mungu akitujalia, ikiwa watashirikiana!

**6:4-6a "hao waliokwisha kupewa... kukionja... kufanywa...kulionja...wakaanguka"** Viambata hivi vyote ni vya wakati uliopita usiotimilifu, ambapo Ebr. 6:6b inaanza na mfuatano wa njeo ya vitenzi vya wakati uliopo. Haya ni kama maelezo imara. Maana inaonekana wazi: walimjua Mungu kwa ngazi nyingine, lakini wakaikana imani kamili katika Kristo. Hata hivyo, mambo mawili Kimuktadha yanahitajika kuchunguzwa: (1) uwepo wa makundi matatu ("sisi" [mistari. 1-3], "wale" [mistari. 4-8], "wewe" [mistari. 9-12]) na (2) mafundisho ya asili ya Kiyahudi kwenye Ebr. 6:1-2. Hii inalenga kwenye sinagogi ambalo Wayahudi waaminio na wasioamini waliabudu na kujifunza pamoja. Wayahudi wasioamini kwa wazi waliona nguvu, utukufu, na ukweli wa injili kwenye machapisho na kwenye usuhuhuda na kubadilisha maisha ya marafiki zao waaminio.

Kuna maonyo mawili yanaonekana kwenye Waembrania: (1) kwa Wayahudi waaminio kusimama mbele za hadhara na kanisa linaloteswa na sio kuurudia Uyahudi na (2) kwa Wayahudi wasioamini kumpokea kwa moyo Kristo. Kwa njia nyingi onyo la awali ni la kipekee kwenye kitabu hiki, lakini la pili ni mfanano sana na dhambi ya kutokusamehewa ya Mafarisayo kwenye injili na dhambi ya kifo ya walimu wa uongo katika 1 Yohana.

**6:5 "nguvu za zamani zijazo"** Mfano mwingine wa kupotea unao husika kwenye nguvu za zamani zijazo ni katika Mt. 7:21-23. Wana nguvu bila ushirika binafsi wa muhimu. Jambo hili hili liliweza kusemwa kwa Yuda Iskarioti (kwenye injili), Simon Magnus (kwenye Mdo), na walimu wa uongo (kama vile. 1 Yn 2:18-19).

Tazama Mada Maalumu katika Ebr. 1:2.

▣**"wakaanguka"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu. Huu ni upeo wa Kitheolojia wa sentensi ya Kiyunani kwamba unaanza katika Ebr. 6:4. Tazama Mada Maalumu: Ukanaji wa Imani katika Ebr. 3:12.

## 6:6

|           |                                   |
|-----------|-----------------------------------|
| NASB      | <b>"baada ya hayo"</b>            |
| NKJV      | <b>"ikiwa"</b>                    |
| NRSV, TEV | <b>"baada ya hayo"</b>            |
| NJB       | <b>"na bado kwenye chuki hii"</b> |

Kuna kutokubaliana kati ya wanazuoni wa Kiyunani kama muundo huu ni tabia ya kiungwana au ni muundo wenyе msimamo ulio sambamba kutoka mstari wa 4. Wale wote wanaothibitisha kwenye muundo wa tabia hufanya kwa ajili ya kutetea kusudi la kiteolojia kwamba mstari wa 6a ni hali ya kufikilika. Hata hivyo, sifa hizi zote za kisarufi zinadokeza kwamba zote zimejitokeza.

1. Kurudia rudia mwelekeo endelevu wa wakati uliopita usiotimilifu (kupewa nuru, kukionja, washirika, kilionja na wakaanguka)
2. Kurudia rudia matumizi ya "kai" (na) na tatu mwishoni
3. Makala ya mashitaka ya wingi kwa mwanaume kwenye Ebr. 6:4 ambayo yanasmusilia yote endelevu katika mistari 4-6

|            |                      |
|------------|----------------------|
| NASB, TEV, |                      |
| NJB        | <b>"haiwezekani"</b> |
| NKJV, NRSV | <b>"haiwezekani"</b> |

Neno limejitokeza katika Ebr. 6:4, lakini muktadha mkubwa unahusisha Ebr. 6:6. Hili ni neno la Kiyunani *dunatos* (weza) na kiambishi awali hasi (kutoweza). Maneno haya mawili yametumika na kidokezo cha nini Mungu atatenda na ambacho hatatenda! Imetumika kwenye maandiko ya Kiyunani yaliyo katika mafunjo yaliyopatikana Misri ya (1) mwanadamu hana nguvu za kutosha kufanya kazi na (2) mashahidi hawawezi kuthibitisha. Limetumika mara nne kwa Waembrania.

1. Haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu (6:4)
2. Haiwezekani Mungu kusema uongo (6:18)
3. Haiwezekani kwa sadaka za kuteketezwa za Agano la kale kuoko (10:4)
4. Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu (11:6)

Kwa kila hali neno linamaanisha haiwezekani. Hivyo basi, inashangaza kwamba Lowe na Nida's *Greek English Lexicon of the New Testament* says "kwenye Ebr. 6.4 kutumia *adunaton* inaonekana kuwa mfano wa kutia chumvi kwenye mtazamo wa maonyo dhidi ya ukanaaji wa imani (tazama Ebr. 5.11-6.12). Hivyo basi, mmoja yumkinii akatafsiri *adunaton* katika Ebr. 6.4 kama "ni vigumu sana" (uk. 669). Hii inaonekana ni kiteolojia zaidi kuliko msamiati pale mengine yote yanatumia neno madai kwa Waembrania "haiwezekani".

Kutaka kulichukulia neno hili kwa kawaida ndio sababu inayoongoza kwenye teolojia "kuwa nje mara zote ni kuwa nje" ikiwa hii inarejelea waaminio waliozikana imani zao. Makundi yale ya madhehebu yanayofundisha ukanaaji wa imani pia yanahubiri kutubu na urejesho. Andiko hili linapunguza thamani eneo hili.

Kwa njia nyingi mpangilio wa kihistoria ni ufunguo wa kutafsiri.

1. Makundi mawili yanaelezewa (waaminio na Wayahudi wasioamini)
2. Kundi moja (Wayahudi waaminio ambae hawajafikia ukomavu na na sasa wana kusudia kurudi kwa Musa)

Huu ni mfanano wa Myahudi wa Galatia ambae anajaribu kuamini desturi za Agano la kale (ongeza na Kristo).

Paulo anadai kwamba wameanguka kutoka katika hali ya neema (kama vile Gal. 5:4).

■ "kuwafanya upya" Tazama Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM: KUFANYA UPYA (*ANAKAINŌSIS*)

Neno hili la Kiyunani katika muonekano wake tofauti (*anakainōō*, *anakainizō*) lina maana mbili za msingi

1. "Kukifanya kitu kuwa kipyta na cha tofauti (yaani., bora)" -Rum. 12:2; Kol.3:10
2. "Kufanya badiliko toka kwenye hali ya nyuma iliyokuwa ikipendelewa" -2 Kor. 4:16; Ebr. 6:4-6

(limechukuliwa toka kwa Louw and Nida's *Greek-English Lexicon*, juzu. 1, kur. 157, 594)

Moulton and Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, anasema kuwa neno hili (yaani., *anakkainōsis*) haliwezi kupatikana katika fasihi za Kiyunani mapema zaidi kuliko Paulo. Huenda Paulo amelitunga neno hili mwenyewe (uk. 34).

Frank Stagg, *New Testament Theology*, ana hoja ya kufurahisha.

"kuzaliwa upya na kufanywa upya kunamhusu Mungu mwenyewe. *Anakainōsis*, neno kwa ajili ya "kufanywa upya," ni nomino ya kitendo, na linatumika katika Agano Jipya, likiwa na miundo wa kitenzi, ikielezea hali ya mwendelezo wa kufanyika upya, kama ilivyo katika Warumi 12:2, '....' na 2 Wakorintho 4:16, '....' Wakolosai 3:10 inamwelezea 'mtu mpya' kama 'yule aliyefanywa upya kwa mpangilio kutokana na taswira ya yule aliye muumba.' Kwa maana hiyo ni 'mtu mpya,' 'maisha mapya' 'kuzaliwa upya' au 'kufanywa upya' hata hivyo usanifishwaji, unaangaliwa kwenye kitendo cha awali na kitendo endelevu cha Mungu kama mtoaji na mwezeshaji wa maisha ya milele" (uk. 118).

■ "kwa kuwa wamsulibisha kwa nafsi zao" Mchanganyo wa Kiyunani (*anastauroō*) unaweza kumaanisha "sulibisha" (au "gongomea msumari," muundo huu wa mkazo ni kwenye tafsiri za JB, NEB na Moffatt) au "sulibisha tena" (tafsiri za NASB, NKJV, NRSV, TEB, NJB, NIV). *The Greek-English-Lexicon of the New Testament* na Bauer, Arndt, Gingrich, na Danker, inasema "katika Biblia ya ziada ya Kiyunani neno hili mara zote linamaanisha *sulibisha*" (uk. 61). Tertullian anatumia kifungu hiki kudai kwamba sehemu ya ubatizo wa dhambi hausameheki.

Mababa wa awali wa Kiyunani wanatambua muktadha huu na mchanganyo wa *ana hitaji* "sulibisha tena," Ambayo inafuatwa na tafsiri kubwa za kisasa za kiingereza. Ni kwa namna gani hii teolojia inasimulia ukajani wa imani? Inadokeza waamini; hata hivyo, ikiwa muundo wa mkazo "gongomea msumari binafsi" unafuatwa, kisha wasioamini yawezekana wanarejelewa. Wafasiri lazima waruhusu andiko, sio upendeleo wa teolojia zao au utaratibu wa teolojia, kuongea. Hivyo andiko hili kwa hakika ni gumu kulitafsiri. Mara nyingi tumefikiria kujua kwamba inaweza kuwa nini au isiyo na maana kabla ya kutafiti na

1. Kitabu chote
2. Maonyo manne maalumu
3. Muktadha maalumu

Hata hivyo moja linatafsiri maandiko haya, maonyo ni makali!

■ "na kumfedhehi kwa dhahiri" Neno hili limetumika kwenye Mt. 1:19 kwa ajili Yusufu asitaka kumwaibisha Mariamu hadharani. Ni kwa namna gani hili linasimuliwa katika muktadha? Yumkini hasa inarelejea mwanzo wa kusulibishwa kwa Yesu kama "fedheha mbele ya hadhira" bila kidokezo cha "tena."

**6:8** Yumkini hiki kikawa ni kielelezo kilichochukuliwa kutoka Mwa. 3:17-19 au Isa. 5:1-2 au kinaweza kuwa hata mfano wa udongo unazungumziwa katika Mathayo 13. Kuzaa- matunda ni ushahidi wa kawaada wa kazi inayofaa! Kuzaa- matunda (kama vile Yn. 15:5-6), sio kuchipua, ni ushahidi wa uhusiano wa kweli na Kristo. Matunda ni ushahidi wa, usio wa mashaka!

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 6:9-12

<sup>9</sup> Lakini, wapenzi, ijapokuwa twanena hayo, katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi, na

**yaliyo na wokovu.**<sup>10</sup> Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu, na hata hivi sasa mngali mkiwahudumia.<sup>11</sup> Nasi twataka sana kila mmoja wenu aidhihirishe bidii ile ile, kwa utimilifu wa matumaini hata mwisho;<sup>12</sup> ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu.

**6:9 "wapenzi"** Kifungu hiki kinaonyesha upendo mkubwa na kujali kwamba mwandishi yuko kwa ajili ya viongozi. Mstari wa 11 umetaja (1) "twataka," ambao unawenza kutafsiriwa "shauku kuu" na (2) "kila mmoja wenu," ambayo inaonyesha uhusika wa mmoja mmoja.

▣"**katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi**" Hii ni kauli timilifu tendwa elekezi wingi. Mwandishi alikuwa makini kwamba kundi la viongozi walikuwa Wakristo na wangeweza kuendelea na wajibu ufaao.

Kwa ajili ya "mazuri zaidi" Tazama muhtasari kamili katika Ebr. 7:7.

|                   |                                 |
|-------------------|---------------------------------|
| <b>NASB, NKJV</b> | <b>"yaliyo na wokovu"</b>       |
| <b>NRSV</b>       | <b>"mambo yaliyo ya wokovu"</b> |
| <b>TEV</b>        | <b>"yaliyo ya wokovu wako"</b>  |
| <b>NJB</b>        | <b>"kwenye njia ya wokovu"</b>  |

Hii tungo ya Kiyunani ni dhahiri "ina (kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo) wokovu" ambayo inaeleza wazi kabisa "mambo yaliyo mazuri zaidi" ya Ebr. 6:9.

**6:10 "hata aisahau kazi yenu"** Mungu atahukumu kwa haki katika msingi wa

1. Kitabu cha uzima (kama vile 32:32-33; Zab. 69:28; Dan. 12:1; Luka 10:20; Fil. 4:3; Ebr. 12:23; Ufu. 3:5; 13:8; 17:8; 20:12,15; 21:27)
2. Kitabu cha matendo (kama vile Zab. 56:8; 139:16; Isa. 65:6; Mal. 3:16; Mt. 25:31-46; Gal. 6:7)

▣"**pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu**" Ingawa hawa Wayahudi waaminio hawakufanana kikamilifu na kanisa, walilisaidia kanisa kwenye nyakati za mateso (kama vile Ebr. 10:32-34). Kumbuka sinagogi lilikuwa linafikiriwa kuwa la haki, ambapo kanisa lilikuwa sio halali katika sheria za Rumi kwa wakati huo!

Neno "watakatifu" (*hagioi*) ni kiteolojia inasimuliwa kuwa neno la Agano la kale "takatifu" (*kadash*), ambalo humaanisha "aliyetengwa kwa ajili ya huduma ya Mungu" (kama vile. 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Rum. 1:1; Efe. 1:1; Fil. 1:1). Mara zote ni wingi katika Agano jipya isipokuwa kwa wakati mmoja kwenye Wafilipi 4:21; hata kule, imetumika kushirikisha muktadha. Kuokolewa ni sehemu ya jamii ya maagano ya imani, familia ya waaminio.

Watu wa Mungu ni watakatifu kwa sababu ya shutuma za haki za Yesu kristo (kama vile. Warumi 4 na 2 Kor. 5:21). Ni mapenzi ya Mungu kwamba waishi maisha matakatifu (kama vile Efe. 1:4; 2:10; 4:1; 5:27; Yakobo 2:14-26; 1 Pet. 1:16). Waaminio nao wote wanatangazwa watakatifu (mahali patakatifu) na wameitwa kuishi maisha matakatifu (utakatifu wa kuendelea). Hii ni sifa ya theolojia ya wasiwasi katika Agano jipya kati ya "ufalme wa Mungu ulio tayali" na "ufalme wa Mungu ambao haujawa tayali."

## MADA MAALUM: WATAKATIFU (HAGIOS)

Huu ni usawa wa Kiyunani wa neno la Kiebrania kadosh (NOMINO, BDB 871; KITENZI, BDB 872, KB 1066-1067; tazama Mada Maalum: Takatifu), lililo na maana ya msingi ya kumweka mtu katia usawa, kitu fulani, au baadhi ya sehemu tofauti na matumizi ya YHWH yaliyojitenga. Hili linadokeza dhana ya Kiingereza ya "wekwa wakfu." Israeli lilikuwa "taifa takatifu" la YHWH (kama vile 1 Pet. 2:9, ambayo inanukuu Kut. 19:6). YHWH anaweka mbali na ubinadamu kwa kutumia asili Yake (milele, Utatakatifu usioumbwa) na sifa Yake (ukamilifu wa maadili). Yeye ni kipimo ambapo vitu vyote vinapimwa na kuhukumiwa. Yeye yu kila mahali, Mtakatifu, Mtakatifu wa Watakatifu.

Mungu aliwaumba wanadamu kwa ushirika, lakini anguko (Mwanzo 3) liliisababisha kikwazo cha mahusiano na maadili kati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu mdhambi. Mungu alichagua kuurejesha ufahamu Wake wa uumbaji; hivyo, Anawaita watu Wake kuwa "watakatifu" (kama vile Law. 11:44; 19:2; 20:7,26; 21:8). Kwa imani uhusianao wa YHWH na watu Wake ukawa mtakatifu kwa nafasi zao za kiagano ndani Yake, lakini pia wanaitwa kuishi maisha matakatifu (tazama Mada Maalum: Utakaso, kama vile Mt. 5:48; Efe. 4:1,17; 5:2-3,15; 1 Pet. 1:15).

Huku kuishi kitakatifu kunawezekana kwa sababu waamini wamekubaliwa kwa utimilifu na kusamehewa kupitia (1) Maisha ya Yesu na (2) kazi na uwepo wa Roho Mtakatifu ndani ya fikra na mioyo yao. Hili linahimarisha hali ya ukinzani kwa waamini:

1. kuwa watakatifu kwa sababu ya haki ya Kristo iliyowekwa ndani yao (kama vile Warumi 4)
2. walioitwa kuishi kitakatifu kwa sababu ya uwepo wa Roho (Tazama Mada Maalum: Utakaso)

Waamini ni "watakatifu" (hagioi) kwa sababu ya

1. mapenzi ya yule Aliye Mtakatifu (Baba, kama vile Yohana 6:29,40; 1 Pet. 1:15-16)
2. kazi ya Mwana aliye Mtakatifu (Yesu, kama vile 2 Kor. 5:21; 1 Pet. 1:18-21)

uwepo wa Roho Mtakatifu akaaye ndani (kama vile Rum. 8:9-11,27)

Mara nyingi katabu cha Agano Jipya kinawarejelea watakatifu kama WINGI (isipokuwa mara moja katika Flp. 4:21, lajkini muktadha unalifanya neno hili kuwa WINGI). Kuokolewa ni kuwa sehemu ya familia, mwili, ujenzi! Imani ya kibiblia huanza na mapokezi binafsi, bali suala li ndani ya ushirika wa pamoja. Kila mmoja wetu amekirimiwa kama vile 1 Kor. 12:11) kwa ajili ya afaya, ukuaji, na manufaa ya Mwili wa Kristo—kanisa (kama vikle 1 Kor. 12:7). Tumeokolewa ili kutumika! Utakatifu ni sifa ya familia!

Hili linakuwa adimu kwa waamini (kama vile Matendo ya Mitume 9:13,32,41; 26:10; Rum. 1:7; 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2) na njia ya kuonyesha huduma kwa wengine (kama vile Rum. 12:13; 16:2; Efe. 1:15; Kol. 1:4; 1 Tim. 5:10; Ebr. 6:10). Paulo alichukua wakati wa kipekee wa kujitoa kwa makanisa Mataifa kwa watu wahitaji waliokuwa ndani ya Kanisa Mama ndani ya Yerusalem (kama vile Rum. 15:25-26; 1 Kor. 16:1; 2 Kor. 8:4; 9:1).

**6:11 "kwa utimilifu"** Tambua hii inasimulia matendo ya mtindo wa maisha (kama vile Yakobo, 1 Petro, na 1 Yohana). Utimilifu sio mafundisho ya awali ya kuthibitisha, bali ni maisha ya kuishi (kama vile Mt. 7).

▣ "**hata mwisho**" Ustahimilivu ni mafundisho ya kweli ya kibiblia kama ulinzi. Kwa matunda yao utawatambua (kama vile Mt. 7; Yakobo 2:14-26). Tazama muhtasari wa ustahimilivu katika Ebr. 4:14, pia muhtasari mada maalumu katika Ebr. 7:11.

**6:12 "wavivu"** Hili ni neno sawa sawa kama "goigoi" (kama vile Ebr. 5:11). Limetumika katika kinyume cha "bidi" kwenye Ebr. 6:11. Waaminio hawakui katika kumfanana kristo wala utumishi mkuu wa Wakristo kama walivyo (kama vile Ebr. 12:1-3).

▣ "**wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu**" Hii yumkini ikadokeza kugeuzwa wito wa uaminifu kwenye sura ya 11. Hawa waaminio waminifu wa Agano la kale wanashikilia matatizo makuu hata mwisho na majoribu, mara nyingi matokeo ni kwenye kifo cha kimwili (kama vile. Mara nyingi kwenye sura ya 11 na inawezekana katika Ebr. 12:4). Ahadi za Mungu zinalenga katika kifungu, 6:13-20. Wana uhakika na waaminifu kwa sababu yeche na hakika na mwaminifu!

## **MADA MAALUM: URITHI WA MWAMINI (toka 1 Petro 1)**

Katika Agano la Kale kila kabilia isipokuwa la Walawi lilipokea urithi wa ardhi (kama vile Yoshua 14-22). Walawi, kama kabilia la kikuhanini, wahudumu wa hekaluni, na waalimu wa kanisa la mahali, walionekana kuwa na YHWH Mwenyewe kama mrithi wao (kama vile Zab. 16:5; 73:23-26; 119:57; 142:5; Wimb. 3:24). Waandishi wa Agano

Jipya mara nyingi walichukua haki na upendeleo wa Walawi na kuitumia kwa waamini. Hii ilikuwa ni njia yao ya kudai kuwa wafuasi wa Yesu walikuwa watu wa Mungu na kwamba sasa waamini wote wameitwa kutumika kama makuhani mbele za Mungu (kama vile 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6), kama Agano la Kale linavyo watetea Waisrael wote (kama vile Kut. 19:4-6). Msisitizo wa Agano Jipya sio juu ya mtu binafsi kama kuhanaliye na upendeleo Fulani, bali ni katika kweli kwamba waamini wote ni makuhani, wakihitaji ushirika wa mwenendo wa kitumishi (kama vile 1 Kor. 12:7). Watu wa Mungu wa Agano Jipya wamekwisha pewa majukumu ya Agano la Kale ya kueneza injili ulimwenguni (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5b; Mt. 28:18-20; Lk. 24:46-47; Mdo. 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa ukombozi wa Milele).

Hii ni dhana ya Yesu kama mmiliki wa uumbaji kwa sababu alikuwa ni wakala wa Baba kipindi cha uumbaji (kama vile. Yn 1:3,10; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2-3). Sisi ni warithi wenza kwa vile Yeye ni mrithi (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7; Kol. 3:24). Maandiko yanazungumza kuhusu kurithi kwa waamini (kama vile Mdo 20:32; 26:18; Efe. 1:4; Kol. 1:12; 3:24) vitu vingi kwa sababu ya mahusiano yao ya kifamilia na Yesu ambaye ndiye mrithi wa vitu vyote (kama vile Ebr. 1:2). Kwa hiyo, wao pia ni warithi wenza (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7) wa

1. Ufalme (kama vile Mt. 25:34, 1 Kor. 6:9-10; 15:50; Efe. 5:5)
2. Maisha ya milele (kama vile Mt. 19:29; Ebr. 9:15)
3. Ahadi za Mungu (kama vile Ebr. 6:12)
4. Ulinzi wa Mungu wa ahadi zake (kama vile 1 Pet. 1:4-5)

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 6:13-20**

<sup>13</sup> Kwa maana Mungu, alipompa Ibrahimu ahadi, kwa sababu alikuwa hana mkubwa kuliko yeye mwenyewe wa kumwapa, aliapa kwa nafsi yake, <sup>14</sup> akisema, Hakika yangu kubariki nitakubariki, na kuongeza nitakuongeza. <sup>15</sup> Na hivyo kwa kuvumilia akaipata ile ahadi. <sup>16</sup> Maana wanadamu huapa kwa yeye aliye mkuu kuliko wao; na kwao ukomo wa mashindano yote ya maneno ni kiapo, kwa kuyathibitisha. <sup>17</sup> Katika neno hilo Mungu, akitaka kuwaonyesha zaidi sana warithio ile ahadi, jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika, alitia kiapo katikati; <sup>18</sup> ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyio imara, sisi tulioimbilia kuyashika matumaini yale yawekwayo mbele yetu; <sup>19</sup> tulio nayo kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiyo hata mle mlimo ndani ya pazia, <sup>20</sup> alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu, amekuwa kuhanaliye mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki.

**6:13-20** Hii ni ahadi imara ya ulinzi na matumaini ya msingi katika tabia ya Mungu na ahadi zake (kama vile Ebr. 6:18a), ikiwa tu tutaitikia vizuri kwa upekee (kama vile Ebr. 6:18b).

**6:13 "Kwa maana Mungu, alipompa Ibrahimu ahadi"** Ibrahimu ametajwa kwa sababu alifikiria kuwa Baba wa taifa la Waebrania ambaye kwake YHWH alifanya maagano ya ahadi (kama vile Mwa. 12,15,17,18,22), na pia kwa sababu ya uhusiano wake na Melkizedeki (kama vile. Mwanzo 14). Imani yake kwa Mungu ilikuwepo kabla ya sheria kama mfano wa Agano jipya kwa wale wote wanaoitumia imani (kama vile Warumi 4).

Pia inawezekana kiteolojia kwamba Ibrahimu alichaguliwa kwa sababu Mungu alimwahidi yeye sio kwa matendo yake, lakini katika ahadi ya Mungu isiyo na masharti (kama vile Mwa. 15:12-21; kama "maagano mapya," kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambapo maagano ya Musa yalisisitiza katika utiifu, maagano ya masharti (kama vile Kumbukumbu la Torati 27-28).

▣ "aliapa kwa nafsi yake" Hii kihistoria inarejelea katika Mwa. 22:16-17 (Ibrahimu akimtoa Isaka sadaka) au kimuktadha katika Zab. 110:4 (kama vile Ebr. 7:17,21). Kiapo cha Mungu na ahadi zake zinaweza kufungamana (kama vile. Ebr. 6:16-17). Huu ni msukumo wa kifungu kitheolojia. Matumaini yetu ni kwenye tabia isiyobadilika (kama vile Zab. 102:27; Mal. 3:6; Ebr. 13:8) na ahadi zake Mungu (kama vile Isa. 40:8; 55:11). Hivi ni "vitu viwili visivyobadilika" katika Ebr. 6:18!

**6:14** sehemu hii ya Waebrania inahusisha mwandishi kutumia dondo za Agano la kale kwa Ibrahimu. Mungu alifanya ahadi nae juu ya uzao mwingi kupitia kwa Isaka. Tatizo la kitheolojia ni kwamba sio uzao wote wa asili wa

Ibrahimu walikuwa wafuasi waaminifu kwa YHWH. Walikuwa ni watu wa "maagano", "waliochaguliwa", lakini sio wote walitumia imani binafsi (kama vile Ebr. 6:18b).

**6:15** hii haielezei imani kamili ya Ibrahimu (alikuwa na watoto kwa wanawake kadhaa, alijaribu kumpa Sara njia mbili ili kuokoa maisha yake binafsi) kuhusiana na neno la Mungu lakini kwa moyo wenyewe imani na utiifu. Ibrahimu, kama wanadamu wote, ana mtazamo wa kuchanganya imani na hofu, mema na mabaya.

**6:18 "vitu viwili visivyoweza kubadilika"** hii inarejelea kiapo cha Mungu (yaani, Zab. 110:4 dondoo katika Ebr. 5:6; 6:20; 7:17) na ahadi ya Mungu (kama vile Ebr. 6:14). Neno la Mungu ni imani yetu (kama vile Isa. 55:11; Mt. 5:17-18).

❑**"ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema uongo"** Hili yumkini ni dokezo la Hes. 23:19 au 1 Sam. 15:29. Ukweli huu huu umethibitishwa na Paulo kwenye 2 Tim. 2:13 na Tito 1:2. Tazama muhtasari kamili katika Ebr. 6:6.

❑**"sisi tuliokimbia"** Yumkini hii ikafanana na

1. Miji ya makimbilio ya Agano la kale (kama vile Hes. 35:6; Kumb. 4:41-43; Joshua 20)
2. Sitiari kwa ajili ya bandari salama wakati wa dhoruba (kama vile. Ebr. 2:14; 6:19)
3. Sitiari inayomrejelea Mungu kama ngome imara ambayo watu wake hukumbilia (kama vile Zab. 18:1-2; 31:3; 91:2,9; 94:22; 144:2; Isa. 17:10; 25:4; Yer. 16:19; Yoel 3:16; Nah. 1:7)

❑**"kuyashika matumaini yale yawekwayo mbele yetu"** katika mstari wa 18 tuna uwiano wa kiteolojia wa imara, uaminifu, Mungu mwenye enzi (kama vile Ebr. 6:18a) ambaye kwake ni lazima wanadamu wampokee, na kuendelea kuitikia kwa imani hata mwisho (kama vile Ebr. 6:18b).

**6:19 "kama nanga"** Hiki ni kielelezo cha Wakristo wa kale kwa ajili ya usalama, ulinzi, na tumaini. Lilipatikana kwenye kuta za makaburi ya Rumi. Neno hili linareta ufahamu katika muziki,  
"nimeituliza nafsi yangu kwenye pumziko,  
Sitasafiri zaidi katika bahari ya kutisha.  
Tufani yumkini ikaondolewa juu ya dhoruba kuu,  
bali ndani ya Yesu mimi nikao salama zaidi."

❑**"yenye nguvu"** Tazama Mada Maalumu: Dhamana katika Ebr. 2:2.

❑**"yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia"** Hapa nanga ya tumaini ni sambamba na Yesu kuhani mkuu aliyeingia katika Hema takatifu la mbinguni (kama vile Ebr. 8:5; 9:23), hata ndani ya patakatifu pa patakatifu, ambacho ni kielelezo cha uwepo wa Mungu sana. Matumaini ya waaminio kwenye sura hii na ahadi za Mungu na utimilifu wa kazi ya Yesu kristo.

Haya sio mafundisho ya Plato (miundo ya kidunia dhidi ya fikra za kimbingu), lakini taswira ya Hema takatifu la mbinguni ilionyeshwa kwa Musa katika Mlima Sinai (kama vile Ebr. 8:5; Kut 25-40). Aina hii mbili pia imepatikana kwenye hati za kukunjwa katika bahari mfu. Aina hizi za sababu (yaani, kopi ya duniani ya kitu cha mbinguni) zilinyang'anya mwanafalsafa Kiyunani Plato. Inaongelea kutoonekana kwetu lakini matumaini ya uhakika katika Kristo (kama vile Ebr. 9:23 na kuendelea).

**6:20 "mtangulizi wetu"** Neno hili la kiyunani lilitumika kwa ajili ya (1) mkaguzi aliyetangulia mbele, kuangalia na kutengeneza njia sahihi (yaani mwongoza njia) au (2) merikebu ndogo inayointingoza merikebu kubwa salama kuelekea bandarini. Yesu ametangulia mbele ya waaminio kwenye kila njia muhimu- akishinda, mwombezi, mwokozi, kuhani, na sadaka kamilifu!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! Mistari ya 2-4 inaorodhesha misingi ya Mkristo au kweli za Uyahudi?
2. Je! Kitabu cha Waebrania kinafundisha "kuiacha neema"? kwa nini au sio kwa nini?
3. Kwa nini mpangilio wa kihistoria wa kitabu ni wa muhimu katika tafsiri sahihi?
4. Je! Biblia inafundisha kwamba ukombozi wa kweli utashikiliwa hadi mwisho au kwamba wale walioshikilia imani hata mwisho watakombolewa?
5. Wale wanaosemwa kwenye mstari wa 4-6 ni waaminio au wasioamini? Kwa nini?
6. Ni kwa namna gani neno "wewe" la Ebr. 6:9 linahusiana na neno "wale" la Ebr. 6:4?
7. Elezea mateso ya waaminio yanavyowakabili.
8. Ni vitu gani viwili vilivyo katika Ebr. 6:18 visivyoweza kubadilika?
9. Ni kwa namna gani utawala wa Mungu na uhuru wa mwanadamu utakuwa na uwiano katika Ebr. 6:18?
10. Ni kwa namna gani tabia ya Mungu na ukamilifu wa kazi ya Kristo vinasimuliwa katika Ebr. 6:13-20?

## WAEBRANIA 7

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b> |                                     |   |                             |  |
|--|-------------------------------------|---|-----------------------------|--|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                       | <b>NKJV</b>                         | <b>NRSV</b>   | <b>TEV</b>                  | <b>NJB</b>   |
| Ukuu wa Ukuhani<br>Wa Melkizedeki<br>7:1-3   | Mfalme wa Haki<br>7:1-3             | Ukuhani wa Melkizedeki<br>Na Ukuhani wa Kilawi<br>Unalinganishwa<br>7:1-3 | Kuhani Melkizedeki<br>7:1-3 | Melkizedeki<br>7:1-3<br>Melikizedeki<br>Anapokea fungu la<br>Kutoka kwa<br>Ibrahim<br>7:4-10 |
| 7:4-10                                       | 7:4-10<br>Hitaji la Ukuhani<br>Mpya | 7:4-10  | 7:4-10                      | 7:4-10<br>Kutoka Ukuhani wa<br>Kilawi mpaka<br>Ukuhani wa<br>Melkizedeki<br>7:11-19          |
| 7:11-19                                      | 7:11-19                             | 7:11-14   | 7:11-14                     | 7:11-12<br>7:13-14<br>Uondolewaji wa<br>Sheria ya Zamani<br>7:15-19                          |
|  |                                     | 7:15-19<br>Ukuu wa Kuhani<br>Mpya   | 7:15-19                     | Ukuhani wa Kristo<br>Haubadiliki<br>7:20-25  |
| 7:20-25                                      | 7:20-28                             | 7:20-25   | 7:20-22<br>7:23-25          | 7:20-25<br>Ukamilifu wa Kuhani<br>Mkuu wa Kimbingu<br>7:26-28                                |
| 7:26-28                                      |                                     | 7:26-28   | 7:26-28                     | 7:26-28  |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "[Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia](#)")**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 7:1-3**

<sup>1</sup>Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki; <sup>2</sup> ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote; (tafsiri ya jina lake kwanza ni mfalme wa haki, tena, mfalme wa Salemu, maana yake, mfalme

**wa amani; <sup>3</sup>hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu); huyo adumu kuhani milele.**

**7:1 "Melkizedeki"** Alikuwa mfalme/kuhani wa Mataifa wa jiji la zamani la Kanaani liitwalo Salemu ambalo baadaye lilikuwa Yebusi na baadaye kuwa Yerusalem. Jina lake linamaanisha "mfalme wa haki yangu" (sawasawa na jina la mfalme wa Yerusalem katika Yos. 10: 1, "bwana wangu ni haki"). Ukoo wake haukuwahi kutajwa bali Ibrahim anamtembelea. Hii ndiyo sababu ya Yeye kuwa sasa aina ya Agano la Kale la Yesu. Anatajwa tu katika Mwa. 14: 18-20 na Zab. 110:4. Kumekuwa na mjadala mkubwa juu ya utambulisho wake.

1. kwa Philo, ni mfano wa nafsi ya mwanadamu
2. kwa Origen, ni malaika
3. kwa Ambrose, ni malaika wa Bwana
4. kwa wengine, ni malaika wa taifa la Israeli, Mikaeli
5. kwa Epiphano, ni kutokea tena kwa Roho Mtakatifu
6. kwa wafuasi wa Melkizedeki, ni mkuu kuliko Masihi na maombi yote hupitia kwake
7. kwa baadhi ya Wayahudi, Jerome na Luther, yeye ni Shem mwana wa Nuhu

Melkizedeki linatumika kama aina ya ukuhani wa Yesu kwa sababu nne:

1. Ibrahim alitoa Zaka kwake (wadogo siku zote walitoa zaka kwa wakubwa) na kwa tafsiri ya kisheria ya kiyahudi, mlawi pia alitoa zaka (kama vile Ebr. 7: 4-9)
2. Wazazi wake wake hawajaorodheshwa, hivyo thioloji ya kiyahudi inasema hakuwa na wazazi ni hivyo kuwa na umilele (kama vile Ebr. 7:3; Zab. 110: 4b)
3. Alikuwa ni kiongozi katika Jiji takatifu la baadaye la Yerusalem (Salemu, kama vile Mwanzo 14:18)
4. alikuwa ni kuhani wa Mungu Aliye Juu sana (yaani, *El Elyon*, kama vile Mwa. 14: 18)
5. anaruhusu mwandishi kuanzisha ukuhani wa kisheria licha ya ukuhani wa Kilawi.

■ "mfalme.....kuhani" Yeye ni mtu pekee katika Agano la Kale anayeunganisha ufalme na ukuhani (yaani Zaburi 110).

■ "na akambariki" Mkubwa zaidi humbariki mdogo; hivyo Ibrahim (na kwa maana ya kiyahudi ukoo wake, wa kilawi), ulibarikiwa na Melkizedeki (kama vile Mwa. 14: 19), ambalo linaonesha ukuu wake juu ya ukuhani wa Haruni. Pia inaonesha kwamba Yesu aliyekuwa ukoo wa Yuda angekuwa kuhani wa utaratibu mwingine.

**7:2 "sehemu ya kumi"** Tazama kwamba fungu la kumi (kama vile Mwa. 14: 20) ni zamani kuliko sheria ya Musa. Ilikuwa ni njia ya Sabato na matunda ya kwanza ya kuonesha umiliki wa Mungu vyote (kama vile Mwa. 14: 19c).

■ "tafsiri ya jina lake" Asili hasa ya tungo "mfalme wa haki" haijulikani bali jina hilo hilo linatumika kwa masihi katika Yer. 23: 6 ("Bwana wa haki yetu") na 33: 16 ("Bwana wa haki yetu"). Pia Masihi atakuwa haki na kuleta amani (kama vile Isa. 9: 6; 26: 3, 12; 32: 17; na 54: 10).

■ "Mfalme wa haki" Juu ya "haki" angalia Mada Maalum katika Ebr. 1:9.

■ "Salemu" Jiji linaweza kuwa limepata jina lake kutoka neno la Kiebrania *shalom* ambalo linamaanisha "amani." Baadhi ya wasomi wanafikiri linarejerea kwa uungu wa Kiyebusi. Jiji linaitwa Salemu katika Mwanzo 14, laini Zab 76: 2 inaihusianisha na Yerusalem (yaani Sayuni), ambalo liitwa Yebusi wakati wa kipindi cha Wakanaani.

**7:3** Hii ni tafsiri ya sheria za kiyahudi (*midrash*, angalia kiambatisho cha Tatu) kikijikita katika ukweli ukweli kwamba ukoo wa Melkizedeki hautolewi katika Mwa. 14: 18-20. Kama wanadamu wengine wote Melkizedeki alikuwa na wazazi, japo anatumikia aina nyingine ya Masihi wa milele (kama vile Ebr. 7: 8). Hii imekuzwa katika Ebr.7: 8, 12, 16, 17, 21, 24, 25, 28.

■ "mwanzo" Angalia Mada Maalum: *Archē* katika Ebr. 3:14.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 7:4-10

<sup>4</sup> Basi, angalieni jinsi mtu huyo alivyokuwa mkuu, ambaye Ibrahimu, baba yetu mkuu, alimpa sehemu ya kumi ya nyara. <sup>5</sup>Na katika wana wa Lawi nao, wale waupatao ukuhani, wana amri kutwaa sehemu ya kumi kwa watu wao, yaani, ndugu zao, kwa agizo la sheria, ijapokuwa wametoka katika viuno vya Ibrahimu. <sup>6</sup>Bali yeye, ambaye uzazi wake haukuhesabiwa kuwa umetoka kwa hao, alitwaa sehemu ya kumi kwa Ibrahimu, akamariki yeye aliye na ile ahadi. <sup>7</sup> Wala haikanushiki kabisa kwamba mdogo hubarikiwa na mkubwa. <sup>8</sup>Na hapa wanadamu wapatikanao na kufa hutwaa sehemu ya kumi; bali huko yeye ashuhudiwaye kwamba yu hai. <sup>9</sup>Tena yawenza kusemwa ya kuwa, kwa njia ya Ibrahimu, hata Lawi apokeaye sehemu ya kumi alitoa sehemu ya kumi; <sup>10</sup>kwa maana alikuwa katika viuno vya baba yake, hapo Melkizedeki alipokutana naye.

**7:5 "ijapokuwa wametoka katika viuno vya Ibrahimu"** Hii ni ni mantiki ya kisheria ya kiyahudi ikijikita katika walawi kuwepo katika viuno vya Ibrahimu (kama vile Ebr. 7: 10). Huu ni ufanuzi wa maandiko wa Kiyahudi sio ukweli wa kisayansi.

**7:7 "kubwa zaidi"** Shabaha ya kitabu cha Waembrania ni ulinganifu kati ya agano la Musa na agano jipyka katika Kristo .

Ulinganifu huu mara kwa mara unaelezewa kwa neno "kubwa kuliko" (*kreittōu/kreissōu*), ambalo linamaanisha "zuri zaidi," "juu ya," "yenye ubora zaidi," "yenye uthamani zaidi," "enye cheo cha juu." Haya ni maudhui yanayojirudia rudia katika Waembrania.

1. bora zaidi kuliko malaika (kama vile Ebr. 1: 4)
2. mambo bora zaidi yawahuusuyo ninyi (kama vile Ebr. 6: 9)
3. mdogo hubarikiwa na mkubwa (kama vile Ebr. 7:7)
4. tumaini bora zaidi (kama vile Ebr. 7:19)
5. agano bora zaidi (kama vile Ebr. 7: 22; 8:6)
6. wakiwa na dhabihu bora zaidi (kama vile Ebr. 9 23)
7. umiliki bora zaidi (kama vile Ebr. 10:34)
8. ufufuo bora (kama ville Ebr. 11:35)
9. nchi bora zaidi (kama vile Ebr. 11:16)
10. Mungu ametoa kitu chema zaidi (kama vile Ebr. 11:40)
11. amenyunyizia damu inazungumza vyema (kama vile Ebr. 12: 24)

**7:8 "yu hai"** Hii inarejerea umilele wa Melkizedeki kwasababu (1) wazazi wake (ukoo) hautajwi katika mwanzo 14 wala katika kifo chake kuandikwa na pia (2) Zab. 110: 4b maoni yake ya kibayana ("milele").

**7:9-10** Huu ni ufanuzi wa kiyahudi wa maandiko. Kwakuwa Lawi ni kabilia la uzao wa Haruni kutoka kwa Ibrahimu, hivyo kwa ufanano, ukuhani wa kiyahudi (yaani hata Kuhani Mkuu) alitoa fungu la kumi kwa Melkizedeki. Hivyo Melkizedeki yuu zaidi na Yesu ni mkuu kwa makuhani wa Kiyahudi.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 7:11-22

<sup>11</sup>Basi, kama ukamilifu ulikuwapo kwa ukuhani wa Lawi; (maana watu wale waliipata sheria kwa huo); kulikuwa na haja gani tena ya kuhani mwingine ainuke, kwa mfano wa Melkizedeki, wala asihesabiwe kwa mfano wa Haruni? <sup>12</sup>Maana ukuhani ule ukibadilika, hapana budi sheria nayo ibadilike. <sup>13</sup>Maana yeye aliyenewa hayo alikuwa mshirika wa kabilia nydingine, ambayo hapana mtu wa kabilia hiyo aliyeihudumia madhabahu. <sup>14</sup>Maana ni dhahiri kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabilia ambayo Musa hakunena neno lo lote juu yake katika mambo ya ukuhani. <sup>15</sup>Tena hayo tusemayo ni dhahiri sana zaidi, ikiwa ametokea kuhani mwingine mithili ya Melkizedeki; <sup>16</sup>asiyekuwa kuhani kwa sheria ya amri iliyo ya jinsi ya mwili, bali kwa nguvu za uzima usio na ukomo;

<sup>17</sup>maana ameshuhudiwa kwamba,

"Wewe u kuhani milele Kwa mfano wa Melkizedeki."

<sup>18</sup>Maana, kuna kubatiliwa kwa ile amri iliyotangulia, kwa sababu ya udhaifu wake, na kutokufaa kwake; <sup>19</sup>

(kwa maana ile sheria haikukamilisha neno); na pamoja na hayo kuliingizwa matumaini yaliyo mazuri zaidi, ambayo kwa hayo twamkaribia Mungu.<sup>20</sup> Na kwa kuwa haikuwa pasipo kiapo,<sup>21</sup> (maana wale walifanywa makuhani pasipo kiapo; bali yeye, pamoja na kiapo, kwa yeye aliywambia,

“Bwana ameapa  
wala hataghairi, Wewe u kuhani wa milele;”  
<sup>22</sup>basi kwa kadiri hii Yesu amekuwa mdhamini wa agano lililo bora zaidi.

**7:11 "kama"** Hii ni sentensi daraja la pili yenyé masharti ambayo inaitwa kinyume na ukweli. Kauli ya uongo inatolewa ili kutengeneza hoja.Ukuhani wa Kilawi haukuleta ukamilifu wa kiroho au makuzi.

❑ "ukamilifu" Familia ya Kiyunani ya maneno yaliyojikita kwenye *telos* kimsingi humaanisha "kuweka mwisho," "kumaliza," au "kuleta makuzi." Hapa inarejerea kwa mwakilishi mtoshelevu na mwenye ufanisi au mwombezi.

## MADA MAALUM: MWISHO AU KAMILI (*telos*) KATIKA KITABU CHA WAEBRANIA

Huu mwisho wa mambo ya kiroho ni mandhari ya mara kwa mara katika Waebrania.

1. *telos* mwisho, utimilifu (Ebr. 3:6,14; 6:8,11)
2. *teleioō*, "kufanya kamilifu"
  - a. (Yesu) kukamilisha uandishi wa wokovu wao kupitia mateso (kama vile Ebr. 2:10)
  - b. (Yesu) kukamilishwa kupitia mateso (kama vile Ebr. 5:8-9)
  - c. sheria ile haikufanya kitu kamili (kama vile Ebr. 7:19)
  - d. Mwana, kufanywa mkamilifu milele (kama vile Ebr. 7:28)
  - e. kumfanya mkamilifu anayeabudu (kama vile Ebr. 9:9)
  - f. kuwafanya wakamilifu wale walio karibu (kama vile Ebr.10:1)
  - g. Anawakamilisha kwa muda wote wale ambao wanajitakasa (kama vile Ebr.10:14)
  - h. mbali na sisi hawapaswi kufanywa wakamilifu (kama vile Ebr. 11:40)
  - i. roho ya watu wenye haki ilifanya kamilifu (kama vile Ebr. 12:23)
3. *teleios*, wenye kukomaa (kama vile Ebr. 5:14)
4. *teleios*, hema kamilifu zaidi (kama vile Ebr. 9:11)
5. *teleiotēs*, msukumo katika ukomavu (kama vile. Heb. 6:1)
6. *teleiosis*, ikiwa ukamilifu ulikuwa kupitia ukuhani wa Kilawi (kama vile Ebr. 7:11)
7. *teleiōtēs*, mwandishi na ukamilifu wa imani (kama vile Ebr. 12: 2)

Yesu huleta ukomavu na utimilifu ambao Agano la Musa haliwezi kuufanya!

❑"kwa ukuhani wa Lawi; (maana watu wale waliipata sheria kwa huo)" Hii kidhahiri inarejerea kwa (1) Musaakitokea kabila la Lawi na akiwa mjumbe wa Mungu katika kutoa mfumo wa kidhabihu wa Israeli au (2) Walawi na makuhani wakifundisha sheria kwa watu.

**7:12"hapana budi sheria nayo ibadilike"** Kusudi la sheria ya Musa hallikuwahi kuzalisha haki bali kuonesha matokeo yanayoendelea ya anguko na kutokuwa na uwezo wa kumpendeza Mungu (kama vile Gal. 3:24-25). Huu n ukweli mkuu katika kujaribu kutafuta kusudi la Mungu kwenye sheria ya Musa.

Tungo hii katika muktadha lazima irejeree kwa "agano jipyा."

**7:13"ambayo hapana mtu wa kabilia hiyo aliyeihudumia madhabahu"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu ambayo inamaanisha kwamba mfumo wa utoaji dhabihu ulikuwa ukiendelea. Ikiwa ndivyo, Waebrania kiliandikwa kabla ya uharibifu wa Titus wa Yerusalemu mnamo mwaka 70 b.k.

Hakuna nje ya kabila la Lawi na familia ya Haruni ikifanya kazi kama kuhani katika Agano la Kale.Hii haikuwa hivyo katika kipindi cha Warumi walipokuwa wakiaa Palestina (yaani Anna, Kayafa).

**7:14 "Bwana wetu alitoka katika Yuda"** Hii ni kauli ingine tendaji elekezi ya wakati timilifu. Kitenzi "kutokea" humaanisha "kuchipuka kutoka" na inatumika kwa ajili ya

1. kuchomoza kwa jua (kama vile Mt. 5:45)
2. mizunguko ya sayari
3. kuchomoza kwa mimea
4. kisitiari, kwa kutokea kwa familia ya kibinadamu (kama vile Zek. 6: 12; Isa. 11:1; Yer. 23:5-6).

Hapa inarejerea kwa unabii wa Yakobo juu ya wanawe katika Mwanzo 49 (hasa 49: 10).

□ **"Yuda"** Yesu alitokea ukoo wa kifalme wa Daudi wa Yuda (kama vile Mwa. 49: 8-12; 2 Sam. 7: 12-16; Isa. 9:6,7). Kushawishi Wayahudi kwamba Yesu alikuwa kuhani mkuu lilikuwa jambo gumu kwasababu hakuwa kabilo kwa kuhani kama Musa na Haruni.

**7:15 "kama"** Hii ni sentensi daraja la kwanza yenye masharti ambayo inadhaniwa kuwa kweli kulingana na mtazamo wa mwandishi au kwa ajili ya makusudi yake ya kifasihi. Kuhani mwingine amekuja na anatokea ukoo wa Melkizedeki.

**7:16**

|      |  |
|------|--|
| NASB | <b>"si kwa sheria ya amri iliyo ya jinsi ya mwili"</b> |
| NKJV | <b>"si kwa sheria ya amri iliyo ya jinsi ya mwili"</b> |
| NRSV | <b>"si kwa sheria ya amri iliyo ya jinsi ya mwili"</b> |
| TEV  | <b>"si kwa sheria na utaratibu wa kibinadamu"</b>      |
| NJB  | <b>"si kwa sheria ya amri ya mwili"</b>                |

Mamlaka ya kuhani ya Yesu hayakai katika aina ya kabilo au familia aliyotoka bali kutokea umiliki wa maisha ya umilele yasiyoharibiwa (yaani wazazi wa Melkizedeki hawatajwi katika Mwanzo 14 na neno "milele" Linatumwa katika Zab. 104: 4). Yesu ana masihi yasiyo na ukomo ya Mungu (sawasawa na kiapo na ahadi ya Mungu).

**NASB, NRSV**

|      |                                     |
|------|-------------------------------------|
| NJB  | <b>"maisha yasiyo na uharibiwa"</b> |
| NKJV | <b>"maisha yasiyo na ukomo"</b>     |
| TEV  | <b>"maisha yasiyo na mwisho"</b>    |

Hii inaonekana kuhusiana na ufanuzi wa maandiko wa kisheria za wayahudi (*Midrash*) maana yake ikitoka Zab. 110: 4b kwamba Melkizedeki hakuwa na wazazi na hivyo alikuwa wa milele (kama vile Ebr. 7:6,8).

**7:17 "maana ameshuhudiwa"** Hii ni nukuu kutoka Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani la Zab. 110: 4 (kama ilivyo Waibrania 7:21).

**7:18**

|      |                           |
|------|---------------------------|
| NASB | <b>"kuna kuweka kando</b> |
| NKJV | <b>"kuna kubatiliwa"</b>  |
| NRSV | <b>"kuna kuondolewa"</b>  |
| TEV  | <b>"imewekwa pembedi"</b> |
| NJB  | <b>"hivyo inafutwa"</b>   |

Neno hili limepatikana katika mafunjo ya Misri katika namna ya (1) "kuweka kando"; (2) "kufanya batili na tupu"; au (3) "kulipwa kikamilifu."

Mstari huu unazungumza juu ya kuweka kando kwa amri (yawezekana ukoo wa kimwili wa kuhani mkuu). Inashangaza kwamba kifungu kilichovuviwa cha Agano la Kale (kama vile Mt. 5: 17-19) inaweza kuwa "kuweka kando," bado hii ni hasa jambo la Paulo katika Galatia 3, kulingana na makusudi kiukombozi ya sheria ikiwekwa kando. Paulo, hatahivyo anaelezea kwamba ilikuwa ni udhaifu wa mwanadamu (kama vile Warumi 7), sio Agano la

Kale. Mwandishi wa Waebrania inaonesha ukuu wa Yesu juu ya Musa na kuita "Sheria" dhaifu na isiyo faa (kama vile Ebr. 8:13).

◻ "ile amri iliyotangulia" Hii inarejea kwa mfumo wa Kilawi auAgano la Kale inayokuwa na tabia ya usajili wa Musa.

◻ "kwa sababu ya udhaifu wake, na kutokufaa kwake" Warumi 7 na Wagalatia 3 ni ya msaada katika kutafsiri tungo hii. Haikuwa sheria bali asili ya mwanadamu aliyeanguka ile iliyokuwa dhaifu na Sheria ilikuwa haiwezi kufanya kazi ya kazi ya urejesho!

**7:19 "(kwa maana ile sheria haikukamilisha neno)"** Soma Wagalatia 3 na angalia Mada Maalum katika Ebr.7: 11.

◻ "mazuri zaidi" Angalia dokezo kamili katika Ebr. 7:7.

◻ "ambayo kwa hayo twamkaribia Mungu" Hii ni dhana ya msingi (kama vile Ebr. 7: 25; 4: 16; 10: 1). Mwandishi anaelezea kwamba Sheria ya Musa pamoja na ukuhani wa kilawi na dhabihu zilishindwa kumsogea mwanadamu kwa Mungu (kama vile Ebr. 10: 22; Yakobo 4: 7).

Tazama kwamba Yesu analeta agano bora zaidi lakini bado ni agano ambalo wanadamu lazima waitikie kama ambavyo makuhani walivyofanya, kama vile 2 Pet. 2: 5, 9; Ufunuo 1:6).

**7:20 "Na kwa kuwa haikuwa pasipo kiapo"** Ahadi za Mungu zinaweza kuaminiwa kwasababu tabia Yake na nguvu nyuma yake (kaa vile Isa. 46:10). Kiapo hiki ni rejea kwa Zab. 110: 4, ambayo inajadiliwa katika Ebr. 6:13-17.

**7:21** Hii ni nukuu nyingine kutoka Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani ya Zab. 110: 4 (kama ilivyo katika Ebr. 7: 17).

**7:22**

**NASB, NRSV**

|                  |                  |
|------------------|------------------|
| <b>TEV, NJB</b>  | <b>"dhamana"</b> |
| <b>NKJV, ASV</b> | <b>"uhakika"</b> |

Historia ya Nyuma ya Waebrania ni "nadhirini iliyowekwa katika mkono," ambayo inamaanisha uhakika. Ilikuwa kutumika katika Uyunani kwa ajili ya kitu cha kudhaminiwa juu ya mkopo au dhamana ya jela. Pia katika sheria ya Kirumi ilisimama kwa ajili ya kitu ambacho kilikuwa kinalindwa kisheria. Yesu ni dhamana ya Baba juu ya ufanisi wa agano jipya.

◻ "agano bora zaidi" Yer. 31: 31-34 huzungumzia juu ya hili "agano jipya"(kama vile Ezek.36: 22-36) ambapo shabaha inahamasishwa kiundani kisheria na kuzalishwa na Roho, sio kanuni ya nje ambayo inategemea matendo ya mwanadamu.

Kwa "bora kuliko" angalia dokezo kamili katika Ebr. 7:7.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 7: 23-25**

<sup>23</sup> Tena wale walifanywa makuhani wengi, kwa sababu wazuiliwa na mauti wasikae; <sup>24</sup>bali ye ye, kwa kuwa akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka. <sup>25</sup>Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa ye ye; maana yu hai sikuzote ili awaombee.

**7:23** Huu ni ulinganifu mwengine kati ya Yesu na kuhani wa Agano la Kale. Hii inashughulikia na hesabu yao na muda katika ofisi.

**7:24** Hii ni hitimisho la kisheria likijikita katik Mwanzo 14, ambapo ukoo wa Melkizedeki hautolewi na Zab. 110, ambayo ni maelezo kwa Melkizedeki ana anatumia neno "milele" (kama vile Zab. 110: 4b).

7:25

|      |                               |
|------|-------------------------------|
| NASB | "kuwaokoa milele"             |
| NKJV | "kuwaokoa kabisa"             |
| NRSV | "kwa wakati wote kuokoa"      |
| TEV  | "sasa na siku zote, kuokoa"   |
| NJB  | "nguvu ya kuokoa...ni hakika" |

Kama fasiri za Kingereza hapo juu zinavyoonesha, neno hili lina maana kadhaa. Anaweza kuokoa kikamilifu wote, milele (Kama vile Ebr. 10: 14) kwasababu anaendelea "milele" kama kuhani bora zaidi. Angalia mada maaluma juu ya dhamana katika Ebr.3:14.

- ◻ "wale" Huu ni ukaribisho wa kiujumla wa kiulimwengu! Yeyote atakaye atakuja (kama vile Yohana 1: 12; Rum. 10: 9-13; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9).
- ◻ "wao wamjiao Mungu kwa yeye" Yesu ni mpango wa ukombozi (kama vile Yohana 10: 9; 14: 6). Yeyote atakaye anaweza kuja lakini lazima waje kuititia imani katika Yeye na lazima waendelee katika imani (wakati uliopo endelevu).
- ◻ "maana yu hai sikuzote ili awaombee" Kazi ya Yesu haikuishia msalabani bali hata leo bado anaomba na kuombea waaminio (kama vile Ebr. 9: 24; Isa. 53: 12; Rum. 8:34; 1Yohana 2:1).

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 7:26-28

<sup>26</sup> Maana ilitupasa sisi tuwe na kuhani mkuu wa namna hii aliye mtakatifu, asiyekuwa na uovu, asiyekuwa na waa lo lote, aliyetengwa na wakosaji, aliyekuwa juu kuliko mbingu; <sup>27</sup> ambaye hana haja kila siku, mfano wa wale makuhani wakuu wengine, kwanza kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za hao watu; maana yeye alifanya hivi mara moja, alipojitoa nafsi yake. <sup>28</sup> Maana torati yawaweka wanadamu walio na unyonge kuwa makuhani wakuu; bali hilo neno la kiapo kilichokuja baada ya torati limemweka Mwana, aliyekamilika hata milele.

7:26 Hii yawezekana ni nukuu kutoka katika tenzi za kale au ushairi (kama Flp. 2:6-11; 1 Tim.3:16; 2 Tim. 2:11-13; na yawezekana 1 Tim. 1:17;6: 15-16). Neno "mtakatifu" linaweza kumaanisha "mwenye rehema" kutoka LXX (kama vile Zab. 16: 10). Neno "lisilokuwa na mawaa" ni neno la kidhabihu siku zote likitafsiriwa katika Agano la Kale "isiyo na doa." Huu ni muhtasari wa ukiri wa kupendeza.

#### MADA MAALUM: PASIPO LAWAMA, HATIA, KOSA, WALA MAWAA

- A. Maelezo ya ufunguzi
  1. Hii dhana kithiolojia inaelezea asili ya mwanadamu (yaani., Mwanzo 1, bustani ya Edeni)
  2. Dhambi na uasi umekwisha haribu mazingira haya ya ushirika kamili (yaani., Mwanzo 3)
  3. Wanadamu (wa kiume na wa kike) wanatamani urejesho wa ushirika na Mungu kwa sababu wameumbwa kwa sura na mfano wake Mungu (yaani., Mwa. 1:26-27)
  4. Mungu ameshughulika na dhambi ya mwanadamu kwa njia kadhaa kwa kutumia
    - a. Watu wa Mungu (yaani., Abraham, Musa, Isaya)
    - b. mtindo wa utoaji dhabihu (yaani., Walawi 1-7)
    - c. Mifano ya ki-Mungu (yaani., Nuhu, Ayubu)
  5. Hatimaye Mungu anamtoa Masihi
    - a. Kama ufunuo kamili wake mwenyewe (kama vile Yn 1:1-14; Kol. 1:13-17; Ebr. 1:2-3)
    - b. Kama dhabihu kamili kwa ajili ya dhambi (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)
  6. Wakristo waliumbwaa pasipo lawama
    - a. Rasmi kuititia haki ya Kristo iliyowekwa ndani yetu (kama vile. Rum. 4:3,6,8,11,22,23,24;

Yakobo 2:23)

- b. Kwa mwendelezo wa kazi ya Roho (Yn 16:8-1)
  - c. Lengo la Ukristo ni kufanana kama Kristo (kama vile. Rum. 8:28-30; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3; 5:23; 2 The. 2:13; Tit. 2:14; 1 Pet. 1:15), ambao katika ukweli, ni urejesho wa taswira ya Mungu iliyopotea katika anguko la Adamu na Hawa.
7. Mbinguni ndio urejesho wa ushirika kamili wa Bustani ya Edeni. Mbinguni ndiko Yerusalem Mpya inayotegemewa kuja nje ya uwepo wa Mungu (kama vile Ufu.21:2) kwenye ardhi iliyotakaswa (kama vile 2 Pet. 3:10). Biblia ilianza na kuishia kwenye maudhui yale yale ya:
- a. Ushirika binafsi wa ndani na Mungu
  - b. Ndani ya muundo wa bustani (Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)
  - c. Kwa maelezo ya kinabii, uwepo na urafiki wa wanyama (kama vile Isa. 11:6-9)
- B. Agano la Kale
- 1. Kuna maneno mengi ya Kiebrania ya aina tofauti ambayo yanachukua dhana nzima ya utimilifu, pasipo lawama, pasipo hatia ambayo yangalikuwa vigumu kuyataja na kuonyesha namna yahusianavyo
  - 2. Maneno makuu yanayochukua dhana nzima ya utimilifu, kutokuwa na kosa, au kutokuwa na hatia (kutokana na Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kur. 94-99) ni:
    - a. *shalom* (BDB 1022 )
    - b. *thamam* (BDB 1070)
    - c. *calah* (BDB 478)
  - 3. Tafasiri ya maandiko ya Kiyunani (yaani., Biblia ya kanisa la mwanzo) inazitafasiri dhana hizi za Kiebrania kwa maneno ya lugha ya kawaida ya Koine yaliyotumika katika Agano Jipy (angalia hapa chini)
  - 4. Dhana muhimu imejikita kwenye mtindo wa utoaji dhabihu
    - a. *amōmos* (kama vile Kut. 29:1; Law. 1:3,10; 3:1,6; Hes. 6:14)
    - b. *amiantos* and *aspilus* pia yana vidokezo vya kimadhehebu
- C. Agano Jipy
- 1. Dhana ya kisheria
    - a. Kidokezo cha sheria cha kimadhehebu ya Kiebrania kimetafasiriwa kwa neno *amōmos* ( kama vile Efe. 5:27; Fil. 2:15; 1 Pet. 1:19)
    - b. Vidokezo vya sheria za Kiyunani (kama vile. 1 Kor. 1:8; Kol. 1:22)
  - 2. Kristo yule asiye na dhambi, lawama, hatia (*amōmos*, kama vile. Ebr. 9:14; 1 Pet. 1:19)
  - 3. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kumfuata Yeye (*amōmos*, kama vile. Efe. 1:4; 5:27; Fil. 2:15; Kol. 1:22; 2 Pet. 3:14; Yuda 1:24; Ufu. 14:5)
  - 4. Dhana hii pia inatumiwa na viongozi wa kanisa
    - a. *anegklētos*, "pasipo mashitaka" (kama vile. 1 Tim. 3:10; Tit. 1:6-7)
    - b. *anepilemptos*, "zaidi ya shutuma" au "hapana nafsi ya lawama" (kama vile. 1 Tim. 3:2; 5:7; 6:14; Tit 2:8)
  - 5. Dhana ya "kutokuwa najisi" (*amiantos*) imetumika kwa
    - a. Kwa Kristo mwenyewe (kama vile. Ebr. 7:26)
    - b. Uriithi wa Wakristo (kama vile. 1 Pet. 1:4)
  - 6. Dhana ya "ujumla" au "kusikika" (*holoklēria*) (kama vile. Mdo. 3:16; 1 The. 5:23; Yakobo 1:4)
  - 7. Dhana ya kuwa "pasipo kosa," "kutokuwa na hatia" linalelezewa kwa *amemptos* (kama vile. Lk 1:6; Fil. 2:15; 3:6; 1 The. 2:10; 3:13; 5:23)
  - 8. Dhana ya "kutokuwa kwenye lamama" linalelezewa kwa *amōmētos* (kama vile. 2 Pet. 3:14)
  - 9. Dhana ya "kuwa safi," "pasipo doa" mara nyingi zimetumika katika sura zenye moja ya maneno ya hapo juu (kama vile. 1 Tim. 6:14; Yakobo 1:27; 1 Pet. 1:19; 2 Pet. 3:14)
- D. Idadi ya maneno katika Kiebrania na Kiyunani yanayoelezea dhana hii yanaonyesha umuhimu wake. Mungu ametupatia mahitaji yetu kuititia Kristo na sasa anatuita kuwa kama Yeye.

Waamini kihali, kihukumu wametangazwa kuwa "sawa" "wenye haki" "wasio na lawama" kwa kazi ya Kristo.

Sasa waamini wanatakiwa kumiliki nafasi yao. "Tembeeni katika nuru kama Yeye alivyo nuruni" (kama vile. 1 Yn 1:7). "tembeeni kwa thamani ya mwito wenu" (kama vile. Efe. 4:1,17; 5:2,15). Yesu ameirejesha taswira ya Mungu. Ushirika wa ndani sasa ni dhahiri, lakini kumbukeni Mungu anahitaji watu wanaoaksi tabia yake, kama Mwana wake alivyofanya, kwa ulimwengu uliopotea (yaani., mataifa). Hatukuitiwa chochote bali utakatifu (kama vile. Mt. 5:20,48; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:13-16). Utakatifu wa Mungu, sio tu kisheria, bali namna uishivyo!

■ **"aliyetengwa na wakosaji"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Haiaksi juu ya ubinadamu wa Yesu (kama vile Flp. 2:6-7), bali linazungumzia juu ya kutokuwa kwake na dhambi (kama vile Ebr. 4: 15; 9:14; 2 Kor. 5:21; 1 Pet. 2:22; 1 Yohana 2:1; 3:5).

■ **"aliyekuwa juu kuliko mbingu"** Hii inaweza kuwa (1) kauli ya utawala wa hapo kabla; (2) rejea juu ya mtazamo walimu wa uongo wa ujuzi wa wokovu kama kupitia anga la kimalaika (kama vile Ebr. 4:14); au (3) njia ya kurejerea kwenye ufufuo/kupaa.

**7:27** Hii inaonekana kuhusiana na Siku ya Upatanisho (kama vile Law. 16), lakini hapa inatumika katika namna ya matoleo ya kila siku (mwendelezo wa Agano la Kale). Kihistoria na kisheria za kiyahudi inathibitishwa kwamba kuhani mkuu alikuwa moja kwa moja akihusika katika utoaji wa dhabihu katika dini ya kiyahudi lakini yawezekana sio wakati wa siku za hema. Angalia Mada Maalum: Yesu kama Kuhani Mkuu katika Ebr. 2:17.

■ **"alipojitoa"** Hili ni neno lile lile lililotumika katika Isa. 53:11 katika Tafsiri ya Agano la Kale (LXX), "kuchukua." Baadhi wanaona hii kama maelezo ya moshi wa dhabihu.

■ **"alifanya hivi mara moja"** Waebrania wanasisitiza u-kilele wa kifo cha Yesu cha ikisha tolewa mara moja. Hii mara ukishapewa wokovu na kusamehewa basi kila kitu kimemalizika milele (kama vile "mara moja" [epaphax] , Ebr. 7:27; 9:12; 10:10 na "moja kwa vyote"[hapax] , Ebr. 6:4; 9:7,26,27,28;10: 2;12: 26,27). Huu ni ukiri wa kidhabihu uliokamilishwa ambao unajitokeza tokeza mara mara.

■ **"alipojitoa"** Yesu kama kuhani mkuu (kama vile Zab.110: 4) mwathirika (kama vile Isa.53:10) wa madhabahu ya kimbingu (kama vile Ebr. 9:24). Hii ni nguzo ya msisitizo wa Agano Jipya juu ya mbadala na upatanisho usio wa moja kwa moja (kama vile Marko 10:45; Rum. 8:3; 2Kor. 5:21).

**7:28** "Sheria inateua wanadamu kama makuhani walio dhaifu, bali neno la kiapo abalo lilikuja baada ya sheria" Huu ni utofautiano kati ya maandiko ya taratibu za Musa na "kiapo" cha Zab. 110:4.

■ **"limemweka Mwana"** Yesu ni kuhani aliye juu sana kwasababu ni sehemu ya familia ya Mungu (yaani mwana, "kama vile Ebr. 1:2; 3:6; 5:8). Hii rejea inaunganisha Zab.2 na Zab. 110 ambazo ziliikuwa ni Zaburi za kifalme na kikuhani. Anaunganisha vyote ofisi zilizopakwa mafuta za Agano la Kale katika Yeye mwenyewe na kipao cha Baba yake.

■ **"aliyekamilika hata milele"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Amefanya mkamilifu (kwa kuzungumza kibinadamu) kwa mateso na ukamilifu huu kuendelea (Kama vile Ebr. 2:10; 5:8-9). Angalia Mada Maalum katika Ebr.7:11.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini mwandishi anachukua muda mrefu kukuza dhana ya Yesu kama kuhani mkuu?
2. Ni kwa namna gani Walawi wanaunganishwa na Melkizedeki?
3. Ni kwa namna gani Zab. 110 inafanana na Mwanzo 14:18-20?
4. Kwanini Melkizedeki anatumika kama aina ya Masihi?
5. Melkizedeki alikuwa ni nani?

## WAEBRANIA 8

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b> |                                 |                                |   |  |
|--|---------------------------------|--------------------------------|---|--|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                       | <b>NKJV</b>                     | <b>NRSV</b>                    | <b>TEV</b>                              | <b>NJB</b>   |
| Kuhani Mkuu wa Agano Jipy na Bora<br>8:1-6   | Huduma Mpya ya Kikuhan<br>8:1-6 | Madhabahu ya Kimbingu<br>8:1-7 | Yesu Kuhani wetu Mkuu<br>8:1-2<br>8:3-6 | Ukuhani Mpya na Madhabahu mpya<br>8:1-5<br>Kristo ni Mpatanishi Wa Agano Kubwa Zaidi<br>8:6-13 |
| 8:7-13                                       | Agano Jipy<br>8:7-13            |                                | 8:7-13                                  |  |
|  |                                 | 8:8-13                         |   |  |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "[Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia](#)")**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
5. N.k

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA WAEBRANIA 8:1- 13**

- A. Hii ni sehemu ya muktadha uliouunganishwa kuhusiana na hitaji la msomaji kukomaa. Sehemu hii inaanzia kutoka Waebrania 5: 11-10: 18 pamoja na maelezo ya ziada za onyo kutoka kwa Waebrania 5: 12-6: 20.
- B. Kadiri Waebrania 2 inavyokua ikitumia Zaburi 8, Sura za 3 na 4 inakua kutumia Zaburi 110, na sura za 8 zinatumia Yer. 31: 31-34 (Waebrania 10 itatumia Zaburi 40).
- C. Hema la kweli mbinguni ambalo linaelezewa katika Waebrania 6: 19-20 na 8: 2 haitakua vizuri kikamilifu mpaka sura ya 9.

#### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

##### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 8:1-13**

<sup>1</sup> Basi, katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili: Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni, <sup>2</sup>mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu. <sup>3</sup>Maana kila kuhani mkuu huwekwa ili atoe vipawa na dhabihu; kwa hiyo lazima huyu naye awe na kitu cha kutoa. <sup>4</sup>Kama angekuwa juu ya nchi, asingekuwa kuhani; maana wako watoao sadaka kama iagizavyo sheria; <sup>5</sup>watumikiao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni, kama Musa alivyoagizwa na Mungu, alipokuwa tayari kuifanya ile hema; maana asema, Angalia ukavifanye vitu vyote kwa mfano ule ulioonyeshwa katika mlima. <sup>6</sup>Lakini sasa amepata huduma ilio bora zaidi, kwa kadiri alivyo

mjumbe wa agano lililo bora, lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora.<sup>7</sup> Maana kama lile la kwanza lingalikuwa halina upungufu, nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili.<sup>8</sup> Maana, awalaumupo, asema

“Angalia, siku zinakuja, asema Bwana,  
 Nami nitawatimizia nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda agano jipy;  
<sup>9</sup> Halitakuwa kama agano lile nililoagana na baba zao,  
 atika siku ile nilipowashika mikono yao niwatoe katika nchi ya Misri.  
 Kwa sababu hawakudumu katika agano langu,  
 Mimi nami sikuwajali asema Bwana.  
<sup>10</sup> Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Israeli  
 Baada ya siku zile, asema Bwana;  
 Nitawapa sheria zangu katika nia zao,  
 Na katika miyo yao nitaziandika;  
 Nami nitakuwa Mungu kwao,  
 Nao watakuwa watu wangu.  
<sup>11</sup> Nao hawatafundishana kila mtu na jirani yake,  
 Na kila mtu na ndugu yake,  
 akisema, Mjue Bwana;  
 Kwa maana wote watanijua,  
 Tangu mdogo wao hata mkubwa wao.  
<sup>12</sup> Kwa sababu nitawasamehe maovu yao,  
 Na dhambi zao sitazikumbuka tena.”

<sup>13</sup> Kwa kule kusema, Agano jipy, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka.

## 8:1

NASB, NKJV

|      |               |
|------|---------------|
| NRSV | “suala kubwa” |
| TEV  | “jambo kubwa” |
| NJB  | “sasa basi”   |

Hii inatoka katika muundo wa neno la Kiyunani “kichwa,” (*kephalē*) ikitumiwa kisitiari kwa ajili ya jumla yote ya fedha (kama vile Mdo. 22: 28). Watu wa kale waliongeza namna yao kimafumbo ya juu badala ya chini. Neno hili lili kuwa na nyongeza ya (1) sehemu ya muhimu zaidi ya hoja ya kitabu au (2) muhtasari wa hoja iliyokwisha tolewa tayari.

■“kuhani mkuu” Cheo hiki kwa Yesu kinapatikana tu katika Waebrania (kama vile Waebrania 2: 17; 3: 1; 4: 14-15; 5: 10; 6: 20; 7: 26; 8: 1, 3; 9: 11, 25). Asili ya kikuhani ya Masihi inafunuliwa katika Zaburi 110 na Zakaria 3 na 4. Yeye ni vyote kuhani na dhabihu (kama vile Isaya 53). Anasimama mbele za Mungu kwa niaba ya wanadamu na kujitoa yeye mwenyewe kama suluhisho la tatizo la dhambi.

■“aliyeketi katika kitu” Huku ni kuendelea kwa matumizi ya Zaburi 110 (yaani Waebrania 8: 2). Inarejerea kwa kazi iliyokwisha malizika ya Kristo. Hatahivyo ina maana ya kifalme wala si ya kikuhani. Hakuna kuhani aliyewahi kukaa chini, ni wafalme tu (kama vile Waebrania 1: 3).

■“katika mkono wa kuume” Hii ni tungo inayotumia lugha ya kibinadamu kuelezea sehemu ya mamlaka na nguvu (kama vile Waebrania 1: 3, 13; 8: 1; 10: 12-13; 12: 2; Mdo. 2: 33-35).

■“cha enzi ya Ukuu mbinguni” Mungu hana kitu cha enzi kinachoshikika cha kibinadamu kwasababu yeye ni roho. Hii ni tungo yenye kutumia lugha ya kibinadamu ikimuelezea Mungu katika uelewa wa kibinadamu. Ni mzunguko au njia ya kimafumbo ya kumrejerea Mungu bila kutaja jina lake (kama vile Waebrania 12: 2). Neno “mbingu” ni wingi kama inavyotumika katika Agano la Kale. Ni wingi kwasababu inarejerea viwango kadhaa

1. anga juu ya nchi ambapo ndege hupaa na mawingu hutengenezwa (kama vile Mwanzo. 1: 1)
2. anga lenye kupanbwa nyota, anga ya mianga ya kimbingu, jua, mwezi, nyota na sayari (kama vile Mwanzo 1: 14)
3. uwepo dhahiri wa Mungu mwenyewe na uwepo wa kimalaika

Walimu wa sheria wa kiyahudi walibishana ikiwa kulikuwa na mbingu tatu (kama vile 2 Kor. 12: 2) au mbingu sabab (yaani haipo katika Biblia lakini katika vyanzo vya karne ya kwanza vya walimu wa sharia wa Kiyahudi). Dhana hii ya viwango kadhaa inaweza kuonekana katika Kumb. 10: 14; 1 Wafalme. 8: 27; na Zab. 68: 33; 148: 4. Wajuzi wa Sheria waliitumia dhana hii ya mbingu kadhaa kuelezea viwango vya mamlaka ya kimalaika. Hatahivyo Yesu amevipita (kama vile Waebrania 4: 14). Wingi dhidi ya umoja wa ufahamu wetu (mbingu) inaonekana kutokuwa na umuhimu kithiolojia katika Waebrania (kama vile Waebrania 9: 23 dhidi ya 9: 24).

**8:2 "hema"** Hii ni rejea kwa hemu halisia katika mbingu (kama vile Waebrania 6: 19-20), ambayo ile iliyofunuliwa kwa Musa ju ya Mlima Sinai na kuijenga wakiwa jangwani kipindi kile (kama vile Kutoka 25-40) ilikuwa ni nakala tu (kama vile Waebrania 9: 11, 24).

▣ "ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu" Haya yanaweza kuwa ni maelezo ya Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani (LXX) fasiri ya Kutoka 33: 7 (sehemu maalumu ya kukutana na Mungu) au inaweza kuwa tu njia nyingine ya kurejereha hemu la kimbingu (kama vile Ebr. 11: 10).

**8:3 "atoe"** Huu ni msisitizo wa Ondoleo la dhambi la dhabihu ya Kristo. Dhabihu yake itakuwa Uhai wake

**8:4 "kama angekuwa juu ya nchi, Asingekuwa kuhani kabisa"** Hii ni sentensi daraja la pili yenye masharti ambayo inaongelea ukinzano wa ukweli (kama vile Ebr. 4: 8; 7: 11; 8: 4, 7; 10: 2; 11: 15). Yesu hakuwa wa kabile la kikuhanu wa kabile la kilawi bali alitokea katika kabile la kifalme la Yuda. Huduma ya kikuhanu ya Yesu kwa kilele ilifanyika mbinguni.

**8:5 "mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni"** Matumizi ya maneno "nakala" na "kivuli" ni muhimu kwa Maandiko ya Philo wa Iskandria, mwandishi wa Kiyahudi na mwanafalsafa aliyeishi tokeaa mnamo mwaka 20 k.k. mpaka mwaka 42 b.k na akimfuatia Plato. Alitumia stiari katika Agano la Kale katika jaribio kulifanya liwe na uhusiano kwa jamii ya Kiyunani na kutetea nadharia za Plato kama namna ya kumfafanua YHWH.

Hatahivyo kifungu hiki hakiaksi Philo bali desturi za kale za kiyahudi ambazo Musa alipewa pale Mlima Sinai. Sinai ni nakala ya madhababu ya kimbingu—hemu ya kipindi cha safari ya jangwani. Aina hii hii ya kufikiru ipo katika Magombo ya Bahari ya Chumvi ambayo yanaonesha kuwa haikuwa ya kipekee kwa Plato (yaani Falsafa ya Kiyunani). Inafurahisha kwamba mwandishi wa Waebrania hajadili aidha hekalu la Suleimani wala la Herode (wala taratibu zao). Hizi hazikuwahi kuamriwa na Mungu kama ilivyokuwa katika hemu (kama vile Kut. 25-40), ingawa 1 Mambo ya Nyakati 28: 19 inajongea karibu na kudai kwamba mipango ya Suleimani ilikuwa imevuvuviwa kiungu.

Desturi ya Kiyahudi kwamba hemu la kale lilikuwa ni nakala ya hemu la kweli katika mbingu inaweza kunekana katika (1) Kut. 25: 9, 40; (2) Ufu. 11: 19; 13: 6; 15: 5; (3) II Baruch 4: 5; (4) Kufa kama Shahidi wa Mungu na Kuupaa katika Isaya 7: 10; (5) Hekima 9: 8; (6) *Mabaki ya kale ya Flavius Josephus ya Wayahudi* 3: 6: 1

Kifungu hiki hakiaksi nadharia za Plato kwasababu Hema katika Mbingu ilikuwa na nalaka au uhalisia. Katika nadharia za Plato mbingu ilikuwa ni halisia, ya kifikra, uhalisia wa kiroho lakini katika Biblia ni uhalisia unaoshikika. Mbingu si tu jambo jema la kutamanika/dhana bali sehemu ya kweli ya uumbaji (kama vile Kol. 1: 16).

Hili Hema ya Kimbingu siku moja inafika mwisho wa kutokuwepo (kama vile Ufu. 21: 22). Ilifanya kazi ya kutumikia kusudi wakati wa zama hizi lakini haitaitajika wakati wa matukio ya siku za mwisho!

▣ "Asema" Hii ni nukuu ya Kut. 25: 40. Hema halikuwa mpango wa Musa bali Ufunuo wa Mungu.

**8:6 "lakini sasa amepata huduma iliyobora zaidi"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati Timilifu. Maelezo haya haya ya ubora wa Yesu yanatumika kwa muunganiko na malaika katika Ebr. 1: 4.

■ "mjambe wa agano lililo bora zaidi" Vitenzi vyote katika Ebr. 8: 6 ni timilifu. Kama kilichotangulia, hii pia ni kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu.

Neno "mpatanishi" ni neno la kisheria linaloelezea msuluhishi. Kama kuhani asimamavyo kati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu mwenye dhambi, ndivyo pia Yesu alivyo mpatanishi (kama vile Ebr. 9: 15; 12: 24; 1Tim. 2: 5). Hii ni njia nyingine ya kuashiria kazi ya Kuhani Mkuu.

■ "agano lililo bora lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora" Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu. Maandishi wa Waembrania na uwasilishaji wake wa mamlaka ya Yesu juu ya agano la Musa unafunuliwa kwa kutumia neno "bora kuliko" (angalia dokezo katika. 7: 7).

## MADA MAALUM: AGANO

Neno la Agano la Kale *berith* (BDB 136, KB 157), "Agano," sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihilisha kutoleta ushawishi. Yumkini ubashiri mzuri ni "kukata" ikimaanisha sadaka ya mnyama inayojumuishwa kwenye agano (kama vile Mwa. 156:10,17). Hata hivyo, kiini dhahili cha dhana yenye we kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji.

Agano ni namna ambayo Mungu wa kweli (angalia Mada Maalum: Uwepo wa Mungu Mmoja) anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadmu kwa wazi unaonekana katika dhana ya Agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. Uumbaji wenye we (kama vile Mwanzo 1-2)
2. Utunzaji na ahadi ya Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)
3. Wito wa Abrahamu (kama vile Mwanzo 12)
4. Agano pamoja na Abraham (kama vile Mwanzo 15)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. Kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. Kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. Kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. Kwa imani Musa anawatoa wana wa Israel toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana (kama vile Walawi 26, Kumbu kumbu la Torati 27-28)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika "agano jipya" (kama vile. Yer. 31:31-34; Ebr. 7:22; 8:6,8,13; 9:15; 12:24). Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Ezek. 18:31 na Ezek. 36:27-38 (tendo la YHWH). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Lengo la yote ni sawa:

1. Urejesho wa ushirika na YHWH uliopotea katika Mwanzo 3
2. Uimalishaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubarifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenye we pasipo utosherevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano la Mungu, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Mwanzo 3; Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea, angalia Mada Maalum: Kuamini katika Agano Jipya). Yesu anaita ushirika

wake mpya na waamini "agano jpya" (kama vile Mt. 26:28; Mark 14:24; Lk 22:20; 1 Kor. 11:25). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15), maelezo elekezi ya ukubalifu (Warumi 4) wito wa ushurutishi wa kuwa mtakatifu (kama vile Mt. 5:48)! Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, lakini ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10; 2 Kor. 3:5-6). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio njia ya wokovu (yaani., Yakobo na 1Yohana). Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekena kwa wazi katika maonyo yanayoonekana katika Agano Jipy (angalia Mada Maalum: Uasi)

**8:7 "kama"** Hii ni sentensi daraja la pili yenye masharti nyingine ambayo inaitwa kinyume na kitendo (kama vile Ebr. 8: 4). Hili ni suala linguine kubwa la hoja. Kauli isiyi ya kweli ya dhahiri inatumika kuweka suala la kithiolojia. Agano la kwanza halikuzalisha matokeo yaliyokuwa yakitarajiwa ya urejesho na haki.

**8:8 "Maana awalaumupo"** Sio sheria bali udhaifu wa kibinadamu ndio ilikuwa tatizo (kama vile Rum.7: 12, 16; Wagalatia 3).

▣**"Asema"** Mistari ya 8-12 ni nukuu zinazoendelea kutoka Yer. 31:31-34. Tazama "Yeye" inarejerea kwa YHWH; hatahivyo katika Ebr. 10: 15 tungo hii hii inapewa sifa kwa Roho Mtakatifu. Uvuvio wa Agano la Kale wakati mwengine linahusianishwa na Roho na wakati mwengine Baba.

▣**"agano jipy"** Tungo hii katika Yeremia (kama vile Yer. 31:31-34) ni kutajwa tu katika Agano la Kale juu ya agano "jipy", lakini ikielezea katika Ezekiel 36: 22-38. Hii ingeshangaza sana kwa Wayahudi.

▣**"Nyumba ya Israeli"** Hii inamaanisha kuungana kwa watu wa Mungu baada ya Ufalme ulioungana (Sauli, Daudi, Suleimani) kugawanyika mnamo mwaka 922 k.k , Makabila ya kaskazini chini ya Yeroboamu I aliiwa Israeli na makabila ya kusini chini ya Rehoboamu waliitwa Yuda.

**8:9 "sio kama agano"** Tofauti haipo katika umuhimu au shabaha bali katika mbinu.

▣**"Katika siku ile nilipowashika mkono"** Hii inarejea kwa YHWH kama Baba (kama vile Hosea 11:1-4).

▣**"Mimi nami sikuwajali"** Hii inafuatia Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani (LXX). Andiko la Kimasoteri (MT) lina "ingawa nilikuwa mume kwao."

**8:10 "nia"** Hii inafuatia Tafsiri ya Agano la Kale (LXX) lakini andiko la Kimasoteri (MT) lina "ndani yao. "Hivi ndivyo agano la kale linavyotofautiana na jipy. La kale linaundwa na sifa za Ezek.18: 31, jipy na Ezek. 11: 19; 36: 26-27.

▣**"mioyo"** Hii inarejerea kwa mtu mzima (kama vile Kumb. 6: 6; 11: 18; 30: 6,14). Angalia katika Mada Maalum katika Ebr.3: 8.

▣**"Nami nitakuwa Mungu kwao na wao watakuwa watu wangu"** Hii ni kanuni ya kiagano ya Agano la Kale.

**8:11**Kuna tofauti ya maandiko ya Kiyunani katika neno "raia" dhidi ya "jirani." Katika ufahamu wa uelewa wa ndugu wa kiagano, utofauti hautengenezi tofauti ya ufasiri wa maana. Kadiri maandiko ya kale na zidi maandiko ya Kiyunani yanavyotegemewa inavyotarajiwa, "raia" ni chaguo bora (kama vile P<sup>46</sup>, Κ, Α, Β, Δ, Κ, Λ, na baadaye maandiko madogo).

**8:12** Huu ni usawa wa agano jipy (kama vile Yer. 31: 31-34). Inatajwa katika Agano Jipy katika Luka 22: 20; 1 Kor. 11: 25; 2 Kor. 3: 6; na Ebr. 8: 8; 9:15. Hakutakuwa na hitaji kwa viongozi, wote watamua Bwana na Mapenzi Yake na njia zake. Dhambi ambazo Mungu husamehe, husahau (kauli kanushi ya nguvu inayojirudia mara mbili).

Agano la Kale lina ahidi msamaha kamili na wa kupendeza (kama vile Zab.103:3,8-14; Isa.1:18;38: 17;43:25; 44: 22;Mika 7:19).

**8:13**

**NASB** “lakini chochote ambacho kimepiutwa na wakati na kinachozeeka kiko tayari kupotea”

**NKJV** “Sasa chochote ambacho kimepitwa na wakati na kuzeeka kiko tayari kupotea”

**NRSV** “Na chochote ambacho kinazeeka na kuchakaa punde kitapotea”

**TEV** “Chochote ambacho kinazeeka na kuchakaa punde kitapotea”

**NJB** “Na chochote kizee na chenye kuwa na umri mkubwa kiko tayari kupotea”

Tungo hii inahitaji maoni kadhaa. Kwanza kumbuka mazingira ya kihistoria. Kuna kundi la watu wanaochagizwa na kurudi kwa Sheria ya Musa.

Cha pili, Hii inahusiana na Sheria tu kama namna ya wokovu. Hakika Agano la Kale lilikuwa na ni ufunuo wa Mungu (kama vile Mt.5:17-19). Sheria ya Musa bado ina kusudi katika mpango wa Mungu (kama vile Gal. 3). Inawaleta watu kwa Kristo kwa kuwaonesha binadamu walioanguka hali yao ya dhambi na hitaji la wokovu. Inatusaidia kumuelewa Mungu na njia Zake. Inahusiana na agano jipya kama ahadi kwa utimilizwaji. Halikuwa na uwezo wa kuleta wokovu kwasababu ya udhaifu na hali ya dhambi ya wanadamu walioanguka.

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini mwandishi wa Waebrania anaweka mkazo sana wa kuhani mkuu Yesu aliye juu ya wote?
2. Je kitabu cha Waebrania kinashawishiwa na Falsafa ya Kiyunani (Nadharia za Plato)?
3. Kwanini Yeremia 31: 31-34 ilinukuliwa?
4. Kwanini mstari wa 12 ni ahadi ya thamani kubwa namna hiyo?
5. Ni kwa namna gani agano la Musa linahusiana na Wakristo wa agano jipya?

## WAEBRANIA 9

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>             |  |  |  |  |
|--|--|--|--|--|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                                   | <b>NKJV</b>                              | <b>NRSV</b>                            | <b>TEV</b>   | <b>NJB</b>                                       |
| Kusafishwa kwa Duniani na Mbinguni<br>9:1-5              | Kusafishwa Duniani<br>9:1-5              | Huduma ya Makuhani wa Kilawi<br>9:1-5  | Ibada ya Mbinguni na Duniani<br>9:1-5              | Kristo Anaingia kwa Kusafishwa<br>9:1-5          |
|  | Ombolezo la Kusafishwa Duniani<br>9:6-10 |  |  |  |
|  | 9:6-10                                   | 9:6-10                                 | 9:6-10   | 9:10   |
|  |  | Sifa za Dhabihu ya Kristo (9:11-10:18) |  |  |
| 9:11-14  | 9:11-15                                  | 9:11-14                                | 9:11-14  | 9:11-14  |
|  |  |  |  | Kristo Analiihdhinisha Agano Jipyा Kwa Damu yake |
| 9:15-22  | Kifo cha Mjumbe Muhimu<br>9:16-22        | 9:16-22                                | 9:15   | 9:15-28  |
| Dhambi Iliondolewa Kwa dhabihu ya Kristo<br>(9:23-10:18) | Ukuu wa Dhabihu ya Kristo<br>9:16-22     |  | Dhabihu ya Kristo Iliiondoa Dhambi<br>(9:23-10:18) |  |
| 9:23-28  | 9:23-28                                  | 9:23-28                                | 9:23-28  |  |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

**KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili

3. Aya ya tatu
4. N.k.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 9:1-5

<sup>1</sup>Basi hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida za ibada, na patakatifu pake, pa kidunia. <sup>2</sup> Maana hema ilitengenezwa, ile ya kwanza, mlimokuwa na kinara cha taa, na meza, na mikate ya Wonyesho; ndipo palipoitwa, Patakatifu. <sup>3</sup>Na nyuma ya pazia la pili, ile hema iitwayo Patakatifu pa patakatifu, <sup>4</sup>yenye chetezo cha dhahabu, na sanduku la agano lililofunikwa kwa dhahabu pande zote, mlimokuwa na kopo la dhahabu lenye ile mana, na ile fimbo ya Haruni iliyochipuka, na vile vibao vya agano; <sup>5</sup>na juu yake makerubi ya utukufu, yakikitia kivuli kiti cha rehema; basi hatuna nafasi sasa ya kueleza habari za vitu hivi kimoja kimoja.

**9:1 "la kwanza"** Maagizo ya dhabihu na ibada yalihusianishwa na hema katika Kitabu cha Mambo ya Walawi.

■"**agano**" Neno hili liko katika andiko la Kiyunani. Tafsiri nyingi za lugha ya Kiingereza zinakuwa na madhaanio juu ya neno hili. Hata hivyo, H. E. Dana, katika kitabu chake cha *Jewish Christianity*, uk. 255, anaanini kwamba hililazima litafsiriwe kama "huduma ya kwanza" kwa sababu sura ya 9 inawasilisha ushahidi mwingine wa ukuu huduma ya Yesu (kama vile Ebr. 8:6). Yeye pia anausawiri ulinganifu ulio katika uk. 255.

#### Huduma ya Kwanza

Huduma ya kimbingu—  
"ya ulimwengu wake."  
Kumwanda Mwanadamu—  
"kulikuwa na hema lililotengenezwa."  
Matokeo ya nje—  
"haiwezi kuigusa dhamiri kumfanya  
aliye abudiwa kuwa kamili."  
Asili yake ni muda mfupi—  
"uwekaji wa maagizo ya kimwili  
kwa kuungoja wakati wa matengenezo."

#### Huduma ya Pili

Huduma ya Kimbingu—  
"si ya uumbaji huu"  
Maandalizi ya Kiungu—  
"halikufanywa kwa mikono"  
Matokeo ya ndani  
"inasafisha dhamiri yako"  
kutokana na matendo mafu ili kumtumika Mungu aliye hai  
Asili yake ni ya kudumu—  
"ahadi ya urithi wa milele"

**9:2 "hema"** Neno hili linairejelea hema yenye kuhamishika ndani ya jangwa, ambayo linaelezwa kwa undani katika Kut. 25-27 na kujengwa katika 36-38, 40. Mwandishi wa kitabu cha Waembrania analirejelea kusudio la ndani kama lilivyo (la nje) hema la kwanza (mahali patakatifu) na hema la pili (ya ndani) (Patakatifu pa Patakatifu).

■"**kinara cha taa**" Kipengele hiki kinakirejelea moja ya kinara chenyetaa zake sabazenye kuuteketiza mzeituni, kilichowekwa mahalai patakatifu. Hiki kinarejelewa katika Kut. 25:31-40 na Law. 24:1-4. Hiki kiliitwa *Menorah*, ambapo hili ni neno la Kiebrania la "kinara." Suleimani alikipanua kinara hadi mikono kumi (kama vile 1 Wafalme 7:49; 2 Nya. 4:7). Hiki kinaashiria nuru ya haki na ufunuo.

■"**meza, na mikate ya Wonyesho**" Meza hii ilikuwa imewekwa mahali patakatifu ikiwa imebeba mikate mikubwa kumi na miwili (15 lb.). Hii ilitolewa kwa juma na kuwa chakula cha Makuhani (kama vile Kut. 25:23-30; 37:10-16; Law. 24:5-9). Hii iliwakilisha utoaji wa kimwili uliohaidiwa kwa ajili ya makabila kumi na mawili ya Yakobo.

■"**Patakatifu**" Hiki ni chumba cha nje cha banda kilichotumiwa na makuhani kufanya huduma siku nzima. Hiki kilikuwa na vipimo vipatavyo dhira 20 kwa dhira 10 (kama vile Kut. 25-27). Mara nyingi mwandishi wa kitabu cha Waembrania analitumia hili neno (*hagia*) pamoja na kiambata (kama vile Ebr. 9:8,25; 13:11) na analitumia kwa sehemu ya ndani au ya pili ya hema la maonyesho lililoitwa Patakatifu pa Patakatifu (kama vile Ebr. 9:3) mahali ambapo Sanduku liliwekwa, lakini katika mstari huu kiambata hakipo na neno linairejelea sehemu ya

nje mbili ya tatu ya hema ya wonyesho, iliyoitwa patakatifu.

**9:3 "pazia la pili"** Hili lilitigawa hema katika sehemu mbili (kama vile Kut.26:31-35). Kitabu cha Waembrania kina najina mawili maalum, moja kwa ajili ya pazia la mbele, ambalo litikuwa likifunguliwa mara kwa mara, na moja pazia la ndani, ambalo halikufunguliwa kamwe. Ni kuhani mkuu pekee aliyeingia (mara mbili) katika Siku ya Upatanisho (kama vile Law. 16).

**■"Patakatifu pa patakatifu"** Hapa palikuwa ukamilifu wa dhira 10. Hili ilihuisha sanduku ambapo kiishira YHWH alikaa katikati ya bawa la kerubi. Sanduku hili ishara ya kimwili ya Mungu asiyeonekana. (baada ya wao kuingia katika Nchi ya Ahadi).

**9:4 "chetezo cha dhahabu"** Hiki kilikuwa kipande cha samani kilichoumbwa kwa ajili ya madhabahu ambapo uvumba uliwekwa katika ubora wa hali ya juu kwa ajili ya Siku ya Upatanisho kwa ajili ya kutoa moshi mwembamba uliotanda kuonyesha uwepo waYHWH ju ya sanduku la agano. Mwandishi wetu anaonekana kukiweka chombo hiki ndani ya Partakatifu pa patakatifu. Hili liliwasababisha watoa maoni kukichukuwa kifungu hiki na kulirejelea neno "chetezo" kwa sababu hivi ndivyo Agano la Kale la Kiebrania linavyolitafsiri neno hili (kama vile Law. 16:12; 2 Kor. 26:19; Eze. 8:11; IV Mak. 7:11). Hata hivyo, Philo na Josephus wanalitumia neno lile lile la Kiyunani kwa ajili ya kuifukiza madhabahu. Katika Agano la Kale madhabahu inatambuliwa kwa ukaribu kutokanana Patakatifu pa Watakatifu (kama vile Kut. 30:1-10, 37; lakini hasa 1 Fal. 6:22).

Majivu yalichukuliwa toka katika madhabahu kuu ya dhabihu mlangoni mwa hema na kuwekwa katika kinara hiki kidogo. Kisha uvumba ulichanganya na majivu ili kusabisha kiwango kikubwa cha moshi. Moshi huu wenye harufu ya kushangaza uliyazuia macho ya kuhani kutomuona YHWH, aliyekaa juu ya sanduku la agano kati ya mabawa ya kerubi, katika Patakatifu pa Patakatifu.

**■"sanduku la agano"** Sanduku hili linaelezwa katika Kut.25:10-22 na 37:1-9.

## MADA MAALUM: SANDUKU LA AGANO

- I. Mpangilio wake (Kutoka 25: 10-22)
  - A. sanduku la mbao lilitofunikwa na dhahabu (Kut. 25: 20-11)
  - B. dhira 2½ kwa dhira 1½ na dhira 1½ (kama vile Kut. 25:10; kwa "dhira" tazama [MADA MAALUM: DHIRAA](#))
  - C. inayochukulika na pete na miti (Kut. 25: 12-16)
  - D. kifuniko cha sanduku kilikuwa tofauti (Kut. 25:17-21)
    1. Imefanywa kwa dhahabu na inafaa juu ya sanduku la mbao (Kut. 25: 10,21)
    2. kulikuwa na makerubi mawili juu ya kifuniko chake, wakikabiliana (Kutoka 25: 18-20)
- II. Mahali na kusudi lake
  - A. mahali pa kukutana na Israeli (Kutoka 25:22)
  - B. mahali ambapo YHWH alikaa (yaani, sakafu ya miguu yake, ona 1 Nya. 28: 2, Zab. 132: 7, Isa. 66: 1) pamoja na watu wake, katika sanduku la agano kati ya mabawa ya *makerubi* (tazama [MADA MAALUM: MAKERUBI](#))
  - C. mahali pa msamaha wa dhambi (yaani, kiti cha huruma), kwa watu wote (kama vile Israeli, Mambo ya Walawi 16 na 1 Wafalme 8: 27-30; wageni, 1 Wafalme 8: 41,43,60)
  - D. kipande pekee cha samani katika Patakatifu pa Patakatifu, ndani ya pazia
- III. Yaliyomo
  - A. Utamaduni wa walimu wa sheria za Kiyahudi
    1. vidonge viwili vya jiwe ambalo YHWH aliandika mazungumzo (kama vile Kut. 31:18; 32:15-16)
    2. nguzo mbili za fedha ambazo zinashikilia vibao (hakuna kumbukumbu za kibiblia)
    3. vipande vya vibao vya awali vilivyovunjwa na Musa kwa sababu ya Israeli (Haruni) na kufanya ibada ya ndama ya dhahabu (kama vile Kut. 32:19, Kumb. 9:17; 10: 2)

4. nakala ya Torati nzima (kama vile Kut. 25:16)
5. majina ya Mungu (kama vile 1 Wafalme 8:29) yaliyotengenezwa huko Kabbalah, ujuzi wa Kiyahudi
- B. marejeo ya kibiblia kuhusiana na yaliyomo (hayajulikani kama haya yanataja vitu ndani ya sanduku au vilivyo pemberi mwake)
1. gudulia la mana (kama vile Kut. 16: 31-36)
  2. fimbo ya Haruni iliyotengeneza (kama vile Hesabu 17: 4,10, Waembrania 9: 4)
  3. matoleo kosa ya Wafilisti (panya 5 wa dhahabu na majipu ya dhahabu, tazama 1 Sam 6: 3-4,8)
  4. nakala ya Amri Kumi za Mungu (kama vile Kut. 25: 16,21; Kumb. 10: 4-5; 31:26)
- C. wakati wa kujitolea kwa Hekalu la Sulemani katika 1 Wafalme 8 Sanduku inasemekana kuwa na vidonge viwili vya jiwe (yaani, Maneno Kumi, kama vile 1 Fal. 8: 9)
- IV. Liko wapi kwa sasa?
- A. chaguzi za kihistoria
1. alichukuliwa Misri na Shishaki (935-914 kb) alipopigana na Yuda mwaka wa tano (926 kb) wa Rehoboamu (mwana wa Sulemani) kutawala (kama vile 1 Fal.14: 25-26, 2 Nya. 12: 9)
  2. Kupelekwa Misri (Zoan, Tanis, Avaris - majina tofauti kwa mji mkuu wa delta wa Seti I) na Farao Necco II, ambaye pia alihamisha mbegu ya Yehoahazi (mwana wa Yosia) mwaka 597 kb. (kama vile 2 Fal.23: 31-35; 2 Nya 36: 1-4)
  3. kupelekwa Babeli kwenye hekalu la Marduk na Nebukadreza wa II wakati Zedekia alipokuwa akihamishwa (586 k.k) na Hekalu likawaka (kama vile 2 Fal. 25: 9, 13-17, 2 Nya. 36:18)
- B. Desturi za Kiyahudi
1. kufichwa juu ya Ml. Nebo / Pisga na Yeremia kabla ya kuanguka kwa Yerusalem (2 Mak .2: 4-5)
  2. kitabu cha Apocrypha ya 2 Baruki anasema malaika aliificha
  3. kufichwa kwa njia isiyojulikana, lakin i tarudiwana Eliya kabla ya Masihi kuja (kama vile Mal. 4: 5)
  4. kufichwa juu ya Ml. Gerizim (Shekemu) ambapo Wasamaria walijenga hekalu yao kwa YHWH
  5. kuzikwa chini ya Hekalu (yaani, Ml. Moria) kabla ya Nebukadreza kukamata Yerusalem.

■ "kopo la dhahabu lenye ile mana" Agano la Kale la Kiebrania naPhilo lina kivumishi "dhahabu "lakini Andiko la Kiebrania la Kimasoteri halina kifungu hiki (kama vile Kut. 16:31-36). Josephus anasema hili lilikuwa painti Zipatazo 4. Ni muujiza kwamba manna haikuza (kama vile Kut. 16:18-21,22-25).

■ "fimbo ya Haruni iliyochipuka" Fimbo hii ilikuwa ishara yaYHWH ya kuuthibitisha uongozi wa Musa na Aruni wakati wa uasi ya Kora (kama vile Hes. 17:1-11; 20:8-11).

■ "vibao vya agano" Kifungu hiki kinazirejelea mbao mbili za mawe zilizokuwa na amri za Mungu (maneno kumi) yaliyokuwa yameandikwa juu yake kwa kutumia kidole cha Mungu (kama vile Kut. 25:16; Kumb. 9:9,11,15;10:3-5; 31:18; 32:15). Vitabu vya Kumbukumbu la Torati na Yoshua 24 vinaufuatisha muundo wa Wa-Hiti (wa milenia ya pili k.k.). Mara nyingi maagano yao yalikuwa na nyaraka mbili, moja kwa ajili ya mjakazi wa mfalme kwa ajili ya kuisoma kwa mwaka na moja kwa ajili ya kuitenga kwa minajiri ya Uungu. Hivyo, mbao mbili za mawe zingekuwa nyaraka nara dufu.

**9:5 "makerubi ya utukufu"** Maelezo haya yanavirejelea viumbe viwili ya kimalaika ambapo kwa kila kimoja kinashia na kiti cha rehema (kinafunika), ambaye mabawa yake yalilifunika sanduku (kama vile Mwa. 3:24; Kut.25:18-22; Eze. 10:14, lakini si yule aliye katika Eze. 41:18 hawa wana nyuso mbili, si nne). Uchaguzi mpya kutoka katika Historia ya video, "Rekodi ya Kitabu cha Kutoka" unadai kwamba hawa walikuwa ndege aina ya finaksi. Biblia haifunui habari zaidi kuhusu ulimwengu wa kimalaika.Mara nyingi uchunguzi wetu unaenda mbali

zaidi ya kweli iliyofunuliwa. Kwa neno "utukufu" tazama maelezo katika Ebr. 1:3.

▣ **"kiti cha rehema"** Hiki kinarejelea ukingo wa dhahabu wa sanduku la mbao ulichoitwa "sanduku la agano." Hili lilikuwa eneo maalum kwa "kufunika" dhambi. Viashiria vinaonekana kuwa

1. YHWH alikaa katikati ya mabawa ya viumbe viwili nya kimalaika (walimu wa sheria walisema kuwa hii ilikuwa sehemu ya kuwekea miguu yake)
2. sanduku lilikuwa na "amri kumi" (Amri za Mungu)
3. Kuhani mkuu, katika Siku ya Upatanisho (kama vile Mambo ya Walawi 16), alikwenda katika Patakatifu pa Patakatifu mara mbili kuiweka damu juu ya kiti cha rehema, kwa ajili ya dhambi yake na kwa ajili ya dhambi isiyokusudiwa kama taifa zima (kama vile Ebr. 9:7)

Mahitaji ya Sheria yalifunika, yalifunika kutoka machoni pa YHWH kwa dhabihu ya damu ya mnyama asiye na dosari (uhai u katika damu; dhambi huihitaji uhai).

▣ **"basi hatuna nafasi sasa ya kueleza habari za vitu hivi kimoja kimoja"** Hili ni kanusho. Mwandishi wetu anatumia ufanuzi wa kiundani toka hema la kale ambalo sasa halijulikani.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 9:6-10**

<sup>6</sup>Basi, vitu hivi vikiisha kutengenezwa hivyo, makuhani huingia katika hema hiyo ya kwanza daima, wakiyatimiza mambo ya ibada. <sup>7</sup>Lakini katika hema hiyo ya pili kuhani mkuu huingia peke yake, mara moja kila mwaka; wala si pasipo damu, atoayo kwa ajili ya nafsi yake na kwa dhambi za kutokujua za hao watu. <sup>8</sup>Roho Mtakatifu akionyesha neno hili, ya kwamba njia ya kupaingia patakatifu ilikuwa haijadhihirishwa bado, hapo hema ya kwanza ilipokuwa ingali ikisimama; <sup>9</sup>ambayo ndiyo mfano wa wakati huu uliopo sasa; wakati huo sadaka na dhabihu zinatolewa, zisizoweza kwa jinsi ya dhambi kumkamilisha mtu aabuduye, <sup>10</sup>kwa kuwa ni sheria za jinsi ya mwili tu, vyakula na vinywaji na kutawadha kwingine kwingine, zilizoamriwa hata wakati wa matengenezo mapya.

**9:6 "huingia katika hema hiyo ya kwanza daima"** Iliwalazimu makuhani kuvijaza vyombo vilivyokuwa juu ya menorah kwa mafuta (kama vile Kut. 27:20-21), kuuondoa mkate wa juma (kama vile Law. 24:8-9), na kukiondoa kiwango kidogo cha uvumba katika madhabahu ya uvumba (kama vile Kut. 30:7-8).

**9:7 "kuhani mkuu . . . mara moja kila mwaka"** Huyu ndiye mtu wa pekee aliyeingia Yom Kippur, Siku ya Upatanisho (kama vile Law. 16). "Kipper" linamaanisha "kufunika"; Akkadian cognate linamaanisha "kuteketeza." Kitabu cha Waebrania 9 kinazitazamia taratibu za Siku ya Upatanisho kuliko sura zingine zilizo katika Agano Jipy.

▣ **"kutokujua"** Ni dhambi zilizofanyika pasipo hatia pekee ambazo zingeshughulikiwa kwa mfumo wa kidhabihu. Dhambi za kimataifa, au "dhambi za mkono mkuu" (KJV) zisingepatanishwa (kama vile Law. 4:2; Hes.

15:24,27,30,31; Zab. 51:17). Hii Siku ya Upatanisho hapo awali ilikuwa ikishughulika na mambo ya unajisi yaliyokuwa yakitendwa na taifa.

**9:8-10** Mistari hii inaonyesha (1) asili ya kwanza ya agano la Musa na (2) ukuu wa agano jipy. Ni kwa namna gani agano jipy katika Kristo ni bora?

1. katika lile la kale kuhani mkuu alilingia mahali patakatifu mara moja kwa mwaka kwa sababu ya dhambi zake na dhambi za Israeli zisizokusudiwa (kwa upenyo wenye mipaka na nsamaha usio na mipaka).
2. Katika agano jipy waamini wote wanasogezwa karibu na Mungu kwa sababu ya Yesu kutokuwa na dhambi na ondoleo la tofauti kati ya dhambi za kukusudiwa na dhambi zisizokusudiwa (upenyo kamili na timilifu).

Agano jipy (kama vile Yer. 31:31-34), lilijikita katika kazi ya Kristo iliyokwisha kukamilika, si tunu ya utendaji wa mwanadamu wa kanuni za nje, uliowapa ujasiri wale waabuduyo (moyo mpya, roho mpya, kama vile Eze. 36:20-27) kumkaribia Mungu mtakatifu, si kuititia kanuni za matukio au liturujia (kama vile Ebr. 6:1-2), bali kuititia injili

**9:8**

- NASB "hema ya kwanza"  
 NKJV "hema ya kwanza"  
 NRSV "banda la kwanza"  
 TEV "banda la kwanza"  
 NJB "banda la awali"

Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania anaiita sehemu hii ya kwanza ya hema "hema ya kwanza," akiparejelea "patakatifu." Hili lingewakilisha agano la Musa la ibada, ambalo haliikuruhusu kumfikia kikamilifu Mungu. Pazia la Hekalu la Herode liliopasuka toka juu hadi chini wakati Yesu alipokata roho (kama vile Mt. 27:51) liliashiria upenyo mpya kupitia Kristo.

**9:9 "zisizoweza kwa jinsi ya dhambi kumkamilisha mtu aabuduye"** Agano la Kalekuisafisha hatia ya dhambi kutokana na dhamiriya mwanadamu (kama vile Ebr. 9:14). Dhamiri iliyo katika Agano Jipy (si Agano la Kale) ni mwongozo wa kimaadili (kama vile 1 Pet. 3:21). Hatari ni kwamba hii inaweza kuwa amrishi au matumizi mabaya kitamaduni katika namna ya ukimya (kama vile Mt. 23:25-26). Hiki ni kijalizo cha Agano Jipy cha kifungu "sauti ya upole iliyotoka katika namna ya upopo au "sauti ndogo, ya utulivu" cha 1 Fal. 19:12.

Mjadala wa natumizi ya neno hili wenye kuvutia sana katika Kitabu cha Waebrania unapatikana katika Robert B. Girdlestone's

*Ufanano wa Agano la Kale*

"Vifungu vilivyo katika waraka kwa Waebrania vinayo maneno ambapo kila neno linalojitokeza linavutia sana na ni la muhimu. Kutokana na Ebr. 9.9, tunagundua kwamba sadaka zilizoendeshwa chini ya Agano la Kale hazikuwa na uwezo wa kumfanya mtu kuwa kamilifu kama ilivyohusiana na dhamiri yaani., zisingeiondoa dhana ya dhambi ambayo ilikuwa imemgubika mwanadamu kutoka umoja na Mungu. Hizi zisingeiondoa dhambi, kama kiini, na zisingeweza, kutokana naasili ya mambo; ikiwa matokeo ya mfumo wa Kilawi yalikuwa ni kuwafanya watu kuwa wakamilifu, yaani katika kuwa wamoja na Mungu, sadaka zisingehitaji kurudiwarudiwa. Ikiwa waabuduo wamekuwa wakisafishwa mara moja kwa ajili ya wote, hizi zisingekuwa na dhamiri zaidi juu ya dhambi (Ebr. 10.2). Bali utakaso wa damu ya Kristo kwa dhamiri ya mwanadamu kutoka matendo mafu, na kumwezesha kumtumikia Mungu aliye hai (Ebr. 9.14); na moyo wake ndiyo 'dhamiri mbaya tumeoshwa (10.22). Katika maneno mengine, uaminifu wa ukubalifu wa dhabihu ya Kristo unaiondoa dhana ya dhambi ambayo imekuwa kizuizi kati ya mwanadanu na Mungu, na kumwezesha mwanadamu kutoishi kama mtumwa, bali kama mwana" (uk. 73).

▣"kumkamilisha" Tazama Mada Maalum katika Ebr. 7:11.

**9:10**

- NASB "wakati wa matengenezo mapya"  
 NKJV "wakati wa marekebiso"  
 NRSV "wakati unakuja kuyaweka mambo sawa"  
 TEV "wakati Mungu atahimarisha mpango mpya"  
 NJB "wakati unakuja kuyaweka sawa"

Hiki kinalirejelea agano jipy lililoanzishwa katika Yesu. Kifungu hiki kilikuwa kikitumiwa na walimu wa sheria za Kiyahudi wa "Jubilee" iliyopita wakati ambao angekuja Masihi. Hiki kinatumika katika maana ya kimaadili iliyo katika Yer. 7:3,5.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 9:11-14**

<sup>11</sup> Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu, <sup>12</sup>wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe alilingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele. <sup>13</sup>Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe walivyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili; <sup>14</sup> basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye

**kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?**

**9:11 "Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu"** Hili lilitokea:

1. kabla ya uumbaji (kama vile Ufu. 13:8)
2. huko Kalvari (kama vile Ebr. 9:12)
3. baada ya kupaa kwa mkono wa haki ya Baba (aliingia patakatifu huko mbinguni, kama vile Ebr. 9:24-25)

Je! Yesu alijitoa mara mbili? Ikiwa ni hivyo, kwa nini nkazo u juu ya "kwa ajili yetu?" Huenda alijitoa kama dhabihu ya Kalvari, lakini atenda kama kuhani mkuu baada ya ufufuo wake au inaweza kurahisishwa kama (1) sura ya kithiolojia au (2) hiolojia ya walimu wa sheria za Kiyahudi iiliyovuviwa.

▣ "**wa mambo mema yatakayokuwapo**" Tofauti ya machapisho ya Kiyunani: (1) "mambo yajayo" katika, **A** (NASB, NKJV, NJB) na (2) "mambo yaliyokwisha kuwepo hapa" katika **P<sup>46</sup>**, **B**, **D\*** (RSV, NEB, TEV, NIV).

▣ "**isiyofanyika kwa mikono**" Wengine wanakiona kifungu hiki kama rejea ya waamini waliofufuliwa miili yao (kama vile 2 Kor. 5:1) na mwili wa Kristo (kama vile Marko 14:58). Hata hivyo, muktadha unaonekana kulirejelea hekalu la mbinguni (kama vile Ebr. 8:2; 9:24).

**9:12 "si kwa damu ya mbuzi na ndama"** Mbuzi walikuwa kwa ajili ya dhambi za watu (kama vile Law. 16:11) na ndama walikuwa kwa ajili ya dhambi za makuhani wakuu (kama vile Law. 16:11). Mfumo wa Agano la Kale wa utuaji dhabihu (kamavile Law. 1-7) ulikuwa utoaji wa neema ya Mungu wa kumruhusu (kama kukitabiri kifo cha Kristo) mnyama asiye na hatia kuilipia adhabu ya kifo kwa ajili ya dhambi ya mwanadamu (kama vile Law. 17:11).

▣ "**bali kwa damu yake mwenyewe**" Kihisishi cha Kiyunani "*dia*" kinaweza kumaanisha (1)"kupitia" (NASB, NIV) au (2) "pamoja" (NKJV, NRSV, NJB).

▣ "**Patakatifu**" Hapa hiki kinamaanisha "Patakatifu pa patakatifu" cha hekalu la mbinguni.

▣ "**mara moja**" Mara nyingi huu ni msisitizo wenye kurudiwa rudiwa(kama vile Ebr. 7:27; 9:28; 10:10). HUU unasistiza juu ya ukamilifu wa Kristo na dhabihu iliyokwisha malizika. Tazama Maelezo kamili katika Ebr. 7:27.

**9:12**

**NASB, NKJV**

**NRSV**      "ukombozi wa milele uliokwisha patikana"

**TEV**      "wokovu wa milele uliokwisha patikana"

**NJB**      "kwa kuupata ukombozi wa milele"

Hii ni kauli ya kati endelevu, yenye kudokeza tendo lililikamilika lenye kusistiza juu ya ushiriki wa mtu na matakwa yake. Hili neno "milele" linaweza kuhusiana na (1) ubora wake, "maisha ya enzi mpya" au (2) uzito wake, "maisha yasiyo na mwisho." Pamoja na maonyo yaliyo katika kitabu cha Waebrania yenye kusismua sana, huenda #1 inaendana vema. Tazama Mada Maalum: Milele katika Ebr. 6:2.

▣ "**ukombozi**" Neno hili linairejelea fidia iliyolipwa kwa uhusianao wa karibu kwa ajili ya tamko la mtu. Hii ni "*go'el*" ya Agano la Kale (kama vile Ruthu 4; Isa. 43:1; 44:22,23; 48:20; 12:9; 63:9; Hos. 13:14).

**9:13 "ikiwa"** Hii ni sentensi daraja la kwanza yenye kudhaniwa kuwa ya kweli. Mungu aliuukubali mfumo wa Musa kama njia ya kuifunika dhambi hadi Kristo!

▣ "**majivu ya ndama ya ng'ombe**" Haya najivu ya ndama ya ng'ombe mwekundu yalitumika katika taratibu za kujitakasa (kama vile Hesabu 19).

■ "waliyonyunyiziwa" Hii ilikuwa sehemu ya taratibu zaMusa zilizohusisha vimiminika (damu au majivu ya ndama ya ng'omb mwekundu vilichang'anywa na maji). Hii ilikuwa njia ya kuubadili utakatifu au nguvu ya utakaso. Robert B. Girdlestone katika kitabu chake cha *Synonyms of The Old Testament* anayo maoni yeny kuvutia.

Kifungu "waliyonyunyiziwa (*shantismoi*) hasa kilichorejelewa katika Warakakwa Waebrania ni cha aina mbili—ambacho pamoja na majivu ya ndama ya mg'ombe mwekundu kwa mtu aliyenajisika (Ebr. 9.13), na ile ilifanya kwa damu kwa watu na Kitabu katika kulifanya agano la kale; pia katika hekalu na vyombo mbalimbali vilivyohusiana na kutengwa kwa ajili ya huduma (Ebr. 9.19,21).

Mambo ambayo haya ni kivuli chake yananyunyiziwa damu ya Yesu, inenayo mema kuliko ya Abeli (Ebr. 12.24)" (uk. 152).

**9:14"si zaidi"** Kwa kuyalinganisha maagano dhanira ya kitabu (kama vile Ebr. 2:1-3; 3:3; 8:6; 10:28-29).

■ "ambaye kwamba kwa Roho wa milele" Kwa vyo vyote vile hii ni roho ya Kristo iliokwisha kuwako au Roho Mtakatifu.

Umoja wa Vyama vya Biblia 'A Handbook on The Letter to the Hebrews' na Ellingworth na Nida, unaorodhesha kasabu kadhaa zilizoufanya kuiandika herufi "s" kwa herufi ndogo ambapo idadi kubwa ya tafsiri za sasa (NASB, NKJV, NRSV, TEV, NJB, NIV) zinaiandika herufi hii kwa herufi kubwa

1. hapa hakuna kibainishi cha wazi
2. mara nyangi mwandishi anamzungumzia "Roho Mtakatifu" na kumweleza kwa hili jina kamili
3. kifungu hiki kinawenza kuwa sawa na kifungu "nguvu ya maisha ya milele" katika Ebr. 7:16 (uk. 196).

Katika maoni yake kuhusianana kitabu cha Waebrania yaliyo katika *New International Commentary Series*, F. F. Bruce yanatengeneza maoni yeny kuvutia kwamba dhana ya Roho ni dokezo na vipengele vya Isaya vilivyo na kifungu "Nyimbo za mtumishi" (sura za 40-54). Katika kipengele hiki, 42:1 anasema "nimetia roho yangu juu yake" (uk. 205). Katika kitabu kama Waebrania, kinakitungia kitabu cha Agano la Kale kwa uhuru sana, hili naitengeneza maana nzuri.

■ "alijitoa nafsi yake" Hili ni tendo la Kristo lililo la hiari (kama vile Yohana 10:17-18; 2 Kor. 5:21; Fal. 2:8, Isa. 52:13- 53:12). Tazama [MADA MAALUM: YESU KAMA KUHANI MKUU](#) katika Ebr. 2:17.

■ "isiyo na mawaa" Tazama Mada Maalum katika Ebr. 7:26.

■ "na matendo mafu" Kifungu kama hiki kinajitokeza katika Ebr. 6:1 kama chenye kinazirejelea taratibu na hatua za Agano la Kale kama njia ya kuupata wokovu. Maana kamili ni damu ya mbadala ya upatanisho wa Mwana-kondoo wa Mungu iliokwisha kukamilishwa (kama vile Yohana 1:29; 1 Yohana 3:5). Kwa ukweli nayakubali maoni ya M. R. Vincent katika kitabu chake cha *Word Studies in the New Testament*, yeny kuyahusianisha matendo mafu na sheria ya haki binafsi:

"Hii inabadilisha tabia ya matendo kwa kuyaweka mbali na hali ya mauti. Hali hii si ya kazi zilizotambuliwa kama dhambi na kutendwa na wanadamu wenyenye dhambi tu, bali kwa kazi zinazotendeka chini ya jina la kidini, na ambazo zinatendwa kwa makusudi ya roho ya sheria. Mbali na hayo, kwa sababu huu ni misingi wa imani ya dini, Ukristo hutumia matakwa na misingi ya kuzijaribu kazi. Kwa uaminifu Professor Bruce anasema kwamba 'uzito wa kuijribu nguvu ya Kristo ya ki-ukombozi ni uwezo wake wa kuiondoa mipaka yeny kushamiri katika dini ya sheria, ambapo wengi walioukwepa utawala wa mabaya wamefungwa, tabia za dhambi'" (kr. 1139-1140).

■ "kumwabudu Mungu aliye hai" Tambua kwamba waamini wanaokolewa ili kutumika (kama vile Warumi 6). Wokovu ni uhuru toka nguvu ya dhambi, kuelekea ubwana wa Mungu! Wokovu si zao (tiketi iliopatikana hapo awali kwa ajili ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya majanga ya moto), bali uhusiano wa imani, utii na huduma. Waamini wote wamekirimiwa kwa ajili ya huduma (kama vile Efe. 4:11-12) na huduma kwa ajili ya mwaili wa Kristo (kamavile 1 Kor. 12:7,12).

Hiki kivumishi "hai" ni mbinu ya uchezaji wa maneno unaohusu jina la agano la Agano la Kale lihusulo Uungu, YHWH, ambalo linatokana na asili ya kitenzi "kuwa." YHWH anaishi milele, ndiye Aishiye pekee!

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

### A. *El*

1. maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataaluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, “kuwa shupavu” au “kuwa mwenye nguvu” (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb. 7:21; Zab. 50:1).
2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra)
3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika njia ya kuainisha tabia za Mungu.
  - a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sana), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
  - b. *El-Roi* (“Mungu aonaye” au “Mungu ajifunuaye Mwenyewe”), Mwanzo 16:13
  - c. *El-Shaddai* (“Mungu Mkuu” au “Mungu mwenye huruma zote” au “Mungu wa mlima”), Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3
  - d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, II Sam. 7:13,16
  - e. *El-Berit* (Mungu wa Agano”), Waamuzi 9:46
4. *El* inalinganishwa na
  - a. YHWH katika Zaburi. 85:8; Isa. 42:5
  - b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu5:8, “Mimi ni *El*, *Elohim* wa baba yako
  - c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
  - d. “wivu” katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
  - e. “rehema” katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31; “mwaminifu” katika Kumb. 7:9; 32:4
  - f. “mkuu na mzuri” katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
  - g. “maarifa” katika I Sam. 2:3
  - h. “kimbilio langu” katika II Sam. 22:33
  - i. “mlipa kisasi wangu” katika II Sam. 22:48
  - j. “mtakatifu” katika Isa. 5:16
  - k. “muweza” katika Isa. 10:21
  - l. “wokovu wangu” katika Isa. 12:2
  - m. “mkuu na mwenye nguvu” katika Yer. 32:18
  - n. “anayepatiliza: katika Yer. 51:56
5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Joshua 22:22 (*El*, *Elohim*, *YHWH*, kurudiwa)

### B. *Elyon*

1. Maana yake ya msingi ni “juu,” “aliyetukuzwa,” au “kuinuliwa” (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; II Wafalme. 18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
  - a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
  - b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14
  - c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
  - d. *El* - Hes. 24:16
  - e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya “Mungu aliye Juu”) katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
  - a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
  - b. Balaamu, Hes. 24:16
  - c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
  - d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)

- C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja), inatumika kimsingi katika ushairi
1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
  2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahim walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Josh. 24:2).
  3. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)
  4. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104). Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*elohim*) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.
  5. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa Israeli lakini siku zote lina kitenzi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.
  6. Neno hili linapatikana katika vinywa vya wasiokuwa Waisraeli kama jina la Uungu.
    - a. Melkizedeki, Mwanzo. 14:18-22
    - b. Balaamu, Hes. 24:2
    - c. Musa anapozungumzia mataifa, Kumb. 32:8
  7. Inashangaza kwamba jina lililozoleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
    - a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa "wingi wa ukuu," mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
    - b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7).
    - c. Inawezekana hata inaaksi ufunuo wa Agano Jipywa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipywa Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).
- D. YHWH
1. Hili ni jina ambalo linaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi, mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na *Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo (1) Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili) na (2) Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu. Mwanzo 2:4 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.
  2. Katika Mwanzo 4:26 inasema "wanadamu wakaanza kuliiitia jina la BWANA" (YHWH). Hatahivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezewa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hatahivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa utani maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo. 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).
    - a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, "kuonesha upendo wa dhati"
    - b. kutoka katika mzizi wa kiarabu "kupuliza" (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
    - c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) "kuzungumza"
    - d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KAULI SABABISHI ENDELEVU ikimaanisha "Yeye"

- anayetosheleza," au "yeye anaye anzisha"
- e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* "Yeye ambaye yupo," au "Yeye aliyepo sasa" (katika namna ya wakati ujao, "Yeye atakayekuwako")
  - f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* "yeye asababishaye kuwa"
  - g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania "kuishi" (mfano Mwanzo. 3:20), maana "Mungu mmoja tu aishiye milele"
  - h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, "nitaendelea kuwa vile nilivyokuwa" au "nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa" (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezewa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili
    - (1) *Yah* (mfano Hallelu - yah)
    - (2) *Yahu* (majina mfano Isaya)
    - (3) *Yo* (majina mfano Joeli)
3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lilifasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania "mmiliki," "Mkuu," "mume," "bwana"—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka "bwana." Hii ndio maana YHWH inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.
  4. Kama ilivyo kwa *El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwangi wa maneno, hapa ni baadhi.
    - a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa), Mwanzo. 22:14
    - b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), Kutoka. 15:26
    - c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu), Kutoka. 17:15
    - d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye), Kut. 31:13
    - e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani), Waamuzi. 6:24
    - f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii
    - g. *YHWH - Ro'I* (YHWH ni mchungaji wangu), Zab. 23:1
    - h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu), Yer. 23:6
    - i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa), Eze. 48:35

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 9:15-22

<sup>15</sup> Na kwa sababu hii ni mjumbe wa agano jipya, ili, mauti ikiisha kufanyika kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza, hao walioitwa waipokee ahadi ya urithi wa milele. <sup>16</sup> Maana agano la urithi lilipo, lazima iwepo mauti yake aliyelifanya. <sup>17</sup> Kwa maana agano la urithi lina nguvu palipotukia kufa kwa mtu; kwa kuwa halina nguvu kabisa, akiwa yu hai yeye aliyelifanya. <sup>18</sup> Kwa hiyo hata lile la kwanza halikuanzwa pasipo damu. <sup>19</sup> Maana kila amri ilipokwisha kunenwa na Musa kwa hao watu wote, kama ilivyoamuru sheria, aliiitwaa damu ya ndama na ya mbuzi, pamoja na maji na sufu nyekundu na hisopo, akakinuyunizia kitabu chenyewe, na watu wote, <sup>20</sup> akisema, Hii ni damu ya agano mliloamriwa na Mungu. <sup>21</sup> Na ile hema nayo na vyombo vyote vya ibada alivinyunizia damu vivyo hivyo. <sup>22</sup> Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo.

9:15 "mjumbe" Tazama Mada Maalum katikaEbr. 8:6 (kama vile Ebr. 12:24; 1 Tim. 2:5).

▣ "wa agano jipya" Kwa mara ya kwanza neno hili linatumika katika Ebr. 8:8,13, lakini linadokezwa katika Ebr. 7:22. Hili neno lenye kuogofya linapatikana katika andiko la Agano la Kale pekee (kama vile Yer. 31:31-34) na kuelezwu katika Eze. 36:22-38. Mistari ya 15-18 inacheza na maneno ya neno "agano," pamoja na maana zake mbili za mkataba wa sheria au makubaliano (Waebrania) na mapenzi na agano la mwisho (Kiyunani na Kilatini).

■ "kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza, hao walioitwa waipokee ahadi ya urithi wa milele" Kumbuka kwamba kitabu cha Waebraniani ulinganifu wa Agano la Kale na Agano Jipy. Agano la Musa lilikuja kuwa hukumu ya kifo (kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14) kwa uumbaji mkuu wa Mungu (mwanadamu) kwa sababu baada ya Mwanzo 3 hawakuwa na uwezo wa kuyatii na kuyaishi maagano ya Mungu. Agano la kwanza la Mungu linasema "tenda na ishi," lakini hakuna mtu awezaye kuyakamilisha nahitaji yake. Agano la Kale lilieleza "lakini kila mtu atakuifa" (kama vile 2 Fal. 14:6; Eze. 18:4,20). Jibu la Mungu halikuwa na dhambi, Waisraeli waliorakamilifu ambao wangelipa gharama kwa ajili ya wote, kwa wakati wote (kama vile Isa. 52:13-53:12).

Kifungu hiki "hao walioitwa" kinaurejelea wito asilia wa Mungu ili kumjua yeye (kama vile Ebr. 3:1; Yohana 6:44,65; Rum. 8:28,30; 9:24). Tazama maelezo kamili katika Ebr. 3:1.

Dhana ya "urithi" inahusianishwa na upekee wa uhusiano wa Kilawi kwa YHWH. Hawa walikuwa urithi wake na yeye ni wake (si ardhi yalivyo makabila mengine). Waamini wa Agano Jipy sasa ni makuhani wa Agano la Kale (kama vile 2 Pet. 3:5,9; Ufu. 1:6). Waamini wanao urithi wa milele, ambao unaletwa na Kristo, akitunzwa na Mungu (kama vile 1 Pet. 1:3-5).

## MADA MAALUM: FIDIA/KOMBOA

### I. AGANO LA KALE

- A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.
  - 1. *Ga'al* (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno *go'el* unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nydingi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25,27), au ndugu na (kama vile Ruthu 4:14; Isa. 29:22) hili linaawilishwa kitheolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).
  - 2. Neno *Padah* (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
    - a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
    - b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozik wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)
    - c. YHWH ataikomboa Israeli katoka katika dhambi na uhasi wao (Zab. 130:7-8)
- B. Dhana ya kitheolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
  - 1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
    - a. Kimaumbile
    - b. Kijamii
    - c. kiroho (kama vile Zab. 130:8)
  - 2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
    - a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
    - b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
  - 3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya *ga'al* mara nydingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (i.e., *go'el*, BDB 145).
  - 4. Mara nydingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
    - a. Baba
    - b. Mme
    - c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kuititia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

### II. AGANO JIPY

- A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kitheolojia.
  - 1. *Agorazō* (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu

tusioyandesha maisha yetu wenyewe. Sisis ni wa Kristo.

2. *Exagorazō* (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laanae" utedaji uliojikita ndani ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenyewe dhambi wasingeitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamili, ukubalifu, na upenyo!
  3. *Luō*, "kuweka huru"
    - a. *Lutron*, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulimwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
    - b. *Lutroō*, "kuwekwa huru"
      - 1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)
      - 2) kujitoa mwenyewe kwa ajili ya kuwakomboa na kuwatakasa watu (Tito 2:14)
      - 3) Kuwa wasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
    - c. *Lutrōsis*, "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
      - 1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68
      - 2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
      - 3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
  4. *Apolytrōsis*
    - a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Matendo 3:19-21)
      - 1) Luka 21:28
      - 2) Warumi 8:23
      - 3) Waefeso 1:14; 4:30
      - 4) Waembrania 9:15
    - b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
      - 1) Warumi 3:24
      - 2) 1 Wakorintho 1:30
      - 3) Waefeso 1:7
      - 4) Wakolosai 1:14
  5. *Antilytron* (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhabihu pekee iliyokubaliwa, yeye aliywafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).
- B. Dhana ya kitheolojia katika Agano Jipya.
1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18,23; 6:23).
  2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambia kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
  3. Yesu, Mwana-Kondoo asie na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenunuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
  4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).
  5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, theolojia ya Enzi za Kati), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoa kwa ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!

6. Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa ufanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbingu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

◻ "halikuanzwa" Tazama dokezo katikaEbr. 10:20.

**9:19 "mbuzi, pamoja na maji na sufu nyekundu na hisopo"** Mwandishi anaonekana kuunganisha kusafisha kwa kumnyunyizia damu mwenye ukoma katikaLaw. 14:6-7 kwa utakaso wa wa Amri Kumi katika Sinai katika Kut. 24:1-9. Hekalu halikuwepo katika sura ya 24 (kama vile Kutoka 40). Josephus anatwambia kwamba kunyunyizia damu ilikuwa sehemu ya taratibu za Kutoka 40.

Neno "mbuzi" halipo katika machapisho mengi ya kale ya Kiyunani (P<sup>46</sup>, N<sup>c</sup>, K, L) pamoja na tafsiri za Kishamu na andiko la Kiyunani linalotumiwa na Origen. Mara nyingi Mbuzi walitumika kwa ajili ya sadaka za dhambi, uthibitisho wa agano (ijapokuwa hatengwi, kama vile Mwa. 15:9). Mbuzi wanaondolewa katika uthibitisho wa "maneno kumi" (Torati) katika Kut.24:1-8. Huenda neno "mbuzi" ni dokezo lingine la Siku ya Upatanisho, Mambo ya Walawi 16, ambapo mbuzi ni sehemu muhimu ya taratibu.

Kutokana na mtazamo wetu wa sasa ni vigumu kudai kwamba 7 (hotuba ya Stefano) na mwandishi wa Kitabu cha Waerbrania (maelezo ya sura ya 9 ya hema ya kale) si sahihi. Kuna vitu vingi ambavyo havijulikani kuhusu taratibu za kale na mila za walimu wa sheria zisizobadilika zenyen kuhusiana nao.

**9:20** Hii ni nukuu toka Kutoka 24:8.

**9:22 "karibu vitu vyote"** Katika mfumo wa Agano la Kale mambo mengine yalisafishwa pasipo damu (1) Law. 5:11; (2) Hes. 16:46; (3) Hes. 31:22-23; (4) Kut. 19:10; 32:30-32; Law. 15:5; 16:26, 28; 22:6; (5) Zaburi 51. Tazama maelezo hapa chini.

◻ "pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo" Katika Agano la Kale tendo la kusafisha lilihitaji (1) moto, (2) maji, au (3) damu. Mwandishi huyu anaichukulia dhambi kwa umakini sana. Msamaha uhusisha maisha ya kujitoa (kama vile Law. 17:11,14).Mfumo wa Agano la Kale (kama vile Mambo ya Walawi 1-7) unaweka hatua nne za uelewa wetu wa ubadala wa kifo cha Kristo (kama vile. Mt. 26:28; Marko 10:45; 1 Kor. 11:25; 2 Kor. 5:21).

Katika Agano la Kale kulikuwa na njia za mambo kadhaa/watu walisafishwa pasipo damu.

1. kwa moto (kama vile Law. 13:52,55; 16:27; Hes. 31:23)
2. maji (kama vile Kut. 19:30; Law. 15:5; 16:26,28; 22:6; Hes. 31:24)
3. dhabihu ya unga (kama vile Law. 5:11-13)
4. uvumba (kama vile Hes. 16:46-48)
5. maombi ya kusihi (kama vile Kut. 32:30-32)
6. Maombi ya kukiri na kuungama (kama vile Zab. 32 na 51)

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 9:23-28

<sup>23</sup> Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo, lakini mambo ya mbinguni yenye kwa yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo. <sup>24</sup> Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu; <sup>25</sup>wala si kwamba ajitoe mara nyingi, kama vile kuhani mkuu aingiavyo katika patakatifu kila mwaka kwa damu isiyo yake; <sup>26</sup> kama ni hivyo, ingalimpasa kuteswa mara nyingi tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu; lakini sasa, mara moja tu, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake. <sup>27</sup> Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu; <sup>28</sup>kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za

watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.

**9:23 "nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe"** Hii dhana ya mambo yaliyo mbinguni kuchafuliwa kwa dhambi ya mwanadamu katika nchi si ya kawaida, lakini si ya kipekee kwa mwandishi huyu (kama vile Rum. 8:18-22).

Siku ya Upatanisho, inayodekezwa mara kwa mara katika sura hii, inahisisha kulisafisha hema kkwa mwaka kutokanana unajisi wa miviga (kamavile Kut. 30:10; Law. 16:11-20). Mbingu inaweza kuchafuliwa kwa

1. anguko la mwanadamu (kama vile Rum. 8:18-22; Kol. 1:20)
2. uwepo wa Shetani (kama vile Ayubu 1-2; Zek. 3)
3. dhana pekee iliyo katika desturi za walimu wa sheria za Kiyahudi

**9:24 "aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu"** Kazi ya ukuhani wa Yesu ilifanyika katika viwango viwili: (1) kama dhabihu juu ya nchi na (2) kama kuhani mbinguni. Kifungu hiki kinaweza kueleweka katika namna mbili: kinuktadha kinairejelea dhabihu yake ya kifo badala ya nwanadamu aliyeanguka, lakini inaweza kueleweka kama rejea kwa huduma yake ya maombi ya kusih (kama vile Ebr. 7:25; Rum. 8:34; 1 Yohana 2:1).

Hili neno "aonekane" ni *emphanizō*, ambapo inamaanisha "kujidhihirisha" (kama vile Mt. 27:53). Katika Ebr. 9:26 hili neno "kudhihirisha," *phaneroō*, (kama vile 2 Kor. 5:10; Kol. 3:4; 1 Pet. 5:4; 1 Yohana 2:28; 3:2) linatumika katika Ebr. 9:28 hili neno "aonekane," *optomai* (kama vile Mt. 17:3; Luka 1:11; 9:31; 22:43; 24:34; Matendo ya Mitume 2:3; 7:2,30,35; 9:17; 16:9; 26:16).

Inashangaza kuona mwandishi anayatumia maneno matatu ya visawe.

**9:25** Hili linauendeleza msisitizo wa kithiolojia wa kitabu cha Waebrania kwamba Yesu alijitoa "mara moja" (kama vile Ebr. 7:27; 9:11,25-28; 10:10) ambapo, ukuhani wake mkuu, dhabihu, na utakaso ni ukuu kwa dhana za Agano la Kale.

**9:26**

- NASB "kama ni hivyo, ingalimpasa kuteswa mara nyingi"  
NKJV "hivyo ingalimpasa kuteseka maa kwa mara"  
NRSV "hivyo ingempasa kuteseka tena"  
TEV "hivyo ingalimpasa kuteseka mara kwa mara"  
NJB "au ingelimpasa kuteseka tena na tena"

Katika *Word Pictures in the New Testament*, A. T. Robertson anadai kwamba hii ni amrishi sentensi daraja la pili yenye kudhaniwa (Juzu. V, uk. 404), ambayo ingedokeza sentensi isio sahihi yenye matokeo ya hitimisho lisilo la kweli. Yesu aliteseka mara moja, si dhabihu za mara kwa mara.

- NASB "tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu"  
NKJV "katika miisho ya ulimwengu"  
NRSV "katika miisho ya ulimwengu"  
TEV "na sasa miisho yote ya nyakati inakaribia mwisho"  
NJB "katika miisho ya zama zilizopita"

Kuna maneno kadhaa ya Kiyunani yenye kuhusiana na neno "wakati," "umilele," na "ulimwengu." Katika sura ya 9 kuna mtiririko rejea zilizotumika:

1. Ebr. 9:9, "wakati huu uliopo sasa," yaani., Agano la Kale
2. Ebr. 9:10, "wakati wa matengenezo mapya," yaani., Agano Jipy (kuanza kwa ulimwengu mpya,)
3. Ebr. 9:26, "miisho ya ulimwengu," yaani., ulimwengi mpya wa haki (uthibitisho wa ulimwengu mpya, kama vile Mt. 13:39,40,49; 24:3; 28:20)

Walimu wa sheria za Kiyahudi na waandishi wa Agano Jipy walipendekeza zama mbili (a uwili wa wima): (1) zama za uovu zinazobainishwa na uasi wa mwanadamu na laana ya Mungu na (2) zama zijazo zenyekubainishwa na Masihi, siku ya haki.

Agano la Kale linatazamia ufalme, ujio wa Masihi wenye nguvu kama Mwamuzi na Mtawala, lakini kama mafunuo ya Agano Jipy, Yeye atajkuja mara mbili, moja kama mtumishi atesekaye, Mwana-kondoo wa Mungu; na baadaye, kama njia ya Agano la Kale iliyoتابiriwa. Hii tofauti ya ujaji mara mbili ulio tofauti imesababishwa na kupishana kwa hizi zama mbili za Kiyahudi. Ufalme wa Mungu umekuja na kuzaliwa kwa Yesu lakini hautatimia hadi kurudi kwake kwa utukufu. Waamini ni raia wa falme mbili: Ufalme wa milele na ufalme wa muda.

**9:27** Mistari hii hakika inalikataa wazo lo lote lihusulo kuhama kwa nafsi, mchanganyiko wa *kharma*, au maisha yaliyopita, ambayo ni mafundisho yenyenye kuogofya kwa yule aliyeanguka, mwanadamu mwenye dhambi! Huu ni mtazamo wa Kikiristo kwa ulimwengu mzima wa "maisha ya aina moja, kisha hukumu" wenye kuusukuma unuhimu wa injili; wenye kuiharibu dhana ya kithiolojia kuhusu ulimwengu (wanadamu wote wataokolewa wakati wa miisho ya dunia); wenye kudai amri kuu (kama vile Mt. 28:19-20) isiyorudishwa katika mapendekezo mazuri au uchaguzi mkuu!

**9:28 "azichukue dhambi za watu wengi"** Hili linaweza kuwa dokezo la Isa. 53:12 (kama vile 1 Pet. 2:24). Hili neno "wengi" haliwekwi pembedi (baadhi), bali lina ufanano na "wote" la 53:6 (kama vile Rum. 5:18, "wote"; 5:19, "wengi"). Hili neno "azichukue" pia linaweza kuwa dokezo la Isa. 53:4,11,12. Kitendi cha Kiebrania kinamaanisha "kuchukua" au "kuondoa" (kama vile 1 Pet. 2:24). "Yesu alilipa madeni ambayo hakustahili; tulikabiliwa na madeni ambayo tusingekuwa na uwezo wa kuyalipa."

▣ **"atatokea mara ya pili"** Kifungu hiki huenda kinarejelea Kuja kwa kwa KristoMara ya Pili. Dhima ya sasa ya Agano Jipy (kama vile Mt. 24:3,27,30,37,39,42,44; 26:64; Marko 13:20; 14:62; Luka 21:27; Yohana 14:3; Matendo ya Mitume 1:11; 1 Kor. 1:7; 15:23; Flp. 3:20-21; 1 The. 2:19; 3:13; 4:15-16; 5:23; 2 The. 1:7,10; 2:1,8; 1 Tim. 6:14; 2 Tim. 4:1,8; Tito 2:13; Ebr. 9:28; Yakobo 5:7-8; 1 Pet. 1:7,13; 2 Pet. 1:16; 3:4,12; 1 Yohana 2:28). Tazama Mada Maalum: Vitenzi vya Nyakati za Kiyunani Viliviyotumika kwa neno Wokovu katika Ebr. 1:14.

Hata hivyo, inawezekana, kimuktadha, ambayo inamrejela Kristo kuiacha hema ya mbinguni baada ya fanikio lake kuu la dhabihu (kama vile *New Testament Transline* na Michael Magill, uk. 846, #32 na 35). Kitu chenye kufanana na Kuhani Mkuu wa Agano Jipy mwenye kuondoka Patakatifu pa Patakatifu katika Siku ya Upatanisho.

**NASB        "pasipo dhambi"**

**NKJV        "mbali na dhambi, kwa ajili ya wokovu"**

**NRSV, TEV    "asioshughulika na dhambi, bali kuokoa"**

**NJB        "shambi haipo... kuleta wokovu"**

Kifungu hiki kinaonekana kudokeza kwamba Kristo alikuja kwa wakati wa kwanza kushughulika na matatizo ya dhambi za mwanadamu, lakini atarudi tena kujikusanya (kama vile 1 The. 4:13-18) wale waliomwamini na kukusubibiri kurudi kwake (kama vile Rum. 8:19,23; 1 Kor. 1:7; Flp. 3:20; Tito 2:13).

▣ **"kwa hao wamtazamiao kwa wokovu"** Hili linaweza kuwa dokezo lingine la taratibu za Siku ya Upatanisho, ambapo Waisraeli walimgoja Kuhani Mkuu kwa shauku wakati wa kutoka Patakatifu pa Patakatifu alipokuwa, ambapo iliashiria ukubalifu wa YHWH huduma ya maombi ya kusihi.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini mwandishi wa kitabu cha Waebrania anaijadili hema ya kale ya jangwani?
2. Kwa nini 9:9 kithiolojia ni ya muhinu?
3. Je! mbinguni kuna hema yenye kuonekana kwa macho ambayo kiukweli Kristo aliingia na kutoa dhabihu?

4. Nini maana nyingine mbili za neno "agano" ambazo zinatumwiwa na mwandishi katika nistarai ya 15-18?

## WAEBRANIA 10

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>                    |   |  |   |                                   |
|---|---|--|---|-----------------------------------|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>  | <b>NKJV</b>                                       | <b>NRSV</b>                                  | <b>TEV</b>  | <b>NJB</b>                        |
| Dhambi<br>Zinaondolewa kwa<br>Dhabihu ya Kristo<br>(9:23-10:18) | Dhabihu ya mnyama<br>isiyotosha                   | Sifa za dhabihu ya<br>Kristo<br>(9:11-10:18) | Dhabihu ya Kristo<br>inaonda dhambi<br>(9:23-10:18) | Dhabihu ya kale<br>iliyo dhaifu   |
| 10:1-4  | 10:1-4  | 10:1-10                                      | 10:1-4  | 10:1-10                           |
|   | Kifo cha Kristo<br>Kilitimiza mapenzi<br>Ya Mungu |  |   |                                   |
| 10:5-10   | 10:5-10   |  | 10:5-10   |                                   |
|   | Kifo cha Kristo ni<br>Utakaso kamili              |  |   | Dhabihu ya Kristo<br>inayofaa     |
| 10:11-14  | 10:11-18  | 10:11-18                                     | 10:11-14  | 10:11-18                          |
| 10:15-18  |   |  | 10:15-18  |                                   |
| Ushawishi na Onyo<br>10:19-25                                   | Shika ungamo lako<br>10:19-25                     | Ushawishi na maonyo<br>10:19-25              | Na tumkaribie<br>Mungu<br>10:19-25                  | Nafasi ya Mkristo<br>10:19-25     |
|   | Ishi kwa imani                                    |  |   | Hatari ya ukaraji<br>imanu        |
| 10:26-31  | 10:26-39  | 10:26-31                                     | 10:26-31  | 10:26-31                          |
| 10:32-39  |   | 10:32-39                                     | 10:32-39  | Kusudi la kustahimili<br>10:32-39 |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. Nk.

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Kipengele cha fasihi kinaanza kwenye Ebr. 8:1 na kuendelea kupitia Ebr. 10:18.

- B. Hii inadokeza njia kuu tatu za huduma ya Yesu kwenye huduma ya makuhanani wa Kilawi.
1. Yesu ni sadaka kuu (kwa damu yake, kama vile. Ebr. 9:12-14)
  2. Sadaka ya Yesu mara moja kwa ajili ya wote (tazama muhtasari kamili katika Ebr. 7:27)
  3. Yesu wa mbinguni, sio duniani, utakatifu (kama vile. Ebr. 9:11)

- C. Kitenzi *teleioō* kimetumika kwa kurudiwa kwenye Waebrania.

1. Ebr. 2:10, Yesu alifanywa mkamilifu kwa kupitia katika mateso
2. Ebr. 5:9, Yesu alifanywa mkamilifu na hatimae kuwa chanzo cha wokovu wa milele
3. Ebr. 7:19, sheria ya Musa haikufanya chochote kiwe kimekamilika
4. Ebr. 7:28, Yesu alifanywa mkamilifu
5. Ebr. 9:9, sheria za Musa haziwafanyi waabudio kuwa wakamilifu
6. Ebr. 10:1, sheria za Musa haziwezi kuwafanya waabudio kuwa wakamilifu
7. Ebr. 10:1, sadaka ya Yesu huwafanya waaminio kuwa wakamilifu daima
8. Ebr. 11:40, watakatifu wa Agano la kale na Agano jipya wote ni wakamilifu pamoja
9. Ebr. 12:23, roho za watu wenye haki huwafanya kuwa wakamilifu

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 10:1-10

<sup>1</sup> Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao.

<sup>2</sup>Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi? <sup>3</sup>Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka. <sup>4</sup> Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi. <sup>5</sup>Kwa hiyo ajapo ulimwenguni, asema,

"Dhabihu na toleo hukutaka,

Lakini mwili uliniwekea tayari;

<sup>6</sup>Sadaka za kuteketezwa na sadaka za dhambi hukupendezwa nazo;

<sup>7</sup>Ndipo niliposema, Tazama, nimekuja

(katika gombo la chuo nimeandikiwa)

Niyafanye mapenzi yako, Mungu"

<sup>8</sup>Hapo juu asemapo, Dhabihu na matoleo na sadaka za kuteketezwa na hizo za dhambi hukuzitaka, wala hukupendezwa nazo (zitolewazo kama ilivyoamuru torati), <sup>9</sup>ndipo aliposema, Tazama, nimekuja niyafanye mapenzi yako. Aondoa la kwanza, ili kusudi alisimamishe la pili. <sup>10</sup>Katika mapenzi hayo mmeepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.

**10:1 "kivuli"** Utungaji wa sheria ya Musa ("torati") na taratibu za ibada ilikuwa ni aina na kivuli cha Yesu kijacho cha huduma ya ukuhani kwenye Hema takatifu la mbinguni, lisilofanywa kwa mikono ya wanadamu (kama vile. Ebr. 8:5; 9:23-28). *The Jerome Biblical Commentary* lina wazo lenye shauku:

"hapa mwandishi hakutumia 'kivuli' kama alivyotumia kwenye Ebr. 8:5, ambapo mafundisho ya mbinguni-duniani ya Pilato kwa kinyume ni mapana, lakini katika maana ya Pauline ya kivuli kijacho ambacho kwamba kinakuja kupitia kwa Kristo (kama vile Kol. 2:17). . .kila mwaka ilirudiwa sadaka za siku ya upatanisho ambayo hakuweza kuondoa dhambi; walidokeza kivuli kijacho cha sadaka ya Yesu" (uk. 399).

▣"cha mema yatakayokuwa" kwenye Ebr. 9:11 hii inarejelea kwa huduma ya ukuhani mkuu wa Kristo.

**NASB** "wala si sura yenewe ya mambo hayo"

**NKJV** "wala si picha yenewe ya mambo hayo"

**NRSV** "wala si muundo wa kweli wa kweli hizi"

**TEV** "wala si kamili na aina ya uaminifu wa vitu halisi"

**NJB "wala si picha halisi kwao"**

Hili ni neno la Kiyunani *icon*, ambalo humaanisha mfano kamili kwamba unafanana na uhalisia (kama vile 2 Kor. 4:4; Kol. 1:15). Hapa linakanusha na muunganiko wa kisarufi wa "kivuli."

▣**"kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima"** Yesu alitoa dhabihu moja ya thamani. Makuhani walitoa dhabihu tena na tena.

▣**"kuwakamilisha"** Neno hili linamaanisha "kuleta ukamilishaji," "ukamilifu kamili." Neno hili (*teleioō* na Miundo yake mingine) lina dhana imara juu ya kitabu. Tazama Mada Maalum katika Ebr. 7:11.

Neno *telos*

1. linamaanisha "ukamilisho," "kufikia lengo," au "mwisho" (kama vile. Ebr. 3:6,14; 6:11)
2. kwenye Ebr. 5:14 *teleios* limetumiwa kwa mtu mkomavu
3. kwenye Ebr. 6:1 *teleiotes* ni wito wa ukomavu
4. maneno yametumika kwenye muunganiko na huduma ya Melkizedeki na Hema takatifu la mbinguni kwenye Ebr. 7:11 na 9:11

▣**"wakaribiao"** katika Agano la kale hii inarejelea kwa makuhani waliomkaribia YHWH kwa ajili ya kuabudu au huduma. Lakini hapa, chini ya maagano mapya (kama vile Yer. 31:31-34), inarejelea kwa waaminio wote (kama vile. Yakobo 4:8) ambao sasa wana haki ya kumsogelea Mungu kwa ukaribu kupitia kwa Kristo (kama vile. Ebr.4:16; 7:19,25; 10:1,22)

**10:2**

**NASB, NRSV,**

**NJB "kama ndivyo"**

**NKJV "hivyo basi"**

**TEV "ikiwa"**

Hii ni sentensi hali daraja la pili, mara nyingi huitwa "ukweli wa tofauti." Madai ya mwongo ni kufanya msukumo wa lengo la kithiolojia (kama vile Ebr. 4:8; 7:11; 8:4,7; 10:2; 11:15).

Mstari wa 2 unaweza kutafsiriwa kama

1. swalilinalotarajiw "ndiyo" jibu, kama kwenye toleo la NASB, NRSV, NAB
2. sehemu ya swalil, kama kwenye toleo la NKJV, NIV
3. maelezo, kama kwenye toleo la TEV, NJB, REB

▣**"Dhabihu hazingekoma kutolewa"** hii yumkini ikadokeza (kama vile Ebr. 10:11; 7:28) kwamba Hekalu liliendelea kufanya kazi; hata hivyo, Waebrania labda kiliandikwa kabla ya mwaka 70 B.K, wakati hekalu (na Yerusalem) vyote viliangamizwa na jemadari wa Rumi (baadae mfalme) Tito.

▣**"maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi"** hili lilikuwa ni tatizo na sheria za Musa: haikuweza kusafisha moyo na dhamira yenye hatia (kama vile Ebr. 9:9,14). Maagano mapya katika Kristo yanatoa haki kwa Mungu na ujasiri (dhamira njema)!

**10:3 "kumbukumbu la dhambi kila mwaka"** Hii inaonekana inarejelea siku ya upatanisho (kama vile Law. 16), tangu hili lisitisizwe sura 9, lakini inaweza kurejelea utaratibu mzima wa sadaka. Ukweli ni kwamba dhabihu za kila mwaka zilihitajika kusafisha Hema takatifu na taifa, iliendelea kuwakumbusha wana wa Israeli umakini na kurudirudia hatia na dhambi ya mwanadamu (kama vile Galatia 3).

**10:4 "Maana haiwezekani"** neno haiwezekani limetumika mara kadhaa katika Waebrania (tazama muhtsari kamili katika Ebr.6:6).

1. Ebr. 6:4 (katika Kiyunani, lakini 6:6 katika rejeo la NASB).haiwezekani kuwafanya wao upya kwa toba
2. Ebr. 6:18, haiwezekani kwa Mungu kusema uongo
3. Ebr. 10:4, haiwezekani kwa damu za wanyama kusafisha dhambi
4. Ebr. 11:6, pasipo imani haiwezekani kumpendezza Mungu

Kwa mwandishi wa Waebrania neno la Kiyunani "haiwezekani" halimaanishi "vigumu"!

## **10:5**

|             |   |
|-------------|---|
| <b>NASB</b> | <b>"Kwa hiyo ajapo ulimwenguni, asema"</b>                    |
| <b>NKJV</b> | <b>"Kwa hiyo ajapo ulimwenguni, alisema"</b>                  |
| <b>NRSV</b> | <b>"ajapo Kristo ulimwenguni, alisema"</b>                    |
| <b>TEV</b>  | <b>"alipotaka kuja Kristo ulimwenguni, alisema kwa Mungu"</b> |
| <b>NJB</b>  | <b>"na hii ndio maana alisema, ajapo ulimwenguni"</b>         |

Hii inatambulisha dondoo (kama vile Ebr. 10:5-7) kutoka Zab. 40:6-8, ambayo inamwonyesha kutofurahishwa YHWH na Dhabihu za Agano la kale kwa sababu hazikuambatana na maisha ya imani. Mwandishi wetu ametumia Zab. 40:7 kama taswira ya ujio wa Masihi ambaye atampendezesa kikamilifu Mungu.

Dondoo hii pia inadokeza maisha ya Kristo kabla ya kuzaliwa (kama vile Yn. 1:1-2; 8:57-58; 2 Kor. 8:9; Fil. 2:6-7; 1 Yn 1:1). Hakuna wakati ambao Kristo hakuwepo kamwe! Umoja wake wa roho na Baba unawezwa kuthibitishwa kutoka katika Yn 5:18; 10:30; 14:9; 10:28.

▣"**mwili uliniwekea tayari**"dondoo hii inafuata tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania ya Zab. 40:6. Andiko la kimasoreti lina "sikio ulilonichimbia." Maana pekee ya kutajwa mwili ulioandaliwa kwa ajili ya Masihi unaweza pia kuwa na kazi mwishoni mwa karne ya kwanza kupambana na mwanzo wa mafunuo. Yesu alikuwa mwanadamu kamili.

**10:6** Kuna vifungu kadhaa kama hivi kwenye Agano la kale (kama vile 1 Sam. 15:22; Isa. 1:11-17; Hosea 6:6; Amosi 5:21-27; Mika 6:6-8). Sio lazima itafsiriwe kama Mungu aliukataa utaratibu wa dhabihu, ambao ulikuwa ni tendo la neema yake ili kuhusika na dhambi za mwanadamu na tatizo la ushirika kwa muda uliopangwa. Lakini anguko la mwanadamu lilichukua nafasi ya utaratibu na kuwageuza wao kuwa watendaji wa desturi za kiibada bila kufikiria na kawaida ya ibada badala ya moyo mkunjufu wenye toba na imani. Mungu alikataa uzembe wa taratibu za kidini wa kujionyesha na kawaida ya ibada kwamba haiaksi moyo na maisha ya imani (kama vile Isa. 1).

**10:7 "katika gombo la chuo nimeandikiwa"**Hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea, ambayo inarejelea Agano la kale. Kwa asili Agano la kale lilikuwa limeandikwa katika sehemu za magombo ya bahari ya chumvi. Magombo ya bahari ya chumvi yalipatikana mwaka 1947 yakiwa na kopi za Isaya zilizoandikwa kwa urefu wa mita ishirini na tisa kwenye magombo ya bahari ya chumvi.

▣"**Niyafanye mapenzi yako, Mungu**"Mapenzi ya Mungu ni maagano mapya na wanadamu wote yaliyoimarishwa kwa kifo cha Yesu na ufufuo (kama vile. Marko 10:45; 2 Kor. 5:21; Ebr. 10:9). Wanyama wapokufa wakati wa dhabihu ya kuteketezwa hawana chaguo. Yesu kwa hiari aliutwaa uhai wake (kama vile Yn. 10:17-18).

**10:8 "dhabihu"** hii ni orodha ya maneno manne kwenye mstari wa 8 unaonekana kufunuka aina zote za sadaka za kuteketezwa (Walawi. 1-7). Neno "dhabihu" kwa dhahili linamaanisha sadaka ya hiari.

▣"**matoleo**" Hii inarejelea hiari" matoleo ya chakula."

▣"**sadaka za kuteketezwa**" Hizi ni hiari kamilifu, dhabihu ziliteketezwa kabisa.

▣"**sadaka kwa ajili ya dhambi**" Hili ni daraja lingine la sadaka za lazima zilizotajwa kwenye Walawi sura 4-5.

▣ "(**zitolewazo kama ilivyoamuru torati**)" kusudi la mwandishi ni kuonyesha ukuu wa dhabihu ya Yesu juu ya dhabihu za Walawi. Hata pale dhabihu za Agano la kale zilipoonyesha na dhamira ifaayona taratibu, zilikua ni kivuli kijacho cha cha kazi ya Kristo pekee.

**10:9 "alipo"**KIWAKILISHI NOMINO hiki kilichotangulia kina utata. Kinaweza kumrejelea Baba kama mmoja anaeanzisha maagano. Pia tungo "mwili wa Yesu Kristo" katika Ebr. 10:10 inadokeza sio yeze anaepaswa. Hata hivyo, VITENZI vyote vya dondo vinavyotoka katika Zab. 40:6-8 (Ebr. 10:5-7) vinamchukulia Kristo kama lengo lao.

▣ "**la kwanza**"Hii inarejelea maagano ya Musa (kama vile Kol. 2:14).

|                   |                           |
|-------------------|---------------------------|
| <b>NASB, NKJV</b> | <b>"Aondoa"</b>           |
| <b>NRSV</b>       | <b>"aharibu"</b>          |
| <b>TEV</b>        | <b>"alitupilia mbali"</b> |
| <b>NJB</b>        | <b>"aliharibu"</b>        |

Hili ni neno imara la Kiyunani kwa ajili ya "kuharibu" (*anaireō*). Swalni kwa namna gani utaelewa hili neno katika uhusiano wa Agano la kale? Kama ufunuo kutoka kwa Mungu ni wa milele (kama vile. Mt. 5:17-19). Paulo mara nyingi ametumia dondo za Agano la kale kama ushawishi kwa waaminio. Hata hivyo, kama maana ya wokovu au msamaha wa dhambi ulikuwa ni mwanzo pekee wa hatua (kama vile Gal. 3). Umetimizwa na zaidi kwenye Agano jipya katika Kristo. Muktadha ni lazima uamue kama neno hili litafsiriwe "ondoa" (limetimizwa) au "kuharibu" (kuangamizwa).

▣ "**la pili**" hii inarejelea maagano mapya (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-36) katika Yesu.

**10:10**

|                   |   |
|-------------------|---|
| <b>NASB, NKJV</b> | <b>" Katika mapenzi hayo mmepeata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu"</b>  |
| <b>NRSV</b>       | <b>"na kwa mapenzi ya Mungu tumepeata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu kwa wote"</b>                                       |
| <b>TEV</b>        | <b>"kwa sababu Yesu Kristo alitenda alichotaka Mungu, wote tumetakaswa kutoka katika dhambi kwa kutolewa mwili wake mara moja tu na kwa wote"</b> |
| <b>NJB</b>        | <b>"na kwa mapenzi yake kwetu tulifanywa watakatifu kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja kwa wote"</b>                                     |

Je! "mapenzi" inarejelea mapenzi ya Kristo (kama vile. Ebr. 10:7,9 na NASB, NJB) au kwa mapenzi ya Baba (NRSV,TEV)? Tangu Yesu alioongee mwenyewe katika Ebr. 10:5 (kama vile Ebr. 10:9), ndivyo muktadha unavyopendekeza mapenzi yake.

▣ "**mmepeata utakaso**" Hili ni fumbo la kauli timilifu tendwa endelevu la hali ya kuendelea. Malengo ya Ukristo ni watu wenye haki. Na hili pia ni lengo la Agano la kale. Utakatifu au utakaso kimsingi ni kuondolewa laana na hatia za anguko (kama vile Mwa. 3), uhariifu wa sura ya Mungu kwa mwanadamu. Maagano mapya yanalezea hitaji hili katika njia mbili: (1) kwa tangazo halali, eneo maalumu (elekezi) na (2) kwa wito wa utakatifu (shurutishi). Waaminio wana haki na kutakaswa kwa imani inayotubu ili kuupokea ukombozi wa Mungu kwa kuitia dhabihu ya Yesu. Tunapookolewa, Roho mtakatifu anakaa ndani yetu, tunatiwa hamasa na sheria ya uzima wa milele, tamanio la milele (moyo mpya na roho mpya) ili tumfanane Kristo (kama vile Rum. 8:29; Gal. 4:19; Efe. 1:4). Utakaso unagusa wote tusimamao mbele za Mungu na sifa ya familia yetu mpya inaonekana kwenye maisha kila siku. Tazama Mada Maalum katika Ebr. 2:11.

▣ "**kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo**"Anguko la mwanadamu halikumshikilia Mungu (kama vile. Isa. 53:6; Rum. 3:10-18); Mungu aliwashikilia wao! Aliandaa njia kwa ajili ya wanadamu wote kurudi katika ushirika nae (kama vile. Marko 10:45; 2 Kor. 5:21; Isa. 53).

▣ "mara moja tu" Hii ni dhana inayojirudia rudia (kama vile Ebr. 7:27; 9:12,28; 10:10, tazama muhtasari kamili katika Ebr. 7:27). Inaonyesha ukuu wa dhabihu ya Yesu juu ya dhabihu zilizotelewa mara kwa mara kwenye maagano ya Musa (kama vile Ebr. 10:11-12). Kila jambo lililohitajika kufanyika kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu tayali lilikwisha andaliwa. Wote ni lazima tuipokee ahadi ya Mungu kwa njia ya imani kupitia kazi aliyokamilisha Kristo. . "Yeyote atakaye na aje" (kama vile Rum.10).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 10:11-18**

<sup>11</sup> Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi; ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi. <sup>12</sup> Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu; <sup>13</sup>tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake. <sup>14</sup> Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa. <sup>15</sup>Na Roho Mtakatifu naye amshuhudia; kwa maana, baada ya kusema,

<sup>16</sup> "Hili ni agano nitakaloagana nao  
baada ya siku zile, anena Bwana,  
Nitatia sheria zangu moyoni mwao,  
Na katika nia zao nitaziandika;

ndipo anenapo,

<sup>17</sup>Dhambi zao na uasi wao  
sitaukumbuka tena kabisa."

<sup>18</sup> Basi, ondoleo la hayo likiwapo, hapana toleo tena kwa ajili ya dhambi.

**10:11 "kila kuhani"** Chapisho A la kale la Kiyunani lina "kuhani mkuu." Mwandishi mara nyingi ametumia maneno yote kwa ajili ya Yesu.

▣ "husimama" Makuhani husimama kila mwaka kutoa dhabihu, lakini Yesu "aliketi" (Ebr. 10:12), kazi yake imekamilika!

**10:12 " alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele "** Yesu alihusika na tatizo la dhambi ya mwanadamu. Hakuna aliye potea kwa sababu ya "dhambi." Kizuizi pekee kwa ulimwengu wote ili uokolewe ni kutokuamini. Mungu aliandaa njia kwa ajili ya wote, kwa wakati wote.

Neno la Kiyunani *diēnekēs*, linatafsiriwa "milele," au "daima," limejitokeza mara tatu katika Waebrania (kama vile Ebr. 7:3; 10:12,14). Kwa kawaida linahusiana na neno au tungo kwamba iliyotangulia, ambayo inaweza kusimulia "dhabihu moja kwa ajili ya dhambi." sio sehemu ya Zab. 110:1 dondo inayofuata.

▣ "aliketi mkono wa kuume wa Mungu" hii ni taswira inayojirudia katika Zab. 110:1a (kama vile Ebr. 1:3; 8:1; 12:2). "mkono wa kuume" ni sitiari ya sehemu ya nguvu za kifalme, mamlaka, na Enzi kuu. Pia ni sehemu ya upatanisho (kama vile Rum. 8:34; Ebr. 7:25; 1 Yn 2:1). Yesu ni kuhani (kama vile Zab. 110:4) na Mfalme (kama vile Zab. 110:1-3), kama Melkizedeki (sura ya 7) ambae huenda mbele zetu na kuandaa kila mahitaji tunayoyataka.

**10:13 "tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake "** hii ni dondo nyiningine kutoka Zab. 110:1b. Vita vya kiroho vilikuwa vimeshinda (kama vile Kol. 2:15), lakini bado kutimiliza.

**10:14** Mstari huu unaonyesha umakini wa kitabu kizima kwa upande wa usalama. Yesu dhabihu moja idumuyo hata milele ilikuwa kamilifu daima (kauli timilifu tendaji elekezi ya hali ya kuendelea) kwa waaminio (tazama Mada Maalum katika Ebr. 7:11). Dhabihu ilitosha na kamilifu ya kutimiza kazi ya ukombozi wake (sio kama maagano ya Musa, kama vile Ebr. 7:11,19; 9:9).

Waaminio ni lazima waendelee kuipokea imani yao, ambayo huwatakasa wao (kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo). Imani inayoendelea ni ufunguo wa kila mmoja mmoja kuuthibitisha wokovu. Moyo mpya na dhamira mpya (kama vile Eze. 36:22-38) hutia hamasa ya waamnino kuishi maisha ya ucha- Mungu kwa kushukuru kwa ajili

ya uhuru, ukamilifu, na wokovu mpana zaidi. Kwenye kitabu hiki hakuna swali juu ya utoshelevu wa dhabihu ya Yesu, lakini kuna swali juu ya mwitikio wa kila mmoja mmoja- kazi moja ya kundi la kwanza na kazi inayoendelea ya kundi la pili.

**10:15 "Roho mtakatifu"** Hii inaonyesha mtazamo wa mwandishi katika msukumo wa Agano la kale (kama vile Mt. 5:17-19; 2 Tim.3:16).

**10:16-17** Hii ni dondo kutoka Yer. 31:33-34, lakini mpango wa tungo umerudishwa nyuma. Mwandishi anaonekana ana dondo kutoka katika kumbukumbu kwa sababu dondo hii ni tofauti kutoka andiko la kimasoreti na tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania, kama alivyofanya vile vile dondo katika Ebr. 8:10-12 (isipokuwa yalikuwa ni makusudi ya nyuma).

**10:18** huu ni upeo wa mwisho wa hoja za waaminio na tumaini letu kuu (njia ya kwanza imekwisha kupita, kama vile Ebr. 8:13).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 10:19-25**

<sup>19</sup>Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, <sup>20</sup>njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake; <sup>21</sup>na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu; <sup>22</sup>na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi. <sup>23</sup>Na mlisike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yeze aliyeahidi ni mwaminifu; <sup>24</sup>tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; <sup>25</sup>wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia.

**10:19**

NASB, NRSV      "kwa kuwa tuna ujasiri"

NKJV                "tuna ujasiri"

NJB                 "tuna . . . ujasiri kamili"

Neno *parrhēsia* linamaanisha "ujasiri" au "uhuru wa kuongea" kama vile Ebr. 3:6; 4:16; 10:19,35). Neno hili linaelezea maana mpya ya waaminio ya kukubali ushirika wa karibu na Mungu. Hiki ndicho torati ya Musa ilishindwa kuandaa (kama vile Ebr. 9:9)! Ujasiri huu ni lazima ushikiliwe kwa haraka kwa imani (kama vile Ebr. 3:6,14; 4:14). Ujasiri unasisitizwa katika utimilifu wa kazi ya Kristo (kama vile Efe. 2:8-9), sio matendo ya mwanadamu! Ujasiri unadumishwa kwa kuishi maisha ya ucha- Mungu (kama vile Efe. 2:10).

#### **MADA MAALUMU: UJASIRI (*parrhēsia*)**

Neno hili la Kiyunani ni muungno wa maneno "yote" (*pan*) na "" (*rhēsis*). Uhuru huu au ujasiri katika usemi mara nyingi una maana nyingine ya ushujaa katikati ya upinzani au ukataliwayi (kama vile Yohana 7:13; 1 The. 2:2).

Katika maandiko ya Yohana (limetumika mara 13) mara nyingi huonesha tangazo la wazi wazi (kama vile Yohana 18:20, pia katika maandiko ya Paulo, Kol. 2:15). Hata hivyo, wakati mwingine kwa maana ya kawaada ni "kwa uwazi" (kama vile Yohana 10:24; 11:14; 16:25,29).

Katika Matendo Mitume wanazungumzia ujumbe unaomhusu Yesu katika namna ile ile (kwa ujasiri) kama Yesu alivyozungumza kumhusu Baba na mipango na ahadi Zake (kama vile Matendo 2:29; 4:13,29,31; 9:27-28; 13:46; 14:3; 18:26; 19:8; 26:26; 28:31). Pia Paulo ilihitaji msaada wa maombi ambapo kwa ujasili angeliweza kuihubiri injili (kama vile Efe. 6:19; 1 The. 2:2) na kuiishi injili(kama vile Flp. 1:20).

Tumaini la Paulo la mambo yahusuyo kifo, hukumu na pepo katika Kristo lilimpa ujasiri na kijiamini katika kuihubiri injili katika zama hizi za sasa za uovu (kama vile 2 Kor. 3:11-12). Pia aliquwa na iamani kwamba wafuasi wa Kristo wangefanya kazi kwa namna ya kufaa sana (kama vile 2 Kor. 7:4).

Kuna kipengele kimoja zaidi cha neno hili. Kitabu cha Waebrania kinatumia neno hili katika maana ya kipekee ya ujasiri wa mwamini, kumwendea Mungu na kuzungumza Naye (kama vile Heb. 3:6; 4:16; 10:19,35). Waamini wanakubaliwa na kwa ukamilifu na kukaribishwa katika ukaribu na Baba kupitia Mwana (kama vile 2 Kor. 5:21)!

Katika Agano Jipyali linatumika katika njia kadhaa.

1. imani, ujasiri, au moyo wa kujihamini inahusiana na
  - a. wanaume (kama vile Matendo 2:29; 4:13,31; 2 Kor. 3:12; Efe. 6:19)
  - b. Mungu (kama vile 1 Yohana 2:28; 3:21; 4:12; 5:14; Ebr. 3:6; 4:16; 10:19)
2. kuzungumza wazi, dhahiri, au bila na utata (kama vile Marko 8:32; Yohana 7:4,13; 10:24; 11:14; 16:25; Matendo 28:31)
3. kwa kuzunza hadharani (kama vile Yohana 7:26; 11:54; 18:20)
4. muundo uhusianao (*parr̄hēsiazomai*) unatumika kuhubiri kwa ujasiri katikati ya mazingira magumu (kama vile Matendo 18:26; 19:8; Efe. 6:20; 1 The. 2:2)

■ "kupaingia patakatifu" kumbuka, moja ya dhana ya ufunguo wa kitabu ni njia ya kumfikia Mungu kwa maana ya msamaha wetu kupitia maisha ya Kristo na kifo badala yetu. Kuhani mkuu wa Agano la kale aliingia patakatifu pa patakatifu katika Hema takatifu mara mbili kwa siku katika mwaka (kama vile. Ebr. 9:25), siku ya upatanisho (kama vile Walawi 16). Lakini sasa kupitia dhabihu ya Kristo waamino wote wanaendelea kuingia kwa ukaribu kwa Mungu (sitiari nyine kwa ajili ya njia ya kuingia ni pazia kupasuka toka juuhata chini, kama vile. Mt. 27:51, kama vile. Marko 15:38).

■ "kwa damu ya Yesu" hii sio damu ya uchawi, lakini ni damu ya mwanadamu. Iliwakilisha dhabihu ya kifo cha Yesu badala ya dhambi za mwanadamu (kama vile Mdo. 20:28; Rum. 3:25; 5:9; Efe. 1:7; 2:13; Kol. 1:20; Ebr. 9:12,14; 12:24; 13:12; 1 Pet. 1:2,19; Ufu. 1:5; 5:9).

**10:20 "mpya"** neno *prosphatos* linamaanisha "mauaji mapya" na limetumia hapa pekee kwenye Agano jipy.

■ "iliyo hai" huu ni uthibitisho wa ufuluo. Aliuawa, lakini sasa yu hai (kama vile Ufu. 5:6) milele na milele!

|           |                                   |
|-----------|-----------------------------------|
| NASB      | "aliyotuanzia"                    |
| NKJV      | "iliyowekwa wakfu kwa ajili yetu" |
| NRSV, TEV | "aliyotufungulia"                 |
| NJB       | "aliyoifungua kwetu"              |

Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Hii "njia mpya iliyo hai" ni hodari, kihistoria, halisia kiroho.

*The Greek-English Lexicon* na Walter Bauer, iliyoboreshwa na Arndt, Gingrich, na Danker, inataja tofauti mbili za tafsiri kwa ajili ya neno kwenye muktadha huu.

1. kufungua njia (Ebr. 10:20)
2. kuanzisha au kuweka wakfu na kuandamana na taratibu za ibada (Ebr. 9:18) (uk. 215).

Muktadha unashauri kwa ukaribu kwangu muunganiko kati ya matukio haya mawili ya neno hili lisilo la kawaida la Agano la kale. Tena, mlingano wa maagano ni katika mtazamo; kwa damu yake Yesu alifungua njia bora zaidi ya kumkaribia Mungu na kudumisha ushirika.

■ "ipitayo katika pazia" Hii inasimulia kwa pazia la ndani kwenye Hema takatifu kati ya sehemu takatifu na Patakatifu pa Patakatifu (kama vile Mt. 27:51). Hapa pazia lilikuwa "mwili" wa Yesu. Hii inaweza kurejelea mwili wa Yesu uliovunjwa kwa ajili ya dhambi zetu, hivyo basi, kuandaa njia ya kupitia kwenda kwa Mungu (kama vile Isa. 52:13-53:12). Mwandishi kwa Waebrania anaona sehemu ya nje ya madhabahu (patakatifu) kama badala ya ufalme wa kimwili na madhabahu ya ndani (Patatifu pa Patatifu) ufalme wa kiroho. Katika nuru hii Hema takatifu la mbinguni ni tofauti na kielezo cha duniani (kama vile Ebr. 6:19).

**10:21 "kuhani mkuu"** Tazama Mada Maalum: Yesu kama kuhani mkuu katika Ebr. 2:17.

■ "**nyumba ya Mungu**" hii inarejelea Agano la kale (kama vile Ebr. 3:5) na Agano jipya (kama vile Ebr. 3:6; 1 Tim. 3:15; 1 Pet. 4:17) waaminio (kama vile Efe. 2:11-3:13). Kama vile Musa alivyokuwa mtumishi katika nyumba ya Mungu, Yesu ni kuhani mkuu na mwana!

**10:22 "na tukaribie"** hii ni kauli ya kati (yenye shahidii) tegemezi ya wakati uliopo. Ujasiri wa waaminio unasisitizwa kwenye kazi iliyotimizwa na Yesu, lakini manufaa haya na faida kubwa ni lazima yapokelewe kwa moyo! "tukaribie" imetumika kwa waabudio wanaomkaribia Mungu. tambua mfuatano:

1. na tukaribie kwa moyo wa kweli (Ebr. 10:22)
2. na tulishike sana ungamo la tumaini letu (Ebr. 10:23)
3. tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana (Ebr. 10:24)

Maagano mapya (kama vile Yer. 31:31-34) ni moyo mpya na roho mpya; pendo la milele na sheria ya nje; neema ya bure kwenye kazi iliyokamilishwa na Kristo, lakini pia ilihitajika, tunda lilotarajiwa, matokeo ya kutazamika! Matokeo ya ujasiri wa wokovu ni kuishi maisha ya ucha-Mungu! Sio mafundisho ya awali ya kuthibitisha, wala teolojia ya kumbatio, lakini kufanana na Kristo (sio na dhambi) ambayo ni ushahidi kwa wote!

Tambua orodha inayohitajika kwa ajili ya "kukaribia."

1. na moyo wa kweli
2. kwa utimilifu wa imani
3. hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamira mbaya
4. tumeosha miili kwa maji safi

■ "**moyo wa kweli**" fikra ifaayo ni ufunguo mpya wa maagano ya imani (halisi, kama vile. Ezek. 36:22-36; ukanushi, Isa. 29:13). Tazama Mada Maalum katika Ebr. 3:8.

■ "**kwa utimilifu wa imani**" utimilifu kamaili ni muunganiko katika imani! Utimilifu unasisitizwa kwenye

1. maisha ya imani kama ushahidi wa badiliko (kama vile. Yakobo 2:14-26)
2. kazi iliyotimizwa ya Kristo (kama vile. 2 Kor. 5:21)
3. mashahidi wa Roho (kama vile Rum. 8:16)

Juhudi za mwanadamu haziwezi kamwe kureta wokovu au utimilifu. Hata hivyo, badiliko na maisha ya imani yanayobadilika ni ushahidi wa kweli kwamba umeokolewa. Matokeo ya kawaida ya kukutana na Mungu mtakatifu ni maisha matakatifu ya huduma.

Utimilifu wa kibiblia hakuwa kamwe na maana ya kubadilika katika uthibitisho wa mafundisho, lakini kuishi katika maisha! Kwa ajili ya wale ambao hutangaza kumjua Kristo lakini wakiishi maisha ya kutojali, kutowajibika, maisha ya kiulmwengu, kujifikilia mwenywewe, wasio zaa matunda, maisha yasiyo mcha-Mungu hakuna utimilifu! Tazama Mada Maalum katika Ebr. 3:14.

■ "**hali tumenyunyiziwa mioyo**" Hii ni kauli timilifu tendwa endelevu ya hali ya kuendelea ambayo ni dokezo la kuanzisha njia ya taratibu za ibada ya maagano ya awali (kama vile Kut. 24:8; 1 Pet. 1:2). Kunyunyiziwa damu ya maagano mapya ilikuwa na thamani zaidi katika kusafisha hatia la anguko la mwanadamu (kama vile Ebr. 9:9,14).

■ "**kutoka dhamiri mbaya**" Hiki ndicho Agano la kale lilishindwa kukiondoa (kama vile Ebr. 9:9; 10:2). Hata hivyo, , 1 Pet.3:21 mistari sambamba ina uhusiano kati ya ubatizo na dhamira safi.

■ "**tumeosha miili kwa maji safi**" Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo. Inawezekana hili ni dokezo lingine la matendo ya kuhani mkuu katika siku ya upatanisho, kihistoria inafanana na kuoshwa kwa kunyunyizwa katika Agano la kale (kama vile Law.8:6; 16:4; Kut.29:4; 30:17-21;Hes.19:7-8). Hii hairejelei kwa ubatizo wa Ukristo.

Hii ni taswira nyingine ya Agano la kale ya kufuata utaratibu wa kusafisha. Ni wazi kwamba utaratibu wa kutumia maji unaweza kurejelea kwa (1) kifo, maziko, na ufuluo (kama vile Rum. 6:1-11 na Kol. 2:12) na (2) kusafisha dhambi (kama vile Mdo. 22:16; 1 Kor. 6:11; Efe. 5:26; Tito 3:5; na 1 Pet. 3:21). Maji sio mbinu, lakini ni sitiari. Tangu kanisa la awali halikuwa na majengo, watu hawakuja mbele ya hadhira ili kumwamini Kristo kama wafanyakyo leo hii kwenye makanisa mengi. Toba na maungamo yao mbele ya hadhira ilikuwa ni ubatizo. Lilikuwa ni tukio na dokezo la msamaha wa dhambi na kumpokea Roho (kama vile Mdo. 2:38) sio maana.

**10:23 Na mlishike sana ungamo la tumaini letu lisigeuke"** Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo imetumika kama shurutishi. Hii ni ya pili kati ya kauli tegemezi za wakati uliopo tatu ambazo huonyesha imani itarajiwayo (lakini sio na uhakika) jibu.

▣ "tumaini" Toleo la KJV lina "imani," lakini hakuna chapisho la Kiyunani linalosaidia. Neno "tumaini" mara nyingi hurejelea utukufu wetu wakati wa ujio wa pili (kama vile Ebr. 3:6; 6:11,18; 7:19; 1 Yn. 3:2).

- |             |  |
|-------------|--|
| <b>NASB</b> | "ye ye aliyahidi ni mwaminifu"                             |
| <b>NKJV</b> | "ye ye aliyahidi ni mwaminifu"                             |
| <b>NRSV</b> | "ye ye aliyahidi ni mwaminifu"                             |
| <b>TEV</b>  | "kwa sababu tunamwamini Mungu anaweza kutimiza ahadi yake" |
| <b>NJB</b>  | "kwa sababu ye ye aliyahidi ni mwaminifu"                  |

Kitenzi pekee ni kauli ya kati (shahidi wa maandishi) endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu, "aliyahidi." Huu ni uwiano wa tatu kitheolojia "na tu...." maelezo ya Ebr. 10:22-24. Ukweli huu kinzani wa wokovu wa bure, kuandaa, kufanyiza na kulindwa na Mungu, lazima kulete maagano yafaayo kupokolewa na mwanadamu! Utawala wa Mungu na uhuru wa mwanadamu wote utakuwa katika ukweli wa kibiblia na lazima ushikiliwe kwenye mvutano.

Uaminifu wa Mungu ni ujasiri imara kwa waaminio (kama vile Ebr. 11:11). Ahadi za Mungu ni hakika; neno la Mungu ni kweli!

**10:24 "tukaangaliane"** Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo. Mwandishi ametumia maneno kadhaa tofauti kusimulia fikra zetu juu ya mambo ya kitheolojia.

1. tafakari, *katanoeō*, Ebr. 1:1; 10:24 (kama vile Luka. 12:24,27)
2. angalia, *theōreō*, Ebr. 7:4
3. mtafakarini, *analogizomai*, Ebr. 12:3
4. kuuchunguza, *anatheōreō*, Ebr. 13:7

Waaminio ni lazima wafikilie kuititia imani zao.

1. kwa nini iwe kweli
2. inatumikaje
3. tuwasaidieje wengine
4. ni nini kusudi lake kuu

▣ "sisi kwa sisi na kuhimizana" Hili ni neno imara la kawaida la Kiyunani na kidokezo hasi. Limetumika mara mbili pekee kwenye Agano Jipya. Sehemu nyingine ni mabishano ya Paulo na Barnaba kwenye Mdo. 15:39. Hii kwa yumkini ikaaksi mvutano kati ya waaminio na Wayahudi wasioamini waabudio kwenye sinagogi, ambayo inafafanua kwa ubora zaidi katika makundi ("sisi," "wewe," na "wao") ya Waebrani 6.

▣ "katika upendo na kazi nzuri" haya ni matunda ya kweli ya Ukristo!

**10:25** mistari ya 24-25 inataja vitu vitatu kwamba waaminio wanaweza kutenda.

1. kuhimizana sisi kwa sisi katika upendo na kazi nzuri
2. tusiache kukusanyika pamoja (maana ya asili ya "sinagogi," limetumika hapa pekee kwenye Agano jipya)
3. kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia

Hili ni andiko pekee kwenye Agano jipya ambalo hutia moyo waaminio wakusanyike kwa ajili ya kuabudu. Hii yumkini huaksi mpangilio wa kihistoria wa mateso ya Rumi kuulenga Ukristo (dini isiyokubalika) dhidi ya kuukubali undugu wa Uyahudi (dini inayokubalika). Yumkini pia ikaaksi siku tofauti za kuabudu. Kanisa la awali lilianza kusambaa ndani ya Uyahudi, walimu wa sheria (yaani, uamsho wa Uyahudi wa kifarisayo katika Jamnia Mwaka wa 90 B.K) waliendeleza "laana" kiapo kilihitajika kwa kila mwanajumuia wa sinagogi, ambao walihusika na kumkataa Yesu wa Nazareti kama Masihi aliyeahidiwa. Kwa kiwango hiki waaminio wengi waliacha sinagogi na taratibu za Sabato lakini waliendelea kuabudu siku ya jumapili kanisani. Yakobo 2:2 ametumia neno "sinagogi" kurejelea sehemu ya kuabudu Wakristo, kama alivyofanya kwenye Ebr. 10:25.

▣ "siku ile" hii inarejelea ujio wa pili. Katika mwanga wa mistari ifuatayo, pia inasimulia siku ya hukumu.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 10:26-31**

<sup>26</sup>Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; <sup>27</sup>bali kuna kuitazamia hukumu yenyekutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao. <sup>28</sup>Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu. <sup>29</sup>Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanya Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyatkaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanya jeuri Roho wa neema? <sup>30</sup>Maana twamjua yeeye aliyesema, Kupatiliza kisasi ni juu yangu, mimi nitalipa. Na tena, Bwana atawahukumu watu wake. <sup>31</sup>Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.

**10:26 "kama"** Hii sio sentensi amrishi yenyekufanana. Inawezekana ni chanzo kabisa (*hamartanontōn hēmōn*) cha kazi kama kauli shurutishi (kama kishazi).

Kwa mshangao kisarufi cha mwandishi kinamfanana mwenyewe na makusudi ya kundi la waovu, lakini yumkini hii ikawa mbinu ya fasihi (wingi wa mhariri) unaofanana na Ebr. 2:3. Mtu wa kwanza kwa ujumla hafanani na kundi linaloongelewa kwenye Ebr. 10:26-29. Aina hii hii ya mbinu ya fasihi imetumia mtu wa kwanza inaweza kupatikana kwenye 1 Kor. 13:1-3.

▣ "dhambi kusudi" "kusudi" imewekwa awali katika Kiyunani kwa ajili ya mkazo. Inawezekana neno linafanana na "fanya jambo kwa kiburi" dhambi ya Agano la kale (kama vile. Muhtasari wa Ebr. 5:2). Muundo wa kisarufi wa kitenzi (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo milikishi ya kiume mtu wa kwanza wingi) umetumika na baadhi ya maoni kwamba hii inarejelea kwa waaminio ambao wanaendelea katika dhambi. Ikiwa wataweza kuacha dhambi wataepuka hukumu. Hata hivyo, hii haifai kwenye onyo la muktadha wa Ebr. 6:1-6 na Ebr. 10:26-29. Haya ni maisha au onyo la kifo, mara moja nje, mara zote ni onyo! Kumkataa Yesu kwenye uwepo wa nuru ya ufunuo iletayo giza katika usiku wa kiroho.

▣ "baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli" kitenzi kwenye kiingereza, "kuupokea," sio kauli tendaji ya kitenzi jina cha wakati uliopita usiotimilifu. Huu ni msingi wa tatizo la kutafsiri. Ikiwa mara moja watapokea maarifa ya ufahamu kamili *nōskō* wa (kibainishi cha wazi) ukweli; hii ni nzuri kama waaminio! Hili ni jambo la kitheolojia lile lile kama Ebr. 6:4-6.

Ni lazima iruhusiwe hakuna rahisi, dhahili, tafsiri ya wazi. Hofu ya maisha yangu ni kwamba upendeleo wangu yumkini ukatawala andiko kwa uwazi zaidi. Ni lazima nizue kwenda kimbini, kutawala mpango ambao utanyamazisha nguvu hii, andiko lililovuviwa. Tatizo sio waaminio watenda dhambi. Tatizo ni waaminio ambao huacha kuamini! Siwezi kukubaliana na nadharia kwamba (1) wokovo hufanyika kutegemea matendo ya mwanadamu au (2) kuubadili utimilifu kuwa tangazo kabisa la mafundisho yasiyosimulia maisha ya Mkristo. Kataa nadharia ya kupoteza, kuokolewa, kupotea, kuokolewa! I pia kataa nadharia ya "kuokolewa mara moja, kuokolewa daima" ambayo hayasimulii kendelea kiimani na maisha ya kuishi kwa imani. Hata hivyo, nitafanya nini? Nalifafanua andiko: katika mpangilio wa kihistoria. Katika uwazi wa muktadha, kwenye maelezo ya kisarufi chake, katika chaguo la maneno yake, kwa aina yake, na vifungu vyake sambamba. Ni lazima niruhusu kwamba ikiwa nitafanya kazi zote na Ebr. 6:4-6 na 10:26-29, inawezekana kuna uchaguzi mdogo lakini kwamba waaminio wako mbali na neema. Hata hivyo,

1. mpangilio wa kihistoria, kitabu cha Kiyahudi, na uwepo wa mateso ni jambo kuu
2. fasihi ya muktadha (kama vile. Ebr. 5:11-6:12) na makundi matatu (kama vile. "sisi," "wewe," na "wale amba'o") inaonekana kufunua mpangilio wa Kiyuhudi wa "Wayahudi waaminio" na "Wayahudi wasioamini" waabudio na washiriki kwenye mpangilio wa sinagogi
3. dondoor nyingi zimetumika kwenye Agano la kale kusimulia Hema takatifu, neno sinagogi limetumika (kama vile. Ebr. 10:25), na wito wa imani, yote yalilenga kwa kiongozi wa familia na Agano la kale.

Hata hivyo, baada ya ufanuzi wa andiko nafikilia ufanuzi kwa ujumla (pasipo matatozi yake na dhana) ni dhanio la kihistoria la ujenzi mpya wa R. E. Glaze, Jr. katika *No Easy Salvation*, liochapishwa na Insight Press, 1966.

Waembrania inaonekana kuegemea katika kitabu, kuchagua kundi. Ina maana kwamba haina kifungu kwa ajili ya siku za leo? Maonyo ya mwandishi yaliyovuviwa (pamoja na Yakobo, Petro, na mwandishi wa I na 2 Yohana) yanaweza kuwatia hamasa waaminio kuendelea kukimbia mbio (tazama F. F. Bruce, *Answers to Questions*, uk. 124-125)! Jibu haliko kwenye kuamini kirahisi, wala katika kufanyiza-hofu ya ushikiliaji mno wa sheria, lakini katika maisha ya imani ya ucha-Mungu, kujitahidi kuuelekea utakatifu, kufanywa kwa mwelekeo wa shukrani kamili, yamekwisha, na mwishowe wokovu (kama vile Ebr. 10:14) kuititia kwa Kristo kwa imani.

**10:27 "hukumu"** mwandishi anatumia mkazo tena na tena tumaini la ajabu kwamba waaminio wako ndani ya Kristo, lakini ukanaji upande unavutia sana; hukumu inakuja, na wote tutasimama mbele za Mungu Mtakatifu (kama vile Ebr. 9:27; Gal. 6:7).

▣ "ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao" Hili ni dokezo la Isa. 26:11. Moto mara nyingi unahusiana na utakatifu au kutakaswa. Mungu ni mwenye haki; uumbaji wake ni haki kweli. Wanadamu wasivunje sheria zake, wajiharibu wenywewe kwenye sheria zake.

## MADA MAALUM: MOTO (BDB 77, KB 92)

Moto unavyo vidokezo chanya na hasi katika maandiko.

- A. Chanya
  1. Husisimua (kama vile Isaya 44:15; Yohana 18:18)
  2. Huwasha nuru (kama vile Isaya 50:11; Mt. 25:1-13)
  3. Hupikia (kama vile Kut. 12:8; Isaya 44:15:16; Yohana 21:9)
  4. Husafisha (kama vile Hes 31:22-23; Mithali 17:3; Isaya 1:25; 6:6-8; Yer 6:29; Malaki 3:2-3)
  5. Utakatifu wa Mungu (kama vile Mwa. 15:17; Kutoka 3:2; 19:18; Eze. 1:27; Waembrania 12:29)
  6. Uongozi wa Mungu (kama vile Kutoka 13:21; Hes. 14:14; Wafalme 1. 18:24)
  7. Uwezeshaji wa Mungu (kama vile Mdo. 2:3)
  8. Ulinzi wa Mungu (kama vile Zekaria 2:5)
- B. Hasi
  1. Huunguza (kama vile Yos 6:24; 8:8; 11:11; Mt. 22:7)
  2. Huangamiza (kama vile Mwa 19:24; Walawi 10:1-2)
  3. Hasira (kama vile Hes 21:28; Isaya 10:16; Zek. 123:6)
  4. Adhabu (kama vile Mwa. 38:24; Walawi 20:14; 21:9; Yoshua 7:17)
  5. Ishara ya mbaya ya siku ya mwisho (kama vile Ufunuo 13:13)
- C. Hasira ya Mungu dhidi ya dhambi mara nyingi hudhahirishwa kwa tanuru ya moto.
  1. Hasira yake huunguza (Kama vile Hos 8:5; Sefania 3:8)
  2. Humimina moto (kama vile Nah 1:6)
  3. Moto wa milele (kama vile Yer. 15:14; 17:4; Mt. 25:41; Yuda aya ya 7)
  4. Hukumu ya siku ya mwisho (kama vile Mt. 3:10; 5:22; 13:40; Yohana 15:5; The. 2. 1:7; Petro 2. 3:7-10; Ufu 8:7; 16:8; 20:14-15)
- D. Moto mara nyingi huonekana katika tanuru
  1. Mwa. 15:17
  2. Kutoka 3:2

- 3. Kutoka 19:18
- 4. Zaburi 18:7-15; 29:7
- 5. Eze. 1:4, 27; 10:2
- 6. Ebr. 1:7; 12:29
- E. Kama sitiari yingi katika Biblia (yaani chachu, simba) moto unaweza kuwa Baraka au kufuatana na mazingira au muktadha.

**10:28**

- NASB "Mtu aliyeidharau sheria ya Musa"  
 NKJV "Mtu aliyeikataa sheria ya Musa"  
 NRSV "Mtu aliyeikiuka sheria Musa"  
 TEV "Mtu ambae hakuitii sheria ya Musa"  
 NJB "Mtu aliyepuuza sheria ya Musa"

Hili ni neno imara la kukataa makusudi. katika *A Handbook on the Letter to the Hebrews*, Ellingworth na Nida wanasema:

"neno kwa ajili ya **kutokutii** ni neno imara, halikutumika kwa ajili ya tukio la dhambi, lakini kwa ulimwengu kuvunja maagano (Ezek. 22:26), kwa mfano, ibada ya sanamu (Kumb. 17:2-7), unabii wa uongo (Kumb. 18:20), au kukufuru (Law. 24.13-16)" (uk. 236).

▣ "hufa pasipo huruma.... mashahidi wawili au watatu" katika Agano la kale kesi kubwa mara zote walihitajika mashahidi wawili (kama vile Kumb. 17:6; 19:15). Kuna matokeo ya kutokutii!

**10:29 "iliyo kubwa zaidi"** haya ni mabishano kutoka kwa mdogo (maagano ya Musa) hadi kwa mkuu (maagano ya Yesu). Ulinganishi huu ni dhana ya Waebrania.

▣ "aliyemkanyaga" picha hii humaanisha kumtendea kwa dharau (kama vile Ebr. 6:6). Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu, ambayo hudokeza tendo kamilifu, kama lilivyofanyika katika endelevu lijalo.

▣ "Mwana wa Mungu"

## MADA MAALUMU: MWANA WA MUNGU

Hii ni moja kati ya nyadhifa kubwa alizopewa Yesu katika Agano Jipya. Ni wazi kabisa ina kidokezo cha Uungu. Inamjumuisha Yesu kama "Mwana" au "Mwana wangu," pia Mungu anaelezewa kama "Baba" (angalia Mada Maalumu: Ubaba wa Mungu). Linatokea mara 124 katika Agano Jipya. Hata usanifu wa Yesu mwenyewe kama "Mwana wa Adamu" ina kidokezo cha Uungu toka Dan. 7:13-14

Katika Agano la Kale usanifu wa neno "Mwana" ingalirejea kwenye makundi maalumu manne (angalia Mada Maalumu: "Wana wa.....")

- A. Malaika (mara nyingi iko katika hali ya WINGI, kama vile Mwa. 6:2; Ay. 1:6; 2:1)
- B. Mfalme wa Israeli (kama vile 2 Sam. 7:14; Zab. 2:7; 89:26-27)
- C. Taifa la Israeli kwa pamoja (kama vile Kut. 4:22-23; Kumb. 14:1; Hos. 11:1; Mal. 2:10)
- D. Waamuzi wa Israeli (kama vile Zab. 82:6)

Ni utumiaji wa mara ya pili ambao unahusianishwa na Yesu. kwa njia hii "Mwana wa Daudi" na "Mwana wa Mungu" semi zote zinahusianishwa na 2 Samwel 17; Zaburi 2 na 89. Katika Agano la Kale neno "Mwana wa Mungu" kamwe halitumiki hasa kwa Masihi, isipokuwa kama ni mfalme wa siku za kiama kama mmoja wa "wapakwa mafuta" wa Israeli. Hata hivyo, katika magombo ya bahari ya chumvi wadhifa unaohusiana na Masihi ni wa kawaida (angalia nukuu maalumu katika *Dictionary of Jesus and the Gospels*, uk. 770). Pia "Mwana wa Mungu" ni wadhifa wa Kimasihi katika miingiliano miwili ya kazi za mafunuo ya Kiyahudi (kama

vile II Esdras 7:28; 13:32,37,52; 14:9 na I Enoch 105:2)

Mazingira ya nyuma ya Agano Jipyka kama inavyorejerea kwa Yesu kwa uzuri imefupishwa kwa namna mbali mbali.

1. Uwepo wake kabla (kama vile Yohana 1:15-30; 8:56-59; 16:28; 17:5; 2 Kor. 8:9; Flp. 2:6-7; Kol. 1:17; Ebr. 1:3; 10:5-8)
2. Kuzaliwa kwake kwa njia ya pekee (kama vile Isa. 7:14; Mt. 1:23; Luk. 1:31-35)
3. Ubatizo wake (kama vile Mt. 3:17; Mk. 1:11; Luk. 3:22. Sauti ya Mungu toka mbinguni ikiunganisha ufalme wa kifahali wa Zaburi 2 na mtumishi mwenye mateso wa Isaya)
4. Majaribu ya shetani (kama vile Mt. 4:1-11; Mk 1:12,13; Luk 4:1-13. Anajaribiwa kuwekeea mashaka uwana wake au kutimiliza kusudi lake kwa njia tofauti na ile ya msalaba.)
5. Uthibitisho wake na wale wakiri wasiokubalika
  - a. Mapepo (kama vile Mk 1:23-25; Luk. 4:31-37,41; Mk. 3:11-12; 5:7; angalia Mada Maalumu: Pepo [roho wachafu])
  - b. Wasioamini (kama vile Mt. 27:43; Mk. 14:61; Yohana 19:7)
6. Uthibitisho wake kupitia wanafunzi wake
  - a. Mt. 14:33; 16:16
  - b. Yohana 1:34,49; 6:69; 11:27
7. Uthibitisho wake mwenyewe
  - a. Mt. 11:25-27
  - b. Yohana 10:36
8. Utumiaji wake wa stiari ya kawaida ya Mungu kama Baba
  - a. Utumiaji wake wa neno *abba* kwa ajili ya Mungu
    - 1) Mk. 14:36
    - 2) Rum. 8:15
    - 3) Gal. 4:6
  - b. Utumiaji wake wa sasa wa jina Baba (*patér*) kuelezea uhusiano wake na Uungu.

Kwa ufupi, wadhifa wa neno "Mwana wa Mungu" una maana kubwa ya kithiolojia kwa wale waliofahamu Agano la Kale na ahadi zake, lakini waandishi wa Agano Jipyka waliogopeshwa kuhusu utumiaji wao na watu wa mataifa kwa sababu ya mazingira ya nyuma ya wapagani ya "miungu" ikiwachukulia wanawake na matokea ya watoto kuwa "majitu."

▣ "kuihesabu" Hii humaanisha umuhimu wa matokeo ya uchaguzi kwenye majadiliano.

▣ "kitu ovyo" Hii inarejelea kwa kitu Fulani kwamba katika utaratibu wa kidini ni najisi, hakifai kwa kusudi lake lililopangwa.

▣ "damu ya agano aliyatakaswa kwayo" swalii hapa linasimuliwa kwa kiteni (kauli tendewa elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu). Je hii inarejelea kwa kukataliwa kwa awali kwa maagano mapya au hii ni kutupilia mbali kutoka katika maagano mapya? Kauli endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu katika tungo iliyopita na kauli tendwa ya wakati uliopita usiotimilifu katika tungo inayofuatia inadokeza kukataliwa awali.

Tatizo la tafsiri hii ni kwamba kila sehemu kwenye Waembrania isemayo kwamba "kutakaswa" imetumika kurejelea kwa waaminio (kama vile Ebr. 2:11; 9:13; 10:10,14; 13:12). Kwangu mimi jambo ni utunzaji – maagano. Mungu mtawala alifanya maagano yanayosimulia wokovu. Ni huru; ni kwa ajili ya wote, lakini ni lazima yapokelewe (kwa mapenzi mwanadamu aliye huru), sio kupokea kwa mhemko (kama vile. Mt. 13:20-22), wala kwa kuunganika na kanisa (kama vile 1 Yn 2:19). Kuamini ni ufunguo. Wale wanao amini/imani/tumaini (yawezekana zote ni tafsiri ya *pisteuō*) wataokolewa na wana utimilifu. Maonyo mawili kwa Waembrania ni kwa (1) kupokea injili ya bure na (2) na kutembea ndani yake. Ikiwa mmoja hataipokea—hukumu; ikiwa mmoja ameacha kuamini—hukumu!

■ "kumfanyia jeuri Roho wa neema" Anaitia dhambi hatiani, anatureta kwa Kristo, tubatizwe katika Kristo na muundo wa Kristo ndani yetu kama waaminio (kama vile. Yn 16:8-11). Roho hufedheheka au kumtendea uovu pale waaminio wanapokataa kumuunga mkono na kumtia hatiani. Baadhi ya wapokeaji wa kitabu hiki walimkataa Kristo kwenye uwepo wa ufunuo dhahili kutoka kwa baadhi ya wanajumuia wa sinagogi (tazama utangulizi, Wapokeaji).

**10:30 "kisasi"** Hii ni dondoo kutoka katika tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania kutoka Kumb. 32:35a na 36a. hii sio hasira, lakini haki kamili isiyoweza kudhitiwa kwa wote wanaohusishwa.

■ "Bwana atawahukumu watu wake" Hii ni dondoo zaidi kutoka katika tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania ya Kumb. 32:36a. Andiko la kiebrania lina "thibitisha" badala ya "hakimu." Je tungo hii inadokeza kwamba mwenye dhambi makusudi ni mtu wa Mungu? Kwa kawaida kipengele kimoja cha dondoo ni cha kudhamiri katika Agano la kale. Ni dhahili "hakimu" kwamba inalenga lengo la dondoo, sio kwamba ni muktadha asili unaorejelea ibada ya sanamu katika Israeli. Mwandishi ametumia kukataliwa kwa Mungu na watu wake katika hukumu kama maonyo kupitia katika kitabu hiki.

**10:31 "Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai"** tungo hii (kama vile Ebr. 3:12) inaksi jina la Mungu wa maagano, "YHWH" (kama vile. Kumb.3:14), kutoka kitenzi cha Kiebrania "kuwa" (kama vile. Mt. 16:16). Tazama Mada Maalum katika Ebr. 2:7. Wasioamini watavuna hasara ya milele!

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 10:32-39

<sup>32</sup>Lakini zikumbukeni siku za kwanza, ambazo, mlipokwisha kutiwa nuru, mlistahimili mashindano makubwa ya maumivu; <sup>33</sup>pindi mlipotwezwa kwa mashutumu na dhiki, na pindi mliposhirikiana na wale waliotendewa hayo. <sup>34</sup>Maana mliwaonea huruma wale waliokuwa katika vifungo, tena mkakubali kwa furaha kunyang'anywa mali zenu, mkijua kwamba nafsini mwenu mna mali iliyo njema zaidi, idumuyo. <sup>35</sup>Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. <sup>36</sup>Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi.

<sup>37</sup>Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana,

Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia.

<sup>38</sup>Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani;

Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye.

<sup>39</sup>Lakini sisi hatumo mionganoni mwao wasitao na kupotdea, bali tumo mionganoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu.

**10:32 "zikumbukeni siku za kwanza"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo, inawezekana inarejelea katika Ebr. 5:12.

■ "mlipokwisha kutiwa nuru" Hii imetumika kwa kundi la wasioamini katika Ebr. 6:4. Ninaamini kuna makundi mawili yanaelezewa.

1. Wayahudi wale walioziona nguvu za Mungu katika maisha yao na ushuhuda wa marafiki zao waaminio.
2. Wayahudi waaminio ambao bado wanaendelea kuabudu kwa kufuata utaratibu wa sinagogi.

Neno "wewe" la Ebr. 10:32-36 ni kinyume cha Ebr. 10:26-31(kama ni 6:9-12 na 6:4-8).

■ "mlistahimili" Hii ni sitiari kutoka katika mashindano ya riadha (kama vile Ebr. 12:1,2,3,7).

■ "mashindano makubwa ya maumivu" Hii inarejelea mateso ambayo yalitokea katika kanisa, lakini sio sinagogi, kwa sababu Uyahudi ilikuwa ni dini halali chini ya utawala wa Rumi, lakini sio Ukristo. Kifungu hiki kinaonyesha kudokeza kwamba waliwasidia wengine waliopitia mateso na hivyo wakashiriki baadhi ya mashutumu (kama vile. Ebr. 10:33-34; 6:10).

**10:34 "katika vifungo"** Baadhi ya Wakristo walifungwa gerezani, lakini sio wapokeaji wa nyaraka. Walikuwa waaminio, lakini hawakufanana kikamilifu na kanisa. Hii yumkini inathibitisha mtazamo kwamba walikuwa ni waaminio wa Kiyahudi walioendelea kuhudhuria katika sinagogi (tazama Utambulisho, Wapokeaji).

Toleo la KJV lina "katika mapatano yangu," ambapo wengi wa wafasiri wametumia kama ushahidi kuthibitisha uandishi wa Paulo. Hata hivyo, inawezekana kuna aina kadhaa mbalimbali za machapisho: (1) "kwenye mapatano" (P<sup>13</sup>, A, D\*, na tafsiri za Vulgate na Peshitta); (2) "katika mapatano" (P<sup>46</sup>, Ψ, na andiko ya Kiyunani lilitumiwa na Origen); na (3) "kwa mapatano yangu" Κ, D2, K, L, P naandiko la Kiyunani lilitumiwa na Clement wa Alexandria).

▣ "mkakubali kwa furaha kunyang'anywa mali zenu" Huu ni ushahidi wa ukweli wa tumaini letu katika Kristo na urithi wetu kwake (kama vile. Ebr. 9:15; 11:16; 13:14; Mt. 5:12; Luka 6:22-23; Rum. 5:3; 8:17).

▣ "zaidi" Tazama maelezo kamili katika Ebr. 7:7.

**10:35-36** mistari hii ya makala inawahitaji kundi la wanaoamini (1) wasiutupe mbali ujasiri wao (kama vile. Ebr. 3:6; 4:16; 10:19) na (2) kustahimili (kama vile. Ebr. 12:1-3). Kwa njia nyingi bora kama ujumbe kwa makanisa saba ya Ufu. 2-3 (kama vile. Ufu. 2:3,5,7,10,11,13,16,17,19,25,26; 3:2,3,5,10,11,12,20). Imani ya kweli ni imani inayovumilia (kama vile 1 Y 2:19). Ahadi za maagano ya Mungu lazima yapokelewe na kushikiliwa. Tazama Mada Maalum katika Ebr. 4:14.

Jambo la kweli katika usalama sio waaminio kushindana, lakini kundi kubwa la wanajumuia wa kisasa katika kanisa la magharibi ambao hawana ushahidi wa imani katika maisha yao. Kuamini kirahisi, wameunganishwa na mkazo wa juu katika usalama, umeyajaza makanisa yetu Wakristo wachanga na kupoteza watu kwenye vazi la Ukristo kwa thamani! Uanafunzi na wito wa msingi wa utakatifu umepotea ulimwenguni, upotoshaji, tamaduni za kisasa za magharibi. Wokovu umegeuzwa kuwa bidhaa (kibali cha mbinguni mwisho wa maisha ya kujipenda mwenyewe au sheria ya kujikinga na moto dhidi ya dhambi inayoendelea) badala ya kila siku, kukua, uhusiano binafsi na Mungu. Lengo la Ukristo sio tu kwenda mbinguni wanapokufa (uumbaji), lakini sasa kumfanana Kristo!! Mungu anataka kurejesha sura yake kwa mwanadamu hivyo anaeeza kumfikia mwanadamu alieanguka na wokovu wake wa bure katika Kristo. Tumeokolewa ili tutumike! Usalama ni kwa uumbaji wa maisha ya huduma na uanafunzi.

## MADA MAALUMU: USTAHIMILIVU

Mafundisho ya kibiblia yaliyohusiana na maisha ya Mkristo ni vigumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika namna ile ile ya mashariki, milinganyo ya kirahaja (tazama Mada Maalumu: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya kibiblia]). Milinganyo hii inaonekana kuwa na mkanganyiko, bado mihimili yote ni ya kibiblia.

Wakristo wa Mashariki walielekea kuchagua ukweli ulio mmoja na kuachana au kukashifu kweli iliyo kinyume.

Baadhi ya Mifano ni:

1. Je! Wokovu ni maamuzi asilia ya kumwamini Kristo au ni maisha yenye wajibu ya kiuwanafunzi?
2. Je! Wokovu ni uchaguzi kwa maana ya neema kutoka katika mamlaka ya Mungu au imani na mwitikio wa toba kwa sehemu ya mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu?
3. Je! wokovu, unapopokelewa, haiwezekani kuupoteza, au kuna uhitaji wa jitihada endelevu

Jambo hili la ustahimilivu limekuwa la kibishi katika historia nzima ya kanisa. Tatizo linaanza na muonekano wa mgogoro wa vifungu vya Agano Jipy:

1. maandiko yahusuyo uhakika
  - a. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 6:37; 10:28-29)
  - b. semi za Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Flp. 1:6; 2:13; 2 The. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
  - c. semi za Petro (1 Pet. 1:4-5)
2. maandiko yahusuyo umuhimu wa ustahimilivu

- a. semi za Yesu katika Injili za Kimhutasari (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13)
- b. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 8:31; 15:4-10)
- c. semi za Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Flp. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
- d. semi za mwandishi wa Kiebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
- e. semi za Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21; 21:7)

Mambo ya wokovu ndani ya biblia hutoka katika pendo, huruma, na neema ya mamlaka ya Mungu wa Utatu. Hakuna mwanadamu awezaye kuokolewa pasipo kuingiliwa na Roho (kama vile Yohana 6:44,65). Mungu alikuja na kupangilia mambo muhimu, lakini alidai kwamba wanadamu wanapaswa kuitikia katika imani na toba, katika namna zote kwa uanzilishi na kwa uendelevu. Mungu hutenda kazi na wanadamu katika uhusiano wa agano. Kuna upendeleo na majukumu!

Wokovu umetolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kilihuisika na tatizo la dhambi ya uumbaji ulioanguka! Mungu ameleta njia na anahitaji wale wote walioumbwa kwa mfano Wake kuliitikia pendo Lake na utoaji katika Yesu. Kama ungependa kusoma zaidi juu ya somo hili tazama

1. Dale Moody, *The Word of Truth*, Eerdmans, 1981 (kur. 348-365)
2. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
3. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inashughulikia matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuchukulia imani kama msimamo wa kuishi bila kuzaa matunda, maisha ya ubinafsi au (2) kuwatia moyo wale wanaopambana na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kwamba makundi yasiyo sahihi yana uchukuwa ujumbe usio sahihi na kutengeneza mifumo ya kitheolojia yenye vifungu vya kibiblia vyenye kuwekewa mipaka. Baadhi ya Wakristo wakiwa katika hali ya kukata tamaa wanahitaji ujumbe wa kuwatia moyo, wakati wengine wanahitaji kuonywa kwa ukali kuhusiana na uvumilivu! Wewe uko ndani ya kundi lipi?

Kuna mabishano ya historia ya kitheolojia iliyomuhusisha Augustine dhidi ya Pelagius na Calvin dhidi ya Arminius (semi-Pelagian). Jambo hili lilihuisisha swali la wokovu : kama mtu akiokolewa kiukweli, yampasa kustahimili katika imani na uamiifu?

Wafuasi wa Calvin wamesimama nyuma ya maandiko yale ya kibiblia ambayo yanadai kwamba mamlaka ya Mungu na nguvu idumuyo (Yohana 10:27-30; Rum. 8:31-39; 1 Yohana 5:13,18; 1 Pet. 1:3-5) na vitenzi vya nyakati kama kauli tendewa timilifu endelevu ya Efe. 2:5,8.

Wafuasi wa Arminius wamesimamia maandiko yale ya kibiblia ambayo yanamuonya yule aaminiye "kusimama imara," "kudumu," au "kuendelea" (Mt. 10:22; 24:9-13; Marko 13:13; Yohana 15:4-6; 1 Kor. 15:2; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Mimi binafsi siamini kwamba Waibrania 6 na 10 zinatumika, lakini wafuasi wengi wa Arminius wanazitumia kama onyo dhidi ya uasi. Mfano wa Mpanzi katika Mathayo 13 na Marko 4 inashughulikia suala la imani, kama inavyofanya Yohana 8:31-59. Kama wafuasi wa Calvin wanavyo nukuu vitenzi vya kauli ya wakati uliopo timilifu vilivyotumika kueleza wokovu, Wafuasi wa Arminius wana nukuu vifungu vya kauli ya wakati uliopo kama 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15.

- Huu ni mfano kamili wa namna mfumo wa kitheolija unayotumiwa vibaya njia ya uhakiki wa fasiri za maandiko. Mara nyingi kanuni inayoongoza au andiko kuu linatumika kutengeneza ufito wa kitheolojia ambapo maandiko mengine yote yanatazamiwa. Kuwa makini na mfumo kutoka vyanzo vyo vyote vile. Vitokana na ufanuzi wa mantiki ya mashariki, si ufunuo. Biblia ni kitabu cha mashariki. Inawakilisha kweli katika mvutano uliokamilishwa, ulinganifu wa mafumbo yaonekanayo. Wakristo wanamaanisha kukubaliana na yote na kuishi ndani ya mvutano huo. Agano Jipya linawasilisha vyote yaani ulinzi wa mwaamini na dai la imani endelevu na uovu. Ukristo ni mwitikio wa mwanzo wa toba na imani inayofatiwa na mwitikio endelevu wa toba na imani. Wokovu si kama matokeo (tiketia ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto), bali uhusiano. Ni maamuzi na uwanafunzi. Inaelezwa katika Agano Jipya 3:5

- utimilifu (tendo lililokamilishwa na matokeo endelevu), Efe. 2:5,8
- inawasilisha (tendo endelevu), 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15
- wakati ujao (matukio yajayo au matukio fulani), Rum. 5:8,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28

katika vitenzi vyote ni vya nyakati:

- kauli (tendo timilifu), Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito

**10:36** mstari huu unathibitishwa na matukio yasiyoonekana!

▣ "mapenzi ya Mungu" Tazama Mada Maalum katika Ebr. 13:21.

▣ "mpate ile ahadi" hii inarejelea ahadi za maagano mapya katika Kristo (yaani, Ebr. 9:15)!

**10:37-38** Hii ni dondo kutoka tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania ya Hab. 2:3-4, lakini kwa vishazi viwili vya mwisho vimerudiwa kwa ajili ya mkazo.

▣ "Yeye ajaye atakuja" Andiko la kimasoreti la kiebrania lina "huyo," lakini tafsiri ya maandiko ya kale ya kiyunani inalifanya pekee, ambalo linadokeza Masihi.

**10:38 "ataishi kwa imani "**

### MADA MAALUMU: Kusadiki, Amini, Imani na Uaminifu katika Agano la Kale (אַמְנָה)

#### I. Maelezo ya awali

Inahitajika kuanza kwamba utumiaji wa dhana ya kithiolojia, ni wa muhimu katika Agano Jipya, hauko wazi kama ulivyoelezewa katika Agano la Kale. Hakika upo, lakini umethibitishwa katika aya na watu muhimu waliochaguliwa.

Vitu ambavyo havikupatana katika Agano la Kale

- Watu binafsi na jamii
- Ukabiliano binafsi na utii wa agano

Imani kwa ujumla ni ukabiliano binafsi na stadi ya maisha ya kila siku! Ni rahisi kuelezea katika maisha ya mfuasi mwaminifu kuliko katika muundo wa kinahau (yaani., usomaji wa neno). Dhana hii binafsi imeelezewa vizuri katika

- Ibrahim na uzao wake
- Daudi na Israel

Watu hawa walikutana/kukabiliana na Mungu na maisha yao yalibadiliwa jumla (sio maisha kamilifu kihivyo, lakini ni kuendelea katika imani). Majoribu yalifichua udhaifu na nguvu ya imani yao ya kukabiliana na Mungu, lakini hatima, uhusiano wa kuamini umeendelea muda wote! Imani ilijaribiwa na kusafishwa, lakini ikaendelea kama ushuhuda kwa moyo wao wa ibada na stadi ya maisha.

#### II. Asili kuu iliyotumika

- אַמְנָה (BDB 52, KB 63)

- KITENZI
  - Shina la neno *Qal* -kutegemeza, kustawisha (yaani 2 Fal. 10:1,5; Ester 2:7, matumizi yasio ya kithiolojia)
  - Shina la neno ni *phal*-kuhakikisha au fanya imara, kuanzisha, kuhakiki, kuwa mwaminifu
    - Kwa watu, Isa. 8:2; 53:1; Yer. 40:14
    - Kwa vitu, Isa. 22:23
    - Kwa Mungu, Kumb. 7:9; Isa. 49:7; Yer. 42:5
  - Shina la neno *Hiphil* –kusimama imara, kusadiki, kuamini

- 1) Ibrahimu alimwamini Mungu, Mwa. 15:6
  - 2) Waisrael katika Misri waliamini, Kut. 4:31; 14:31 (ilikanushwa katika Kumb. 1:32)
  - 3) Waisrael wakamwamini YHWH alipoongea kupitia Musa, Kut. 19:9; Zab. 106:12,24
  - 4) Ahazi hakuamini katika Mungu, Isa. 7:9
  - 5) Yeyote aliyeamini katika Yeye, Isa. 28:16
  - 6) Ukweli wa kuamini kuhusu Mungu, Isa. 43:10-12
  2. NOMINO (JINSI YA KIUME) –kubaki kuwa mwaminifu (yaani., Kumb. 32:20; Isa. 25:1; 26:2)
  3. KIELEZI-kweli kabisa, kweli, nakubali, iwe hivyo (kama vile Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Isa. 65:16; Yer. 11:5; 28:6). Hii ni namna ya liturujia ya neno “amina” katika agano la kale na agano jipya.
- B. **נָמָס** (BDB 54, KB 68) nomino jinsi ya kike, uimarifu, kuwa mwaminifu, kweli
1. Kwa watu, Isa. 10:20; 42:3; 48:1
  2. Kwa Mungu, Kut. 34:6; Zab. 117:2; Isa. 38:18,19; 61:8
  3. Kwenye ukweli, Kumb. 32:4; 1 Fal. 22:16; Zab. 33:4; 98:3; 100:5; 119:30; Yer. 9:5; Zak. 8:16
- C. **עַמּוֹנָה** (BDB 53, KB 62), uimara, kusimama imara, uaminifu
1. Katika mikono, Kut. 17:12
  2. Katika muda, Isa. 33:6
  3. Katika watu, Yer. 5:3; 7:28; 9:2
  4. Kwa Mungu, Zab. 40:11; 88:11; 89:1,2,5,8; 119:138
- III. Matumizi ya Paulo juu ya dhana ya Agano la Kale
- A. Paulo anaegemea uelewa wake mpya kuhusu YHWH na Agano la Kale juu ya ukabiliano wake na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:1-19; 22:3-16; 26:9-18).
  - B. Alipatwa kuungwa mkono na Agano la Kale kwa uelewa wake mpya katika aya mbili muhimu za Agano la Kale ambazo zilitumia asili ya neno (**נָמָס**).
    1. Mwa. 15:6- ukabiliano binafsi wa Abrahamu ulioanzishwa na Mungu (Mwanzo 12) ukasababisha maisha matiifu ya imani (Mwanzo 12-22). Paulo analidokeza hili katika Rum. 4 na Wagalatia 3.
    2. Isa.28:16- wale walioamini ndani yake (yaani., kujaribiwa kwa Mungu na uwekaji wa jiwe kuu la pemberi kwa uthabiti) kamwe hautakuwa
      - a) Rum. 9:33 “aibisha” au “katisha tamaa”
      - b) Rum.10:11, kama ilivyo hapo juu
    3. Hab. 2:4-wale wote wanaomfahamu Mungu Yule aliye mwaminifu lazima waishi maisha ya uaminifu (kama vile Yer. 7:28). Paulo analitumia neno hili katika Rum. 1:17 na Gal 3:11 (pia angalia Hab. 10:38)
- IV. Matumizi ya Petro ya dhana ya Agano la Kale
- A. Petro anaunganisha
    1. Isa. 8:14 – 1 Pet. 2:8 (jiwe la kujikwaa)
    2. Isa. 28:16 – 1 Pet. 2:6 (jiwe kuu la pemberi)
    3. Zab. 118:22 – 1 Petr. 2:7 (jiwe lililokatariwa)
  - B. Alibadilisha lugha ya kipekee ambayo ilielezea Israel kama “jamii iliyochanguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa teule, watu waliomilikiwa ya Mungu mwenyewe” toka
    1. Kumb. 10:15; Isa. 43:21
    2. Isa. 61:6; 66:21
    3. Kut. 19:6; Kumb. 7:6

Na sasa anatumia kwa minajili ya imani ya kanisa katika Kristo (kama vile 1Petr. 2:5,9)

1. Matumizi ya Yohana kwenye dhana hii
  - A. Utumiaji wake kwenye Agano Jpya

Neno “aaminiye” linatokana na neno la Kiyunani pisteuō ambalo pia laweza kutafasiliwa “kuamini,” “sadiki,” au “imani.” Kwa mfano, nomino haionekani kwenye injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi.

Katika Yohana 2:23-25 kuna mashaka kama kwenye uhalisia wa kundi kujitoa kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha wao. Mifano mingine wa utumiaji wa kubabiababia wa neno hili “kuamini” unapatikana katika Yohana 8:31-39 na Mdo. 8:31; 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi kuliko ukubalifu wa awali. Lazima uambatane na mchakato wa uanafunzi (Mt. 13:20-22,31-32).

B. Utumiaji wake ukiwa na vivumishi

1. eis inamaanisha “ndani ya” muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani yao kwa Yesu
  - a. ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
  - b. ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45 48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Flp. 1:29; 1 Petr. 1:8)
  - c. ndani yake (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
  - d. ndani ya mwana (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
  - e. ndani ya Yesu(Yohana 12:11; Mdo. 19:4; Gal. 2:16)
  - f. ndani ya nuru (Yohana 12:36)
  - g. ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
2. ev inamaanisha “katika” kama ilivyo katika Yohana 3:15; Marko 1:15; Mdo. 5:14
3. epi ikimaanisha “katika” au “juu ya” kama ilivyo katika Mat. 27:42; Mdo. 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
5. hoti, likimaanisha “kuamini kwamba,” inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
  - a. Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
  - b. Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
  - c. Yesu ndani ya Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
  - d. Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
  - e. Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
  - f. Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
  - g. Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
  - h. Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
  - i. Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye “Mimi ndiye” (Yohana 8:24; 13:19)
  - j. Tutaishi naye (Rum. 6:8)
  - k. Yesu alikufa na kufufuka tena (1Thes. 4:14)

V. Hitimisho

- A. Imani ya Kibiblia ni ukubarifu wa mwanadamu katika neno/agano la Kiungu. Mungu siku zote huanzisha (yaani., angalia Mada Maalumu: Agano)

1. Toba (angalia Mada Maalum: Toba)
2. Sadiki/amini (angalia Mada Maalum)
3. Utii
4. Usitahimilivu (angalia Mada maalum: Usitahimilivu)

- B. Imani ya Kibiblia ni

1. Uhusiano binafsi (imanzi ya awali)
2. Uthibitisho wa kweli wa Kibiblia (imanzi katika ufunuo wa Mungu, yaani., andiko)
3. Kuwajibika katika utii sahihi (uaminifu wa kila siku)

Imani ya Kibiblia sio tiketi ya kwenda mbinguni au utaratibu wa bima. Ni mahusiano binafsi. Na hili ndio kusudi la uumbaji, mwanadamu aliumbwa katika sura na mfanano (kama vile Mwa. 1:26-27) wa Mungu. Suala hapa ni kwamba “urafiki wa karibu.” Mungu anapendelea ushirika, sio msimamo fulani wa kithiolojia! Lakini ni ushirika na Mungu aliye mtakatifu anataka kuwa wana waonyeshe tabia za “kifamilia” (yaani., utakatifu, kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Petr. 1:15-16). Anguko (kana vile Mwanzo) liliathiri uwemo wetu kuwajibika kwa usahihi. Kwa hiyo, Mungu akatenda kwa niaba yetu (kama vile Eze. 36:27-38), akitupatia “moyo mpya” na “roho mpya”

inayotuwezesha kupertia imani na toba ili kuwa na ushirika na Yeye na kumtii Yeye!  
Yote haya matatu ni muhimu. Yote haya matatu yanapaswa kudumishwa. Kusudi ni kumjua Mungu (wote kwa maana ya Wayunani na Waebrania)

C. Uaminifu wa mwanadamu ni matokea (Agano la Jipy), na sio msingi (Agano la Kale) wa uhusiano na Mungu: imani ya mwanadamu katika uaminifu wake; kusadiki kwa mwanadamu katika kuamini kwake. Moyo wa Agano Jipy katika mtazamo wa wokovu ni kwamba mwanadamu lazima mwanzoni kabisa awajibike na aendelea kuwajibika kwenye neema na rehema ya Mungu, ilioonyeshwa katika Kristo. Alipenda, alitumwa, alitoa, lazima tuwajibike katika imani na kuamini (kama vile Efe. 2:8-9 na 10)

Mungu aliye mwaminifu anawahitaji watu waaminifu kujidhihilisha kwao kwa ajili ya ulimwengu usio na imani na kuwaleta wote kwenye imani binafsi katika Yeye.

■ "wangu" kuna chapisho tata la Kiyunani kama kiwakilishi binasi kilichotangulia. Inasimulia kwa labda "wenye haki" au "imani." Mwandishi wetu ametumia utata wa tafsiri za Andiko la Kimasoreti na toleo la LXX ili kutilia mkazo (1) ujio wa Masihi na (2) hitaji kwa ajii ya waaminio waaminifu.

Katika machapisho ya kale ya Kiyunani A & C, "wangu" yanasisimulia kwa weny haki. Katika toleo la LXX, Peshitta, na ms D\*, "wangu" yanasisimulia imani. Katika P<sup>13</sup>, D<sup>c</sup>, H<sup>c</sup>, K, P na Textus Receptus "wangu" halipo (kufuatia Paulo kuacha dondoo yake kutoka Hab. 2:4 kwenye Rum. 1:17; Gal. 3:11).

Neno "ikiwa" katika sehemu ya pili ya mstari huu ni sentensi amrishi hali daraja la tatu, ambayo humaanisha tendo linalowezekana.

**10:39** mwandishi anafafanua ujasiri wake kwa viongozi wake wastahimilivu (kama vile. Ebr. 6:9-12)!

■ "mionganoni mwa wasitao" Hili ni dokezo la Habakuki 2:4 katika toleo la LXX "ikiwa watarudi nyuma, roho yangu haitapendezwa nao." Jambo kwenye Waebrania kwa ajili ya waaminio ni uaminifu hata mwisho. Hatari kubwa ni "kurudi nyuma".

Swali la fasiri kwenye mstari huu ni nani tungo hii inamrejelea "mionganoni mwa wasitao".

1. Waisraeli siku za Habakuki
2. makundi mawili ya Ebr. 6:1-12, mmoja Myahudi na wayahudi wengine wanaoamini; kundi la wasioamini wamerudi nyuma kutoka katika ushahidi wa injili ya wazi hadi katika kupote
3. waaminio kwa ujumla ambao hawakushikilia uaminifu hata mwisho

Muktadha wa kitabu kama chote na Ebr. 6:9-12 unategemea #2.

■ "kupotea" neno hili mara nyingi limetumika kwa wale ambao hawana uzima wa milele (kama vile. Mt. 7:13; Fil. 1:28; 3:19; 2 The. 2:3; 1 Tim. 6:9; 2 Pet. 2:1,3; 3:7). Hili halifahamiki kama maangamizi ya mwisho ya wasioamini, lakini kupoteza maisha ya kimwili. Sitiari ile ile iliyotumika ni utele kwenye Agano la kale. Moja ya kipengele chake cha siri na maumivu ya milele jehanamu (kama vile. Dan. 12:2; Mt. 25:46).

**NASB**      "bali tumo mionganoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu"

**NKJV**      "bali tumo mionganoni mwa wanaoamini na kutuokoa roho zetu"

**NRSV**      "bali mionganoni mwa walio na imani na kuokolewa"

**TEV**      "badala, tuna imani na kuokolewa"

**NJB**      "tutunzao imani mpaka tuokolewe roho zetu"

Kinyume cha "kupotea" ni uaminifu. Dondoo hii inatoka katika Habakuki na imetumika kwa njia tofauti zaidi kuliko Paulo alivyoitumia kukazia hitaji la kwanza la imani mbali na kazi (kama vile. Rum. 1:17; Gal. 3:11), ambapo Waebrania ametumia kwa ajili ya imani inayoendelea. Maelezo haya yamepangiliwa kwa ajili ya wito wa uaminifu kwenye sura ya 11.

Wito huu mkubwa unaonyesha kwamba imani mara nyingi husababisha mateso, hata kifo. Unatilia mkazo kwamba waaminio hawa wa Agano la kale, hata katikati ya hali ngumu sana (kama vile Ebr. 10:32-33) waendelee katika imani! Mwandishi wa Waebrania anatetea ujasiri wake kwamba viongozi wake walio amini pia wataendelea katika imani hata mwisho.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini ni muhimu kwamba Kristo alitoa sadaka “mara moja kwa ajili ya wote”?
2. Ni lini na nini mwisho kamili wa wokovu?
3. Elezea neno (*telos*) “ukamilifu” katika Agano la kale.
4. Nini kusudi la siku ya upatanisho? Ni kwa namna gani dhabihu ya Agano jipya inasimuliwa katika 10:8?
5. Kwa nini mwandishi wetu anadhani jumbe za Agano la kale zinamhusu Yesu na Roho?
6. Je! utakaso ni mara moja kwa ajili ya matendo yote (Ebr. 10:10) au maendeleo (Ebr. 10:14)?
7. Kwa nini 10:18 ina maana?
8. Orodhesha vitu vya utendaji tunavyotiwa hamasa kuviweka kwenye maisha yetu kwa sababu ya kuingia Kwa Mungu kupitia Kristo.
9. Je mistari ya 26-29 inafundisha ukanaji wa imani?
10. Kwa nini ilikuwa “kukusanyika pamoja” lilikuwa ni tatizo la wapokeaji wa nyaraka hii?
11. Je mateso ni mapenzi ya Mungu? (kama vile. Ebr. 10:32-36).

## WAEBRANIA 11

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b> |                                |   |                               |                                   |
|--|--------------------------------|---|-------------------------------|-----------------------------------|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                       | <b>NKJV</b>                    | <b>NRSV</b>                             | <b>TEV</b>                    | <b>NJB</b>                        |
| Imani  | Kwa Imani Tunaelewa            | Wito wa Mashujaa wa<br>Kike na wa Kiume | Imani                         | Imani ya Kipekee ya<br>Wazee Wetu |
| 11:1-2                                       | 11:1-3                         | 11:1-3                                  | 11:1-2                        | 11:1-2                            |
| 11:3   | Imani na Mwanzo<br>Wa Historia |   | 11:3                          | 11:3                              |
| 11:4-7                                       | 11:4-7                         | 11:4-7                                  | 11:4<br>11:5-6                | 11:4<br>11:5-6                    |
|  | Ibrahimu Mwaminifu             |   | 11:7                          | 11:7                              |
| 11:8-12                                      | 11:8-12                        | 11:8-12                                 | 11:8-10                       | 11:8-10                           |
|  | Tumaini la Kimbingu            |   | 11:11-12                      | 11:11-12                          |
| 11:13-16                                     | 11:13-16                       | 11:13-16                                | 11:13-16                      | 11:13-16                          |
|  | Imani za Mababa<br>Wa Imani    |   |                               |                                   |
| 11:17-22                                     | 11:17-22                       | 11:17-22                                | 11:17-19<br>11:20<br>11:21    | 11:17-19<br>11:20-22              |
|  | Imani ya Musa                  |   | 11:22                         |                                   |
| 11:23-31                                     | 11:23-29                       | 11:23-28                                | 11:23<br>11:24-26<br>11:27-28 | 11:23-29                          |
|  | Kwa imani<br>Walishinda        | 11:29-31                                | 11:29                         |                                   |
|  | 11:30-40                       |   | 11:30-31                      | 11:30-31                          |
| 11:32-38                                     |                                | 11:32-38                                | 11:32-35a<br>11:35b-38        | 11:32-40                          |
| 11:39-40                                     |                                | 11:39-40                                | 11:39-40                      |                                   |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

A. Sura ya 11 ni mfululizo wa mifano ya Agano la Kale la wale ambao walikuwa waaminifu katika hali ngumu (kinyume cha 2 Petro 2 na Yuda). Hizi zimekusudiwa kutia moyo wasomaji wa asili na waaminio wa kila kizazi kudunu katika uaminifu bila kujali mazingira ya kimwili yanayowakabili (kama vile Ebr. 10: 32-39).

B. Pia tazama kwamba hizi sio maungamo ya imani bali maisha ya imani chini ya Agano Jipy. Mwisho wa uaminifu ni ushahidi wa mwanzo wa kweli. Waaminio wanaanza na imani, wanaendelea na imani na kufa katika imani. Mwandishi wa Waebrania anatathmini maisha ya waaminio kutoka katika mwisho wa waaminifu.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 11:1-7

<sup>1</sup> Basi imani ni kuwa na hakika ya *mambo* yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. <sup>2</sup> Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa. <sup>3</sup> Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwu kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanya kwa vitu vilivyo dhahiri. <sup>4</sup> Kwa imani Habilii alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hiyo, ijapokuwa amekufa, angali akinena. <sup>5</sup> Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa aliquwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu. <sup>6</sup> Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeze yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao. <sup>7</sup> Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.

**11:1 "imani"** Hii sio maana ya kithiolojia ya imani bali picha ya utendakazi wake. Neno linatumika mara ishirini na nne katika sura hii. Kutoka katika Agano la Kale, wazo la msingi ni "uaminifu" au "kutumainika." Hii ni kinyume na ukonaji wa Imani. Neno la Kiyunani kwa "imani" (*pistis*) linafasiriwa na maneno matatu ya Kingereza: "imani," "mtazamo wa imani," na "tumaini." Imani ni mwitikio wa kibinadamu kwa uaminifu wa Mungu na ahadi Yake. Tunatumaini katika kutumainika Kwake, sio juu yetu wenywewe. Tabia yake ndio msingi.

|            |  |
|------------|--|
| NASB, NRSV | "kuwa na uhakika juu ya <i>mambo</i> yatarajiwayo" |
| NKJV       | "hakika ya mambo yatarajiwayo"                     |
| TEV        | "kuwa na uhakika wa mambo yatarajiwayo"            |
| NJB        | "uhakika wa Baraka ambazo tunazitarajia"           |

Neno hili la Kiyunani kwa "hakika" (*hypostasis*) kimsingi linamaanisha "kuweka chini" au "kusimama chini ya" hivyo kutoa msingi wa chini au msingi wa kitu. Hivyo ilikuwa na maana mbali mbali pana katika ulimwengu wa kale. Hasa ilikuwa imezoeleka katika maandiko ya Kiyunani ya Kifalsafa kuashiria udhihirisho ulio wazi wa kitu. Ilikuwa vile ambavyo ilikuwa kweli dhidi ya ile ambayo hajajulikana.

1. katika Ebr. 1:3 inarejerea kwa umuhimu
2. katika Ebr. 3:14 inarejerea kwa uhalisia wa ukiri /maungamo ya waaminio
3. katika Ebr. 11: 1 inarejerea kwa injili inayoishi wakati wa sasa lakini isiyotimilika mpaka hapo baadaye Neno hili limepatikana katika mafunjo ya ki-Misri yenye maana "hati ya kiwanja" (kama vile NJB). Kwa namna hii inaaksi matumizi ya Paulo ya Roho kama "makini" (kama vile 2 Kor.1:22; 5: 5; Efe. 1: 4).

Maneno ya Kiyunani yaliyotumika katika LXX yanalipendekeza kufasiriwa *tōhelet* (*The Cambridge History of the Bible*, ukur. 9), ambayo inaashiria "mtazamo wa mgonjwa na kwa ujasiri akisubiria jambo Fulani, hali ya kurajia kwa ujasiri" (yaani tumaini). Kumbuka waandishi wa Agano Jipy walikuwa watu wanaofikiria kwa kwa Kibrania ila wakiandika kwa Kiyunani cha Koine na kutumia desturi za ufasiri wa Tafsiri ya Agano la Kale.

Baadhi wameona maana zinazoleweka zaidi katika muktadha huu zikiaksiwa katika nukuu ya Agano la Kale katika Ebr.10: 38 (Hab. 2: 2-4). Sura ya 11 ni orodha ya mifano ya wale ambao "hawakurudi nyuma." Andiko hili ni kinyume cha kile ambacho wasomaji wa kwanza walikuwa wako katika hatari ya kukifanya.

▣ "hakika" Neno hili linatokea hapa katika Agano la Kale. Linarejerea kwa "uthibitisho wa jaribu." Tungo mbili katika Ebr. 11.1 zinafanana (zote ni kauli tendwa endelevu za wakati uliopo); hivyo, "hakika" na "uthibitisho wa ndani" vinafungwa pamoja na kutoka katika hivyo waaminifu huishi maisha yao. .

■ "mambo yasiyoonekana" Mifano ifuatayo ya watu wanaoishi katika (1) tumaini katika wakati uliopo na matendo yajayo ya Mungu na (2) ujasiri katika ahadi za kiroho za Mungu (kama vile Ebr. 10: 23). Mitazamo yao ya kiulimwengu unaongoza maamuzi yao ya kila siku, sio mazingira, vitu wala ubinafsi. Uhalisia unaoonekana ni sawasawa na uhalisia usioonekana wa kiroho (kama vile Ebr.11:3).

Uhalisia wa mwilini unajulikana kwa fahamu tano na sio umilele bali ipitayo kwa muda tu. Kweli, uhalisia wa milele hauonekani (kama vile Ebr.11:27) na; hivyo lazima kushikiliwa kwa imani. Hatahivyo ni halisia na kweli kwa waaminio kiasi kwamba inaongoza na kuamua vipaumbele vyao.

**11:2**

|      |                                    |
|------|------------------------------------|
| NASB | " <b>kupata kibali</b> "           |
| NKJV | " <b>kupata ushuhuda mzuri</b> "   |
| NRSV | " <b>kupata kibali</b> "           |
| TEV  | " <b>kupata kibali cha Mungu</b> " |
| NJB  | " <b>kutambuliwa</b> "             |

Hii ni sawasawa na matumizi ya Paulo ya "imani" katika Rum. 1:17; Gal. 3:11. Maisha yao ya imani hayakuwaokoa bali yaliweka ushuhuda wa Roho wa Mungu ndani yao (kama vile Yakobo 2: 14-26).

**11:3**

|             |                      |
|-------------|----------------------|
| NASB, NKJV, |                      |
| NRSV        | " <b>ulimwengu</b> " |
| TEV, NIV    | " <b>ulimwengu</b> " |
| NJB         | " <b>zama</b> "      |

Hili ni moja ya maneno mawili ya Kiyunani (*kosmos*, kama vile Ebr. 1: 6 na *aiōn*, hapa) linatumika kuelezea ulimwengu huu unaonekana wa wakati huu. Hii "*aiōn*" inarejerea nyakati za kiroho na majira ikijumuisha vyote ulimwengu wa kiroho na kimwili (kama vile Ebr. 1:2; 6: 5; Rum. 12: 2; 1 Kor. 1:20; 2:6, 8; 3:18; 2 Kor. 4:4; Efe. 1:21; 6:12). Angalia Mada Maalum katika Ebr. 1: 2.

■ "neno la Mungu" Hili sio neno la Kiyunani *logos* bali *rhēma* ambalo linatumika juu ya neno linalozungumzwa. Hii hivyo inarejerea kwa uumbaji wa imani, kwa neno la kuzungumzwa (kama vile Mwa. 1: 3, 6, 9, 14, 20, 24; Zab. 33: 6, 9). Kutoka Ebr.1: 2 tunajua kwamba *logos* ya Mungu ilikuwa msaidizi wa Mungu wa uumbaji (kama vile Yohana 1:1, 10; 1 Kor. 8: 6; Kol.1:16).

Huu ukiri wa imani unafanya mtazamo wa ulimwengu mbao kutokana na huo waamini wanaishi maisha yao ya duniani. Hii haikatai utafiti wao wa kisayansi bali inaiweka katika mtazamo wa imani. Waaminio wanaruhusu sayansi kubaini mbinu za utaratibu wa uumbaji (ufunuo wa asili), lakini ukikiri ukulele wa Mungu pekee (angalia John L. Walton, *The Lost World of Genesis*, ambaye anafunuliwa katika Biblia na katika ukuu katika Yesu Kristo.

■ "hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri" Huu kimsingi sio ukiri wa uumbaji wa *ex nihilo* (kuumba kutoka kwenye hakuna), bali mfano wa uhalisia dhidi ya kutokuwepo kwa uhalisia wa Ebr. 11: 1. Waaminio wanakiri kile ambacho wao binafsi hawajakiona au walichowahi kukutana nacho wakijikita katika ufunuo wa Mungu. Hii sio sana tamko la kithiolojia kama maisha ya imani.

**11:4 "Habili"** Huyu ni mwana wa pili wa Adamu na Hawa aliyeuwawa na ndugu yake, Kaini (kama vile Mwa. 4: 3 na kuendelea).

■ "dhabihu iliyo bora kuliko" Haikuwa aina ya sadaka ambayo Kaini na Habili walivyota iliyosababisha utofauti bali mtazamo (imani) ambayo ilitumika kutoa. Hili haliwezi kuwa andiko la uthibitisho wa ukuu wa sadaka zenye damu.

■ "ijapokuwa amekufa, angali akinena" Hii imenukuliwa katika Mwa. 4:10; Ebr. 12:24. Katika muktadha huu ni ukiri wa imani ambayo inaikabili mauti na kuishangiliza juu yake. Wasomaji wawalikuwa wakirudi nyuma kutoka katika mateso. Lazima kuwa na imani kama Habilii.

**11:5 "Henoko"** Alikuwa mtu wa kwanza baada ya anguko kutoguswa na mauti (kama vile Mwa. 5: 24). Agano la Kale halielezei juu ya mazingira bali linaelezea kwamba "alitembea" pamoja na Mungu.

■ "alihamishwa" Hii inamaanisha "kupelekwa eneo lingine." Hii haimaanishi "ufufuo" bali "kubadilishwa" kama Eliya (kama vile 2 Wafalme 2:11). Kuna utofauti wa wazi katika Biblia

1. watu wanaorejeshewa uhai (kuhuishwa)
2. watu waliochukuliwa mbinguni bila kifo cha mwili (kubadilisha )
3. Yesu akisha kuwa na mwili mpya wa kiroho (ufufuo)

■ "amempendeza Mungu" Hii inafuatia Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani bali Andiko la Kimasoreti lina "kutembea pamoja na Mungu."

**11:6 "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza"** Haya ni maelezo ya msingi ya kipengele hiki cha kifasihi. Sio tu imani ya kuanzia bali imani g'ag'anizi ndiyo inayompendeza Mungu. Mifano yote hii ilibaki ya uaminifu mpaka mwisho bila kujalisha mwisho huo unakujaje. Imani ni njia ambayo wanadamu wanaamini, wanapokea, wanakubali ahadi za Mungu. Wokovu na uanafunzi vyote haviwezekani bila imani. Imani katika Mungu kwa wakati uliopita (uumbaji, ufunuo); imani katika uwepo wa Mungu kwa wakati uliopo (mateso, dhiki hata mauti); Imani katika matendo yaliyohaidiwa na Mungu kwa wakati ujao (wokovu, mbingu).

Kwa ajili ya "isiyowezekana" angalia dokezo kamili katika Ebr. 6:6.

■ "lazima aamini" Neno la Kiyunani *pistis* linatafsiriwa katika maneno matatu ya kingereza: "iman," "amini," na "tumaini." Shabaha sio katika katika kweli za kiufahamu pekee bali kutumaini kibinagsi katika utumainifu wa Mungu; Kuwa na imani katika uaminifu wa Mungu! Sio tu ukiri bali mtindo wa maisha.

Neno "lazima" ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo ambalo linamaanisha "inalazimu," "ni muhimu." Imani ni muhimu!

■ "huwapa thawabu wale wamtafutao" Hii inarejerea kwa mwitikio wa imani ya kwanza na mwitikio wa imani inayoendelea

**11:7 "akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado"** Huu hapa ni utaratibu wa imani. Watakatifu hawa wa Agano la Kale lilifanya kazi kwenye kile ambacho walikuwa wamepokea kutoka kwa Mungu. Matendo yao yalithibitisha imani yao kwamba haikuwa maneno matupu! Unaweza kufikiri dharau na mateso Nuhu aliyyapitia katika jengo kubwa kama meli ile, mbali kabisa na maji, ikiwa na wanyama!

■ "safina" Hii haikuwa meli iliyo tengenezwa tengenezwa tu bali chombo kilichokusudiwa kuelea kama gogo. Neno lilitumika kama "kifua" kama sanduku la agano.

■ "hivyo akauhukumu makosa ulimwengu" Ni kwa namna gani Nuhu aliuhukumu ulimwengu? Kulikuwa na uwezekano wa aina mbili: (1) kwa matendo yake ya imani (2) kwa mahubiri yake (kama vile 2 Pet. 2:5).

■ "akawa mrithi wa haki" Katika Mwanzo 6-8 Nuhu alikuwa mtu wa kwanza katika Biblia kuitwa "mwenye haki" (kama vile 2 Pet. 2:5). Haimanishi kwamba hakuwa na dhambi bali kwamba Nuhu alitembea katika ufahamu aliokuwa nao katika imani na kumtumaini Mungu. Kama Imani ya Ibrahimu ilihesabiwa kwake baadaye kama haki (kama vile Mwa. 15:6), hivyo pia ndivyo alivyokuwa Nuhu. Kwa kujifunza neno juu ya "Haki" angalia Mada Maalum katika Ebr. 1:9.

## ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 11:8-12

<sup>8</sup> Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliiitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako. <sup>9</sup> Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile. <sup>10</sup> Maana alikuwa akiutazamia mji wenyewe misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu. <sup>11</sup> Kwa imani hata Sara mwenyewe alipokea uwezo wa kuwa na mimba; alipokuwa amepita wakati wake; kwa kuwa alimhesabu yeye aliyahidi kuwa mwaminifu. <sup>12</sup> Na kwa ajili ya hayo wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu, *watu wengi* kama nyota za mbinguni wingi wao, na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika.

**11:8 "Ibrahimu.....alitii"** Kwa namna Fulani ni uwakilishi wa mawazo wa maisha ya watu hawa. Agano la Kale ni pekee katika fasihi ya kale katika namna kwamba inaweka kumbu kumbu ya vyote hasi na chanya ya wahusika wake. Ibrahimu alikuwa ni mchanganyiko wa kushangaza wa hofu na imani

1. Hofu
  - a. Mungu alisema iache familia yako; alimchukua baba yake na Lutu
  - b. Mungu aliahidi mtoto; alijaribu kupata mtoto kuitia mijakazi wa Sara na baadaye alijaribu kumuondoa Sara kwa wote Mmisri na mfalme wa Kifilisti ili kuweza kuokoa maisha yake
2. Imani
  - a. Aliondoka Uru
  - b. Aliamini Mungu angempa uzao
  - c. alikuwa tayari kumtoa Isaka (kama vile Mwa. 22)

Mungu hatafuti "watakatifu walio bora zaidi," bali wanadamu wanyonge ambao wataitikia kwake kwa toba na imani na kuishi kwa ajili yake licha ya mazingira.

**11:9 "alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi"** Hili ni neno "alisafiri," ambalo linamaanisha hakuwa na haki kama raia (kama vile Ebr. 11:13).

**11:10 "alikuwa akiutazamia"** Hii ni kauli ya kati elekezi ya kati isiyotimilifu (yenye ushahidi). Aliendelea kutafta!

▣ "mji" Hii ni sitiari iliyozoeleka ya kibiblia (kama vile Ebr. 11:16; 12:22; 13:14; Yohana 14: 2; Gal. 4:26; Ufu. 3:12; 21:2), ambayo inayorejerea eneo la makuzi ya Mungu pamoja na wanadamu tena kama katika Edeni.

Ibrahimu aliishi maisha maisha yake kwa imani asienteengalia uhalisia wake wa sasa. Imani inasema "ulimwengu huu sio nyumbani kwangu"; imani inasema "ahadi za Mungu ni kweli"; imani inasema "uhalisia sio kile ninachokiona bali kile ambacho Mungu anasema"!

## MADA MAALUM: "MIJI" MIWILI KATIKA ISAYA

- A. Isaya 24-27 ni kipengele cha kifasihi kilicho katika hitimisho la mfululizo wa hukumu ya Mungu dhidi ya mataifa yaliyozunguka yapatikanayo katika Isaya 13-23. Hukumu siyo neno la mwisho! Mungu wa neema na rehema ana mpango wa milele, jumuishi na ukombozi (angalia [Mada Maalum: Mpango wa Milele wa Ukombozi wa YHWH](#))!
- B. Sehemu nzima ni tamthilia ya miji miwili.
  1. Miji iliyotengenezwa na wanadamu watoto wa Kaini aliyeanguka, aliyejaribu kutimiza mahitaji yao kiukamilifu kwa rasilimali zake mwenyewe (yaani Mwanzo 4:10-11).
  2. Mji wa Sayuni, ambapo (yaani juu ya mabawa mawili ya makerubi katika sanduku la agano katika patakatifu pa patakatifu pa hekalu katika Yerusalem) na ambapo wafuasi wake waaminifu (Wayahudi na Mataifa) huja kwake na kumuabudu Yeye (kama vile Isa. 2:2-4; 19:18-25; Ebr. 11:10; 12:22; 13:14; Ufu. 21:1-2).
- C. Miji inawakilisha makundi ya watu/mataifa.

**Miji ya kibinadamu**

**Mji wa Mungu**

|   |  |
|---|--|
| Isa. 1:7,8, miji ya Wayudea iliyochomwa                 | Isa. 1:26, mji wa haki, mji wa waaminifu   |
| Isa. 1:21, mji wa uaminifu umekuwa mji wa kahaba        |  |
| Isa. 6:11, miji ya Wayudea ikiharibiwa                  |  |
| Isa. 14:17,21, miji yote ikiharibiwa                    |  |
| Isa. 14:31 miji ya Filistia                             |  |
| Isa. 17:1-3,9, Miji ya Shamu ikiharibiwa                |  |
| Isa. 19:2, miji ya Misri iharibiana yenyewe kwa yenyewe | Isa. 19:18-22, miji ya Misri ikimwabudu Mungu<br>Isa. 19:23-25, Misri yote na Ashuru ikijumuishwa katika watu wa Mungu |
| Isa. 22:2,9, mji wa furaha, Yerusalemu inaanguka        |  |
| Isa. 23, Tiro ikiharibiwa                               |  |
| Isa. 24:1-25:5, uharibifu wa kiujumla wa miji           |  |
| Isa. 25:10-12, Moabu na sehemu yake, ikiwekewa ngome    | Isa. 25:6-9, karamu katika mlima wa Mungu (yaani, miji ikikanyaga Yerusalemu)  |
| Isa. 26:5, mji usioshindwa, yawezekana Moabu            | Isa. 26:1, mji imara, Yerusalemu, unarejeshwa  |
| Isa. 27:10, mji wenye ngome unaanguka                   |  |
| Isa. 29:1, "Ariel" (Yerusalemu)                         |  |
| Isa. 33:2,19, mji wa furaha (Yerusalemu)                |  |
| Isa. 48:2, mji mtakatifu, japo kwa jina langu           | Isa. 45:13, Mji wangu (kama vile Isa. 44:23)   |
|   | Isa. 52:1-6, mji mtakatifu   |
|   | Isa. 60:14, mji wa Bwana   |
|   | Isa. 62:12, mji usiosahauliwa  |
|   | Isa. 66:6, sauti ya shangwe, sauti ya hekalu   |

**11:11 "Sara"** Baadhi ya maandiko ya kale ya Kiyunani (P<sup>46</sup>, D) yanaongeza "tasa." Ni muhimu kwamba hakuna mke wa yoyote kati ya mababa wa imani (isipokuwa Lea) angeshika mimba bila msaada wa Mungu. Pia hakuna mtoto yoyote mzaliwa wa kwanza aliyekuwa mrithi wa ahadi. Mungu alitendea kazi kuonesha kwamba alikuwa yupo katika utendaji!

Sara, kama Ibrahimu, alikuwa mchanganyiko wa hofu na imani. Alimpa Ibrahimu mjakazi wake; pia alizicheka ahadi za Mungu (kama vile Mwa. 18:12).

**11:12 "kama nyota za mbinguni wingi wao, na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika"** Hii ilikuwa ni sehemu ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu kwa Ibrahimu, Isaka na Yakobo (kama vile Mwa. 15:5; 22:17; 32:12). Kumbuka wanawake wao wote (isipokuwa Lea) walikuwa tasa.

▣ "alimhesabu yeye aliyahidi kuwa mwaminifu" Alitenda akijikita katika ahadi ya Mungu na sio uhalisia wa sasa. Tungo hii ni sawasawa na Ebr.10:23 (kama vile Ebr. 6: 17-18). Wasomaji pia wanatakiwa kutenda katika namna hii.

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 11:13-16

<sup>13</sup> Hawa wote wakafa katika imani, wasijapiroea zile ahadi, bali wakaziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi. <sup>14</sup> Maana hao wasemao maneno kama hayo waonyesha wazi kwamba wanatafuta nchi yao wenye. <sup>15</sup> Na kama wangaliikumbuka nchi ile walijotoka, wangalipata nafasi ya kurejea. <sup>16</sup> Lakini sasa waitamani nchi iliyo bora, yaani, ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea mji.

**11:13 "Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi"** Huu ni msingi wa ulinganifu wa watu wa imani wa Agano la Kale katika Sura ya 11 kwa wapokeaji wa Kiyahudi waaminio waliokuwa katika hati hati ya "kurudi nyuma" (kama vile Ebr. 10:38; Pia 2 Pet. 2:20-22).

▣ "akiisha.....aki.....na aki" Tazama maelezo ya aina tatu, tungo zinazorandana!

▣ "walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi" Kibayana, wakaazi wageni ambao hawakuwa na haki kama raia (kama vile LXX Mwa. 23: 4; Zab. 39:12; Flp. 3:20; 1 Pet. 2:11). Uhalisia wa kimwili si wa kweli, uhalisia wa milele. Ulimwengu huu haukuwa makao yao.

**11:15 "kama"** Hii ni sentensi daraja la pili yenye masharti iitwayo "kinyume na kweli." Walitoka nje na hawakurudi!

**11:16** Uhalisia wa kweli ni wa kiroho, kama inavyoonekana katika sitiari ya mji wa mbinguni ambao mjenzi wake na mtengenezaji ni Mungu (kama vile Ebr. 11: 10). Mungu anaitikia kwa imani na tumaini (kama vile Ebr. 2:11; 11:2, 39; 13:14). "Nchi" na "mji" (kama vile Ebr. 11:10) ni sambamba kithiolojia kama sehemu zilizoandaliwa na Mungu kwa ajili ya imani kwa watoto Wake!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 11:17-22**

<sup>17</sup> Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu; na ye ye aliyezipokea hizo ahadi alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee; <sup>18</sup> na am, ye ye aliyeambiwa, Katika Isaka uzao wako utaitwa, <sup>19</sup> akihesabu ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kuzimu; akampata tena toka huko kwa mfano. <sup>20</sup> Kwa imani Isaka akawabariki Yakobo na Esau, hata katika habari ya mambo yatakayokuwa baadaye. <sup>21</sup> Kwa imani Yakobo, alipokuwa katika kufa, akambariki kila mmoja wa wana wa Yusufu, akaabudu akiegemea kichwa cha fimbo yake. <sup>22</sup> Kwa imani Yusufu, alipokuwa amekaribia mwisho wake, alitaja habari za kutoka kwao wana wa Israeli, akaagiza kwa habari ya mifupa yake.

**11:17 "alipojaribiwa"** Mtu anapolinganisha Mwa. 22:1 pamoja na Mt. 6:13 na Yakobo 1:13-14, kuna mgongano wa wazi. Hatahivyo kuna maneno mawili katika Kiyunani kwa "jaribu" pamoja na visawe tofauti. Mtu anatakiwa kujaribu kuelekea uharibifu (*peirazō*) na mwingine anatakiwa kujaribu kwa mtazamo wa uthibitisho na kutiwa nguvu (*dokimazō*). Angalia Mada Maalum katika Ebr. 2: 18.

Mungu anatoa fursa kwa ajili ya watoto Wake kuonesha na kukuza imani zao (kama vile Mwa. 22: 1; Kut. 15:25; 16:4; 20:20; Kumb. 8:2, 16; 13:3; Amu. 2:22; 2 Nyakt. 32:31). Majoribu yanafanyika aidha kikwazo au fursa.

▣ "akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee" Kiwango cha imani ya Ibrahimu inaonekana katika utayari wake kumrudishia Mungu mwana wa ahadi aliyekuwa amemsubiri kwa miaka kumi na tatu (kama vile Yakobo 2: 21).

Matumizi ya *monogenēs* ("wa pekee") kwa kuhusianishwa na Isaka haiwezi kumaanisha "wa pekee" kwa kuwa Ibrahimu alikuwa na watoto wengine. Hakika inamaanisha "mwana wa ahadi," "mwana wa pekee." Hii pia ni maana ya Yohana 3:16.

**11:18** Hii ni nukuu kutoka Mwa. 21:12, ambayo ilikuja kabla ya jaribu!

**11:19 "aweza kumfufua kutoka katika wafu"** Ibrahimu alimtegemea Isaka kurudi pamoja naye (kama vile Mwa. 22:5). Andiko halisemi namna gani hii ingetokea. Waebrania inaelezea kwamba angeweza kuwa ametegemea kuhuishwa.

▣ "kwa mfano" Mwandishi amekuwa akitumia Agano la Kale kama aina ya kuonesha kabla uhalisia wa sasa (kama vile Ebr. 9: 9; 10: 1; 11: 19). Hapa mfano unaonekana kwamba Ibrahimu alimtoa mwanawe wa ahadi pia naye Mungu alimtoa Mwanawe kama kuonesha upendo wake, rehema na neema!

**11:20** Baraka za Isaka na wanawe inapatikana katika Mwa. 27:27 na kuendelea, wakati Baraka ya kwanza ya Yakobo iko katika Mwa. 48: 14 kwa wana wa Yosefu na baadaye Baraka yake ya pili katika Mwa. 49 kwa ajili ya wanawe wengine. Baraka mara baada ya kutoplewa ilikuwa haiwezi kurudishwa. Huu ni mfano wa namna mwandishi anaichukulia historia ya Agano la Kale kwa namna ya kibaguzi (kama Mambo ya Nyakati). Anataja tu vipengele chanya.

**11:21 "akiegemea kichwa cha fimbo yake"** Hii ni nukuu kutoka Mwa. 47:31. Andiko la Kimasoteri lina "kusujudu katika kichwa cha kitanda." Maneno ya Kiebrania kwa ajili ya "kitanda" na "fimbo" yana konsonanti ile ile ya kiebrania, (mth), ni nafasi za baadaye tu za irabu ndizo zinazotofautiana. Kutoka muktadha wa Agano la Kale Yakobo kwa namna Fulani anatambua kutimilizwa kwa ndoto ya Yusufu (kama vile Mwa. 37:5-11), hivyo kutambua mamlaka ya kiraia ya Yusufu kuititia unabii au kumtambua Yusufu kama "mkombozi" wa watu wake kama Musa na Joshua na Masihi ajaye.

**11:22 "akaagiza kwa habari ya mifupa yake"** Ilitakiwa kuchukuliwa Misri na kuzikwa katika Nchi ya Ahadi baada ya safari ya kutoka Misri (kama vile Mwa. 50: 24-25; Kut. 13: 19; Yosh. 24: 32).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 11:23-29**

23 Kwa imani Musa, alipozaliwa, akafichwa miezi mitatu na wazazi wake, kwa sababu waliona kwamba ni mtoto mzuri; wala hawakuigopa amri ya mfalme. 24 Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; 25 akaona ni afadhalii kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo; 26 akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri; kwa kuwa aliyatazamia hayo malipo. 27 Kwa imani akatoka Misri, asiogope ghadhabu ya mfalme; maana alistahimili kama amwonaye yeye asiyonekana. 28 Kwa imani akaifanya Pasaka, na kule kunyunyiza damu, ili yule mwenye kuwaangamiza wazaliwa wa kwanza asiwaguse wao. 29 Kwa imani wakapita kati ya Bahari ya Shamu, kama katika nchi kavu; Wamisri walipojaribu kufanya vivyo wakatoswa.

**11:23 "na wazazi wake"** Toleo laTafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani lina "wazazi," wakati Andiko la Kimasoteri lina "mama" Pekee.

▣ "kwa sababu waliona kwamba ni mtoto mzuri" Desturi za Kiyahudi zinasema Musa alikuwa mtoto mzuri wa sura. Wazazi gani ambao wao huwa hawadhani kwamba mtoto wao ni mzuri? Lakini hii si hoja kithiolojia. Huyu alikuwa maalum, mtoto aliyetumwa na Mungu.

▣ "wala hawakuigopa amri ya mfalme" Mwandishi anataja tungo hii kwa macho yaki akielekezea wasomaji wa kisasa (kama vile Ebr. 11:27).

**11:24 "mwana wa binti Farao"** Haya yalikuwa maelezo ya kiofisi na jina la kimamlaka.

**11:25-26** Tena mwandishi anaweka muuunganiko kwa jaribu linalowakabili wasomaji. Lazima wakaze macho yao kwenye wakati ujao, ahadi ya hakika ya Mungu, sio kwenye mazingira yao ya sasa. Uaminifu kwa Kristo ndio kilele!

**11:27 "akatoka Misri"** Hii inaonekana kurejerea kwa hofu kwa Wamidian, sio safari ya Kutoka (kama vile Kutoka 2: 14-15). Tena mwandishi anachora badara ya kuweka picha ya wazo ya kusudi la Musa.

▣ "kama amwonaye yeye asiyonekana" Wana wa Israeli waliamini kwamba kumuona YHWH kulisababisha mauti kwasababu ya Utakatifu wake (kama vile Mwa. 16: 13; 32: 30; Kut. 3:6; 33:17-23; Waamuzi 6:22-23; 13:22; 1 Wafalme 19:11-13; Mdo.7: 32).

**11:28** Haya ni maelezo kwa Kutoka 12. Hili ni pigo la mwisho lililoathiri Misri yote ikijumuisha nchi ya Gosheni. Hata Waebrania walitakiwa kuyatii maagizo ya Mungu na kutenda kwa imani ili kuachwa na malaika wa mauti.

◻ "wazaliwa wa kwanza" Angalia Mada maalum katika Ebr. 1: 6.

◻ "mwenye kuwaangamiza" Hii inarejerea Malaika wa Mauti (kama vile LXX, Kut.12:23; 2 Sam. 24:16-17).

**11:29** Huu ni muhtasari wa habari inayopatikana katika Kut. 14:21 na kuendelea.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 11:30-31**

<sup>30</sup> Kwa imani kuta za Yeriko zikaanguka, zilipokwisha kuzungukwa siku saba. <sup>31</sup> Kwa imani Rahabu, yule kahaba, hakuangamia pamoja na hao walioasi; kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi kwa amani.

**11:30**"Yeriko zikaanguka" (kama vile Yos. 6:20; 2 Kor. 10:4)

**11:31**"Rahabu, yule kahaba" Huyu Mkanaani alifanyika mwamini (Yakobo 2:25). Hata inawezekana kwamba ni yeze aliye orodheshwa katika ukoo wa Masihi katika Mt.1:5

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 11:32-38**

<sup>32</sup> Nami niseme nini tena? Maana wakati usingenitosha kuleta habari za Gideoni na Baraka na Samsoni na Yeftha na Daudi na Samweli na za manabii; <sup>33</sup> ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa vya simba, <sup>34</sup> walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga. Walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni. <sup>35</sup> Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa. Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufuluo ulio bora; <sup>36</sup> wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani; <sup>37</sup> walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya; <sup>38</sup> (watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao), walikuwa wakizunguka-zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi.

**11:32** "Gideoni" (kama vile Amu. 6-8)

◻ "Baraka"(kama vile Amu. 4-5)

◻ "Yefta"(kama vile Amu. 11-12)

◻ "Daudi"(kama vile 1 Sam. 16: 1)

◻ "Samweli"(kama vile 1 Sam. 1: 20)

**11:33**"haki" Angalia Mada maalum katika Ebr. 1:9.

◻ "walifunga vinywa vya simba" Hii inaweza kumaanisha kwa Samsoni, Daudi, Danieli au kwa tukio lisilojulikana.

**11:34** "walizima nguvu za moto" Hii nirejea ya kuokolewa kutoka katika moto inaweza kurejereha hasa kwa Danieli 3 au kwa baadhi ya tukio la kihistoria lingine lisilojulikana. Kuna uwezekano kwamba kuokolewa huku kunatajwa katika 1 Kor. 13:3. Hatahiyyo kuna tatizo la kimaandiko la Kiyunani linalohusiana na 1 Kor. 13:3. Maandiko ya kale ya Kiyunani ya P<sup>46</sup>, Χ, Α, na Β yana "kwamba nijivune" (*auchēsōmai*) au Ζ, Δ, Φ, Γ, Κ, na Λ yana "kwamba nichomwe" (*kauthēsomai*). Ya kwanza ina (1) maandiko bora na (2) neno linatumika mara kwa mara na Paulo.

◻ "Walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu" (kama vile 2 Kor. 12:9)

**11:35 "Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa"**Ukizungumza kithiolojia huu sio ufufuo bali kurudishiwa uhai (kama vile 1 Wafalme 17: 17-23; 2 Wafalme 4: 31-37).Kumekuwepo tu na ufufuo ambao ulisababisha katika mwili wa milele, Yesu.

**NA SB, NKJV**

**NRSV**

**"ufufuo ulio bora"**

**TEV, NJB**

**"maisha bora"**

Hii ni rejea kwa heshima na ushindi wa kifo cha shujaa. Katika siri ya mpango wa Mungu na mapenzi kwa sayari ilioanguka hii baadhi ya kimwili yamerejeshwa (yaani "wanawake walirejeshewa tena wafu wao kwa ufufuo") na kwa wengine haikutokea. Ya kwanza ni kubwa na ya kupendeza lakini ya pili ni ushuhuda wenye nguvu zaidi wa imani, imani mpaka mwisho.

Hii inaweza kuhusiana na thawabu za kiroho lakini ikiwa hivyo msingi ni moyo wa imani sio mazingira ya kifo cha mtu.Waaminio wanaitwa kuishi kwa ujasiri kwa ajili ya imani yao (kwa YHWH na Yesu). Ushindi ndio uaminifu wao! YHWH ni mwaminifu kwa ahadi zake; Yesu ni mwaminifu katika matendo yake; waaminio lazima watembee katika imani. Kwa "bora zaidi" angalia dokezo kamili katika Ebr.7:7.

**11:36 "dhihaka na mapigo"**Hii yawezekana ni rejea ya kipindi cha Makabayo (kama vile Mak. 1: 62-64; 7: 34; 2 Mak. 6:18-20; 7:1-42).

**11:37 "walipigwa kwa mawe"**Desturi zinasema kwamba Yeremia alipigwa mawe huko Misri na Wayahudi. Kuhani (sio mwandishi wa Agano la Kale) aliyeitwa Zakaria kama kupigwa mawe katika 2 Nyakt. 24: 20-21; Luka 11: 51.

▣**"walikatwa kwa misumeno"**Desturi (*Ascension of Isaiah* 5: 1-14) zinasema kwamba Isaya aliwekwa katikati ya gogo lenye uwazi katikati na kuchanwa kwa msumeno katika pande mbili kwa amri ya Manase.

▣**"walijaribiwa"**Hii inaonekana kuwa kama kauli ya ujumla katikati ya kauli zinazozungumzia mateso na dhiki. Maandiko ya kale ya mafunjo P<sup>46</sup> yanaondoa tungo. Wakosoaji wa maandiko wanazungungumza kwamba kwakuwa tungo zilizoungana "walikatwa katika vibande viwili" (*epristhēsan*) ni sawasawa na hii "walijaribiwa" (*epeirasthēan*) ambayo yawezekana nyongeza ya kiuandishi ilitokea mapema katika desturi za kimaandiko. Kuna utofautiano mwangi katika maandiko ya Kiyunani (mpangilio wa maneno, njeo za maneno). Toleo la andiko la Kiyunani la The United Bible Societies lililohaririwa sehemu ya nne linaondoa tungo.

▣**"waliuawa kwa upanga"** (yaani 1 Wafalme 19:10,14; Yer. 2:30; 26:23).

**11:38** Hii inaelezea historia mbaya ya dhiki kwa wafuasi wa Mungu. Kwanini wasomaji wa sasa washangazwe na dhiki zao?

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 11:39-40**

<sup>39</sup> Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; <sup>40</sup> kwa kuwa Mungu aliquwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.

**11:39 "wakiisha kushuhudiwa"**Hii inaunganisha kurudi 11:2 (kama vile Ebr. 2:11). Maisha ambayo unayaishi kwa imani kati kati ya mazingira magumu, humpendeza Mungu.

**11:40** Mungu anahaidi kuunganisha waaminio wote wa umri, kabilia, taifa, tabaka la kijamii-uchumi kwa elimu zote (kama vile Gal. 3:28; Kol. 3:11). Watu wote hawa wa Agano la Kale walimtzamia Mungu kwa siku mpya. Imekuja katika Kristo huko Bethlehemu na itahitimishwa katika Kristo kutoka Mbinguni akilipua mbingu yake wazi ya mashariki! Ufufuo wake ni tumaini ambalo waaminio wote, wa Agano la Kale na Jipyu wanatazamia katika imani (kama vile 1 Yohana 3:2).

▣ "kilicho bora" Angalia dokezo kamili katika Ebr. 7: 7.

▣ "kukamilishwa" Angalia dokezo kamili katika Ebr. 10:1.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Toa maana ya maneno ya Kiebrania na Kiyunani kwa ajili ya imani.
2. Maneno *fiat* na *ex nihilo* humaanisha nini?
3. Je Mungu hujaribu waaminio (kama vile. Ebr. 11:17 dhidi ya Yakobo 1:13-14)?
4. Je kuna heshima maalum kwa ajili ya mateso? Je Wakristo wote wanateseka?
5. Kwa nini mwandishi wa Waembrania anaandika wito huu wa imani?

## WAEBRANIA 12

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b> |                               |                               |                           |   |
|--|-------------------------------|-------------------------------|---------------------------|---|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                       | <b>NKJV</b>                   | <b>NRSV</b>                   | <b>TEV</b>                | <b>NJB</b>                                  |
| Nidhamu ya Bwana<br>12:1-3                   | Mashindano ya Imani<br>12:1-2 | Maonyo na Maelekezo<br>12:1-2 | Mungu Baba Yetu<br>12:1-2 | Mfano wa Yesu Kristo<br>12:1-4              |
|  | Nidhamu ya Mungu<br>12:3-11   | 12:3-11                       | 12:3-11                   | Maelekezo ya Ki-Baba<br>Ya Mungu<br>12:5-13 |
| 12:4-11                                      |                               |                               |                           |   |
| 12:12-13                                     | 12:12-17                      | 12:12-13                      | 12:12-13                  | Kukosekana kwa<br>Uaminifu<br>Kunaadhibiwa  |
| Onyo dhidi ya<br>Kukataa Neema               |                               |                               |                           | 12:14-17                                    |
| Ya Mungu<br>12:14-17                         |                               | 12:14-17                      | 12:14-17                  | Maagano Mawili                              |
|  | Kundi la Utukufu<br>12:18-24  | 12:18-24                      | 12:18-21<br>12:22-24      | 12:18-29                                    |
|  | Sikia Sauti ya                |                               |                           |   |
|  | Kimbingu<br>12:25-29          | 12:25-29                      | 12:25-27<br>12:28-29      |   |

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "[Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia](#)")**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 12:1-2**

<sup>1</sup> Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile itizingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu,<sup>2</sup> tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuumi wa kiti cha enzi cha Mungu.

**12:1 "Basi"** Mstari wa 1 ni ambababni ya utatu isiyokuwa ya kawaida (*toigaroun*) inayopatikana hapa tu na katika 1 Thes.4:8. Ikijikita katika mifano iliyotangulia ya uaminifu, wasomaji wanatakiwa kuishi maisha ya utauwa ambayo yanasaidia kutia moyo wengine.

■ "wingu" "Wingu" mara kwa mara inatumika katika fasihi ya kundi la watu (kama vile Herodotus VIII.109).

■ "mashahidi" Neno hili linaweza kumaanisha

1. shahidi wa kisheria katika mahakama
2. mtu anayeshirikisha kile ambacho wameona, wanajua au kukipitia
3. mtu ambaye ameuwawa (kuuwawa kama shahidi wa Kristo) kwa imani yao katika Kristo
4. maelezo ya kisitari ya mifano ya imani katika Ebr. 11

Kwasababu ya muktadha wa Ebr. 11 inaonekana kuwa bora zaidi kutochukulia mstari huu kama fundisho kwamba "wao"wanatutazama, lakini kwamba tunatakiwa kuangalia maisha yao ya uaminifu kama mifano ya kufuata (NASB Study Bible, ukur. 1798). Mstari huu mara kwa mara unatumika, nafikiri isivyokawaida kusaidia mawazo mtazamo kwamba kuamini kwetu kwamba waliowapenda wako wanatutazama mbinguni maisha yetu ya hapa duniani. Waaminio hakika watajuana na kuunganishwa katika ushirika Siku ya Ufufuo lakini Biblia iko kimwa juu ya kuunganishwa wakati wa kifo au wao kuwa na uwezo wa kutazama maisha ya waliowapenda duniani.

*The Handbook on The Letters to the Hebrews* cha Ellingworth na Nida, kutoka United Bible Society ,inafasiri kinyume , "Wazo ni kwamba mashujaa wa Agano la Kale wanatuzama namna mwandishi wa Waebrania na wasomaji wake wanavyopiga mbio katika maisha ya Wakristo kwakuwa wokovu wao wenye unaunganishwa na ule wa Wakristo (Ebr. 11:40)" (ukurasa wa 287).

■ "na tuweke" Hii inafasiriwa kama tegemezi lakini kitenzi cha kwanza ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. Tegemezi haitokei mpaka "na tuvipige."

Tazama kile ambacho waaminio wanatakiwa kufanya kwa ufahamu wa mashahidi waaminifu wa Agano la Kale.

1. kuweka kando kila kwazo, Heb. Ebr. 12:1
2. kuweka kando kila dhambi ambacho inatuzinga kwa upesi, Ebr.12: 1
3. kupiga vita vya uvumilivu, Ebr.12:1
4. kukaza macho yetu kwa Yesu, Ebr. 12:2

■ "na tuweke kando" Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopita usio timilifu "weka kando kama vazi" (kama vile Mdo. 7:58). Huu muuundo wa kisarufi unamaanisha hali ya kibinasi (yaani sauti irabu ya kati), ya kimaamuzi (yaani njeo ya wakati uliopita usio timilifu) maamuzi. Hatahivyo Paulo anatumia neno kimafumbo katika namna ya kimaadili (kama vile Rum. 13:12; Efe. 4: 22, 25; Kol. 3:8-9 na "kuvaa " katika Efe. 4:24; Kol. 3:10, 12, 14). Wakristo sharti wawe watendaji wakijijumuishwa katika wokovu wao huru (kama vile Flp. 2: 12-13). Kuna mbio za kukimbia, usuhuda wa kufanya, vita vya kupigana (Flp. 3:12-14)!

NASB "kila kwazo"

NKJV, NRSV "kila uzito"

TEV "kila kitu kilicho katika njia"

NJB "kila kitu kinachovuta chini"

Neno hili kibayana ni "kinene" au "uzito." Wale walioshiriki katika mashindano ya riadha ya Kiyunani walikimbia karibia na uchi. Linatumika

1. kibayana juu ya unene wa mwili
2. ya uzito wa mazoezi ya riadha
3. katika fasihi ya Kiyunani inatumika kama sitiari ya fahari
4. kifalsafa kama kuwa makini juu ya "vyema" kama adui wa "vilivyobora zaidi"

■ "dhambi" Hii aidha inarejerea kwa (1) asili ya dhambi; (2) ishara ya kutenga; (3)kutoamini; au (4) huu muktadha wa pekee unaweza kutoa maana ya nyongeza "kurudi nyuma" (kama vile Ebr. 10:38). Nyaraka hii/kitabu/mahubiri yameelekezwa kwa waaminio wa Kiyunani na Wayahudi wasioamini.

NASB "ituzingayo kwa upesi"

NKJV "ituzingayo kwa upesi"

|                  |                                    |
|------------------|------------------------------------|
| <b>NRSV, NJB</b> | " <b>itukaribiayo kwa karibu</b> " |
| <b>TEV</b>       | " <b>itushikiliyo sisi sana</b> "  |

Maandiko ya kale ya mafunjo P<sup>46</sup> lina "kupoteza kiwepesi." Rejea hii ni kwa chochote ambacho kinachochea mwamini katika mbio za maisha. Inawezekana kuwa dhambi inayojirudia rudia, shauku inayopita kipimo au hata uwepo wa vitu vingi-chochote ambacho kinasababisha wao kuacha vitu ambavyo wamekirimiwa na kuitiwa na Mungu.

■"**tupige mbio**" Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo ambayo inazungumzia vitendo endelevu lakini vikiwa na dokezo la tukio lenye uwezekano wa kutokea. Hii hakika inashabihiana msisitizo wa jumla wa maonyo manne yaliyoelekezwa kwa waaminio wa Kiyahudi "kurudi nyuma" mbali na Kristo na Injili.

■"**kwa saburi**" Sura hii inaweza kuwa tamthiliya ya kiyahudi juu ya maneno "vumilia" (nomino, kama vile Ebr. 10:32, 36), ambayo inamaanisha "ya kujitolea, yenye fujo (tendaji), yenye subira (tendwa) uvumilivu." Kitensi kiko katika Ebr.12:2, 3, na 7 na nomino katika Ebr. 12:1. Hii ni dhamira ya kitabu na hasa sura hizi chache za mwisho zilizosalia!

■"**mashindano**" Neno hili la kiyunani *agōna* ni neno la kimichezo ambalo kutokana na hilo tunapata neno la Kingereza "kuumia kwa maumivu." Mara kwa mara linatumika kama kuanzisha uwanja ya mbio.

■"**yaliyowekwa mbele yetu**" Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo (yenye ushahidi) endelevu. Maisha ya Mkristo mara kwa mara yanatabia kama ya mashindano ya riadha (kama vile 1Kor. 9:25; Flp. 1:30; 2 Tim. 2:5; kukimbia, 1 Kor. 9:24, 26; Gal. 2:2; 5:7; Flp. 2:16; mchezo wa ngumi, 1 Kor. 9:26; 1 Tim. 1:18; 6:12; 2 Tim. 4:7; mieleka, Efe. 6:12).

**12:2 "kukaza macho yetu kwa Yesu"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo ikimaanisha "kuangalia kwa kukaza macho." Kumbuka kwamba tunamuangalia Yeye—sio kundi, sio mazingira, si sisi wenywewe. Hii inaweza fumbo la kuendelea kuweka mkazo katika agano jipya (injili).

|             |  |
|-------------|--|
| <b>NASB</b> | " <b>mwanzilishi na makamilishaji wa imani yetu</b> "                      |
| <b>NKJV</b> | " <b>mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu</b> "                       |
| <b>NRSV</b> | " <b>mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu</b> "                       |
| <b>TEV</b>  | " <b>ambaye kwaye imani yetu humtegemea mwanzo mpaka mwisho</b> "          |
| <b>NJB</b>  | " <b>atuongozaye sisi katika imani yetu na kutuleta katika ukamilifu</b> " |

Neno hili la kwanza (*archēgos*) linatumika katika Ebr.2:10 juu ya Yesu kama mwanzilishi wa wokovu; katika Mdo.3:15 juu ya Yesu kama Mfalme (mwenye kuanzisha) uzima; katika Mdo.5:31 juu ya Yesu kama mfalme (kiongozi) na Mwokozi. Angalia Mada Maalum katika Ebr. 2:10.

Neno la pili (*teleiōtēs*) linamaanisha "yeye anayekamilisha na kufanya kuwa bora." Inarejerea kwa kumaliza kikamilifu kwa Yesu moja kwa moja kazi aliopewa ya ukombozi. Katika namna ni kama cheo cha Alpha na Omega (kama vile Ufu. 1:8), wa Kwanza na wa Mwisho (kama vile Ufu.1:17; 2:8). Mwandishi huyu anatumia dhana ya "kuboresha" mara nyingi katika kitabu (kama vile Ebr.2:10; 5:9; 6:1; 7:11, 19, 28; 9:9; 10:1,14; 11:40; na hapa). Angalia Mada maalum katika Ebr.7:11.

■"**imani**" *Pistis* inaweza kurejerea kwa

1. imani binafsi katika mahusiano na Kristo
2. maisha ya kufanana na Kristo kwa uaminifu
3. mafundisho ya Mkristo (kama vile Yuda 1:3, 20)

Ukristo unatakiwa kukaribishwa, kweli juu ya nafsi kuaminiwa (injili), na maisha ya huyo mtu kuaminiwa (yaani kufanana na Kristo)

■ "kwa ajili ya furaha" Kauli anti yenyе upinzani juu ya ukawaida huumaanisha "habari ya" au "kwasababu ya," lakini pia inaweza kumaanisha "badala ya." Ya kwanza ingereejere A Kristo kuacha mbingu (kama vile Flp. 2:5-11), ya pili kwa furaha Yake wakati wa kumaliza ukombozi na wakati wa kupaa (kama vile Isa. 53:10-12).

■ "iliyowekwa mbele yake" Neno hili linatokea katika Ebr. 12:1 ikirejere kwa mashindano (mbio) ya maisha ya Mkristo. Sasa neno linatumika tena juu ya mashindano ya Yesu kuyatoa maisha yake kwa ajili yetu. Hii ni njia ya mwandishi ya kuhimiza waaminio wa Kiyahudi kustahimili. Yesu alifanya sehemu yake; lazima wafanye yao. Wakati alipomaliza kulikuwa na furaha kuu.

■ "msalaba" Walimu wa Kiyahudi wa siku za Yesu waliona hili kama laana ya Mungu kwasababu ya ufasiri wa Kumb. 21:23. Paulo anasema kwamba Yesu alichukua laana hii ya sheria kwa ajili yetu (kama vile Gal. 3:13).

■ "kuidharau aibu" Msalaba ni ushahidi wa wazi wa upendo wa Baba na Mwana (kama vile Yohana 3:16 na Rum. 5:8). Hili ni neno la Kiyunani lenye nguvu. Yesu aliangalia utukufu ujao unaotokana na mateso yake (kama vile Isa. 53:10-12). Msalaba haukuwa rahisi, gharama ya ukombozi sio rahisi!

■ "naye ameketi" Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu ambayo inasisitiza kitendo kilichokamili pamoja na matokeo yenyе kudumu. Huu ni mwendelezo wa maelezo kwa Zaburi 110:1 (kama vile Ebr. 1:3, 13; 8:1; 10:12).

■ "mkono wa kuume" Hii sio bayana bali sitiari ya kibiblia "sehemu ya nguvu" "mamlaka," au "kudumu kwa utawala" (kama vile Mdo. 2:33-36).

■ "kiti cha enzi cha Mungu" Wanadamu walioanguka wanaweza tu kufikiria utukufu na ufalme wa ulimwengu wa kiroho. Sharti iwekwe katika taswira ya kimwili (miji yenyе dhahadu, malango ya lulu, bahari ya kioo). Mungu ni wa milele aliyeko na atakayekuweko wa kiroho aliye kila mahali mwenye ukuu sana kuliko enzi yoyote (kama vile 1 Wafalme 8:27). Angalia [MADA MAALUM: Lughya ya kibinadamu kumuelezea Mungu](#) katika Ebr. 3:11.

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 12:3-11

<sup>3</sup> Maana mtafakarini sana yeye aliyeyastahimili mappingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia miyoni mwenu. <sup>4</sup> Hamjafanya vita hata kumwagika damu, mkishindana na dhambi; <sup>5</sup> tena mmeyasahau yale maonyo, yasemayo nanyi kama kusema na wana,

"Mwanangu, usiyadharau marudia ya Bwana,

Wala usizimie moyo ukikemewa naye;

<sup>6</sup> Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi,

Naye humpiga kila mwana amkubaliye."

<sup>7</sup> Ni kwa ajili ya kurudiwa mwastahimili; Mungu awatendea kama wana; maana ni mwana yupi asiyerudiwa na babaye? <sup>8</sup> Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa

haramu ninyi, wala si wana wa halali. <sup>9</sup> Na pamoja na hayo tulikuwa na baba zetu wa mwili walitorudi, nasi tukawastahi; basi si afadhali sana kujitia chini ya Baba wa roho zetu na kuishi? <sup>10</sup> Maana ni hakika, hao kwa

siku chache walitorudi kama walivoona vema wenyewe; bali yeye kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake. <sup>11</sup> Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenyе amani.

12:3 "Maana" Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu (yenye ushahidi). Kibayana inamaanisha "kuongeza mpaka" na inatumika kusisitiza uchambuzi wa umakini wa kitu. Watu wa kale waliongeza hesabu juu na kuchora mstari juu kwa ajili ya kutafuta jumla.

■ "yeye aliyeyastahimili" Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati timilifu. Kama Yesu alivyovumilia kutendewa vibaya vile kwa aibu kwa ajili ya wokovu wa waaminio, wanahitaji kuishi kwa ajili yake na waaminio wengine (kama vile 1 Yohana 3:16).

■ "juu ya nafsi zao" Kiwakilishi cha umoja kinapatikana katika fasiri zote za kisasa. Hatahivyo maandiko mengi ya kiyunani ya kale, matoleo na nukuu za mababa wa imani zinasaidia wingi. Ingawa imezoleka kukubalika misingi ya ukosoaji wa maandiko (yaani angalia Kiambatisho cha pili) kwamba maandiko yasiyokuwa ya kawaida magumu zaidi yawezekana ya asili, huu wingi haushabihiani na muktadha huu kabisa. Mada iko wazi inamuhusu Yesu. Haya lazima ilikuwa makosa ya kiuandishi ya kale kutoka miaka ya kwanza mia moja mpaka mia mbili kabla ya maandiko mengi ya mafunjo kuandikwa.

■ "msije mkachoka, mkizimia mioyoni mwenu" Haya ni maneno ya kimichezo ya wakimbiasi wakipumua kwa shida na kuanguka baada ya kukimbia sana mbio. Mwandishi wetu anawatia moyo wakimbiasi hawa waaaminio wa Kiyahudi kuendelea hata kama itakuwa ngumu. Onyo hili linaendelezwa katika Ebr.12:15, 25-29.

**12:4 "Hamjafanya vita hata kumwagika damu"** Wasomaji wa asili walikuwa wamepitia mateso lakini bado walikuwa hawajafikia kifo (kama vile Ebr.10:32 na kuendelea). Yesu alikuwa ameteseka kifo kwa ajili yao, lazima wawe tayari Ikuishi au kufa kwa ajili Yake.

■ "mkishindana na dhambi" Hili nii neno linguine la kimshezo kama lilivyotumika katika Ebr.12:1. Linatafsiriwa kwa kupewa maana ya kifasihi kama "kuumia kwa maumivu." Ile "dhambi" katika muktadha wa kitabu kizima unamaanisha

1. dhambi ya kutoamini ikihusiana na kundi la wayahudi wasiaoamini
2. dhambi ya ukanaji wa imani ("kurudi nyuma" Ebr.10:38) inahusiana na kundi la Wayahudi waaminio

**12:5 "mmeyasahau"** Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati timilifu (yenye ushahidi). Neno hili linatumika hapa katika Agano Jipy. Linaashiria

1. kusahau kwa ukamilifu (yaani msisitizo wa njeo)
2. kusahau kwa kutaka (yaani msisitizo juu ya sauti)

■ " usiyadharau..... Wala usizimie moyo" Hii ni nukuu kutoka katika Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale ya Mithali 3:11-12. Hizi shurutishi za wakati uliopo zote za wakati uliopo zina kiambata kanushi ambacho kinamaanisha siku zote kusitisha kitendo ambacho kinaendelea.

■ "nidhamu ya Bwana" Hii inarejerea kwa "mafunzo ya mtoto." Kuna mbinu iliyotumika katika Ebr. 12:5-11. Hii ni sitiari nyingine inayofahamika. Kama wazazi wa duniani wanavyowapa nidhamu watoto wao, ndivyo pia Mungu anavyowarudi watoto Wake (kama vile 1 Kor. 11:32; Ufu. 3:19).

**12:6 "Maana ye ye ambaye Bwana ampenda, humrudi** "Hii ni moja ya sababu kwanini waaminio wanajihuisha na mateso ya imani (kama vile Mt. 5:10-12; Mdo. 8:1b, 4; 14:22; 2 Thes. 1:4-10).

■ "Naye humpiga kila mwana amkubaliye" Hii nukuu inayoendelea kutoka Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale ya Mithali 3:11-12. Hii ni muhimu sana! Yesu amekuwa akiitwa "mwana" mara kadhaa wakati wahusika wa Agano la Kale wamekuwa wakiitwa "watumishi." Sasa waaminio wa Agano Jipy. wanaitwa "wana" (kama vile Ebr. 12:7-8). Baba huwarudi wana

1. kwa ajili ya makusudi ya baba
2. kwa ajili ya faida ya wana
3. kwa ajili ya faida ya familia nzima

**12:7 "mwastahimili"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo au kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo (muundo wa Kiyunani ule ule). Kwa kuwa Ebr.12:5 ina shurutishi za wakati uliopo mbili, hii yawezekana pia ni kauli shurutishi. Neno linamaanisha "uvumilivu endelevu wa kujitoa" (kama vile Ebr.12:1, 2, 3; 10: 32,36). Jaribu hili litapelekea imani yenye nguvu!

■ "Mungu awatendea kama wana" Maudhui haya ya Mungu kama mzazi anayerudi mtoto yanaweza kuwa maelezo ya Kumb. 8:5 kama ilivyo katika Hosea 11:1-4. Kitensi ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo wa neno ambalo linamaanisha "kuleta kitu kwa Yesu au Mungu mara kwa mara kwa namna ya dhabihu; lakini kuna sauti irabu hapa inayoashiria utayari wa kukabiliwa na wanadamu wenyewe dhambi kwa maana ya kupitia dhabihu ya Kristo.

**12:8 "kama"** Hii ni sentensi daraja la kwanza yenyewe masharti ambayo inadhaniwa kuwa kweli kwa makusudi ya mwandishi. Watoto wote wa Mungu wamepitia nidhamu (kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu).

**12:9 "Baba wa roho"** Hili halihusiani na nadharia za asili ya "nafsi." Inatumika kwa namna hii ya chanzo cha kweli cha maisha haya yote. Mungu analinganishwa na mababa wa duniani (kama vile Ebr. 12:9-10).

■ "na kuishi" Hali ya Baba kuturudi inatuletea uzima wa kweli.

**12:10 "bali huwarudi kwa ajili ya mema ili kwamba tuweze kushirikishwa katika utakatifu Wake"** Kila mwamini anatakaswa wakati wa wokovu (nafasi) na anaitwa kuwa mtakatifu (angalia Mada Maalum katika Ebr. 2:11). Haya ni makusudi ya Mungu kwa mwamini (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:28-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 4:13; 1 Thes. 3:13; 4:3, 7; 1 Pet. 1:15). Waaminio wanaamuriwa kabla kuwa watakatifu (kama vile Efe 1:4). Mara kwa mara inatokea tu katika mazingira ya kuweka nidhamu (kama vile Ebr.5:8 na Rum. 8:17).

**12:11 "huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki"** Maisha ya Mkristo yanatoka katika imani mpaka imani, kutoka katika ukiri (maungamo ya imani) mpaka tabia (maisha ya imani, kama vile Rum.5:3-5; Yakobo 1:2-4).

Kwa ajili ya kujifunza juu ya "Haki" angalia Mada Maalum katika Ebr. 1:9.

**ANDIKO LA NASB (LILILLOBORESHWA) WAEBRANIA 12:12-13**

<sup>12</sup> Kwa hiyo inyosheni mikono iliyolegea na magoti yaliyopooza, <sup>13</sup> mkaifanyie miguu yenu njia za kunyoka, ili kitu kilicho kiwete kisipotoshwe, bali afadhali kiponywe.

**12:12** Haya ni maelezo ya Isa. 35: 3, ambayo yanaweza kuwa historia ya nyuma ya mjadala mzima wa sura ya 12. Wakomavu wanatakiwa kutia nguvu walio dhaifu (wale wanaokaribia kurudi nyuma). "Kutia nguvu" ni ubayana wa "kunyoosha," ambayo ni mbinu ya mstari unaofuata.

**12:13 "yanyosheni mapito"** Haya yanaweza kuwa maelezo ya Mithali 4: 26 katika Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale (LXX) au kwa mithali inayojulikana sana ikitumia "mapito" kama sitiari za Agano la Kale kwa ajili ya haki.

■ "njia za kunyoka" Tingo hii inaweza kueleweka

1. kwa namna yake ya Agano la Kale (kama vile 1 Wafalme 18:21) sitiari ya kati ya hoja mbili kama watu wa Israeli walivyokuwa kati ya YHWH na baali.
2. Katika fasihi ya Kiyunani kujenga bara bara ili kwamba viwete wasianguke na kugiumiza wenywewe (kama vile M. R. Vincent's *Word Studies in the New Testament*, ukurasa wa 1168)

■ "bali afadhali kiponywe" Kutiana moyo wenywewe kunapelekea urejesho (kama vile Gal. 6:1; Yakobo 5:16).

**ANDIKO LA NASB (LILILLOBORESHWA) WAEBRANIA 12:14-17**

<sup>14</sup> Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao; <sup>15</sup> mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo. <sup>16</sup> Asiwepo mwasherati wala asiyemcha Mungu, kama Esau, aliyeuuza urithi wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kimoja. <sup>17</sup> Maana mwajua ya kuwa hata alipotaka baadaye kuirithi baraka, alikataliwa (maana hakuona nafasi ya

**kutubu), ijapokuwa aliitafuta sana kwa machozi.**

**12:14-17** Hili ni onyo la mwisho (kama vile Ebr. 2:1-4; 3:7-4:11; 5:11-6:12; 10:19-39; 12:14-17).

**12:14 "Itafuteni amani"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Katika muktadha wa

1. dhiki itokayo nje
2. kutoamini kati ya marafiki (wasioamini wa Kiyahudi ambao wayahudi waaminio walikuwa bado wakiabudu)
3. mashaka ya ndani (hatari ya "kurudi nyuma" (kama vile Ebr. 10:38) mjadala huu wa amani ni muhimu sana.

Kuna vifungu kadhaa vinavyofanana juu ya "amani."

1. Zab. 34:14, "itafute amani, ifuate"
2. Marko 9:50, "kuweni na amani na kila mtu"
3. Rum. 12:18, "ikiwezekana, ili iwategemee ninyi, kuweni na amani na watu wote"
4. 1 Kor. 7:15, "ikiwa asiyeamini ataondoka....lakini Mungu ametuita sisi katika amani"
5. 2 Tim. 2:22, "ifuatie haki, imani, upendo na amani na wote waliitalo jina la Bwana kwa moyo safi."

**▣ "na utakaso"** Neno hili "utakaso" lazima ihusiane na Ebr. 12:10 na inaunganikana na "nidhamu." Mungu anawarudi waaminio kwa ajili ya utakatifu. Lengo la wokovu ni kufanana na Kristo.

Hii ni nafasi ya utakaso (wa papo kwa papo), bali utokanao na kutembea na Mungu, utakaso (unaoendelea). Injili inawasilisha wokovu na maisha ya Mkristo kwa namna mbili zilizojaa mvutano. Kwa namna moja ni kipawa kitokacho kwa Mungu cha bure kilichokamilika ambacho hupewa mara moja na kuendelea kuwa chako (elekezi), lakini pia ni maisha ya imani, utii, huduma na ibada (shurutishi). Waaminio wengi wanasisitiza kipengele kimoja kwa kuondolewa kwa kingine (Augustine dhidi ya Pelagius; Calvin dhidi ya Arminius). Uhusiano wa waaminio pamoja na Mungu unaanzia pale katika muda wa kushuhudiwa ndani kunakopelekea toba na imani japo sharti pia uteombie katika muda wa kilele cha mauti au Kuja kwa Mara ya Pili; uaminifu, haki, ustahimilivu ni muhimu, ushahidi ulio dhahiri wa wokovu wa kweli.

Linganisha maandiko yafuatayo juu ya utakaso.

#### **Maramoja (elekezi)**

- Mdo. 26:18  
Rum. 15: 16  
1 Kor. 1:2-3; 6:11  
2 Thes. 2:13  
Ebr. 2:11; 10:10,14; 13:12  
1 Pet.1:2  
Ebr. 12:14  
1 Pet. 1:15-16

#### **Endelevu (shurutishi)**

- Rum. 6:19  
2 Kor. 7:1  
Efe. 1:4; 2:10  
1 Thes. 3:13; 4:3-4, 7; 5:2  
1 Tim. 2:15  
2 Tim. 2:21

**▣ "ambao hapana mtu atakayemwona Bwana"** Hii inakinzana: (1) waaminio watamwona Bwana siku moja (kama vile Ayubu 19:25-27; Zab. 17:15; Mt. 5:8; 1 Yohana 3:2; Ufunuo 22: 4) na (2) waaminio hawawezi kumuona Bwana sasa (kama vile Kut. 33: 20; Yohana 1:18; 1 Tim. 6:16; 1 Yohana 4:12).

Hii inaweza kurejerea kwa macho ya kiroho kwa namna ya kurejerea kwa injili. Katika muktadha huu kisitiari inamaanisha "uelewa."

**12:15 "mkiangalia"** Kibayana "kuangalia" (*episkopountes*) ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo inayotumika kwa namna shurutishi. Neno hili limejengwa kwa muundo wa moja ya neno ya mchungaji (kibayana askofu, *episkopos*, kama vile Flp. 1:1; 1 Tim. 3:2; Tito 1:7 na Yesu katika 1 Pet. 2:25). Hapa inaweza kurejerea kwa viongozi wa kanisa au waaminio waliokomaa. Ukanaji wa imani inatakiwa ikabiliwe na ukomavu. Hili kundi la waaminio kwa shauku ikihitajika kutenda katika njia ya ukomavu (kama vile Ebr. 5:11-14).

Mkristo SIO kisiwa (kama vile 1 Kor. 12:7). Ukristo ni timu ya michezo! Neno "mtakatifu" siku zote iko katika wingi (isipokuwa wakati mmoja katika Flp. 4:21, ambapo linatumika kwa namna ya jamii). Tu walinzi wa ndugu zetu. Hatutakiwi kubakiza nguvu ya kutiana moyo. Tunapewa na kukirimiwa kwa ajili ya afya ya kundi zima.

■"**mtu asiipungukie neema ya Mungu**" Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo ikitumiwa katika namna shurutishi "kupungukiwa na neema ya Mungu." Neno hili linatumika katika Ebr. 4:1 katika namna ya "kushindwa kufikia," japo katika mstari huu kauli "mbali" (*apo*) inatengeneza kauli tungo "kuangusha na kitu ambacho mwanzoni kilikuwa kinakushikilia" (kama vile Ebr.6:4-6; 10: 23, 38-39; 12:25). Ukanaji wa imani ulikuwa halisi katika hali ya kidesturi. Angalia MADA MAALUM:UKANAJI WA IMANI (APHISTĒMI) katika Ebr.3:12. Au kama nilivyoshikilia, kuna makundi mawili yakielezwa:(1) Wayahudi waaminio walioko katika hatari ya "kurudi nyuma" (Ebr. 12:15) na (2) Wayahudi wasioamini wakisha kuelewa vizuri injili katika maisha na shuhuda za wenza wao wa Sinagogi waaminio, walimkataa Yesu (Ebr.12:25). Nadharia yoyote ni sawasawa, ukweli unabakia kwamba wokovu sio matokeo. Ni zaidi ya mwitikio wa kuanzia. Maonyo ni ya kumaanishwa, yenye changamoto na halisi. Katika muktadha huu ni wito kuwasaidia waaminio wengine walio katika hatari ya "kurudi nyuma" (kama vile Ebr. 10:38).

■"**shina la uchungu**" Haya yanaweza kuwa maelezo ya Kumb. 29:18 katika tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale, ambayo ilionya watu wa Mungu kuhusu hatari za kuabudu sanamu, wote mmoja mmoja na kwa ujumla. Israeli wote haikuwahi kupatana na Mungu, bali mabaki waaminio waaminifu tu. Tungo "shina la uchungu" katika Kumbu kumbu la Torati "ambaye moyo wake unageukla mbali leo kutoka kwa Bwana Mungu wetu."

■"**wakatiwa unajisi kwa hilo**" Uwepo wa mtu najisi ulipelekea kuathiri kundi zima. Imani yetu, matendo na mitazamo inawashawishi wengine. Ni uwajibikaji mzuri kiasi gani!

**12:16 "Esau"** Anakuwa mtu muovu sana katika desturi za dini za kiyahudi (kama vile *Jubilees* 25: 1, 8 na *Genesis Rabba* 70d, 72a). Muktadha huu hatahivyo unamtumia kwasababu alijua ahadi za Mungu lakini hakutenda juu yake.

**12:17 "baraka"** Baraka za mababa wa imani zingeweza kuondolewa. Hii inajumuisha dhana ya Kiyahudi ya nguvu ya neno linalozungumzwa (kama vile Mwanzo 1 na Isa. 55:10-12).

■"**maana hakuona nafasi ya kutubu**" Katika muktadha wa Agano la Kale hii inarejerea kwa huzuni baada ya Isaka, baba yake, alimbariki kaka yake Yakobo na Baraka haikuweza kuondolewa. Mwandishi analitumia hili kama onyo kwa wapokeaji wa barua. Anataka kufanya maamuzi kwa Kristo sasa wakati kuna muda na baadaye kustahimili katika uhusiano huo pamoja na Kristo kwasababu kuna nafasi ya pili (kama vile Ebr. 6: 6;10:26).

### **MADA MAALUM: TOBA (AGANO LA KALE)**

Dhana hii ni ya muhimusana lakini ni vigumu kuitolea ufanuzi. Wengi wetu tunao ufanuzi ambaao unatokana na ushirikishwaji wa kimadhehebu. Hata hivyo, mara nyingi huu "mwelekeo" wa ufanuzi wa kithiolojia unalazimisha maneno kadhaa ya Kiebrania (na Kiyunani) amabayo kwa upekee wake hayamaanishi "elekeea" ufanuzi huu. Lazima ikumbukwe kwamba waandishi wa kitabu cha Agano la Kale (isipokuwa Luka) walikuwa wanafikra wa Kiebrania walitumia maneno ya lugha ya Koine ya Kiyunani, hivyo sehemu ya kuanzia ni ile ya maneno yenyewe ya Kiebrania, ambayo kimsingi ni mawili.

1. *nacham* ( BDB 636, KB 688)
2. *shub* ( BDB 996, KB 1427)

Neno la kwanza, *nacham*, kiuhalisia linaonekana kumaanisha "kueleza pumzi ya ndani" linatumika katika maana kadhaa.

- a. "kupunzika" au "kufariji" (m.f. Mwa. 5:29; 24:67; 27:42; 37:35; 38:12; 50:21; mara nyingi linatumika katika majina, kama vile 2 Fal. 15:14; 1 Nya. 4:19; Neh. 1:1; 7:7; Nahumu 1:1)
- b. "kuhuzuka" (m.f. Mwa. 6:6,7)

- c. "kughairi" (m.f. Kut. 13:17; 32:12,14; Num. 23:19; Ayubu 42:5-6)
- d. "huruma" (m.f. Kut. 32:36)

Tambua kwamba haya yote yanahusisha hisia za ndani! Hapa ndipo palipo na ufubuzi: hisia za ndani ambazo huelekea katika tendo. Badiliko hili la tendo mara kwa mara huelekezwa kwa wengine, lakini pia kuelekea kwa Mungu. Ni hili badiliko la mtazamo na tendo kumwelekeea Mungu ambalo hukazia neno hili kwa umuhimu huu wa kithiolojia. Lakini hapa ungalifu lazima ufanyiwe kazi. Mungu anasemekana "kutubu" (kama vile Mwa. 6:6, 7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:11, 35; Zab. 106:45), lakini hili si matokeo ya sononeko juu ya dhambi au makosa, bali ni njia ya kiaandiko ya kuonyesha huruma ya Mungu na uangalifu (kama vile Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Zab. 110:4; Yer. 4:27-28; Eze.24:14). Adhabu istahiliyo dhambi na uasi inasamehewa ikiwa mtenda dhambi ameamua kwa usahihi kuongoka kutoka dhambini kwake/kwao na kurudi kwa Mungu. Huu ni uthamanisho mpya wa maisha.

Neno la pili, *shub*, linamaanisha "kurudi" (kurudi kutoka, kurejea, kurudi kwa). KITENZI *shub* (BDB 996, KB 1427) kimsingi kinamaanisha "kugeuka" au "kurejea tena" Kitensi hiki kinaweza kutumika kwa

1. kumuelekeea Mungu, Hes. 14:43; Yos. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; 1 Sam. 15:11; 1 Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4
2. kumrudia Mungu, 1 Fal. 8:33,48; 2 Nya. 7:14; 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yn. 4:6,8-11 (tambua hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
3. YHWH anamwambia Isaya hapo awali kwamba Yuda haitaweza/isengeweza kutubu (kamavile Isa. 6:10), lakini si mara ya kwanza katika kitabu hiki, Yeye anawahita warudi Kwake.

Toba si hisia nyingi sana kama ulivyo mtazamo kumwelekeea Mungu. Huu uthamani mpya wa maisha kutoka upekee kuelekea Kwake. Hii inadokeza utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Si ukomavu kamili kuihusu dhambi, bali ukomavu wa uasi unaojulikana! Huu ni ukinyume wa matokeo yaliyo kitovu Anguko la Mwanzo 3. Hii inadokeza kwamba sura na ufanano wa Mungu (Mwa. 1:26-27), ingawa iliharibika, umerejeshwa! Ushirika pamojana Mungu kuititia mwanadamu aliyeanguka inawezakana kurejeshwa tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi inamaanisha "badiliko la tendo," ambapo "toba" katika Agano Jipyaa inamaanisha "badiliko la fikra" (tazama Mada Maalum: Toba [AJ]). Yote haya ni muhimu kwa ajili ya toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kwamba toba ni vyote tendo la awali na hatua endelevu. Tendo la awali linawezakuonekana katika Marko 1:15; Matendo ya Mitume 3:16 na 19; 20:21, ambapo hatua endelevu inawenza kuonekana katika 1 Yohana 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba si uchaguzi (kama vile Luka 13:3,5)!

Ikiwa ni kweli kwamba mahitaji ya maagano mawili ni "toba" na "imani" (m.f. Mt. 3:2; 4:17; Maro 1:4,15; 2:17; Luka 3:3,8; 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3), kisha neno *nachamr* linarejea juu ya hisia zenye nguvu za kutambaua dhambi ya mtu na kugeuka kutoka ndani ya hiyo dhambi, ambapo neno *shub* lingaliweza kurejea juu ya kurudi toka dhambini na kumwelekeea Mungu (moja ya mfano wa haya matendo ya kiroho uko katika Amosi 4:6-11, "hamkunirudia mimi" [mara tano] ana Amosi 5:4,6,14, "Nitafuteni mimi. . .Mtafuteni Bwana. . .Tafuteni mema, wala si mabaya").

Mfano wa kwanza ulio mkuu wa nguvu ya toba ni ile dhambi ya Daudi's sin with Bathsheba (kama vile 2 Samuel 12; Zaburi 32,51). Kulikuwa na matokeo endelevu kwa Daudi, familia yake, na Israeli, lakini Daudi alirejeshwa katika ushirika pamoja na Mungu! Hata Manase aliyekuwa dhalimu aliweza kutubu na kusamehewa (kama vile 2 Nya. 33:12-13).

Maneno yote haya yanatumika kwa usawa katika Zab. 90:13. Lazima kuwepo na utambuzi wa dhambi na nia iliyokusudiwa, kurudi kwa mtu binafsi kuto dhambini, pamoja na shauku ya kumtafuta Mungu na haki Yake (kama vile Isa. 1:16-20). Toba ni hatua tambuzi, hatua binafsi, na hatua ya kimaadili. Haya yote yanahiajika, yote ni kwa ajili ya kuanza uhusiano mpya pamoja na Mungu na kuushikilia uhusiano huo mpya. Hisia za ndani za majuto hurejesha ndani ya utele wa uaminifu kwa Mungu na kwa ajili ya Mungu!

■ "kwa machozi" Hii inatoka katika Mwanzo 27:34 na 38

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 12:18-24**

<sup>18</sup> Maana hamkufikilia mlima uwezao kuguswa, uliowaka moto, wala wingu jeusi, na giza, na tufani, <sup>19</sup> na mlia wa baragumu na sauti ya maneno; ambayo wale walioisikia walisihi wasiambiwe neno lo lote lingine; <sup>20</sup> maana hawakuweza kustahimili neno lile lililoamriwa, Hata mnyama akiugusa huo mlima atapigwa kwa mawe. <sup>21</sup> Na hayo yaliyoonekana jinsi yalivyokuwa ya kutisha, hata Musa akasema, Nimeshikwa na hofu na kutetemeka. <sup>22</sup> Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyangi, <sup>23</sup> mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika, <sup>24</sup> na Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili.

**12:18-21** Sehemu hii ni maelezo ya kutolewa kwa sheria ya Musa juu ya Mlima Sinai (kama vile Kut. 19:16-25; Kumb. 4:11-14).

■ "wingu jeusi, na giza" Hii inawezekana ni maelezo ya Kumb. 5:22.

**12:19 "mlio wa baragumu"** Sauti ya Mungu ilipigwa kama Baragumu (kama vile Kut. 19:16, 19; 20:18)

■ "walioisikia walisihi wasiambiwe neno lo lote lingine" Nguvu kubwa ya YHWH juu ya Mlima Sinai iliogopesha watu (kama vile Kut. 20:19; Kumb. 5:22-27; 18:16).

**12:20 "Hata mnyama akiugusa huo mlima atapigwa kwa mawe"** Hii ni sentensi daraja la tatu lenye masharti. Ni maelezo mengine juu ya utakatifu wa kuvutia wa Mungu ukishuka juu ya Mlima Sinai (kama vile Kut. 19:12-13).

**12:21 "Nimeshikwa na hofu na kutetemeka"** Hii ni nukuu kutoka Kumb. 9:19 ambayo inarejerea ndama wa Haruni wa dhahabu. Tafsiri za kiyahudi za maandiko zilitumia tungo hii kwa hofu ya Musa ya Mungu katika Mlima.

**12:22 "Bali ninyi mmeufikilia"** Huu ni ulinganifu mkuu. Hawa wasomaji waaminio hawaamini katika agano la Mlima Sinai bali katika agano Jipya, Yerusalemu ya kimbingu, Mlima Sayuni mpya, mji mpya. Katika Gal. 4:21-31. Paulo anatumia masimilizi yale yale akitumia milima ya Agano la Kale (Mlima Sayuni dhidi ya Mlima Sinai).

■ "mlima Sayuni" Mwandishi analinganisha agano la kwanza katika mlima Sinai na agano Jipya pamoja na mji mpya wa kimbingu (kama vile Ebr. 11:10, 16; 13: 14; Ufu. 3:12; 21:2,10).

■ "Mungu aliye hai" Hii ni mbinu juu ya jina la kiagano la Mungu, YHWH ambalo ni muundo wa kitenzi cha Kiebrania "kitenzi kisaidizi." YHWH anaishi milele, pekee aishiye. Katika Agano la Kale anaapa kwa nafsi yake mwenyewe, "Mungu aishiye." Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika Ebr. 2:7.

**12:23 "kanisa la mzaliwa wa kwanza"** Kwasababu ya Kut. 4: 22 baadhi ya wafasiri wanaelewa rejea kwa wana wa Israeli wa Agano la Kale japo muktadha unadai kwamba ieleteke kama watu wote wa imani (kama vile Ebr. 11:40). Ile "mzaliwa wa kwanza" ni rejea kwa Kristo, "mzaliwa wa kwanza"

1. wa ndugu wengi (sura ya Mungu, Rum. 8:29)
2. wa uumbaji wote (sura ya Mungu, Kol. 1:15)
3. wa waliokufa (Kol. 1:18 na 1 Kor. 15:20, 23 [malimbuko ya kwanza] )

Angalia njia zote Agano Jipya linalelezewa katika aya hii.

1. Mlima Sayuni
2. Mji wa Mungu aliye hai
3. Yerusalemu ya mbinguni
4. malaika wasio na idadi

For Kwa ajili ya "kanisa" angalia Mada Maalum katika Ebr. 2:12. Kwa "mzaliwa wa kwanza" angalia Mada Maalum katika Ebr 1:6.

■ "**walioandikwa**" Biblia inazungumzia juu ya vitabu viwili vya Mungu (kama vile Dan.7:10 na Ufu. 20:12). Moja ni kitabu cha uzima (kama vile Kut. 32:32; Zab. 69: 28; Dan. 12:1; Luka 10:20; Flp. 4:3; Ufu. 3:5; 17: 8; 20:12,15; 21:27). Kingine ni kitabu cha kumbu kumbu (kama vile Zab. 56: 8; 139:16; Isa.65:6; Mal. 3:16). Ya kwanza ni kwa ajili ya waaminio (kama vile Ufu. 14:13). Hizi ni sitiari kwa ajili ya kumbu kumbu la Mungu. Angalia [Mada Maalum: Vitabu Viwili vya Mungu](#).

■ "**Mungu mwamuzi wa watu wote**" Agano la Kale mara kwa mara linachukulia Mungu kama Hakimu (kama Mwanzo 18:25; Zab.50:6; 96:13; 98:9; Isa.2:4; 51:5; Yer. 11: 20; Omb. 3:59; Ezek.7:3,27). Kuja kwa Masihi pia kunachukuliwa kama Hakimu (kama vile Isa.11:3-4;16: 5). Baba ameweka hukumu yote kwenye mikono ya Mwana (kama vile Yohana 5:22-23, 27; 9:39; Mdo.10: 42; 17:31; 2 Tim. 4:1; 1 Pet. 4:5).

■ "**na roho za watu wenye haki waliokamilika**" Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu "ikifanywa kamilifu na Mungu na matokeo kuendelea." Kwasababu ya Ebr.11:40 hii inaweza kurejerea kwa watakatifu wa Agano la Kale wa sura ya 11 na waaminio wote kabla ya kuja kwa Kristo.

Kwa "ukamilifu" angalia dokezo katika Ebr. 10:1.

**12:24 "Yesu mjumbe"** Yesu kuhani mkuu na dhabihu (1) anasimama mbele za Baba kwa ajili yetu na (2) kuleta agano bora zaidi (kama vile Ebr. 7:22; 8:, 6, 9-10; 9:15; Yer. 31:31-34; Ezek.36:22-36).

■ "**na damu ya kunyunyizwa**" Hii ilikuwa ndiyo njia maagano ya Agano la Kale yalikuwa yanaanzishwa (kama vile Ebr. 9:19; 10: 22; 1 Pet.1:2).

■ "**kuliko**" Angalia dokezo kamili katika Ebr.7:7.

■ "**damu ya Habili**" Damu ya Habili ililia kwa ajili ya kisasi; damu ya Yesu inalia kwa ajili ya rehema, msamaha na upendo.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 12:25-29

<sup>25</sup> Angalieni msimkatae yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyewaonya juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye atuonyaye kutoka mbinguni; <sup>26</sup> ambaye sauti yake iliittemesha nchi wakati ule; lakini sasa ameahidi akisema, Mara moja tena nitatetemesha si nchi tu, bali na mbingu pia. <sup>27</sup> Lakini neno lile, Mara moja tena, ladhihirisha kuhamishwa vile viwezavyo kutetemeshwa, kama vitu vilivyoumbwa, vitu visivyoweza kutetemeshwa vikae. <sup>28</sup> Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho; <sup>29</sup> maana Mungu wetu ni moto ulao.

**12:25 "Angalieni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hili ni neno la Kiyunani tofauti kuliko lile lililotumika katika Ebr.12:15. Onyo hili hili linapatikana katika Ebr. 3:12. Baada ya kutiwa nuru na ukuu wa agano jipya katika Kristo, ni muhimu mtu aitikie sawasawa. Kuna hatari (kwa wote wasioamini na waaminio) katika kuijua kweli na kuitendea kazi.

■ "**msimkatae yeye**" Haili ni moja ya maonyo makubwa mawili. Lingine likiwa ni,"kutorudi nyuma." Hii ni kauli ya kati tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu (yenye ushahidi). Sharti kufanya maamuzi mazuri. Utafanya nini na Yesu, mwanzilishi na mkamilishaji wa imani?

■ "**kama**" Hii ni sentensi daraja la kwanza yenye masharti ambayo inadhaniwa kuwa kweli kutoka katika mtazamo wa mwandishi au kwa ajili ya makusudi yake ya kifasihi. Tena jukumu la kufurahisha la kukataa agano kuu zaidi na mtu nishabaha ya fasiri.

**12:26 "sauti Yake ilitikisa nchi"** Hii ni rejea kwa kutolewa kwa sheria ya Musa juu ya Mlima Sinai (kama vile Kut. 19:18-19), lakini ni marudio kutoka tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale ya Hagai 2:6. Unabii huu unazungumzia kutikisika kupya kwa mbingu nan chi kuunganishwa kwa hekalu la baadaye baada ya kutoka Misri (kama vile Hag. 2:6-9). Hekalu Jipyä litapokea utukufu. Agano Jipyä litakuwa bora kuliko la kwanza. Hekalu Jipyä litaleta amani. Maelezo haya yanatabiri agano jipyä.

**12:27 "Mara moja tena"** Nchi inapita. Sifikirii kama Mungu ataiumba tena upya (kama vile 2 Pet. 3:10) zaidi sana ndivyo ilivyo, bila laana ya Mwanzo 3:14, 17; Zek.14:11; Ufu.22:3. Biblia inaanza na Mungu, mwandamu na wanyama (kama vile Isa.11:6-9) katika mazingira ya bustanini (kama vile Mwa. 1-2) na ndivyo inavyoisha pia (kama vile Ufu.21-22).

**12:28 "ufalme usioweza kutetemeshwa"** Hii inarejerea kwa asili ya agano Jipyä. Ni agano la Mwisho na la kudumu kati ya Mungu na watu wake.

**▣ "ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho"** Maelezo haya yanaelezea kwa uzuri mwitikio waaminio wa agano Jipyä: maisha ya huduma kwasababu ya shukrani kwa neema isiyoltinganishwa ya Utatu wa Mungu (kama vile Ebr. 13:15, 21; Rum.12:1-2). Tuliokolewa ili tutumikie, kutumikia familia ya imani (kama vile 1 Kor.12:7; Efe. 4:12).

## MADA MAALUMU: UFALME WA MUNGU

Katika Agano la Kale Mungu alifikiriwa kama mfalme wa Israel (kama vile 1 Sam. 8:7; Zab. 10:16; 24:7-9; 29:10; 44:4; 89:18; 95:3; Isa. 43:15; 44:6) na Masihi akawepo kama mfalme aliyedhaniwa/kutegemewa (kama vile Zab. 2:6; Isa. 9:6-7; 11:1-5). Na kuzaliwa kwa Yesu pale Bethlehemu (mwaka wa 6-4 K.K) ufalme wa Mungu ukavunjiliwa ndani ya historia ya mwanadamu kwa nguvu mpya na ukombozi ("Agano Jipyä," kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:27-36).

1. Yohana Mbatizaji akatangaza kukaribia kwa ufalme (kama vile Mt. 3:2; Mk 1:15).
2. Yesu wazi wazi akafundisha kwamba ufalme ulikuwa tayari ndani yake mwenyewe na mafundisho yake teachings (kama vile Mt. 4:17,23; 10:7; 12:28; Luka 10:9,11; 11:20; 17:21; 21:31-32). Na bado ufalme unakuja (kama vile Mt. 16:28; 24:14; 26:29; Marko 9:1; Luka 21:31; 22:16, 18).

Katika usambamba wa mihitasari kwenye Marko na Luka tunakipata kifungu, "ufalme wa Mungu." Hii ilikuwa mada ya kawaida katika mafundisho ya Yesu yakijumisha utawala wa Mungu uliopo kiatika mioyo wa watu, ambao siku moja utakamilishwa katika ulimwengu wote. Huu unaakisishwa kwenye maombi ya Yesu katika Mt.6:10. Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, alipendelea kifungu kile ambacho hakitumii jina la Mungu (yaani., Ufalme wa Mbinguni), wakati Marko na Luka, akiwaandikia watu wa mataifa, anatumia usanifu wa kawaida, akiweka jina la Uungu.

Hiki ni kile kifungu cha mfano katika mihitasari ya injili. Hotuba za kwanza na za mwisho za Yesu, na zaidi mafumbo yake, yanashughulika na mada. Zinarejerea utawala wa Mungu katika mioyo ya wanadamu sasa! Inashangaza kuona kwamba Yohana anatumia kifungu hiki mara mbili tu (na kamwe sio kwenye mafumbo ya Yesu). katika injili ya Yohana "uzima wa milele" ni sitiari muhimu.

Mvutano na kifungu hiki unasababishwa na ujio mara mbili wa Kristo, Agano la Kale linatazamisha kwenye ujio mmoja wa Masiha wa Mungu kama afisa wa kijeshi, ujio wa kitukufu-lakini Agano Jipyä linaonyesha kuwa alikuja kwanza kama mtumishi mwenye mateso katika Isaya 53 na mfalme mnyenyekevu katika Zak. 9:9. Enzi mbili za Kiyahudi (angalia mada maalumu: Enzi hii na Enzi inayokuja), enzi ya uovu na enzi mpya ya haki, zimeingiliana. Kwa sasa Yesu anatawala ndani ya mioyo ya waumini, lakini siku moja atatawala juu ya uumbaji wote. Atakuja kama Agano la Kale lilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19)!waamini wanaishi ndani ya ulimwengu wa Mungu "uliotayari" dhidi ya "ule ambao bado" (kama vile Gordon D. Fee na Douglas Stuart's *How to Read The Bible For All Its Worth*, kurasa za. 131-134).

**12:29 "moto ulao"** Hii inaweza kuwa rejea ya Mlima Sinai (kama vile Kumb. 4: 24). Huwa tunajaribu kusahau ni kwa nani tunaitikia (kama vile Ebr. 10:31). Moto unaweza kutusafisha na kutufanya safi au kutuharibu kabisa kabisa. Atakuwa Baba yetu wa Mbinguni.Tunachokifanya na kuendelea kukifanya pamoja na Yesu ni kiashiria. Amini! Subiria hapo!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha tabia za watu wa sura ya 11 na 12:18-29 ambao tunajifunza kwao.
2. Je mstari wa 1 unafundisha kwamba wafu wanayatazama maisha ya walio hai?
3. Kwanini mwandishi anatumia sitiari nyingi za kimichezo katika sura hii?
4. Nini kilikuwa kusudi la sura hii kwa kuhusianisha na kitabu kizima?
5. Ni nini kilele cha makusudi ya Mungu katika maisha yetu? (kama vile Ebr. 12:10, 28)

## WAEBRANIA 13

| <b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b> |                                      |                                      |                       |   |
|--|--------------------------------------|--------------------------------------|-----------------------|---|
| <b>UBS<sup>4</sup></b>                       | <b>NKJV</b>                          | <b>NRSV</b>                          | <b>TEV</b>            | <b>NJB</b>                                |
| Huduma<br>Mwisho                             | Kuhitimisha                          | Kuhitimisha                          | Namna ya              | Nasaha za                                 |
| Inayomfurahisha<br>Mungu                     | Mwongozo wa<br>Maadili               | Makemeo                              | Kumfurahisha<br>Mungu |   |
| 13:1-6                                       | 13:1-6                               | 13:1-6                               | 13:1-3<br>13:4        | 13:1-6                                    |
|  |                                      | Kuhitimisha<br>Miongozo ya<br>Kidini | 13:5-6                |   |
| 13:7-16                                      | 13:7-17                              | 13:7-16                              | 13:7-9<br>13:10-16    | 13:7-16<br>Utii kwa Viongozi<br>Wa Kidini |
| 13:17  |                                      | 13:17                                | 13:17                 | 13:17-19                                  |
|  | Maombi<br>Yanasistizwa               | Ujumbe Binafsi                       |                       |   |
| 13:18-19                                     | 13:18-19                             | 13:18-19                             | 13:18-19              |   |
| Dua na Salamu<br>za Mwisho                   | Dua, Nasaha<br>za Mwisho,<br>Maagano | Dua                                  | Kufunga Maombi        | Habari, Heri na<br>Salamu                 |
| 13:20-21                                     | 13:20-25                             | 13:20-21                             | 13:20-21              | 13:20-21                                  |
|  |                                      | Maandishi ya<br>Baadaye              | Maneno ya<br>Mwisho   |   |
| 13:22-25                                     |                                      | 13:22-25                             | 13:22-23<br>13:24     | 13:22<br>13:23-25                         |
|  |                                      |                                      | 13:25                 |   |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka “[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**  
**KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Mambo kadhaa hayakidhi mazingira ya kihistoria ya neno".
1. Viongozi wa ki-Kristo
  2. Makemeo yaliyo wazi kw wapagani, si kwa Wayahudi
- B. Sura hii ya mwisho inayo sifa kadhaa za uandishi wa Paulo.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 13:1-6

<sup>1</sup>Upendano wa ndugu na udumu. <sup>2</sup> Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua. <sup>3</sup> Wakumbukeni hao waliofungwa kana kwamba mmefungwa pamoja nao; na hao wanaodhulumiwa, kwa vile ninyi nanyi mlivyo katika mwili. <sup>4</sup> Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu. <sup>5</sup> Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa. <sup>6</sup> Hata twathubutu kusema,

"Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa;  
Mwanadamu atanitenda nini?"

13:1

NASB "Upendano wa ndugu na udumu"

NKJV "Ndugu wazidi kupendana"

NRSV "Mzidi kushirikiana kwa upendo"

TEV "Mzidi kupendana kama Wakristo"

NJB "Mwendelee kupendana kama walivyo ndugu"

Hii ni kauli tendaji shurutishi (si tegemezi, kama toleo la NASB linavyotafsiri), lenye kumaanisha "kudumu" au "kuendelea." Kitu ambacho wasomaji yawapasa kuendelea nacho ni "upendo wa kindugu" (*philadelphia*, kama vile Rum. 12:10; 1 The.4:9; 1 Pet. 3:8). Hawa wamelifanya hili wakati uliopita (kama vile Ebr. 6:10; 10:32-35) na wanatiwa moyo kuendelea. Hii ndiyo ishara inayoonyesha dhahiri kwamba mtu anamjua Mungu (kama vile Yohana 13:34-45; 15:12,17; 1 Yohana 2:10; 3:11,14,17-24; 4:7-21; 2 Yohana 5, angalia [Mada Maalum: "Kudumu" katika Maandiko ya Yohana.](#)).

Kuna maneno kadhaa ambatano ya neno *philoō*.

1. upendo wa kidugu, Ebr. 13:1
2. upendo wa kigeni, Ebr. 13:2
3. upendo wa fedha, Ebr. 13:5

**13:2 "Msisahau kuwafadhili wageni"** Hii ni kauli ya kati (yenye ushahidi) shurutishi. Huu ni uambatani wa neno "phileō" na "mgeni" yaani., "kuwafadhiri wageni." Katika siku hizo hapakuwa na hoteli zenyе kuwa na matarajio ya kukiuka maadili katika nyumba za kulala wageni na zilikuwa za gharama sana. Wakristo wanaitwa kuziweka wazi nyumba zao kwa ajili ya kutembelewa na wahudumu(kama vile Mt. 25:35; Rum. 12:13; 1 Tim. 3:2; Tito 1:8; 1 Pet. 4:9; 2 Yohana; Didache 11:4-6).

□ **"wamewakaribisha malaika pasipo kujua"** Hili ni dokezo la Mwanzo 18, ambapo Ibrahimu anakutana na malaika watatu walionekana katika sura ya wanadamu (kama vile pia *Tobiti sura* za 4-7). Pia malaika alimtokea Gideoni (Waamuzi 6); Manoa (Waamuzi 13); Lutu (Mwanzo 19); Hagari (Mwanzo 21). Hii haimaanishi kwamba Wakristo wanaweza kuwa wamewatembelea watu kama malaika; kama watu wa wa zamani walivyowafadhiri wageni na kuzipokea baraka, hivi ndivyo wanavyotakiwa, yawapasa waaamini kufanya hivyo.

**13:3 "Wakumbukeni hao waliofungwa"** Hii ni kauli ya kati (yenye ushahidi) shurutishi ya wakati uliopo. Viongozi hawa wameyafuatisha maneno ya Kristo ya Mt. 25:44-45, kwa Ebr. 10:32-36 wamewasaidia waamini wengine. Kufungwa kwao hakukua kwa ajili ya matendo maovu, bali kwa ajili ya imani yao katika Kristo (kama vile 1 Pet. 4:14-15). Tendo la kufungwa lilikuwa na uwezekano kwa waamini wote wa mwanzo, kama ilivyo kwa waamini wengine wa ulimwengu wa sasa pia.

□ **"kwa vile ninyi nanyi mlivyo katika mwili"** Kifungu hiki kingeweza kurejelea (1) mwonekano wa kimwili (kama vile 2 Kor. 12:2, muundo wa Kiyunani unao fanana), wenye kuathirika na mateso na kufungwa au (2) mwili wa Kristo (ingawa andiko hili halitegemei kuwa na kiambata cha Kiyunani), Kanisa, ambalo lilikuwa chombo cha mateso.

**13:4 "Ndoa na iheshimiwe na watu wote"** Hapa hakuna kitenzi. Ikiwa anagawa kwa kielekezi, "ni," usemi huu u kinyume na mafundisho ya uongo (kama vile 1 Kor. 7:38, ambao kimaadili uliifanya ndoa kuwa duni na kuelekea katika useja au 1 Tim. 4:3). Ikiwa mtu anatumia kauli shurutishi, "na . . . iwe. . . ." kama ilivyo katika toleo la NASB la Ebr. 13:1, huku ni kutia maonyo dhidi ya uelekeo usio wa kimaadili wa utamaduni wa kipagani (Ebr. 13:4 inaweka upendeleo wa uchaguzi huu).

□ **"malazi yawe safi"** Ndoa ni zawadi toka kwa Mungu na desturi kwa wote (kama vile Mwa. 1:28; 9:1,7). Hii si dhambi wala aibu. Dhana ya falsafa ya Kiyunani ihusuyo kujinyima starehe, inatoa mtazamo kwamba mwili ni uovu na ya kwamba tendo la kuyapuuzia mahitaji yakelinaonyesha ukuu wa kiroho, kwenye kuleta hamasa kwa kanisa! Na bado ndivyo ilivyo! Hili neno "yawe safi" linatumika katika Ebr. 7:26 kueleza usafi wa tendo la kujamiiana uliozungumziwa na Yesu, kuhani wetu mkuu. Hili linatumika katika Agano la Kale la Kiebrania kuurejelea uzinzi.

Onyo hili dhidi ya kujamiina kuliko kinyume linashangaza ikiwa kitabu hiki kinaandikwa kwa ajili ya watu wa Kiyahudi. Utamaduni wa watu wa Mataifa wa karne ya kwanza ulibainishwa kwa kujamiiana kwa ukatili, lakini si jamii ya Kiyahudi. Kuna mengi yahusuyo mazingira ya kihistoria na wapokeaji wa Kiyahudi wasiojulikana.

□ **"waasherati"** Katika Agano la Kale neno hili linamaanisha uhusiano wa kingono kati ya watu wasio katika ndoa, bali katika Agano Jipyä hili nina nyingine maana pana ya kujamiiana kinyume na maadili kwa namna yo yote ile. Hapa tunalipata neno la Kiingereza "picha za ngono" kutokana na neno la Kiyunani.

□ **"wazinzi"** Hili linarejelea uhusiano wa zinaa kati ya watu, mmoja au wote walioolewa na watu wengine. Dhambi za zinaa zilikuwa hofu kuu ya kanisa la kwanza kwa sababu ya kuenea kwa maovu na matendo ya ibada za utamaduni wa wapagani (kama vile Gal. 5:19-21).

□ **"Mungu atawahukumia adhabu"** Hukumu ya Mungu juu ya tendo la mwanadamu la kujamiina visivyo inawenza kuonekana katika Rum. 1:24-32; Gal. 5:19- 21; Efe. 4:19; Kol. 3:5; Ufu. 21:8; 22:15. Hata hivyo, kuna vifungu vifungu vingine kama 1 Kor. 5:5 na 1 Tim. 1:9-11, chenye kuhusiana na waamini wanaoyatenda matendo haya yaliyo kinyume na maadili. Ililipasa Kanisa la awali kukumbana na mambo yaliyo kinyume na maadili katika maisha ya waamini na kujaribu kueleza miongozo yake.

1. iliwapasa kutubu

2. iliwapasa waamini kuwasaidia (kama vile Gal. 6:1; Yakobo 5:16,19-20)
3. iliwapasa waamini kutokuwa marafiki "wakubwa" na waamini wasio na maadili (kama vile 1 Kor. 5:9-13). Ushahidiwa Kikristo kuhusiana na maadili, ndoa imara, ukarimu, na upendo wa kidugu kama ilivyo muhimu leo katika karne ya kwanza.

### 13:5

- NASB      "Msiwe na tabia ya kupenda fedha"  
 NKJV      "Mwenendo wenu usiwe wa tamaa"  
 NRSV, TEV "Yaepusheni maisha yenu dhidi kupenda fedha"  
 NJB      "Wekeni shauku zenu mbali maisha yenu"

Hapa hakuna kitenzi, tena ushurutishi unatumika. Nahau ni uambatani wa

1. kiambishi awali hasi
2. neno *phileō* ( ambatani ya tatu *phileō* kwa kuwa 13:1), kupenda
3. sarafu ya fedha

Hii inamaanisha "asiyependa fedha." Tatizo si fedha, bali kupenda fedha (kama vile Luka 12:15;16:14; 1 Tim. 3:3; 6:10,17-19; 2 Tim. 3:2).

▣ "mwe radhi na vitu mlivyo navyo" Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo inayotumika katika maana ya ushurutishi. Hili ndilo suala la msingi katika kuwa na furaha. Huu ni mtazamo wa kiulimwengu kwamba usemi huu hautazamii mambo ya kimwili na uharaka. Suala la kuridhika ni karama ishangazayo itokayo kwa Mungu ambayo lazima ikubaliwe kwa imani na kuishi kwayo kila siku (kama vile 2 Kor. 9:8; Flp. 4:11-12; 1 Tim. 6:6-10).

▣ "Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa" Hii ni nukuu iliyopotea yenyewe ukanushi mara dufu wenye mkazo, uliochukuliwa kutohana na ahadi za Mungu kwa viongozi na watu wake. Mungu yu pamoja nasi na kwa ajili yetu (kama vile Kumb. 31:6- 7; Yos. 1:5; 1 Nya. 28:20; Isa. 41:10,13,14,17). Waamini wanapaswa kuwa na hofu juu ya utoaji wa kila siku (kama vile Mt. 6:19-34).

**13:6 "Bwana"** Hii ni nukuu toka Agano la Kale Kiebrania ya Zab. 118:6, lakini kweli pia inapatikana katika Zaburi 56:4,11.

▣ "Bwana ndiye anisaidiaye" Zaburi 118 ni neno lenye nguvu la ujasiri katika upendo wa Mungu, msamaha, uwepo, na msaada.

Hii ni nomino "msaidizi" linatumika hapa tu katika Agano Jipya (bali kitenzi kiko katika Ebr. 2:18), lakini linatumika katika LXX. Hili linamaanisha "kutoa msaada," "kuja kwa ajili ya ukombozi wa mtu."

▣ "Mwanadamu atanitenda nini" Hii kweli kuu (kama vile Zab. 56:4,11; 118:6) pia linaelezwa kwa uchache sana katika maneno tofauti tofauti Rum. 8:31b na kuelezwu katika Ebr. 8:32-39.

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 13:7-16

<sup>7</sup> Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao. <sup>8</sup> Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele. <sup>9</sup> Msichukuliwe na mafundisho ya namna nyininge nyininge, na ya kigeni; maana ni vizuri moyo ufanywe imara kwa neema, wala si kwa vyakula, ambavyo wao waliokwenda navyo hawakupata faida. <sup>10</sup> Tuna madhabahu ambayo wale waihudumiao ile hemu hawana ruhusa kula vitu vyake. <sup>11</sup> Maana wanyama wale amba damu yao huletwa ndani ya patakatifu na kuhani mkuu kwa ajili ya dhambi, viwiliwili vyao huteketezwa nje ya kambi. <sup>12</sup> Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango. <sup>13</sup> Basi na tutoke tumwendee nje ya kambi, tukichukua shutumu lake. <sup>14</sup> Maana hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao. <sup>15</sup> Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake. <sup>16</sup> Lakini msisahau kutenda mema na kushirikiana; maana sadaka kama hizi ndizo zimpendezazo Mungu.

**13:7 "Wakumbukeni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hili ni dokezo la kuwaombea viongozi na kuwaheshimu! Hii ni tofauti, lakini yenyе kufanana, neno toka Ebr. 13:3. Waamini wanahitaji kuwa na utayari wa kuwa na huitaji wa kuwaombea na kuwaheshimu viongozi wao waipendao huduma kwa ajili ya mwili wa Kristo (kama vile Ebr. 13:3) na viongozi wao (kama vile Ebr. 13:7,17,24; 1 The. 5:12-13).

- ▣ **"wale waliokuwa wakiwaongoza"** Mistari ya 17 na 24 inashughulika na viongozi, hivyo Ebr. 13:7 lazima iwarejelee viongozi walioihubiri injili kwa mara ya kwanza, bali sasa wamekuwa.
- ▣ **"waliowaambia neno la Mungu"** Hii ndiyo kazi ya viongozi wa Kikristo. Hawa hawakuhubiri wala kuufundisha upendeleo/tamaduni binafsi, bali injili ya Yesu Kristo. Kwa ajili ya hili tunawaheshimu, kuwastahi, na kuwaombea.
- ▣ **"kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo yenyе kutumika kama ushurutishi. Viongozi hawa, kama wale walio katika mzunguko wa wito wa imani iliyo katika sura ya 11, wanaendelea kuwa waaminifu katika maisha ya hadi kufa kwao. Maisha yao yanashuhudiwa na uthabiti wa jumbe zao.
- ▣ **"iigeni imani yao"** Hii ni kauli ya kati (yenye ushahidi) shurutishi ya wakati uliopo. Mwandishi wetu anatoa wito kwa wasomaji wake kuiiga imani ya vongozi wao. Mara nyingi Paulo anawasistiza waamini kuiiga imani yake (kama vile 1 Kor. 4:16; 11:1- 2; Flp. 3:17; 4:9; 1 The. 1:6; 2 The. 3:7,9).

**13:8 "Yesu.....ye ye yule"** Wahusika wa Agano la Kale wa sura ya 11 walikuwa mifano mizuri ; viongozi wa mwanzo na wa sasa ni mifano mizuri; Kristo ndiye mfano wetu mkuu sana. Sifa na imani kamwe hawawezi kubadilika (kama vile Zab. 102:26-27, iliyonukuliwa katika Ebr. 1:12). Huu usemi wa kithiolojia wenye kufanana unaundwa kumhusu YHWH katika Mal. 3:6. Sifa ya na huruma ya Mungu ni thabiti na, hivyo hivyo, ni wa Kristo.

**13:9 "Msichukuliwe"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopo yenyе kiambata hasi ambayo mara kwa mara inamaanisha kusitisha tendo ambalo tayari liko katika mchakato. Baadhi ya wasikiliza walitarajia "kusita" (kama vile Ebr. 2:1; 10:38). Kauli tendwa inamaanisha kazi ya Shetani au ya kipepo.

- ▣ **"mafundisho ya namna nyingine nyingine"** Kiuhalsia nini kinahusishwa haijulikani, bali ni mchanganyiko wa matendo ya Kiyahudi na wapagani wenye kufanana unao unashtumiwa katika Kol. 2:16-23.

Kwangu hasa inaonekana kwamba sehemu za sura ya 13 ni ufungaji wa ki-Paulo uliongezwa katika barua ya sinagogi. Sehemu za sura hii (yaani., Ebr. 13:4-5) inaendana utaratibu wa kanisa, si sinagogi.

**NASB** "maana ni vizuri moyo ufanywe imara kwa neema"

**NKJV** "kwa kuwa ni vizuri kuwa moyo umehimarishwa kwa neema"

**NRSV** "kwa maana ni vizuri moyo kuhimarishwa kwa neema"

**TEV** "Ni vizuri kuupokea uhimara wa ndani kutohana na neema ua  
Mungu"

**NJB** "ni bora kuitegemea neema kwa nguvu ya ndani"

Hii ni kauli tendwa endelevu ya kitensi jina cha wakati ulipo. Wasikilizaji hawa wanahitaji kuimariswa kwa ustadi, si katika taratibu, dhabihu za wanyama au sheria za vyakula, bali zisizostahili, zisizo na matunda ya neema ya Mungu katika Yesu Kristo (yaani., injili, kama vile Ebr.13:7). Hizi zilikuwa za kuyumbayumba kati ya Musa na Yesu. Yesu, Neno la Baba lisilobadilika, yu mbali na ukuu wa matendo na maneno ya agano la kwanza.

Kuielewa sifa na upendowa Mungu usiobadilika, vinaeleza dhahiri sana katika maisha, mafundisho, na kifo cha Yesu (injili), ndivyo vinavyowapa uhakika waamini. Miyo, fikra za waamini na wanaimarishwa kuitia maarifa na injili na uhusiano binafsi pamoja na Mchungaji Mkuu, si kuitia taratibu za nje na matendo (agano la kale la Musa).

Mara nyingi mwandishi huyu anaeleza jambo la kiroho la "moyo" (tazama Mada Maalum katika Ebr. 3:8). Huyu anayanakili maandiko kadhaa ya Agano la Kale.

1. Ebr. 3:8,15; 4:7, "Msifanye migumu miyo yenu" (Zab. 95:8)
2. Ebr. 3:10, "waliopotoka miyo hawa" (Zab. 95:10)
3. Ebr. 8:10, "Na katika miyo yao nitaziandika" (Yer. 31:33)

Huyu pia anazifupisha kweli hizi katika Ebr. 3:12; 4:12, na 10:22. Miyo inawakilisha chuma, hisia, na hali za hiari za mwanadamu. Ukriso unashughulika na mahitaji ya ndani ya mwanadamu aliyeanguka, ambapo dini ya Kiyahudi isingeweza.

▣ **"moyo"** Tazama Mada Maalum katika Ebr. 3:8.

▣ **"si kwa vyakula, ambavyo wao waliokwenda navyo hawakupata faida"** Hii ni rejea iliyo wazi yenye kuzungumzia Mambo ya Walawi 11. Sheria za vyakula zimekwisha kupita katika Kristo (kama vile Mt. 15:11; Marko 7:18-23; Matendo ya Mitume 10; Kol. 2:16-23). Hizi hazikuwa na ufungamanifu tena kwa waamini kwa ajili ya wokovu (kama vile Wagalatia 3; Matendo ya Mitume 15), bali katika utaratibu wa kanisa, waamini walikuwa na ufahamu wa "ndugu dhaifu" (kama vile Matendo ya Mitume 15:19-20; Rum.14:1-15:6; 1 Wakorintho 8; 10:23-33) na kutojaribu kuzikosesa dhamiri zao zilizo dhaifu.

**13:10 "Tuna madhabahu"** Ufanano huu unaonekana kuwa wa kiroho (wa kimbingu) hekalu, si madhabahu ionekanayo na, hivyo, hili linairejelea kazi ya dhabahu ya Yesu kwa niaba ya waamini. Hii ni stiari yenye nguvu ya uelekeo wetu kwa Mungu kuitia Kristo.

▣ **"hawana ruhusa kula vitu vyake"** Hili ni dokezo lingine la Mambo ya Walawi 16.

**13:11 "vyao huteketezwa nje ya kambi"** Hilini dokezo lingine la taratibu za Law. 16:27 — Siku ya Upatanisho.

**13:12 "Yesu....nje ya lango"** Hili ni mchezo wa maneno ya sheria za dini za Kiyahudi kama dhabihu za Agano la Kale zilivopelekwa nje ya lango, Yesu alipelekwa nje ya mji wa Yerusalem ili kusulibishwa.

**13:13 "Basi na tutoke tumwendee nje ya kambi"** Huu ni mstari wa msingi katika kitabu hiki. Hii ni kauli ya kati (yenye ushahidi) tegemezi ya wakati uliopo, lenye kuzungumzia tendo endelevu na kuongeza jambo lililo na uwezekano (hili ni kemeo na onyo dhidi ya "kusita sita"). Kwa uwazi waumini wanahitaji kumtambua na maonyo yake pasipokujali għarama zake. Huu ni wito sahihi kwa hawa "waliotunzwa" waamini wa sinagogi kutembea katika mwanga kamili wa Amri Kuu ya Ukristo (kama vile Mt. 28:19-20; Matendo ya Mitume:8).

**13:14 "mji"** Hii ni stiari ya mbinguni yenye kuyatumia makazi ya Israeli ya Nchi Iliyohaidiwa (kama vile Ebr.11:10,16; 12:22; Yohana 14:2). Aina hii hii ya stiari inaonekana katika Ebr. 11:14, "nchi."

**13:15 "kwa njia yake ye ye"** Maelezo haya yanamrejelea Yesu, anayetajwa kwa jina lake katika Ebr.13:12, aliywatoa kafara watu wake kwa damu yake nje ya lango la Yerusalem. Manufaa yote ya kiroho hutoka kwake!

■ "na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima" Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo. Mfumo wa utoaji dhabihu, aliyopewa Israeli kwa ajili ya kuulinda uhusiano pamoja na Mungu kwa kushughulikia tatizo la dhambi, lilihusishwa katika aina za dhabihu.

A. Mbili zilikuwa za lazima

1. ye ye "dhabihu ya dhambi"
2. dhabihu ya kosa au hatia"

B. Kulikuwa tatu za hiari

1. dhabihu zilizo teketezwa kwa ajili ya mema
2. dhabihu za nafaka/chakula
3. dhabihu za ushirika, au amani

Katika na uhusiano na hizi tatu zilizopita ile dhana ya shukrani na sifa inatajwa (kama vile Law. 7:12). Dhabihu hizi zinazeleza kwa undani katika Mambo ya Walawi 1-7. Zaburi inakitaja kipengele cha adhana ya mara kwa mara (kama vile Zab. 27:6;50:14; 69:30; 107:22; 116:17). Hiki kifungu "dhabihu ya sifa" inatoka katika tafsiri ya Kale ya Maandiko ya Kiebrania (kama vile Law. 7:2,3,5; 2 Nya. 29:31; 33:16; Zab.49:14,23; 106:22).

■ "tunda la midomo" Kifungu hiki kinaiakisi 57:19 na Hosea 14:3 toka Tafsiri ya Maandiko ya Kale ya Kiebrania. Vifungu kama hiki vilitumiwa na Waisraeli walipokuwa uhamishoni kuweka mbadala sifa ya kivitendo katika nafasi ya dhabihu za wanyama kwa sababu Hekalu liliharibiwa na Nebukadneza II moja kwa moja, mnamo 586 k.k. mfalme wa Babeli kwa wakati huo. Hili liliharibiwa Rumi kwa mara nyingine mnamo 70 b.k. Tarehe ya kukiandika kitabju hiki haijulikani.

**NASB "iliungamayo jina lake"**

**NKJV "kutoa shukrani kwa ajili ya jina lake"**

**NRSV "ilikiriyo jina lake"**

**TEV "imkiriye kama Bwana"**

**NJB "wale walitambualo jina lake"**

Kwa waamini sifa zetu kwa Mungu ni ukiri wetu (*homologēo*) kumsu Yesu (kwa kulitumia jina lake kama ilivyo katika Mt. 28:19-20 au Rum. 10:9-13) kama Bwna (kama vile TEV, yenyе kuiakisi Flp. 2:6-11).

**13:16 "msisahau kutenda mema"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo yenyе kiambata hasi, ambacho mara nyingi kinamaanisha kustisha tendo lililo katika mchakato. Mungu anatukuzwa pale watoto wake wanapopendana na kusaidiana (kama vile Phil. 4:18).

Katika muktadha wa Kiyahdi hiki kifungu "mema" (*koinōnia*) huenda kinairejelea shukrani (kama vile Mt. 6:1), karama ya utoaji wa fedha kwa kila juma itolewayo na wshiriki wa sinagogi kwa ajili ya manunuzi ya chakula kwa wahitaji. Wayahudi walilichukulia tendo hili kama la haki.

■ "kushirikiana"

### MADA MAALUM: *KOINÔNIA (USHIRIKA)*

Neno "ushirika" (*koinōnia*) unamaanisha

1. Ushirika wa karibu na mtu
  - a. na Mwana (kama vile 1 Kor 1:9; 1 Yohana 1:6)
  - b. na Roho (kama vile. 2 Kor. 13:14; Flp. 2:1)

- c. na Baba na Mwana (kama vile. 1 Yohana 1:3)
- d. na ndugu wa agano wa kiume/kike (kama vile Matendo 2:42; 2 Kor. 8:23; Gal. 2:9; Filemoni aya. 17; 1 Yohana 1:3,7)
- e. usio na uovu (kama vile 2 Kor. 6:14)
- 2. ushirika wa karibu na vitu ama makundi
  - a. na injili (kama vile Flp. 1:5; Philemon aya. 6)
  - b. na damu ya Kristo (kama vile 1 Kor. 10:16)
  - c. usio na giza (kama vile 2 Kor. 6:14)
  - d. na mateso (kama vile 2 Kor. 1:7; Flp. 3:10; 4:14; 1 Pet. 4:13)
- 3. Zawadi ama changizo zilizotolewa kwa mtindo wa ukarimu (kama vile Rum. 12:13; 15:26; 2 Kor. 8:4; 9:13; Flp. 4:15; Ebr. 13:16)
- 4. Kipawa cha Mungu cha neema, kupitia Kristo kinachorejesha ushirika wa mwanadamu na yeye na ndugu zake wa kiume na kike

Hii inatangaza uhusiano wa ulalo (mwanadamu kwa mwanadamu) ambao unaletwa kwa uhusiano wa kweli (mwanadamu na muumbaji). Pia unasisitiza hitaji na furaha ya jumuiya ya Kikristo (yaani, Ebr. 10:25).

- "maana sadaka kama hizi ndizo zimpendezazo Mungu" Tambua katika Ebr. 13:15 dhabihu zilizokubaliwa ilikuwa imani iliyokubalika katika Kristo; na sasa ni maisha ya kumfanana Kristo. Mara nyingi Injili ni vyote!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 13:17**

<sup>17</sup> **Watiini wenyе kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaota hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewafaa ninyi.**

**13:17 "Watiini . . . kuwanyenyekea"** Hii ni kauli tendwa ya wakati uliopo (A. T. Robertson anaorodhesha hii kama kauli ya kati) shurutishi na kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Japokuwa watu wako huru katika Kristo yatupasa kuzaa matunda katika mamlaka ya kiroho kwa ajili ya ukuaji na huduma (kama vile Ebr. 13:7; 1 Kor. 16:16; 1 The. 5:12-13).

Neno hili lenye kusistiza unyenyekevu kwa viongozi wa Kikristo linahitajika katika hizi siku zetu za kuitotii mamlaka ya aina yo yote ile, na msisitizo zaidi wa haki na mamlaka mtu binafsi. Mungu amewatoa wengine kuwa kama viongozi mionganii mwa watu wake (angalia Hes. 16:3-5). Tunawaheshimu kwa sababu ya wito wao, kufunza, kujitoa, na huduma. Hata hivyo, kuna kinyume cha neno "kuendelea hadi mwisho." Wito wa Mungu umekuwa ukitumiwa visivyo na baadhi ya malaka za watu wa aina fulani. Lazima tuweke ulinganifu, heshima shirikishi, roho shirikishi kati ya watu wa Mungu na viongozi wa Mungu. Waamini wote wanaitwa kwa ajili ya wengine kwa ajili ya heshima kwa Kristo (kama vile Efe. 5:21).

□ "wao wanakesha" Hili neno linamaanisha "kuamka," "kuwa waangalifu" (kama vile Marko 13:33; Luka 21:36; Efe. 6:18), ambalo ni stiari ya juhudhi za kukesha na kuduma (kama vile Isa. 62:6; Eze. 3:17; 33:7-9).

□ "kama watu watakaota hesabu" Viongozi wanao wajibu wa huduma yao na watatoa hesabu kwa Mungu (kama vile 1 Kor. 3:10-15). Hawa ni watumishi!

□ "wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua" Mtazamo uhusuo kusanyiko huutambulishi huduma, bali tendo la kufurahisha auu kuumiza.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 13:18-19**

<sup>18</sup> Tuombeeni; maana tunaamini kwamba tuna dhamiri njema, tukitaka kuwa na mwenendo mwema katika mambo yote. <sup>19</sup> Nami nawasihi zaidi sana kufanya hayo ili nirudishwe kwenu upesi.

**3:18 "Tuombeeni"** Maombi ya uongozi na kwa ajili ya uongozi ni ya muhimu (kama vile Efe. 6:18-19; Flp. 4:6; 1 The. 5:25; 1 Tim. 2:1-2,8). Huu wingi unaweza kuirejelea huduma ya kundi ikiwemo Timotheo (kama vile Ebr. 13:23).

▣ "maana tunaamini kwamba tuna dhamiri njema, tukitaka kuwa na mwenendo mwema katika mambo yote" Mtazamo na mtindo wa maisha ndiyo mambo yawekayo msingi wa uongozi. Mwandishi wa kitabu cha Waeraniani amelitaja neno "dhamiri" mara kadhaa (kama vile. Ebr. 9:9,14; 10:2,22; 13:18). Nguvu ya ukombozi wa Yesu na Roho akaaye ndani ina hofu ya Mungu aibu ya dhambi zilizopita na kuziondoa kupitia furaha, amani, ujasiri, si katika utendaji wa kibinadamu, bali katika injili! Hii maarifa ya injili ndiyo kofia ya wokovu (kama vile Efe 6:17; 1 The. 5:8).

Baadhi ya watoa maoni wameuona mstari huu kama wenye kuhusiana na baadhi ya mashtaka yaliyofunuliwa kwa mwandishi (sawa na hali ya Paulo iliyo katika 1 Wakorintho na Wagalatia).

**13:19** Huu ni mstari wa siri zaidi. Kwa kiasi fulani kuja kwa mwandishi kulihusiana na maombi yao. Hili linaleta maana sana kama ile ya Paulo (kama vile Filemoni 22). Maombi huiachilia nguvu kamili ya Mungu kwa ajili ya huduma. Mambi ya waamini hungusa Mungu na wengine.

Baadhi ya watoa maoni (m.f., H. E. Dana's *Jewish Christianity*, uk. 268) wamedhani kwamba jambo hili linayarejelea maradhi ya mwandishi, au hata kufungwa kwake (hili neno "upesi" pia linatumwiwa na Timotheo katika Ebr. 13:23).

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 13:20-21

<sup>20</sup> Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, ye ye Bwana wetu Yesu, <sup>21</sup> awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake, naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo; utukufu una ye ye milele na milele. Amina.

**13:20 "Basi, Mungu wa amani"** Hili jina la Mungu Baba linatumika hapa tu na katika maandiko ya Paulo (kama vile Rum. 15:33; 16:20; 1 Kor. 14:33; 2 Kor. 13:11; Flp. 4:9; 1 The. 5:23; "Bwana wa Amani" 2 The. 3:16).

▣ "aliyemleta tena kutoka kwa wafu" Mara nyingi Agano Jipya linamtabiri Mungu Baba kama aliyemfufua Yesu toka katika wafu (kama vile Matendo ya Mitume 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 6:4,9; 10:9; 1 Kor. 6:14; 2 kor. 4:14; Gal. 1:1; Efe. 1:20; Kol. 2:12; 1 The. 1:10). Hili linaonyesha Baba kuyakubali maisha ya Yesu, mafundisho, na dhabihu. Hata hivyo, kuna maandiko mengine yenye kueleza kuwa kazi ya ufufuo ilikuwa ya Roho (kama vile Rum. 8:11) au Mwana mwenywewe (kama vile Yohana 2:19-22; 10:17-18). Kwa kunena kithiolojia, nafsi zote tatu za Utatu ni tendaji katika matendo yote ya ukombozi.

▣ "Mchungaji Mkuu" Hili neno "Mchungaji" ni sitiari ya Agano la Kale ya

1. YHWH (kama vile Mwa. 49:24; Zab. 23:1; 78:52; 80:1; Mhu. 12:11; Isa. 40:11; 63:11; Yer. 31:10; Eze. 34)
2. uongozi wa watu wake (kama vile Yer. 10:21; 50:6-7; Eze. 34:2-3; Zek. 11:3,5,15,17)
3. ujio wa Masihi, mwana wa Daudi (kama vile Zab. 78:70-72; Eze. 34:23-24; 37:24; Mika 5:4; 7:14; Zek. 13:7; Yohana 10:2,11,14; 1 Pet. 2:25; 5:4)

Mara kadhaa katika Agano la Kale (kama vile Hes. 27:17; 1 Fal. 22:17; 2 Nya. 18:16; Eze. 34:5; Zek. 10:2) Watu wa Mungu wanaelezwa kama waliotawanyika bila mchungaji, lakini Mchungaji Mkuu amekuja. Yeye ameletwa kwetu na yu pamoja nasi!

- "kwa damu" Kifungu hiki kinayarejelea maisha yake ambayo yalilihimarisha agano jipy (kama vile Zek. 9:11; Marko 14:24; 1 Kor. 11:25).
- "ya agano la milele" Ni vigumu kuzibaini tofauti za maagano ya "milele" kwa sababu, kama kitabu cha Waembrania kinavyoonyesha, agano la Musa lilikuwa la amri na kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu, si la milele. Agano la Kale linayanukuu maagano ya amri na yasiyo ya amri (yaani., Kutoka, Mwa. 15:17-21). Lile agano na Ibrahim, ambapo mataifa yote yangebarikiwa, si ya amri (yaani., agano la milele), na ambapo, ni la milele (kama vile Mwanzo 17:7,13,19; Zaburi 105:9-10). Agano la Daudi, kwa mara ya kwanza lilitunuliwa katika 2 Samueli7, hili linamtabiri Masihi, mwana wa Daudi, ambalo si la amri, na ambapo, ni la milele (kama vile Zab. 89:3-4). Agano jipy linatajwa kama siku mpya ya haki (enzi mpya ya Roho) kwa watu wa Mungu (kama vile Isa. 55:3; 59:21; 61:8; Yer. 31:33; 32:40; 50:5; Eze. 16:60; 37:26). Mtu anaweza kuona namna Wayahudi wa Kipindi cha Yesu walivyotiwa na hofu juu ya ujumbe wake. Mara nyingi huyu amekuwa mpango wa Mungu wa ukombozi, lakini Israeli kushindwa kuzitunza amri za Mungu alizompa Musa kulionyesha uhitaji wa njia nyingine ya wokovu kuliko utendaji wa mwanadamu (kama vile Wagalatia 3). Tazama [MADA MAALUM: UMILELE](#) katika Ebr. 6:2.

## **MADA MAALUM: MILELE ('olam)**

Maelezo ya asili ya neno la Kiebrania 'olam, עולם (BDB 761, KB 798) hayajulikani (NIDOTTE, juzu. 3, uk. 345). Yametumika katika maana mbali mbali (mara nyingi yanapimwa na maudhui). Ifuatayo ni mifano iliyochanguliwa tu.

1. vitu vya kale
  - a. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
  - b. mahari, Isa. 58:12; 61:4
  - c. Mungu, Zab. 93:2; Mith. 8:23; Isa. 63:16
  - d. Vitu, Mwa. 49:26; Ayubu 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
  - e. muda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
2. muda/ wakati ujao
  - a. maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
  - b. heshima ya hali ya juu kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
  - c. uwepo endelevu
    - 1) dunia, Zab. 78:69; 104:5; Mhu. 1:4
    - 2) mbinguni, Zab. 148:5
  - d. uwepo wa Mungu
    - 1) Mwa. 21:33
    - 2) Kut. 15:18
    - 3) Kumb. 32:40
    - 4) Zab. 93:2
    - 5) Isa. 40:28
    - 6) Yer. 10:10
    - 7) Dan. 12:7
  - e. Agano
    - 1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19
    - 2) Kut. 31:16
    - 3) Ufu. 24:8

- 4) Hes. 18:19  
 5) 2 Sam. 23:5  
 6) Zab. 105:10  
 7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8  
 8) Yer. 32:40; 50:5
- f. Agano maalumu na Daudi
- 1) 2 Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
  - 2) 1 Fal. 2:33,45; 9:5
  - 3) 2 Nya. 13:5
  - 4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
  - 5) Isa. 9:7; 55:3
- g. Masihi wa Mungu
- 1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4
  - 2) Isa. 9:6
- h. Sheria za Mungu
- 1) Kut. 29:28; 30:21
  - 2) Ufu. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
  - 3) Hes. 18:8,11,19
  - 4) Zab. 119:89,160
- i. Ahadi za Mungu
- 1) 2 Sam. 7:13,16,25; 22:51
  - 2) 1 Fal. 9:5
  - 3) Zab. 18:50
  - 4) Isa. 40:8
- j. Uzao wa Ibrahimu na nchi ya ahadi
- 1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
  - 2) Kut. 32:13
  - 3) 1 Nya. 16:17
- k. Sikukuu za ahadi
- 1) Kut. 12:14,17,24
  - 2) Ufu. 23:14,21,41
  - 3) Hes. 10:8
- l. umilele, kudumu milele
- 1) 1 Fal. 8:13
  - 2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
  - 3) Isa. 26:4; 45:17
  - 4) Dan. 9:24
- m. Zaburi inasema yapi yanayowapasa kufanya milele
- 1) kushukuru, Zab. 30:12; 79:13
  - 2) kudumu katika uwepo Wake, Zab. 41:12; 61:4,7
  - 3) amini katika huruma zake, Zab. 52:8
  - 4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
  - 5) imba nyimbo za sifa, Zab. 61:8; 89:1
  - 6) tangaza haki zake, Zab. 75:7-9
  - 7) tukuza jina lake,Zab. 86:12; 145:2
  - 8) baliki jina lake, Zab. 145:1
- n. linatumiwa na Isaya kueleza enzi mpya
- 1) agano la milele, Isa. 24:5; 55:3; 61:8
  - 2) YHWH kama mwamba wa milele, Isa. 26:4
  - 3) furaha ya milele,Isa. 35:10; 51:11; 61:7

- 4) Mungu wa Milele, Isa. 40:28  
 5) Wokovu wa milele, Isa. 45:17  
 6) Wema wa milele, Isa. 54:8  
 7) Ishara ya milele, Isa. 55:13  
 8) Jina la milele, Isa. 56:5; 63:12,16  
 9) Nuru ya milele, Isa. 60:19,20
- Matumizi yenye hali ya ukarushiana na adhabu ya milele kwa waharifu inapatikana katika Isa. 33:14, "moto wa milele." Isaya kila wakati anatumia "moto" kuelezea hasira ya Mungu (kama vile. Isa. 9:18,19; 10:16; 47:14), lakini katika Isa. 33:14 "ndipo anasema wa milele"
3. Wakati wa kurudi nyuma na kwenda mbele ("toka milele hadi milele")
- Zab. 41:13 (sifa kwa Mungu)
  - Zab. 90:2 (Mungu pekee)
  - Zab. 103:17 (huruma zake)
- Kumbuka,muktadha huamua maudhui ya maana ya neno. Maagano ya ahadi za milele ni ya masharti (yaani, Yeremia 7, tazama Mada Maalumu: Agano). Kuwa mwangalifu unaposoma maoni ya kisasa kuhusu muda au Agano Jipyia la theolojia iliopangwa katika matumizi ya kila siku ya neno hili dhaifu katika Agano la Kale. Kumbuka pia, Agano Jipyia linajumuisha ahadi zote za Agano la kale (tazama Mada Maalumu: utabiri wa mambo yajayo ya Agano la Kale dhidi ya utabiri wa mambo yajayo ya Agano Jipyia.).

**13:21**

- NASB "awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema"  
 NKJV "awafanye kuwa wakamilifu katika kila kazi njema"  
 NRSV "awafanye kuwa wakamilifu katika kila jeama"  
 TEV "awape kwa kila jema"  
 NJB "awaandae...katika kila tendo lililo jeama"

Hiki kitensi (*katartizō*), ni kauli adimu tendji chaguzi ya wakati usio timilifu, yenye kueleza matarajio au shauku) yenye kumaanisha mtu fulani au kitu fulani kwa utoshelevu, muhimu, au chenyeh sifa (kama vile Luka 6:40; 1 Kor. 1:10; 2 Kor. 13:11; 1 The. 3:10; 1 Pet. 5:10). Kithiolojia hili linafana na Efe. 2:10. Mapenzi ya Mungu ni kwamba waamini wanafananishwa na sura ya Yesu (kama vile Rum. 8:29), yenye kuleta matokeo katika maisha ya ki-Mungu yenye kuwashawishi wale waliokwenda tofauti na Kristo.

- "kuyafanya mapenzi yake" Yesu aliyafanya mapenzi ya Baba katika kuja kama Mtumishi Ateswaye (kama vile Ebr. 10:7). Na sasa wafuasi wake wanaitwa pia kuyafanya mapenzi yake (kama vile Ebr. 10:36).

## MADA MAALUMU: MAPENZI (*THELĒMA*) YA MUNGU

"Mapenzi" ya Mungu yamejikita katika namna mbalimbali.

### INJILI YA YOHANA

- Yesu alikuja kuyatenda mapenzi ya Baba yake (kama vile Yohana 4:34; 5:30; 6:38)
- Kuwafufua siku ya mwisho wale wote Baba aliowampa Mwana (kama vile Yohana 6:39)
- Kwamba wote waamini katika Mwana (kama Yohana 6:29; 40)
- Maombi yaliyojibowi kuhusiana na kuyatenda mapenzi ya Mungu (kama vile Yn 9:31 na Yn 5:14)

### VODOKEZO VYA INJILI

- Kuyatenda mapenzi ya Mungu ni jambo la muhimu (kama vile. Mt. 7:21)
- Kuyatenda mapenzi ya Mungu hutufanya kuwa kaka na dada pamoja na Yesu (kama vile Mt. 12:50; Marko 3:35)

- Sio mapenzi ya Mungu kwa yejote kuangamia (kama vile Mt.18:14; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9)
- Kalvari ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa Yesu (kama vile Mt. 26:42; Luka 22:42)

#### NYARAKA ZA PAULO

- ukomavu na huduma ya waamini wote (kama vile Rum. 12:1-2)
- waamini waliondolewa kutoka katika enzi hii ya maovu (kama vile Gal. 1:4)
- mapenzi ya mungu ulikuwa ni mpango wake wa ukombozi (kama vile Efe.1:5, 9,15)
- waamini wanapitia na kuishi maisha yaliyojazwa na Roho (kama vile 5:17-18)
- waamini wamejazwa na maarifa ya Mungu (kama vile Kol. 1:9)
- waamini wanafanya kuwa imara na wakamilifu (Kol. 4:12)
- waamini wanatakaswa (kama vile 1 The. 4:3)
- waamini watoa shukrani katika vitu vyote (kama vile The.5:18)

#### NYARAKA ZA PETRO

- Waamini wanatenda haki (yaani, kunyenyeka kwenye mamlaka ya chini) na, kwa hiyo wanawanyamazisha watu wajinga, hivyo kuwapa fursa kwa kuijua injili/matendo mema (kama vile 1Pet. 2:15)
- Mateso ya waamini (kama vile 1 Pet. 3:17; 4:19)
- Waamini hawapaswi kuishi maisha ya ubinafsi (kama vile 1 Pet. 4:2)

#### NYARAKA ZA YOHANA

- waamini kuendelea kudumu milele (kama vile Yohana 2:17)
- waamini ni kielelezo kwa maombi yaliyojibwa (kama vile 1 Yohana 5:14)

◻ "utukufu una yeye milele na milele. Amina" Kifungu hiki, ni cha kawaida sana katika maandiko ya Paulo na Petro, ni cha utata. Wakati mwengine kinamrejeleaMungu Baba (kama vile Rum. 11:36; Efe. 3:21; 1 Pet. 4:11; 5:11; Yuda 25; Ufu. 1:6; 7:12), wakati mwengine kwa Yesu Mwana (kama vile 2 Tim. 4:18; 2 Pet. 3:18) na wakati mwengine kwa wote (kama vile Rum. 16:27; 1 Tim. 1:17; Ufu. 5:13 na hapa). Mara nyingi waandishi wa Agano Jipya wanayatumia majina yale yale, matendo, na vifungu kutoa maelezo ya wote Baba na Mwana kama njia ya kueleza ubora na Uungu wa Yesu wa Nazarethi.

◻ "Amina" Neno halisi la Kiebrania linamaanisha "kukiri" Hili liliboreshwa katika maana ya kistiari izungumziao uaminifu, utegemezi, na tuaini (kama vile Hab. 2:4). Baadaye lilikuja kutumika katika maana ya "nakiri" au "nakubali" kwa usemi fulani.

## MADA MAALUM: AMINA

### I. AGANO LA KALE

- Neno "Amina" linatoka kwenye neno la Kiebrania lenye maana ya
  - "ukweli" (emun, emunah, BDB 53)
  - "Uaminifu" (emun, emunah, BDB 53)
  - "imani" au "uaminifu"
  - "amini" (dmn, BDB 52)
- Asili yake ya neno inadokeza mkao wa mwili wa mtu ulivyo imara. Kinyume cha hili kinaonyesha mwili wa mtu Yule asio imara, unaoteleza (kama vile Zab. 35:6; 40:2; 73:18; Yeremia 23:12) au kizuizi (kama vile Zab. 73:2). Kutokana na utumiaji huu wa fasihi unatengeneza upanuzi wa kisitiari wa imani, uaminifu, utiifu na wa kutegemewa (kama vile Hab. 2:4)
- Utumiaji maalumu (angalia mada maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika agano la kale)
  - Nguzo, 2 Fal. 18:16 (1 Tim. 3:15)

2. Kuthibitika, Kut 17:12
  3. Uimalifu, Kut. 17:12
  4. Uthabiti, Isa. 33:6
  5. Ukweli, 1 Fal. 10:6; 17:24; 22:16; Pro. 12:22
  6. Thabiti, 2 Nya. 20:20; Isa. 7:9
  7. Stahili (sheria alizopewa Musa), Zab. 119:43,142,151,160
- D. Katika Agano la Kale maneno mawili ya Kiebrania yanatumika kwa ajili ya imani thabiti
1. Bathach (BDB 105), imani
  2. Yra (BDB 431), hofu, heshima, abudu (kama vile. Mwa. 22:12)
- E. Kwa maana ya kuamini au uaminifu ulioanzishwa kwa matumizi ya liturujia ambao ultumika kuthibitisha maelezo ya kweli ya mtu mwingine (kama vile. Hes. 5:22; Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Neh. 5:13; 8:6; Zab. 41:13; 72:19; 89:52; 106:48; Yer. 11:5; 28:6).
- F. Kiongozi cha kithiolojia kwenye neno hili sio uaminifu wa mwanadamu, bali ni wa Mungu mwenyewe (kama viirKut. 34:6; Kumb. 32:4; Zab. 108:4; 115:1; 117:2; 138:2). Tumaini la mwanadamu aliyeanguka ni neema, uaminifu, kutii Agano la Mungu na ahadi zake. Wale wanaomfahamu Mungu wanahitajika kufanana naye (kama vile. Hab. 2:4). Biblia ni historia na kumbu kumbu ya Mungu kurejesha taswira yake (kama vile Mwa. 1:26-27) kwa mwanadamu. Wokovu unarejesha uwezo wa mwanadamu kuwa na ushirika wa ndani na Mungu. Hii ndio sababu ya kuumbwa kwetu.

## II. AGANO JIPYA

- A. Utumiaji wa neno “amina” kama hitimisho la kiliturujia kwa minajili ya kuthibitisha ukweli wa maelezo/taarifa ni la kawaida katika Agano Jipy (kama vile. 1 Kor. 14:16; Ufu. 1:7; 5:14; 7:12).
- B. Utumiaji wa neno kama kifungio cha maombi ni wa kawaida kwenye Agano Jipy (kama vile. Rum. 1:25; 9:5; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 6:18; Efe. 3:21; Flp. 4:20; 2 Thess. 3:18; 1 Tim. 1:17; 6:16; 2 Tim. 4:18).
- C. Yesu ndiye yeye aliyalitumia hili neno (limezidishwa mara 25 katika Yohana, yaani., Yohana 1:51; 3:3,5,11; n.k.) kuyatambulisha maelezo muhimu (kama vile Luka 4:24; 12:37; 18:17,29; 21:32; 23:43).
- D. Linatumika kama cheo kwa Yesu katika Ufu 3:14 ( pia angalia 2 Kor 1:20, yamkini jina la heshima la Mungu kutoka Isa. 65:16)

Dhana ya kusadiki au sadiki, au kuamini au amini inaelezewa katika neno la Kiyunani *pistos* au *pistis*, ambalo linatafasiliwa katika Kiingereza kama “imani”, “sadiki”, “kuamini”(angalia mada maalumu: Sadiki, Kuamini au Imani).

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) WAEBRANIA 13:22-24

<sup>22</sup> Lakini nawasihi, ndugu, mchukuliane na neno hili lenye maonyo maana nimewaandikia kwa maneno machache.<sup>23</sup> Jueni ya kuwa ndugu yetu Timotheo amekwisha kufunguliwa; ambaye, akija upesi, nitaonana nanyi pamoja naye. <sup>24</sup> Wasalimuni wote wenye kuwaongoza, na watakatifu wote; hao walio wa Italia wanawasalimu.

**13:22-24** Mistari hii iliyo karibu, 22-24, inafanana na njia aliyoitumia Paulo kuziandika barua zake zilizokamatwa na mwandishi, ambapo huyu alichukua kalamu na kuongeza maelezo machache ya binafsi na baraka.

**13:22 "nawasihi"** Mwandishi anakihita kitabu chake "neno la kusihi." Huyu anawasihi wasomaji wake (kama vile Ebr. 3:13; 10:25; 12:15; 13:15,22). Hawa ni kaka (na dada) katika Kristo, lakini yawapasa kumheshimu, kumfuuata, kumtumikia!

■ "mchukuliane na neno hili lenye maonyo" Hii ni kauli ya kati shurutishi, yenye kusistiza kuhusishwa kwa ujumbe na amri ya kuendelea kusikiliza. Kifungu "neno la kusihi" kinatumika katika Matendo ya Mitume 13:15 ya hotuba ndani ya sinagogi. Wengi wanaamini kwamba hivi ndivyo lilivyokuwa chimbuko la kitabu cha Waebrania, lakini kiliboreshwana kuwa waraka. 13:23

■ "ndugu yetu Timotheo" Paulo anapotumia neno "ndugu," mara nyigi jina la mtu hutangulia (kama vile Rum. 16:23; 1 Kor. 1:1; 16:12; 2 Kor. 1:1; 2:13; Flp. 2:25). Huu ndiyo msingi wa ushahidi dhidi ya uandishi Paulo. Kumbaja Timotheo kunaifunua sura ya wakati wa mpangilio wa kitabu, wakati wa maisha ya Paulo au muda mfupi baada ya kifo chake (68 b.k), kabla ya kifo cha Timotheo.

■ "amekwisha kufunguliwa" Hii ni kauli tendwaji endelevu ya wakati timilifu. Hatujui cho chote kutoka katika Maandiko au po pote pale kuhusu Timotheo kuwa gerezani. Katika kitabu chake cha *Word Pictures in the New Testament*, uk. 451, A. T. Robertson anaeleza kwamba Timotheo aliwekwa gerezani wakati alipokuja kumtembelea Paulo, kama inavyotajwa katika 2 Tim. 4:11,21. Hli neno "kufunguliwa" (kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu) inatumika katika (1) Mt. 27:15; Yohana 19:10; Matendo ya Mitume 3:13; 4:21,23; 5:40 kufunguliwa kutoka kifungoni na (2) Matendo 13:3, kistiani kufunguliwa kutoka katika kazi ya huduma, na inaweza kumaanisha hili.

■ "akija upesi, nitaonana nanyi" Kifungu hiki kinaweza kumaanisha kwamba mwandishi wa kitabu cha Waebrania alitenda kazi na kuambatana na Timotheo.

**13:24 "watakatifu"** Tazama Mada Maalum katika Ebr. 6:10.

■ "hao walio wa Italia wanawasalimu" Kifungu hiki kinaweza kumaanisha

1. mwandishi yuko Italia
2. mwandishi anatoka Italia
3. sehemu ya kundi la umisheni wa mwandishi ilitoka Italia
4. mwandishi alianandikia Italia

Katika *Jewish Christianity*, H. A. Dana anasema kwamba mstari huu unamaanisha kwamba waraka huu uliandikwa kwa ajili ya makundi madogo madogo ya Kiyahudi ya kanisa la huko Rumi. Mtu wa kwanza kikitaja kitabu cha Waebrania alikuwa Clement wa Rumi mnamo mwaka 97 b.k (uk. 270). Hata hivyo, nafikiri hiki kilitumwa kwa sinagogi la Kiyahudi (huenda katika Rumi) kwamba waamini wawe kama washiriki. Maonyo haya yanalekezwa kwa makundi mawili, kundi la Wayahudi waaminio (neno "ninyi" la sura ya 6), kwao hakuna "kusita/kurudi nyuma" (kama vile Ebr. 10:38) na kwa kundi la wasio amini (neno "wale" la sura ya 6) kumkiri/kuungama Yesu kama Masihi na makundi yote kuumbtia Ukristo kwa ukamilifu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) WAEBRANIA 13:25**

<sup>25</sup> Neema na iwe nanyi nyote.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Ikiwa Waebrania ni waraka, ambapo unaonekana kuwa dhahiri kutokana na sura ya 13, kwa nini hakuna salamu za ufunguzi?
2. Je! sura 13 unawaakisi Wayahudi wasio amini au walimu wa uongo?
3. Je! Sura hii inawazungumzia "viongozi" wa Kikristo?
4. Ni kwa namna gani mstari wa 23 unakibainisha kipindi halisi cha kitabu cha Waebrania?

# MAELEZO MAFUPI YA ISTILAHI ZA VISARUFI VYA KIYUNANI

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichobobe, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Meditarania ilianzishwa na Alexandra mkuu (336-323 B.K) na ikadumu mpaka miaka ya (300 K.K-B.K 500). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusini ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusini

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenye (isimu ya mpangilio wa maneno)

## I. NJEO

- A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa "utimilifu" au "utoutimilifu"
  1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukueiezwa.
  2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.
- B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
  1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
  2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA
  3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA TIMILIFU
  4. Kinatokea –WAKATI ULIPO
  5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
  6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno "okoa." Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- "okolewa" (Rum 8:24)

2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA- "ameokolewa na matokeo yake yanaendelea" (Efe 2:5,8)
  3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- "anaokolewa" (kama vile 1Kor 1:18; 15:2)
  4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- "ataokolewa" (kama vile Rum 5:9,10; 10:9)
- C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO "hakuna madoido" kilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida "kisichoainishwa" "kisichotambulika" "kisichochoka." Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
1. NJEO YA WAKATI ULIOPITA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPITA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yalioendelea kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, "umekuwa na unaendelea kuokolewa."
  2. NJEO YA WAKATI ULIOPITA AINISHI. Hii ilikuwa kama nje ya WAKATI ULIOPITA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: "Petro alikuwa akisimama nje mlangoni" (Yoh 18:16)
  3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: "kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi", "kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi" (1Yoh 3:6 & 9).
  4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njeo hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPITA na WAKATI ULIOPITA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: "kwa hiyo Yerusalem yote waliendelea kumwacha" au "Yerusalem yote wakaanza kumwacha"(Mt3:5)
  5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualakini wa tukio. Mfano: "Heri wale....wata..."(Mt 5:4-9).

## II. IRABU

- A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA
- B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.
- C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipyia la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
  1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (kama vile Mt. 1:22; Mdo 22:30)
  2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (kama vile Mt 1:22)
  3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
  4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.
- D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitizia KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;

1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenyewe. Mfano: “kajiangika mwenyewe” (Mt 27:5)
2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenyewe. Mfano: “shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru” ( 2Kor 11:14)
3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: “walishauliana wao kwa wao” (Mt 26:4)

### III. DHAMIRA (au “NAMNA”)

- A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEGEMEZA, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI YA UCHAGUZI).
  - B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna pekee ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.
  - C. DHAMIRA TEGEMEZA kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utotauti ni kuwa UTEGEMEZA unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno “ingalikuwa”, “ingaliweza”, “yawezekana” au “yenye uwezo”.
  - D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambaio kinadharia unawezekana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEGEMEZA. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipy. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. “yawezekana isiwe” (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano (kama vile Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes 1:38, 20:16, Mdo. 8:20 na 1Thes 3:11
  - E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitizia juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPA na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipy.
  - F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipy la Kiyunani, mara nyingi vikielezewa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinayofanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.
  - G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au “kisichotambulika” cha Kuingiza matoeko. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambaio mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.
- IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;
- A. Friberg, Barbara na Timothy. Analytical Greek New Testament. Grand Rapids: Baker 1988
  - B. Marshall, Alfred. Interlinear Greek-English New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1976
  - C. Mounce, William D. The Analytical Lexicon to the Greek New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1993
  - D. Summer Ray. Essential of the New Testament Greek Nashville: Broadman 1950
  - E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kuitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

## V. NOMINO

- A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile liloshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyeshwa na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.
- B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;
1. UHUSIKA WA KIIMA ultumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI “kuwa” au “kufaa”
  2. UHUSIKA MILIKISHI ultumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ultoa kivumishi au thamani ya nenolilofanana nalo. Ulijibu swalii, “aina gani?” mara nyingi ulielezewa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza “ya/za”
  3. UHUSIKA WA KUONDOA ultumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ultumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezewa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza “kutoka”.
  4. UHUSIKA WA WAKATI ultumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ya”.
  5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ndani, juu, ni, katii, kwa, juu ya na mbali na”
  6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno “kwa” au “enye”
  7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU uliusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali “kwa umbali gani” au “kwa namna gani”
  8. UHUSIKA WA KAULI ultumika kuelezea moja kwa moja.

## VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

- A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra (vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.
- B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament
1. Viunganishi vya wakati
    - (a) *epeī, epeđē, hopote, hōs, hote, hotan* (TEGEMEZI)- “lini”
    - (b) *heōs-* “wakati”
    - (c) *hotan, epan* (TEGEMEZI)- “kila, wakati wowote”
    - (d) *heōs, achri, mechri* (Tegemezi)- “mpaka”
      - a. *priv* (kitenzijina)- “kabla”
      - b. *hōs-* “tangu”, “lini”, “kama”.
  2. Viunganishi venye mantiki
    - a. Kusudi/dhumuni
      - 1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs* (TEGEMEZI) *hōs-* “ya kwamba”, “kuwa”

- 2) *hōste*(KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
- 3) *pros*(KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
- b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)
- (1) *hōste*(ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- “ili kwamba”, “hivyo”
  - (2) *hiva*(TEGEMEZA)- “ya kwamba”
  - (3) *ara-* “kwa kiasi hicho”
- c. Chanzo au sababu
- 1) *gar*(chanzo/athari au sababu/hitimisho)- “kwa”, “kwa sababu ya”
  - 2) *dioti, hotiy-* “kwa sababu ya”
  - 3) *epei, epeideē, hōs-* “tangu”
  - 4) *dia*(ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- “kwa sababu ya”
- d. Maamuzi
- (1) *ara, poinun, hōste-* “kwa hiyo”
  - (2) *dio*(KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- “kwa sababu ipi”, “kwa nini”, “kwa hiyo basi”
  - (3) *oun-* “kwa hiyo basi”, “kwa kiasi hicho”, “hatimaye”, “hivyo basi”
  - (4) *tinoun-* “kufuatana na”
- e. –a kinyume au tofauti
- (1) *alla*( yenye KINYUME thabiti)-“lakini”, “isipokuwa”
  - (2) *de-* “lakini”, “ingawa”, “bado”, “kwa upande mwinge”
  - (3) *kai-* “lakini”
  - (4) *mentoi, oun-* “ingawa”
  - (5) *plēn-* “hata hivyo” (haswa katika Luka)
  - (6) *oun-* “ingawa”
- f. Ulinganifu
- (1) *hōs, kathōs* (ingiza vishazi linganifu)
  - (2) *kata*(kwa muunganiko, *katho, kathoti, kathōsper, kathaper*)
  - (3) *hasos*(katika Kiebrania)
  - (4) *ē-* “kuliko”
- g. Enye mlolongo au mtiririko
- (1) *de-* “na”, “sasa”
  - (2) *kai-* “na”
  - (3) *tei-* “na”
  - (4) *hina, oun-* “kile”
  - (5) *oun-* “kasha”(katika Yohana)
3. Matumizi yenye mkazo
- a. *alla-* “kwa hakika”, “naam”, “kwa kweli”
  - b. *ara-* “hakika”, agharabu”, “kweli”
  - c. *gar-* “lakini kweli”, “aghارابو”, “hakika”
  - d. *de-* “hakika”
  - e. *ean-* “hata”
  - f. *kai-* “hata”, “hakika”, “kweli”
  - g. *mentoi-* “hakika”
  - h. *oun-* “kweli”, “kwa hali zote”

- A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiriwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.
- B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiliwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezewa kwa neno “kama.” Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa “tangu”(cf. Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(cf. Mt 12:27)
- C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa “inayopingana na ukweli”. Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
  - 1. “Kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng’ang’ania yeye, lakini hawezi (Thess 7:39)
  - 2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
  - 3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)
- D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi “hiki”. Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16
- E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipy. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

### VIII. VIZUIZI

- A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIPOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: “msijiwekee hazina yenu duniani.....”(Mt 6:19); “msisumbukie maisha yenu.....” ( Mt 6:25); “wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi.....”(Rum 6:13); “wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe 4:30) na “tena msilewe kwa mvinyo.....”(Ef 5:18)
- B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa “udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo” baadhi ya mifano: “msidhani ya kuwa.....”(Mt 5:17); “msisumbuke.....”(Mt 6:31); “msiuonee haya.....”(2Tim 1:8)
- C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenyе msisitizo hasi. “kamwe, katu” au “kwa hali ye yote ile”. Baadhi ya mifano: “kamwe, hataonja mauti.....”(Yoh 8:51); “hakika, kamwe.....”(1Kor 8:13)

### XI.

- A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno “wale, Yule,ile” kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya “muonyeshwaji”, ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai. Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipy. KIBAINISHI CHA WAZI pia chawenza kutenda
  - 1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
  - 2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
  - 3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchouunganisha. Mfano: “Mungu ni Roho” Yoh 4:24, “Mungu ni nuru” 1Yoh 1:5; “Mungu ni upendo” 4:8,16

- B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno “a” herufi ya kwanza ya alfabeti au “an” mbadala wa “a” kwenye irabu zinazoanza na herufi kama “e”, “h”. Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chawea kumaanisha;
1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
  2. Mlengo juu ya aina ya kitu
- C. Waandishi wa Agano Jipywa walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kiliviyotumiwa.

X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYWA LA KIYUNANI

- A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwininge kwenye Agano Jipywa. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.
- B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)
- C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.
1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegeMEA kuonyesha.
    - a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
    - b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
    - c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani
  2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni
    - a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi
      - (1) KITENZI
      - (2) KIIMA
      - (3) SIFA
    - b. VITENZI elekezi
      - (1) KITENZI
      - (2) KIIMA
      - (3) KISHAMILISHI
      - (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
      - (5) KIRAI HUSISHI
    - c. Virai vya NOMINO
      - (1) NOMINO
      - (2) KIVUMISHI
      - (3) KIRAI HUSISHI
  3. Mpangilio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:
    - a. “walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuumi wa shirika” (Gal 2:9) kirai “mkono wa kuumi wa shirika” imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
    - b. Pamoja na Kristo (Gal 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.
    - c. “ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi” (Ebr 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.
- D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na

1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: "mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe....."(Mt 28:20)
2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
  - a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff(ikisisitizia orodha)
  - b. Yohana 14:1 (maada mpya)
  - c. Rumi 9:1 (kifungu kipyta)
  - d. 2Kor 12:20 ( inasisitizia orodha)
3. Urudiaji wa maneno au virai vilivymo katika mazingira tajwa. Mfano: "usifiwe utukufu wa neema yake" (Efe 1:6, 12 & 14). Kirai hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
  - a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama "lala" kwa kifo (Yoh 11:11-14) au "nyayo" kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)
  - b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama "ufalme wa mbingu" (Mt 3:21) au "sauti toka mbinguni" (Mt 3:17)
  - c. Maumbo ya hotuba
    - (1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)
    - (2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)
    - (3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)
    - (4) Kejeli (Gal 5:12)
    - (5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)
    - (6) Mvumo unaokaa kati ya maneno
      - (a) "kanisa"
        - i. "kanisa" (Efe 3:21)
        - ii. "Kuitwa" (Efe 4:1,4)
        - iii. "Kuitwa" (Efe 4:1,4)
      - (b) "huru "
        - i. "Mwanamke huru" (Gal 4:31)
        - ii. "uhuru" (Gal 5:1)
        - iii. "huru" (Gal 5:1)
    - d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana
      - (1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno "chakula" (Yoh 4:31-34)
      - (2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno "hekalu" (Yoh 2:19; Mt 26:61)
      - (3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno "chukia" (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)
      - (4) "wote" dhidi ya "wengi". Linganisha Isa. 53:6 ("wote") na 53:11 & 12 ("wengi"). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.
  5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: "Bwana Yesu Kristo".
  6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*
    - a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa "sawa"
    - b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUJIREJEA- "mwenyewe jinsia ya ME" "mwenyewe jinsia ya KE" au "yenewe/chenyewe"

E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:

  1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.

2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa “neno kwa neno” (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na “mfanano wa karibu” (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)  
Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.
3. Utumiaji wa *The Ephasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).
4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.
  - a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901
  - b. *Young's Lateral Translation of the Bible* cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usomaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maeleo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti nay a kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasomaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usomaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasihi, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.

# Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.

Mhutasari ufuatao utahusika

- I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
    - A. Agano la Kale
    - B. Agano Jipya
  - II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya “maoni dhaifu” pia yanaitwa “uhakiki wa maandiko”
  - III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye
- I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza
- A. Agano la Kale
    1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pemberi, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na viliihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
    2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na “Herufi Aristeas.” Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
    3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitetu waitwao “ Esene”. Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nydingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
    4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
      - a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
        - (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, “Kama vile wengi watakavyo shangazwa Naye.”
        - (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, “Bado kama vile wengi walivyo staajabishwa Nawe.”
        - (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
          - (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, “hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye”
          - (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, “hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi”
      - b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
        - (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, “ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama.”
        - (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, “ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana.....”
      - c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
        - (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), “Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.”

- (2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), “Ataona ..... ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki.”

B. Agano Jipyा

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipyा la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuzwa. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaiita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipyा zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili B.K., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne B.K. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipyा Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipyा hazimaanishi kuwa sio ya kuijendesa yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinukuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinacho julikana kwa herufi ya Kiebrania  $\aleph$  (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipyा la Kiyunani. Ni aina ya “Maandishi ya Kialekzandria.”
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alekzandrianus, kijulikanacho kama “A” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alekzandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama “B” au (03), iliyopatika katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipyा la Kiyunani. Yalikuwa aina ya “Maandishi ya Kialekzandria.”
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama “C” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama “D” au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya karnre ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinacho julikana kama “Maandishi ya Magharibi.” Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipyा la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
  - a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
    - (1)  $P^{75}, P^{76}$  (yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
    - (2)  $P^{46}$  (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
    - (3)  $P^{72}$  (yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
    - (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipyা
    - (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
    - (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni  $\aleph, C, L, W, 33$
  - b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
    - (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
    - (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
    - (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsiri za kale za Kisiria
    - (4) Andiko D la Machapisho ya kale “Bezae” ilifuata aina ya maandishi haya
  - c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
    - (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS

- (2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
- (3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
- (4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipy
- d. aina ya nne iwezekanayo ni ya "Kikaizari" kutoka Palestina
  - (1) kwanza inaonekana katika Mrko tu
  - (2) baadhi ya shuhuda zake ni P<sup>45</sup> na W

II. Matatizo na nadharia ya "ukosoaji dhaifu."

- A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea
  - 1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)
    - a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
      - (1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
      - (2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)
    - b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutoke (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenyenye mfananowa sauti za maneno ya Kiyunani.
    - c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.
  - 2. makusudi
    - a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
    - b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
    - c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
    - d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi (kama vile I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
    - e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili (Yohana 5:4)
- B. Mafundisho muhumu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)
  - 1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
  - 2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
  - 3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
  - 4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
  - 5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
  - 6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
  - 7. nukuu mbili ambazozinzsaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha
    - a. kitabu cha J. Harold Greenless, *Introduction to New Testament Textual Criticism*, "Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning'inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na mwanafunzi wa Agano wa Jipy yanapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimafundisho kuliko msukumo asilia" (uk. 68).

- b. W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye* (Criswell) haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo “angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri.” Criswell alisema “Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa...Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza...” Mababa wa uzao wa SBC wasio wakosaji walidai kuwa “kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu” pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda (Mt. 27 na Matendo 1): “Ni maoni tofauti ya kujinyonga,” Criswell alisema “Kama iko katika Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia.” Criswell aliongeza, “Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana. Ni yenyenye nguvu na kuu...”

III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)

- A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi

1. *Biblical Criticism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
2. *The Textual of the New Testmemt: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
3. *Introduction to New Testament Ttxtual Critism*, na J. H Greenlee

## UFAFANUZI/FAHARASA

**Uasilihaji.** Hili ni moja kati ya maoni ya kale ya uhusiano wa Yesu na Uungu. Kimsingi inadai kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida kwa kila namna na alichukuliwa na Mungu kwa kazi maalumu katika ubatizo wake (Mt. 3:17; Marko 1:11) au katika ufufuo Wake (kama vile Rum.1:4). Yesu aliyaishi maisha haya kama mfano amba Mungu, kwa kiasi chake, (ubatizo, ufufuo) uliyomuasilisha Yeye kama "mwana" Wake (Rum.1:4 Flp. 2:9). Hili lilikuwa kanisa la mwanzo na maoni ya watu wa karne ya nane. Badala ya Mungu kuwa mwanadamu (umbo la kibinadamu) akalirejeresta hili na sasa mwanadamu anakuwa Mungu!

Ni vigumu kusema namna gani Yesu, Mungu Mwana, Uungu uliokuwepo kabla alivyozawadiwa au kuwa mbadala kwa ajili ya maisha yenyenye mfano. Kama Yeye alikuwa tayari ni Mungu, ni kwa namna gani Yeye alitolewa kama zadiwa? Kama Yeye alikuwa na utukufu wa Kiungu wa awali ni kwa namna gani Yeye angeliheshimiwa zaidi? Ingawa ni vigumu kwetu sisi kutambua, kwa namna Baba alivyomuheshimu Yesu katika dhana maalumu ya ukamilifu Wake wa kuyatimiza mapenzi ya Baba.

**Shule ya Alexandria.** Njia hii ya ukalimani wa kibiblia ilikuzwa katika Alexandria, Misri katika karne ya pili B.K. Inatumia misingi ya kanuni za ukalimani ya Philo, ambaye alikuwa mfuasi wa Pilato, mara nydingi inaitwa njia ya kiistiari. Ilitawaliwa katika kanisa hadi wakati wa Marekebisho. Watetezi wake zaidi walikuwa Origen na Augustine. Tazama Moisea Silva, *Has The church Misred The Bible?* (Academic, 1987)

**Ufuasi wa Alexandria.** Haya ni machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano kutoka mji wa Alexandria, Misri ikijumuisha Agano la Kale, lillothibitishwa, pamoja na Agano Jipy. Ni moja ya ushahidi wetu mkubwa katika Agano Jipy zima la Kiyunani (isipokuwa sehemu za kitabu cha Mathayo, Yohana, na II Wakorintho). Wakati ambapo machapisho haya, ambayo yanapewa alama "A, na machapisho ya alama "B" (ya Vatican) yanaafiki juu ya usomaji unaofikiriwa kuwa ya mwanzo na baadhi ya wasomi.

**Istiari.** Hii ni aina ya ukalimani wa kibiblia ambayo kiasili ulianzishwa ndani ya dini ya Kiyahudi huko Alexandria. Ilienezwa na Philo wa Alexandria. Msukumo wake wa msingi ni shauku ya kufanya uhusiano wa Maandiko na utamaduni wa mtu au mfumo wa kifalsafa kwa mpangilio wa historia ya Biblia na/ au muktadha wa maandishi. Inatafuta uficho au kweli ya kiroho nyuma ya kila kifungu cha maandiko. Inapaswa kukubaliwa kwamba Yesu, katika Mathayo 13, na Paulo, katika Wagalatia 4, alitumia istiari kuiwasilisha kweli. Kwa hali yoyote, hii, ilikua katika muundo wa taipolojia (uanishi), na si istiari halisi.

**Uchanganuzi wa misamiati.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti ambacho kinamruhusu mtu kutambua kila muundo wa Kiyunani katika Agano Jipy. Ni mkusanyiko, katika mpangilio wa alfabeti za Kiyunani, wa kimuundo na maelezo ya msingi. Katika muunganiko kwa tafsiri mbalimbali, unaruhusu usomaji wa wasio Wayunani kuchambua visarufi vya Agano la Kale la Kiyunani kimsamiati na kimuundo.

**Ushabihiano wa Maandiko.** Hiki ni kifungu kinachotumika kueleza wazo kwamba Biblia nzima imefunuliwa na Mungu, na ni, kwa hiyo sio mkanganyiko bali ukamilifu. Ukubalifu wa dhanio hili ni msingi kwa matumizi yanayo fanana na vifungu vya maneno katika kufasiri maandiko ya biblia.

**Utata.** Hii inarejea juu ya mashaka ambayo yanaleta matokeo katika nyaraka zilizoandikwa ambapo kuna maana mbili ziwezekanazo au zaidi au wakati vitu viwili au zaidi vinakuwa vikirejewa kwa wakati mmoja. Inawezekana kwamba Yohana anatumia utata huu kwa makusudi.

**Elimu ihusuyo tabia ya mwanadamu.** Inamaanisha kuwa na "tabia zinazohusiana na wanadamu." neno hili linatumika kueleza lugha zetu za kidini kumuhusu Mungu. Linatokana na neno la Kiyunani kumuhusu mwanadamu. Inamaanisha kwamba tunazungumza kuhusiana na Mungu kana kwamba Yeye alikuwa mwanadamu. Mungu anaelezwa katika umbo la mwili lionekanalo, kijamii, maneno ya kisaikolojia ambayo yanahusiana na wanadamu (kama vile Mwa. 3:8; II Wafalme 22: 19-23). Hii, hakika ni mshabihiano pekee. Hata hivyo maarifa yetu kumhusu Mungu, ingawa ni kweli, lakini yamewekewa mipaka.

**Shule ya Antioquia.** Hii njia ya ufasiri wa kibiblia ilianzia huko Antioquia, Syria katika karne ya tatu B.K. kama kuonyesha hisia juu ya utaratibu wa kiistiani wa Alexandria, huko Misri. Msingi wa msukumo wake uliangalia maana ya kihistoria ya Biblia. Iilitafasiri Biblia kama fasihi ya kawaida ya mwaadamu. Shule hii ilikuwa imejumuishwa katika ubishi kumhusu Kristo kama alikuwa na asili mbili (mafundisho kuhusu uwili wa Yesu) au asili moja (Mungu kamili na mwanadamu kamili). Iilitambuliwa kama maoni ya kupinga Ukristo kwa Kanisa Katoriki la Rumi na kuhamishiwa Uajemi lakini shule ilikuwa na umuhimu mdogo. Misingi ya kanuni zake za ufasili wa kibiblia baadaye ikawa kanuni za ufasili wa watu waliioleta mageuzi kwenye dini ya Kiprostanti (Luther and Calvin).

**Kutabaini.** Hii ni moja mionganini mwa njia tatu za uwasilishaji wa neno uliotumika kudokeza uhusiano kati ya misitari ya ushairi wa Waembrania. Unahusiana na misitari ya ushairi yenyenye kukinzana kimaana (kama vile Mit. 10:1; 15:1).

**Fasihi ya mafunuo.** Hii ilikuwa ni namna tanzu ya Wayahudi wenyenye nguvu, hata kuonekana ya kipekee. Ilikuwa ni aina ya uandishi wenyenye mafumbo uliotumika nyakati za uvamizi na umiliki dola yenyenye nguvu ya Kiyahudi. Inafikiriwa kwamba mtu, muumbwaji aliyekombolewa na Mungu na kuyatawala matukio ya ulimwengu, na kwamba Israeli ina upendeleo maalumu na uangalizi kutoka Kwake. Fasihi hii inahaidi ushindi mkuu na kupitia juhudhi pekee za Mungu.

Ni ishara kuu na ya ubunifu sana yenyenye maneno ya mafumbo. Mara nydingi ilieleza ukweli katika rangi, tarakimu, maono, ndoto, upatanishi wa kimalaika, alama za siri za maneno, mara nydingi uwili wa vitu kati ya mema na mabaya.

Baadhi ya mifano tanzu hapa ni (1)katika Agano la Kale, Ezekiel (sura ya 36-48), Danieli (sura ya 7-12), Zekaria; na (2) Katika Agano Jipya, Mathayo 24;Marko 13; II Wathesalonike 2 na Ufunuo.

**Mtetezi.**Hili linatoka katika mzizi wa neno la Kiyahudi “ulinzi wa kisheria.” Haya ni mafundisho ndani ya theolojia ambayo yanatafuta kutoa ushahidi na uwiano wa hoja za kifikra kwa imani za Kikristo.

**Haki ya kutangulia.**Kimsingi huu ni ukaribu wa maana ya neno “dhanio.” Inahusisha ufikiliaji wa wa maana za awali zilizokubalika, kanuni au nafasi iliyo sadiki kwa kweli paspo uchambuzi au uchunguzi.

**Ufuasi wa Arius.**Arius alikuwa mhudumu ndani ya kanisa huko Aexandria, Misri katika karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya nne. Alikubali kwamba Yesu alikuwepo hapo kabla lakini si kwa Uungu (si sawa na asili ya Baba), huenda kwa kufuata Mithali 8:22-31. Alipingwa na askofu wa Alexandria, ambaye alianza (318 B.K) mabishano yalidumu kwa miaka mingi. Ufuasi wa Arius ulikuja kuwa kanuni rasmi katika Kanisa la huko Mashariki. Baraza la Nicaea katika 325 B.K.walimshtumu Arius na kuutetea usawa na Uungu kamili wa Mwana.

**Jamii ya watu wakuu.** Alikuwa mmoja wa wanafalsafa wa kale wa Ugiriki, mwanafunzi wa Pilato na mwalimu wa Iskanda Mkuu.Ushawishi wake, hata sasa, umefika maeneo mengi yanayofundisha mafunzo ya kisasa. Hii ni kwa sababu alisistiza maarifa ni kupitia uchunguzi na upambanuzi. Hii ni moja ya itikadi ya njia za kisayansi.

**Miandiko binafsi.** Hili ni jina lililotolewa kwa maandishi ya mwanzo ya Biblia. Maandiko haya asilia yaliyoandikwa kwa mkono yote yamepotea. Baadhi tu ya nakala zimesalia. Hiki ndio chanzo cha utofauti wa maandishi mbalimbali katika machapisho ya Kiebrania na Kiyunani.

**Maandiko ya asili ya karne ya sita.** Haya ni machapisho ya Kiyunani na Kiratini ya karne ya sita B.K. Yanasanifiwa na alama “D.” Imejumuisha Injili na Matendo na baadhi ya Nyalaka za Jumla. Inabainishwa na nyongeza nydingi za maandishi yenyenye ueledi. Inaunda msingi wa “uundaji wa maandiko”ambayo ni tamaduni za machapisho makuu ya Kiyunani nyuma ya toleo la King James Version.

**Upendeleo.** Hili ni neno linalotumika kueleza maelezo yenyenye nguvu kuhusiana na jambo au mtazamo fulani. Ni mtizamo ambao uadilifu ndani yake hauwezekani kungalia kitu au maoni Fulani. Ni madhara ya kieneo.

**Mamlaka ya Kibiblia.** Ni neno lililotumika katika maana maana ya kipekee. Linaelezwa kama uelewa wa kile alichokisema mwandishi asilia katika siku zile zake na kutumia ukweli huu katika siku zetu. Mamlaka za Kibiblia mara nyingi zinaelezwa kuitazama Biblia yenewe kama kiongozi chetu chenye mamlaka. Hata hivyo, katika hali ya sasa, utafasiri sio sahihi. Nimeweka mipaka juu a dhana ya Biblia kama ilivyotafsiriwa na kanuni za njia ya historia ya kisarufi.

**Orodha ya vitabu vya Agano Jipya.** Hili ni neno linalotumika kuelezea maandishi yanayosadikiwa kuvuviwa kipekee. Limetumika kuangalia maandiko yote ya Agano la kale na Agano jipya.

**Kristo kama kitovu.** Ni neno lililotumika kuonyesha Kristo kama kitovu cha mambo yote. Na lilitumiwa kuunganisha dhana ya kwamba Yesu ni Bwana wa Biblia zote, Mawazo ya Agano la Kale dhidi yake na utimilifu wa malengo yake.

**Fasiri.** Hii ni aina pekee ya utafiti wa kitabu. Inatoa kwa pamoja usuli wa kitabu cha Biblia. Pia inajaribu kuelezea maana ya kila kipengele cha kitabu. Baadhi inatazamisha matumizi, wakati mwiingine zinahusiana na andiko katika hali ya kiufundi. Vitabu hivi ni vya manufaa, lakini lazima vitumike baada ya mtu kufanya uchunguzi wake wa awali. Tafsiri za watoa maoni lazima zisikubalike kuhakiki. Ukilinganisha fasiri nyingi toka kwa mitizamo ya wanathiolojia tofauti utaona inasaidia.

**Itifaki.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti kwa usomaji wa Biblia. Inaorodhesha kila utokeaji wa neno katika Agano Jipya na la Kale. Inasaidia katika njia tofauti: (1) kubainisha maneno ya Kiebrania au Kiyunani yaliyoko nyuma ya maneno ya kiingereza; (2) kulinganisha kurasa ambapo neno lile lile la Kiebrania au Kiyunani limetumika; (3) kuonyesha mahali ambapo maneno mawili tofauti ya Kiebrania au Kiyunani yametafasiriwa kwa neno lie lile la kiingereza; (4) kuonyesha mwendelezo wa kutumia maneno fulani katika vitabu fulani au maandishi; (5) inasaidia mtu kupata somo katika Biblia (kama vile Walter Clark's *How to use New Testament Greek Study Aids*. kurasa za 54-55).

**Magombo ya Bahari ya Chumvi.** Inarejerea mlolongo wa maandiko ya kale yaliyoandikwa katika Kiebrania na Kiarama ambayo yalipatikana karibu na Bahari ya Chumvi mwaka 1947. Palikuwepo na maktaba za kidini ya Kiyunani ya karne ya kwanza. Msukumo wa umilikaji toka Rumi na vita ya kinazi vya miaka ya sitini viliwasababisha wao kuficha magombo yaliyokuwa yamefungashwa ndani ya vyungu kwenye mapango au mashimo. Inatusaidia sisi kuelewa muundo wa kihistoria wa palestina ya karne ya kwanza na kuthibitisha maandiko ya mossoretes kuwa yako sahihi kwa kiasi fulani enzi ya awali kabla ya Yesu K.K.

**Mambo yaliyofasiliwa.** Njia hii ya kimantiki au ufikiliaji inatokana na kanuni ya pamoja ya matumizi maalumu kwa njia ya wazo. Hii ni kinyume toka ufikiliaji wa mambo yaliyofasiriwa, ambayo yanaangazia njia ya kisayansi toka kwenye uchunguzi maalumu kwenda hitimisho la pamoja (nadharia)

**Mbinu pembuzi.** Hii ni njia ya kufikilisha ambapo kile kinachoonekana kuleta mkanganyiko au mafumbo huwekwa pamoja katika hali ya mkazo, ikitafuta jibu la pamoja ambalo linajumuisha pande zote za fumbo. Mafundisho mengi ya Biblia yana upembuzi unaofanana, kuamuliwa kabla-mapenzi huru, ulinzi-ustahimilivu, imani-kazi; uwamuzi-ufuasi; uhuru wa Mkristo-uwajibikaji wa Mkristo

**Wayahudi waliotawanyika katika mataifa mengine.** Hili ni neno la kiufundi la Kiyunani lililotumiwa na wapalestina wa Kiyahudi kuelezea wayahudi wengine walioishi nje ya mipaka ya kijiografia ya nchi ya ahadi.

**Mlinganyo wa nguvu.** Hii ni nadharia ya ufasili wa Biblia. Tafasili ya Biblia inaweza kuangaliwa kama mwendelezo toka ushirika wa "neno kwa neno", mahali ambapo neno la Kiingereza lazima liwekwe kwa kila neno la Kiyunani au Kiebrania, kwenye "ufasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa angalizo la chini ya neno au kifungu cha awali. Katika nadharia hizi mbili ndipo pana "mlinganyo wa nguvu" unaojaribu kuchukua neno la mwanzo kwa umakini

wake, lakini limefasiliwa katika miundo ya visarufi nya kisasa na nahau. Majadiliano mazuri ya kweli ya hizi nadharia mbali mbali za fasili zinapatikana katika makala ya Fee na Stuart *How to Read the Bible For Its Worth*, uk. 35 na katika Robert Bratcher's utangulizi katika Biblia ya TEV.

**Kutofuata mfumo.** Neno hili linatumika katika mahusiano ya uhakiki wa maandiko. Unarejerea kitendo cha kuchagua usomaji toka machapisho tofauti tofauti ya Kiyunani ili kufika kwenye neno linalotakiwa kuwa karibu na maandiko ya mwanzo.

**Kupotosha maana.** Hili neno ni kinyume cha neno fasili ya maandiko. Kama fasili ya maandiko ni "kuondoa" kulingana na kusudio la mwandishi wa awali, basi neno hili litamaanisha "kuingiza" wazo la kigeni.

**Elimu ya asili na historia ya neno.** Hii ni dhana ya usomaji wa neno unaojaribu kuyakinisha maana ya awali ya neno. Kutokana na chanzo cha maana hii, utumiaji wa kipekee unaotambulika kirahisi katika ufasili, elimu ya asili na historia ya neno sio kiini cha mtizamo, mbali na maana ya wakati ule ule na utumiaji wa neno.

**Fasili ya maandiko.** Hili ni neno la kiufundi kwa utendaji wa kutafasili kifungu maalumu. Inamaanisha "uondoaji nje" (wa neno) ukidokeza kwamba dhumuni letu ni kuelewa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika uelewa wa muundo wa kihistoria, mazingira ya kifasihi, sintaksi na maana ile ile ya neno.

**Namna ya Uwasilishaji.** Hili ni neno la Kifaransa ambalo limedokeza aina mbali mbali ya fasihi. Msukumo wa neno hili ni mgawanyiko wa miundo ya fasihi katika namna mbali mbali ambazo zinashirikishana tabia za aina moja. Usimuliaji wa kihistoria, mashairi, mithali, ufunuo na uandikishaji.

**Maarifa ya utambuzi/mafuno.** Zaidi ya maarifa tulionayo kuhusu imani potofu yameletwa toka maarifa ya utambuzi wa maandiko katika karne ya pili. Ingawa mawazo ya awali yalikuwepo katika karne ya kwanza (na kabla). Baadhi ya maelezo ya mafuno ya kinazi ya Valentino na Cerinthin ni (1) mwili na roho vyote vilikuwepo kabla. mwili ni mwovu, na Roho ni nzuri. Mungu, ambaye ni Roho hawesi kuhushishwa moja kwa moja na mwili mwovu (2) kuna asili (*eons au* daraja la kimalaika) kati ya Mungu na mwili. Wa mwisho au wa chini alikuwa YAHWE wa Agano la kale, ambaye aliuumba ulimwengu (*kosmos*); (3) Yesu alikuwa mwanzilishi kama YAHWE lakini akiwa juu ya viwango, karibu na Mungu wa kweli. Wengine walimweka juu zaidi lakini bado yu chini kuliko Mungu na hakika asiye na mwili wa Kiungu (kama vile 1:14). Kwa vile mwili ni mwovu, Yesu asingelikuwa na mwili wa kibinadamu na bado akawa na hali ya Kiungu. Alikuwa ni nafsi ya kufikirika (kama vile 1Yoh 1:1-3; 4:1-6); na (4) wokovu ulipatikana kuititia imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu, yaliyojulikana na watu maalumu. Maarifa (maneno ya siri) yalihiitajika kuititia ulimwengu wa kimbingu. Washikiliaji sana wa kisheria za Kiyahudi nao pia walihitaji kumfikia Mungu. Walimu wa uongo wenye maarifa ya utambuzi walitetea miundo miwili kinzani ya kimaadili (1) baadhi ya stadi za maisha hazikuhusiana na wokovu. Kwao wokovu na utakaso ulifumbwa kwenye maarifa ya siri (neno la siri) kuititia ulimwengu wa kimalaika (*eons*); au (2) kwa wengine stadi ya maisha ilikuwa muhimu katika wokovu. Walisisitiza miundo ya maisha kama kielelezo cha utakaso wa kweli.

**Kanuni za ufasili.** Hili ni neno la kiufundi kwa kanuni zinazoongoza ufasili wa maandiko. Ni seti ya mwongozo maalumu na sanaa/kipawa. Kibiblia, au takatifu, kanuni za ufasili zimegawanyika kwa namna mbili; kanuni za ujumla na kanuni maalumu. Hizi zinahusiana na aina tofauti za fasihi zinazopatikana katika Biblia. Kila aina tofauti (tanzu)zina mwongozo wake wa kipekee lakini zinashirikiana na baadhi ya dhana na namna ya utafasili.

**Uhakiki juu ya maandiko.** Hii ni namna ya utafasili wa kibiblia ambao unatazamisha kwenye muundo wa kihistoria na umbo la fasihi hasa hasa katika kitabu cha Biblia.

**Nahau.** Neno hili linatumika kwenye vifungu vinavyopatikana katika tamaduni tofauti zenyetmaana maalumu na sio vilivyojusiana na maana ya kawaida ya maneno binafsi. Maana ya mifano ya kisasa ni: "iliwu ni vizuri sana" au "umeniu". Biblia pia inajumuisha aina hizi za vifungu.

**Nuru.**Hili ni jina lililotolewa kwenye dhana kuwa Mungu aliongea na mwanadamu. Dhana nzima kwa kawaida imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda kwenye historia ya binadamu: (2) uvuvio-ametoa utafasili sahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) nuru –ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Kudukiza.** Hii ni njia ya kimantiki au kufikiria inayotoka sehemu Fulani na kuenea sehemu yote. Ni njia ya kutegemea majoribio ya kisasa. Kimsingi, huu ni mjongeo wa watu wenyе hadhi ya juu.

**Unasaba.** Hii ni aina ya chombo cha uchunguzi kinachoruhusu wale wasiojua lugha za kibiblia kuchunguza maana yake na muundo. Inaweza tafasili ya kiingereza kwenye ngazi ya neno kwa neno chini ya lugha ya awali ya kibiblia. Chombo hiki kinajumuishwa na “misamiati ya kiuchunguzi” ambayo inatoa miundo na maelezo ya msingi ya Kiebrania na Kiyunani.

**Uvuvio.**Hii ni dhana ya kwamba mungu aliongea na mwanadamu kwa kuwalinda waaandishi wa kibiblia kwa usahihi na uwazi ili kuweka kumbukumbu ya mafunuo yake. Dhana nzima imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) uvuvio-ametoa utafasiri wasahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu Fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) Nuru-ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Lugha ya maelezo.** Hii inatumika pamoja na nahau pale Agano la Kale lilipoandikwa. Inaongelewa juu ya dunia kwa namna jinsi vitu vinavyotokea kwenye milango mitanmo ya fahamu. Sio maelezo ya kisayansi hati yakamaanisha kuwepo.

**Ushikiliaji sana wa sheria.** Mwenendo huu umeainishwa kwa msisitizo zaidi juu ya sheria au matambiko. Unajaribu kutegemea juu ya utendaji wa mwanadamu kama njia ya ukubalifu kwa Mungu. Unajaribu kushusha uhusiano na kuinua utendaji, mwote ambamo dhana muhimu ya mahusiano ya kimaagano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mtenda dhambi.

**Tafasili sisisi.** Hili ni jina jingine la mlengo wa kimaandiko na njia za kihistoria za za kanuni za ufasili toka Antiochia. Ina maana kwamba utafasili unahuksika katika maana dhahili za lugha ya mwanadamu, ingawa inaendelea kutambua uwepo wa lugha za kitamathali.

**Fasihi tanzu.** Hii inarejerea kwenye miundo ya utofauti ili kwamba mawasiliano ya uwanadamu yanaweza kuchukuliwa kama vile ushairi au simulizi za kihistoria. Kila aina ya fasihi ina nji/namna yake maalumu ya kanuni ya ufasili kwa kuongezea kwenye kanuni za pamoja kwa fasihi zote zilizoandikwa.

**Sehemu ya fasihi.** Hii inarejerea mgawanyo wa lengo kuu la kitabu cha Kibiblia. Inaweza kuundwa na misitari, aya, au ibara chache. Ni kijumuishi pekee chenye kiini cha somo.

**Lower criticism- Uhakiki wa kawaida wa maandiko.**

**Maandiko ya asili.** Neno hili linahusiana na nakala mbali mbali za Agano jipya la Kiyunani. mara nyingi limegawanyika katika aina tofauti kwa (1) nyenzo iliyotumika kuandikiwa kwayo (mafunjo, ngozi) au (2) muundo wenyewe wa uandishi. Limefupishwa kwa neno “MS” (umoja) au “MSS” (wingi).

**Andishi la kidesturi la Kiebrania la Biblia ya Kiyahudi.** Hii inarejerea karne ya nane B.K maandiko ya asili ya Kiebrania ya Agano la kale yalitolewa na vizazi vya wasomi wa Kiyahudi ambayo yalijumuisha alama za irabu na mihtasari mingine ya maandiko. Yanatengeneza msingi wa neno kwa Agano letu la kale la Kiingereza.

**Mshabihiano wa neno.** Huu ni namna ya msemo ambao jina la kitu linatumika mbadala wa kitu kingine kinachofanana nacho. Kwa mfano “birika linachemka” ki uhalisia inamaanisha “maji yaliyeko kwenye birika yanachemka”.

**Orodha ya vitabu vya Agano jipya.** Hii ni orodha ya vitabu vya sheria za kanisa la Agano jipya. Iliandikwa huko Rumi kabla ya mwaka 200 B.K. Inatoa vitabu ishirini na saba kama vile vile vya Agano Jipya la Waporostanti. Hii wazi kabisa inaonyesha makanisa madogo madogo ya mahali katika sehemu mbali mbali za milki ya Rumi kulikuwa “kiutendaji” pamewekwa sheria za kanisa kabla ya baraza kuu la kanisa la karne ya Nne.

**Ufunuo wa asili.** Hii ni namna ya Mungu mwenyewe kujifunua kwa mwanadamu. Unajumuisha utaratibu wa kiasili (Rum 1:19-20) na dhamila adilifu (Rum 2:14-15). Umeongeleta katika Zaburi 19:1-6 na Warumi 1-2. Unatofautishwa toka kwenye mafunuo maalumu, ambayo kwa mungu mwenyewe ni muhimu kujifunua katika Biblia na mwanae pekee Yesu wa Nazareti. Uangaliaji huu wa kithiolilia unasisitizwa tena na mwenendo wa “dunia ya zamani” kati ya wanasayansi wa Kikristo (kama vile maandishi ya Hagh Ross) wanatumia uangaliaji huu kwa kuthibitisha kuwa kweli yote ni kweli ya Mungu. Ulimwengu ni mlango ulio wazi wa maarifa ya kumjua Mungu; ni tofauti toka kwa ufunuo maalumu (Biblia); unawapa wanasayansi uhuru wa kufanya uchunguzi juu ya wanasayansi wa ulimwengu wa magharibi.

**Ufuasi wa Nestory.** Nestory alikuwa ni mkuu wa familia ya Constantino kwenye karne ya tano. Alifundishwa huko Antioquia ya Shamu na kuthibitisha kwamba Yesu ana asili mbili, moja ni mwanadamu kamili na nyengine ni Mungu kamili. Maoni haya yalichepushwa toka kwenye mtizamo wa asili wa mtu mmoja wa Orthodox kutoka Alexandria. Kusudio kubwa la Nestory lilikuwa ni cheo cha “mama wa Mungu” alichopewa Maria Magdalena. Nestory alipingwa na Cycil wa Alexandria na, kwa kuwekwa matatani juu ya mafundisho yake huko Antioquia. Antioquia yalikuwa makao makuu ya mtazamo wa kihistoria wa visarufi vya maandiko kwa utafasili wa Kibiblia, wakati Alexandria yalikuwa makao makuu ya shule Nne zilizotengwa kwa ajili ya utafasili. Nestory hatimaye aliondolewa toka ofisini na kukimbilia mafichoni.

**Mwandishi wa awali.** Hii inarejerea wandishi halisi wa maandiko

**Mafunjo/Magombo.** Haya yalikuwa aina mojawapo ya nyenzo toka Misri zilizotumika kuandikiapo maandiko. Yalitengenezwa kwa majani au magome ya miti. Ni nyenzo ambazo nakala za zamani Agano la Kale la Kiyunani zilihifaziwapo.

**Vifungu Mlinganyo.** Ni sehemu ya mtazamo kuwa yote yaliyomo kwenye Biblia yametoka kwa Mungu na, kwa hiyo, ni ufafili wake mahusiano na mlinganyo wa kweli wa kimafumbo. Hili pia ni la msaada pale mtu anapajaribu kutafasili kifungu kisicho wazi au kigumu. Pia inamsaidia mtu kupata kifungu kilicho wazi juu ya somo husika vile vile mtazamo wote wa kimaandiko juu ya somo husika.

**Ufafanuzi/fasili.** Hili ni jina la nadhalia ya utafali wa Biblia. Utafasili wa Biblia unaweza kuangaliwa kama mwendelezo wa mahusiano wa “neno kwa neno” ambapo neno la Kiingreza laweza kuweka kwa kila neno la Kiebrania au Kiyunani kwenye “fasili” ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa mtizamo wa kawaida wa neno au kifungu cha awali. Kati ya nadhalia mbili hizi “mlinganyo wa nguvu” ambao unajaribu kuchukuawa kwa umakini andiko la awali lakini likatafasiliwa katika muundo wa kisasa wa kisarufi na nahau. Kweli kabisa mjadara mzuri wa nadhalia hizi mbali mbali za utafasili zinapatikana katika chapisho la Fee na Stuart *How to Read the Bible For All Its Worth*, Uk. 35.

**Aya.** Huu ni msingi wa ufasili wa fasihi moja kinadhalia. Unajumuisha wazo moja kuu na mwendelezo wake. Tukibaki na musukumo wake mkuu hatutatazama juu ya udogo wake au uzuri wa kusudi la mwandishi wa awali.

**Uparokia.** Hii inahusiana na mapendeleo yaliyofungiwa kwenye muundo wa tamaduni/ thiolojia ya kawaida. Haitambui asili ya mapokeo ya kweli yaliyobadilika ya Kibiblia au matumizi yake.

**Fumbo.** Hii inarejerea kweli zile zinazoonekana kuleta mkanganyiko, na bado zote zikabaki kuwa kweli, ingawa bado zinakinzana. Zinaunda kweli kwa kuwakilisha toka pande zilizo kinyume. Kweli nyingi za Kibiblia zinawakilishwa kimafumbo (au kiupembuzi). Kweli za Kibiblia sio kama nyota zilizotengana, zimetengenezwa kwa ukilimio wa sehemu za nyota.

**Pilato.** Alikuwa ni mmoja ya wanafalsafa wa Ugiriki ya kale. Falsafa yake kwa kiasi kikubwa ulisababisha kanisa la mwanzo kupitia wasomi wa Alexandria, Misri na baadaye, Augustino. Alituma ujumbe kuwa kila kitu duniani ni kiini macho na ni mfano tu wa kielelezo asili wa vitu vya rohoni. Baadaye wanathiolojia wakasawazisha "mtizamo/mawazo" ya Pilato na ulimwengu wa kiroho.

**Dhanio.** Hili linarejerea uelewa wa jambo tulilowaza kabla. Mara nyingi tunaunda wazo au hukumu kuhusu mambo hata kabla hatujatazamisha maandiko yenewe. Uelekezaji huu vile vile hujulikana kama upendeleo, kujitanguliza mbele, kudhania au kuelewa kabla.

**Uhakiki wa maandishi.** Hiki ni kitendo cha kutafasili maandiko kwa nukuu za kifungu bila kuangalia mazingira ya haraka au ukubwa wa mazingira katika fahisi moja. Hii inaondoa vifungu toka kwa kusudio la mwandishi wa awali na mara nyingi unahusha jaribio la kuhakiki maoni binafsi wakati huo likithibitisha mamlaka ya Kibiblia.

**Ualimu wa dini ya Kiyahudi.** Ngazi hii ya maisha ya watu wa Uyahudi yalianza walipokimbilia Babel (586-538 K.K). kama ushawishi wa makuhani na hekalu ulivyoondolewa, masinagogi ya kawaida yakawa mtizamo wa maisha ya Kiyahudi. Hivi vitovu vya kawaida vya tamaduni za Kiyahudi, ushirika, kuabudu na elimu ya Biblia ikawa mtizamo wa maisha ya kidini kitaifa. Katika siku za Yesu, hii "dini ya wandishi" ilikuwa sambamba na ile ya makuhani. Katika kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 70 B.K muundo wa kiandishi, ukitawaliwa na mafalisayo, walidhibiti mwelekeo wa maisha ya kidini ya Kiyahudi. Inachagizwa na utafasili wa kuitendaji, na wa kisheria wa Torah kama ulivyoolezwa katika tamaduni za Talmud.

**Ufunuo.** Hili ni jina lililopewa kwenye dhana ya kwamba Mungu amesemezana na mwanadamu. Wazo zima mara nyingi limeelezewa katika maneno matatu- (1) Ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) Uvuvio-Ametoa tafasili sahihi ya matendo yake na maana yake kwa mtu Fulani aliyemchagua kuweka kumbukumbu ya mwanadamu (3) Nuru-Amempa Roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa ukaribu wake.

**Elimu-maana.** Hii imerejerea kipimo halisi cha maana kinachohusiana na neno. Kimsingi ina vidokezo mbali mbali vya neno katika mazingira tofauti.

**Maandiko ya kale ya Kiyunani.** hili ni jina lililopewa tafasili ya Kiyunani ya Agano la kale la Kiebrania. Mafundisho ya zamani yanasema kuwa yaliandikwa kwa siku 70 na wasomi sabini wa Kiyahudi kwa ajili ya maktaba ya Alexandria, Misri. Tarehe ya kimapokeo ilikuwa 250 K.K (kiukweli yawezekana ilichukua zaidi ya miaka Mia kumaliza kuandika). Tafasili hii ni muhimu kwa sababu (1)inatupatia andiko la kale kulinganisha na andiko la Kiebrania (2) inatuonyesha sisi hali ya utafasili wa Kiyahudi katika karne ya pili nay a tatu K.K (3) inatupatia uelewa wa umasihi wa Kiyahudi kabla ya kumkataa Yesu. Kifupi chake ni "LXX".

**Machapisho ya asili.** Haya ni machapisho ya asili ya Kigiriki ya karne ya Nne B.K Yalivumbuliwa na msomi wa Kijerumani, Tischendorf, katika nyumba ya mtawa Catheline, kwenye eneo la kimila la mlima Sinai. Maandishi haya yameundwa na herufi ya kwanza ya Kiebrania ya alfabeti inayoitwa "eleph" (א). Yanajumuisha Agano la Kale na Agano Jipywa kwa pamoja.

**Kujitakasa.** Hili neno ni kisawe chenye istiari katika maana kuwa linakwenda mpaka kwenye historian a mazingira ya fasihi ya kifungu na kulifasili katika msingi wa jambo lingine.

**Visawe.** Hii inarejerea maana yenyenye kariba au mfano wa maana moja (ingawa kiukweli hakuna maneno mawili yenyenye elimu-maana kamili iliyopishana). Kwa karibu sana yanahusiana kiasi kwamba moja linaweza kuwa mbadala wa lingine katika sentesi bila kupoteza maana. Pia yanatumika kuunda moja kati ya miundo mitatu ya mlinganyo wa ushairi wa Kiebrania. Kwa maana hii inarejesha mistari miwili ya ushairi ambayo inaelezea kweli ile ile (kama vile Zab. 103:3).

**Sintaksi.** Hili ni neno la Kiyunani linalirejereshwa muundo wa sentesi. Inahusiana na namna ya sehemu ya sentesi zinaweza wekwa pamoja kuleta maana kamili.

**Usanisi.** Hii ni moja ya maneno matatu yanayohusiana na aina ya ushairi wa Kiebrania. Neno hili linaongelea juu ya mistari ya ushairi uluojengwa juu ya mwengine katika maana moja, wakati mwengine huitwa “taaluma ya mabadiliko ya hali” (k.v. Zab 19:7-9).

**Thiolojia mpangilio.** Hii ni hatua ya utafasili ambayo inajaribu kuhusisha ukweli wa Biblia katika hali ya pamoja na mlingano. Ina mantiki zaidi kuliko historia tupu, ni uwasilishaji wa thiolojia ya Kikristo kwa namna ( Mungu, mtu, dhambi,wokovu).

**Buku la taratibu na kanuni za Kiyahudi.** Ni wadhifa uliokuwapo kwa ajili ya upangaji wa simulizi za kanuni na taratibu za Kiyahudi. Wayahudi wanaamini ultolewa kwa Musa kwa kusimuliwa na Mungu kwenye mlima Sinai. Ki-ukweli inaelekeea kuwa ni mkusanyiko wa hekima za walimu wa Kiyahudi kwa miaka mingi. Kuna matoleo mawili tofauti yaliyo andikwa juu ya Talmud: ya Babel na fupi la kiparestina ambalo halikwisha.

**Uhakiki wa tofauti za kiuandishi.** Huu ni usomaji wa maandiko wa Biblia. uhakiki wa maandiko ni muhimu kwa sababu hakuna maandiko ya mwanzo yaliyopo na nakala zilizopo zinatofautiana toka moja hadi nyingine. Unajaribu kuelezea utofauti na kufika (karibu iwezekanavyo) na maneno ya awali kabisa ya miandiko ya Agano la kale na jipya. Mara nyingi unaitwa “uhakiki wa asili ya neno”.

**Upokeaji wa Maandiko.** Usanifishaji huu ulianzia kwenye toleo la Elzevir la Agano jipya la Kiyunani katika mwaka wa 1633B.K Kimsingi ni muundo wa Agano jipya la Kiyunani lililozalishwa toka kwenye maandiko machache ya asili ya Kiyunani na matoleo machache ya Erasmo ya Kilatini (1510-1535), Stephano (1546-1559) na Elzevir (1624-1678). Katika *An Introduction to the Textual Criticism of The New Testament uk. 27 cha A.T Robertson* anasema “andiko la Byzantine kiutendaji ni aina ile ile ya uundaji wa maandiko. Andiko la Byzantine ni la thamani ya chini kati ya familia tatu ya maandiko ya awali ya Kiyunani (Kimagharibi, Alexandria na Byzantine). Inajumuisha mkusanyiko wa makosa ya karne nyingi za maandiko na nakala za mkuon. Hata hivyo, A.T Robertson alisema uundaji wa maandiko umetunza kwa ajili yetu andiko sahihi kimalidhawa (uk.21). Mapokeo haya ya maandiko ya asili ya Kiyunani (hasa Erasmo, toleo la tatu la 1522) yanatengeneza msingi wa toleo la King James la mwaka 1611 b.k.

**Sheria za Musa.** Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya “ufundishaji”. Lilitokea kuwa wadhifa rasmi wa maandishi ya Musa (Mwanzo mpaka Kumbu kumbu la Torati). Kwa Wayahudi ulikuwa ni mgawanyo wa kimamlaka wa kanuni za kanisa la Kiebrania.

**Uanishaji.** Hii ni aina ya urasimishaji wa wa utafasili. Mara nyingi unahusisha kweli ya Agano jipya inayopatikana katika vifungu vya kale kwa njia ya analogia. Namna hii ya kanuni za ufasili ilikuwa ni dalili kubwa ya njia za Alexandria. Kwa sababu ya matukano ya aina hii ya utafasili, mtu lazima aweke ukomo wa matumizi yake kwa mfano mahsusii ulioandikwa katika Agano jipya.

**Maandiko ya Vatican.** Haya ni maandiko ya asili ya Kiyunani ya karne ya Nne B.K. Yalipatikana kwenye maktaba ya Vatican. Uwasili wake unajumuisha vitabu vyote vya Agano la kale, ufunuo na Agano jipya. Hata hivyo, sehemu zingine zilipotea( Mwanzo, Zaburi, Waebrania, Filemon na Ufunuo). Inasaidia maandiko ya asili kubadilisha miandiko ya maneno ya awali. Tena yameundwa kwa herufi kubwa “B”.

**Tafasili ya Biblia ya Kilatini.** Ni jina la tafasili ya Biblia ya Kilatini ya Jerome. Ilikuwa ndio msingi au utafasili wa "kawaida" wa kanisa Katoriki la Rumi. Lilifanyika mwaka 380 b.k.

**Hekima ya Fasihi.** Hii ni fasihi tanzu iliyozoleka enzi za kale karibu na pande za Mashariki (na ulimwengu wa kisasa). Kimsingi likuwa ni jaribio la kuelekeza kizazi kipyaa juu ya mwongozo wa maisha ya ushindi kupitia ushairi, mithali, au insha. Ilielezewa zaidi kwa watu binafsi kuliko kwenye jumuiya iliyoungana. Haikutumia viini macho kuweka historia, lakini ilisimamia uzoefu na uchunguzi wa maisha katika Biblia, Ayubu kupita Wimbo ulio Bora, anasadiki uwepo na ibada ya YAHWE, lakini mtizamo huu wa ulimwengu wa kidini sio wa wazi kwa uzoefu wa kila mtu kila wakati.

**Picha ya ulimwengu na Mtizamo wa Kidunia.** Haya ni maneno mwandani. Yote yana dhana ya kifalsafa kuhusiana na uumbaji. Neno "picha ya ulimwengu" inarejerea "kwa namna gani" juu ya uumbaji wakati "mtizamo wa kidunia" unahusiana na "nani." Maneno haya yote ni muhimu kwenye utafasili pale mwanzo 1-2 inaposhughulika hasa hasa na nani, na sio kwa namna gani juu ya ulimwengu.

**YAHWE/YEHOVA.** Hili ni jina la Agano la Mungu katika Agano la kale. Linnelezezwa katika kitabu cha Kutoka 3:14. Ni muundo wa KISABABISHAJI wa neno la Kiebrania "kuwa" ambalo Wayahudi waliogopa kulitamka jina hili ili wasilitamke bure; kwa hiyo, walitumia jina lingine badala yake yaani "Adonai" likimaanisha "Bwana". Hivi ndivyo jina la Agano limetafasiliwa katika Kiingereza.

## **KAULI YA KIMAFUNDISHO**

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ifuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, muumbaji na mkombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendeleo. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa milelekwa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachowenza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo.
4. Binadamu, japo aliumbwaa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenyé nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambaa wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine". Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa

kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake.

Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

“Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo.”